

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Hamsini na Moja – Tarehe 24 Juni, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura Mbunge wa Viti maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini.

Na. 434

Ukosefu wa Vitendea Kazi – Kituo cha Afya Kigoma Ujiji

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. SABREENA H. SUNGURA) aliuliza:-

Kituo cha Afya kilichopo Kigoma Ujiji Manispaa kinahudumia wakazi zaidi ya elfu arobaini katika Kata kumi na moja za Manispaa lakini kina kinakabiliwa na ukosefu wa Chumba cha theatre, X-ray pamoja na Ultra Sound:-

Je, ni lini Serikali itakipatia Kituo hiki vifaa hivyo ili kusaidia wananchi hao wanaohudumiwa na Kituo hicho?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujji ina jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 24, hospitali mbili, vituo vya afya vinne, Zahanati 17 na Kliniki moja. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri imepanga kutumia shilingi milioni 45 za bakaa iliyopo *MSD* kununua mashine 1 ya *Ultra sound*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vilevile katika mwaka wa fedha 2019/2020 Kituo kimetenga kiasi cha shilingi milioni 15.4 kuititia fedha za mradi wa malipo kwa ufanisi (*RBF*) kwa ajili ya ukarabati wa chumba kinachotumika kwa huduma za mionzi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza niishukuru Serikali pale Rombo nina Kituo cha Afya kinaitwa Kituo cha Karume, tulipewa shilingi milioni 500 kwa hiyo ni kimekuwa kituo cha afya cha kisasa kabisa sasa hivi. Hata hivyo viro vituo ambavyo havina kabisa vifaa vya hospitali, na tuna upungufu wa wahudumu wa afya takriban asilimia 58 ya wahudumu wanaotakiwa kuwepo?

Je, Serikali iko tayari kutusaidia ili vituo vingine hivi viweze kupata vifaa ili kusaidiana na ile hospitali ya wilaya katika kuhudumia wagonjwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyo sema tuna shida kubwa sana ya watumishi wa afya; asilimia 58 ya watumishi wanaotakiwa wawepo, hawapo, je katika mgao Serikali iko tayari kufikiria kutupatia mgao wa watumishi wa afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Joseph Roman Selasini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa wa niaba ya Wizara nipokee pongezi, Mheshimiwa Selasini anasema kituo chake ambacho amepata jumla ya shilingi milioni 500, ni miongoni mwa vituo vya kisasa kabisa nchini. Naomba nitumie fursa hii kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge Vituo kama hicho anachokisema Mheshimiwa Selasini viko vimejengwa nchini nzima. Kwa hiyo ni pongezi ambayo inatustahili Serikali kuweza kuipokea kwa sababu ni kazi kubwa ambayo imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake anaongelea suala zima la vifaa; naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wote ambao vituo vya afya vimejengwa kwenye maeneo yao, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vile vituo vyote ambavyo vimejengwa havibaki vikawa ni mapambo, vinatakiwa vikamilike na vipelekewe na vifaa. Hivi ninavyoongea kuna kiasi cha fedha takribani bilioni 40 ambazo tunazifatilia Hazina ili tuweze kuhakikisha kwamba vifaa vinanunuliwa na vinapelekwa vituo vyote vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, anaongelea juu ya umuhimu wa watumishi. Ni kweli, tukiweka vifaa bila kuwa na watumishi napo itukuwa hatujafanya lolote. Naomba nitumie fursa hii kumtaarifu yeye pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wote kwamba katika maombi tumeomba kupatiwa watumishi 12,000 na ni imani yetu kwamba maeneo yatakayozingatiwa ni yale ambayo yana upungufu mkubwa ikiwa ni pamoja na maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Roman Selasini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika llani yake ilieleza kwamba itatoa matibabu bure kwa wazee, kwa Wilaya ya Nyang'hwale kuna wazee takribani 6,000 na wazee hawa ni 100 tu ambao wanapata matibabu bure, Je, Waziri ananiambia nini? Hawa wazee 5,900 waliobaki watapata vitambulisho vya kuweza kupata matibabu bure?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza, naomba tukubaliane naye kwamba si wazee wote ambao tumeahidi kuwapa matibabu bure, tumeahidi kutoa matibabu bure kwa wale wazee ambao hawana uwezo, kwa hiyo hilo lazima tuwekane sawa. Na ni ahadi ambayo iko thabiti baada ya kufata *procedure* zote ambazo zinatakiwa tunaamini kabisa wazee hawa wamefanya kazi kubwa katika kutumikia taifa hili la Tanzania ndio wametufikisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba wale wote ambao hawana uwezo wanatibiwa bure kama ambavyo sera ya Serikali inavyoelekeza. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kigola swali la nyongeza.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Tuna Zahanati iko katika Kata ya Luhunga Kijiji cha Igoda, ile zahanati tulishamaliza kujenga kila kitu na vitanda tulishaweka, na sasa ina miaka miwili hajafunguliwa. Je, ni lini Serikali sasa itaenda kufungua ile zahanati ambayo imejengwa na wananchi ili iweze kuanza kufanya kazi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa maelekezo kwa Waganga wote wa wilaya nchini, kwamba maeneo ambayo wananchi wamejenga zahanati na zimekamilika hakuna sababu ya kuendelea kusubiria zisianze kutoa huduma; na hassa pale anaposema Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari vifaa vyote viro. Kwa hiyo ni vizuri ndani ya Wilaya wahakikishe kwamba wanapeleka watumishi; kazi ambayo inawezekana kabisa; ili zahanati hiyo ianze kufanya kazi na wananchi wafaidi matunda ya jasho lao.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba, Mbunge wa Viti maalum.

Na. 435

**Changamoto Zinazoikabili Sekondari ya
Lanzoni – Wilayani Mkinga**

MHE. YOSEPHER F. KOMBA aliuliza:-

Sekondari ya Lanzoni iliyopo Wilayani Mkinga ilianzishwa mwaka 1995 kwa lengo la kuchukua wanafunzi wa chaguo la pili lakini inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa umeme, maji, usafiri pamoja na makazi ya watumishi:-

Je, Serikali ina Mikakati gani ya kushirikiana na Halmashauri ya Mkinga katika kutatua changamoto hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba Mbunge wa Viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Shule ya Sekondari ya Lanzoni ina changamoto nyingi za kimazingira ikiwemo kutokuwa na umeme wa grid, maji na uhaba wa nyumba za walimu. Pamoja na changamoto hizo, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri kupitia Mpango wa *MMES II*, ilifanikiwa kujenga nyumba mbili (2) mpya za walimu, vyumba viwili vya madarasa na maabara moja ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga imefanya tathmini ya kupeleka maji katika shule ya Lanzoni kutoka katika Mto Zigi na kubaini kuwa kiasi cha

shilingi milioni 7.6 zinahitajika. Halmashauri kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutafuta fedha ili kukamilisha kazi hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Shule ya Sekondari Lanzoni haina umeme wa *grid* na inatumia umeme wa juu. Hata hivyo tayari imeshaingizwa kwenye Mpango wa *REA III* hivyo muda wowote itaunganishwa kwenye umeme wa *grid* Taifa, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba swali la nyongeza.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kama ambavyo aliyejibu swali amekiri kwamba Shule hii ina changamoto nyingi. Shule hii imeanza mwaka 1995 lakini iko ndani la eneo la shamba ambalo lilikuwa la Mkonge la Mjesani *Estate*, na mpaka sasa tunavyoongea shule hii haina hatimiliki ya lile eneo, kwa hiyo walimu na watendaji pale wamekuwa wanaishi kwenye shule ile kama vile wamepanga. Kwa hiyo nilitaka nifahamu, Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha shule hii inapata hatimiki ya eneo ili iweze kufahamu mipaka ya eneo lake kama Shule?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kama ambavyo amesema Mheshimiwa Waziri. kuhusu suala la maj. Pale kuna Mto Zigi ambao ndio wanaoutumia wanafunzi kuchota maji kwa ajili ya matumizi pale shulenii, na kumeshatokea ajali zaidi ya mbili ya wanafunzi pale kutaka kuuawa na mamba, ule mto una mamba. Je, Serikali kama mdau mkuu kwenye hili suala la elimu wako tayari kushirikiana na halmashauri na wadau wengine kuhakikisha milioni 7.6 inapatikana kwa wakati ili kupeleka maji kwenye shule ile?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa

Naibu Spika, ahsante, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yosepher Komba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tunahitaji maeneo yote ya Umma yapimwe na yapate hatimiliki ili kuwa na uhalali wa eneo hilo lakini pia kupunguza migogoro ambayo inatokana na wananchi kuvamia maeneo hayo ya umma ikiwemo Mashule kama alivyotaja. Naomba nimuelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri hii ya Mkinga atume wataalam wapimaji wakapime eneo hilo ili waweze kupata hati na kuondoa migogoro ambayo inaweza kuwepo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili anazungumzia habari ya maji. Tumesema kwamba tathmini imeshafanyika, zinatakiwa shilingi milioni 7.6, na Serikali ipo tayari kushirikiana na halmashauri, na pia Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na sisi. Sote kwa pamoja tuhakikisha kwamba tumepata maji katika eneo hili na watoto wetu waweze kupata huduma nzuri na masomo yaendelee.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na changamoto za maji na umeme katika shule zetu kumekuwa na tatizo kubwa sana katika shule nyingi nchini hasa Mkao wa Mara pamoja na Jimbo la Bunda Mjini; tatizo la matundu ya vyoo. Athari kubwa ni kuleta magonjwa ya mlipuko kwa wanafunzi wetu pamoja na shule kufungwa. Sasa ningependa kuiuliza Serikali, ina mpango gani wa kushirikiana na taasisi mbalimbali katika kuhakikisha kwamba matundu ya vyoo yanajengwa shulenii ili kuwafanya wanafunzi wetu wasome wakiwa katika hali ya usalama zaidi wasipate magonjwa ya mlipuko?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tuna upungufu mkubwa sana wa matundu vyoo nchi nzima kwa shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linapaswa kuwa jambo shirikishi, haiwezi kuwa kazi ya Serikali peke yake. Serikali imetoea Waraka ambao umeanza kutumika, wa mwaka 2016 ambao unaonesha namna ambavyo wadau mbalimbali wakiwepo na wananchi wa kawaida wanaweza kushirikiana kuweza kupunguza changamoto za miundombinu ya elimu. Serikali imekuwa ikifanya kazi hii awamu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha; na mwaka wa fedha ambao unaanza Julai mwaka 2019/2020 tumetenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 184 kwa ajili ya kuondoa kero katika miundombinu ikiwepo matundu ya vyoo. Nimuombe Mheshimiwa Mbunge na wadau wengine tushirikiane; unapokuwa unaweza kuchangia tuchangie ili kuweza kupunguza adha hizi ambazo zipo katika shule zetu, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel swali la nyongeza.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Changamoto hii ya vyoo inawaathiri zaidi watoto wenye mahitaji maalum; watoto wenye ulemavu wanalazimika kutambaa katika uchafu, vinyesi vya watoto wenzao; na hiki ni kilio changu tangu nimeingia Bungeni.

Naomba mkakati madhubuti wa Serikali, wana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba watoto wenye mahitaji maalum wanasoma katika mazingira mazuri na tunawaondoa katika hiyo hali hatarishi ya kuweza kupata magonjwa mbalimbali? Ahsante?. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amina Mollel kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba watoto na watu wote wenye mahitaji maalum wanahitaji *special treatment* ili aweze kuishi pamoja vizuri katika jamii yetu. Serikali imekwishaelekeza majengo yote mapya ambayo yanajengwa, si ya elimu tu, majengo yote ya Umma; wanapojenga jengo la Mkuu wa Wilaya, Mkoa, vituo vya afya zahanati na hospitali za mikoa pamoja na shule zote tunazingatia mahitaji ya watu wenye mahitaji maalum. Lazima kuna chumba maalum cha choo kwa ajili ya watu hao, lakini pia na watoto wa kike wakujisitiri wakati wao wa hedhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, mambo hayo tunaomba yazingatiwe na uongozi wote katika ngazi ya mikoa ya wilaya wafuate maelekezo ya Serikali. Tunapofanya ziara mbalimbali katika mikoa yetu mionganoni mwa kazi ambazo tunafanya tunakagua kama kweli katika choo kilichoengwa kuna choo maalum. Maeneo yote tumefanya hivyo na jambo hilo linaendelea kufanya kazi vizuri. Hata hivyo majengo ya zamani yanapofanyiwa maboresho pia na jambo hili lizingatiwe; mahitaji maalum ni muhimu na limekubalika lazima lifanyiwe kazi, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oliver Semuguruka swali la nyongeza.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona, Shule ya Sekondari ya Mumiterama iliyopo Wilaya ya Ngara imeanzishwa mwaka huu na haijawahi kupatiwa fedha yoyote kwa ajili kuendesha.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka pesa katika shule hiyo, kwa sababu ina changamoto nyingi, maji usafiri na makazi ya watumishi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Shule ya Sekondari ya TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuruku, naomba nijibui swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipokee ombi lake, kwa sababu shule inapokuwa inaanizishwa kwanza kuna mambo ya kuzingatia, tunaangalia vigezo mbalimbali, Ofisi ya Rais TAMISEMI, pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sasa kama shule imesajiliwa imeanza kweli hajawahi kupelekewa fedha naomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi cha maswali na majibu tuwasiliane tuone ni kwa nini hajapata na kama kuna ukweli wowote tuweze kuchukua hatua, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Khatib Said Haji Mbunge wa Konde sasa aulize swali lake.

Na. 436

Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika eneo la Deep Sea Tanga

MHE. KHATIB SAID HAJI aliuliza:-

Athari za mabadiliko ya tabianchi zimesababisha uharibifu mkubwa katika Bandari ya Tanga eneo la *deep sea* lango kuu la kuingia na kutokea katika bandari hiyo:-

Je, Serikali inachukua hatua gani za dharura kudhibiti uhalibifu huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
(MUUNGANO NA MAZINGIRA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said hajji Mbunge wa Konde kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za mabadiliko ya tabianchi zinatofautiana katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo maeneo ya Ukanda wa Pwani ambapo ni muhimu kwa shughuli za uchumi. Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuchukua hatua za makusudi katika kukabiliana na athari hizo ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi wa Mwaka 2007 na Mkakati wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Mwaka 2012. Mipango hii imeelekeza hatua za haraka za kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika sekta muhimu ikiwemo maji, maliasili, miundombinu, afya, nishati, Ukanda wa Pwani na maeneo ya bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la ufukwe lijulikanalo kama *deep sea* lilitopo katika Jiji la Tanga linakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo athari za kimazingira kama vile utupaji holela wa taka hasa za plastiki na taka zingine ambazo huletwa na mifereji ya maji ya mvua inayoingia baharini kuto katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hatua zilizochukuliwa na Serikali na Halmashauri ya Jiji la Tanga katika kuhifadhi na kulinda eneo hili dhidi ya uchafuzi wa mazingira ni pamoja na kufanya kampeni za usafi wa mazingira zikihusisha wavuvi, wafanyabiashara na vikundi vyta mazingira. Pia kutoa elimu kwa wavuvi na wadau wengine katika eneo hili kuhusu usafi wa mazingira na kuhifadhi miti na uoto wa asili kuzunguka fukwe hizo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib Said Haji, swalii la nyongeza.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza nieleze kuridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba wameanzisha kampeni ili kukabiliana na hali hiyo, lakini ukubwa wa tatizo uliopo katika lango lile la kuingilia bandari ya Tanga siyo jambo linalotaka kampeni bali ni jambo linalotaka hatua za dharura ili kuzuia isije ika tokea barabara ile ikabomoka kama ilivyotokea hapo nyuma. Je, Serikali iko tayari sasa kuliona hili na kulichukulia hatua hizo ninazozilomba?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, athari zilizopo katika eneo la *Deep Sea* Tanga linafanana kabisa na athari zilizopo katika eneo la Sijuu Kijiji cha Msuka Jimbo la Konde Kaskazini Pemba ambalo ndiyo Jimbo langu. Nina hakika Mheshimiwa Waziri aliwahi kufika huko, kutembelea na kuiona hali ile: Je, Serikali iko tayari kuchukua hatua za dharura ili kuokoa vijiji vya maeneo yale visiendelee kumomonyoka kutokana na athari za kimazingira?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Konde, kaka yangu Mheshimiwa Khatib. Ni kweli kabisa kama anavyosema eneo hili la *Deep Sea* kuna hatua za dharura ambazo tumeanza kuzichukua mpaka sasa na sasa wataalam wetu wanafanya tathmini na baada ya tathmini

hiyo wataleta andiko ofisini ili tuweze kuweka kwenye mifuko yetu ya kimazingira kuhakikisha tunapata fedha kuokoa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama alivyosema kule kwenye Kijiji cha Msuka kwenye Jimbo lake Konde nilifika na nimhakikishie Mheshimiwa Khatib hatua zote hizi za kufanya tathmini kwenye maeneo haya ambayo yameathirika kwa nchi nzima tunayafanya kwa pamoja na nitafika tena kwa ajili kuhakikisha kwamba eneo hili tunalitatu kama tulivyokuwa tumepanga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yusuf, swali la nyongeza.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Suala la *Sea Erosion* lipo katika nchi yote ya Tanzania ambayo imezungukwa na ukanda wa bahari na linamega kwa kiasi kikubwa ardhi ya Tanzania hali ambayo inahatarisha usalama wa watu wetu, pia kupungua kwa ardhi yetu. Kwa mfano, Msimbati Mkoani Mtwara ardhi ilichukuliwa kwa zaidi ya mita kumi kwa wakati mmoja:-

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhamasisha na wao wenyewe Serikali kushiriki katika kupanda miti ya mikoko maeneo yale ili kuzuia athari hizi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye majibu ya msingi kwamba tayari tunao mpango wa kuhimili mabadiliko ya tabia nchi wa mwaka 2007. Pia tuna mkakati wa mabadiliko ya tabia nchi wa mwaka 2012. Kwa hiyo, mkakati huu ulikwishaanza kwenye maeneo yote yaliyoathirika na nikuhakikishie tu kwamba mkakati unaendelea na pale utakapopata fedha kwa ajili ya kuokoa maeneo haya, maana yake tutafika kwa ajili ya kuhakikisha maeneo haya tunyaweweka salama.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa Mbunge wa Rufiji sasa aulize swali lake.

Na. 437

Tatizo la Maji la Rufiji

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA aliuliza:-

Matatizo ya maji katika Jimbo la Rufiji ni ya muda mrefu kwenye maeneo kadhaa hususan Kata ya Ngarambe maji hupatikana kwa umbali zaidi ya kilometra 7 - 10 na kwa kuwa Serikali sasa inaleta sera ya Maji ndani ya mita 400:-

Je, ni lini Serikali itatua kero ya maji katika Kata ya Ngarambe, Mbwala, Chumbi, Muholo, Kipugila na maeneo mbalimbali ya Tarafa ya Ikwiriri hata kwa kuchimba visima?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya huduma ya maji katika Halmashauri ya Rufiji na kwa sasa tayari baadhi ya kata hizo zimeanza kupewa kipaumbele kwa kujengewa miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Mbwala kuna mradi wa kisima kirefu ambao unatumia teknolojia ya dizeli. Mradi huo kwa sasa una changamoto ya uendeshaji kwani wananchi wanatumia gharama kubwa kwa kununua mafuta ya uendeshaji wa mitambo ya mradi huo. Halmashauri inaendelea na taratibu za kutumia teknolojia ya umeme wa *REA* ambao tayari umeshafika katika kata hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Chumbi vimechimbwa visima viwili ambapo kwa sasa vipo katika

hatua ya usanifu wa miradi. Kata ya Muholo imewekwa katika utekelezaji wa miradi ya awamu ya pili ambapo kwa sasa usanifu katika visima viwili umekamilika. Wizara imeshatoa kibali kwa ujenzi wa miundombinu kwani miundombinu ya awali ilchakaa na haifai tena kwa mradi. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri ya Rufiji imetengewa jumla ya shilingi milioni 871.98 kwa ajili ya kuendelea kukamilisha miradi ya zamani ya kujenga miradi mipyaa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchengerwa, swali la nyongeza.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji kwenye Wilaya ya Rufiji ni kubwa sana hali iliyopelekea nguvu kazi kubwa ya vijana na akina mama kupotea wakijaribu kutembea umbali mrefu, pia wakidiriki kuchota maji kwenye maeneo ya Mto Rufiji na kupelekea wananchi wengi kuchukuliwa na Mamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango gani wa kuja kufanya tathmini ikizingatiwa kwamba Rufiji ni kanda maalum, pia Rufiji tunatekeleza mradi wa uzalishaji wa umeme wa *Stiegler's Gorge*. Je, ni lini Serikali itakuja kufanya tathmini halisi kabisa ya tatizo la maji Wilaya yetu ya Rufiji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tatizo la maji kwenye Kata ya Mbwala ambayo Mheshimiwa Waziri amejibia ni kubwa sana tofauti kabisa na majibu ambayo wenzetu wa Halmashauri walimwandalia. Eneo kubwa la Kata ya Mbwala wananchi wanalazamika kusafiri umbali wa kilometra saba mpaka 10 kufuata maji katika maeneo ya Kikobo na maeneo mengine.

Je, ni lini Serikali itadhamiria kabisa kuchimba visima virefu karibu na kwa wananchi hali ambayo hivi sasa imepelekea vijiji vingi wananchi kuhamza kutafuta maji kwa sababu wanadiriki kusafiri umbali mpaka wa kiklometra 7 - 10?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Nataka niwahakikishie Wandengereko wote, wamechagua jembe wembe na anafanya kazi kubwa sana katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa anataka kujua jitihada za Serikali. Tunatambua kwamba maji ni uhai na ni moja ya changamoto kubwa, lakini sisi kama Wizara ya Maji tumefanya jitihada kubwa ya uchimbaji visima 13 pale yenye thamani zaidi ya shilingi milioni 400, tumeshachimba visima 10. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya ukamilikishaji ule wa visima tutafanya usanifu katika kuhakikisha tunatekeleza miradi mikubwa ili wananchi wako waweze kupata huduma hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nikuhakikishie kutokana na Kata hiyo ya Mbwala, mimi kama Naibu Waziri nitapata nafasi ya kuja katika Jimbo lako na nitafika katika Kata ya Mbwala ili tuweze kushauriana na kuangalia namna gani tunaweza tukatatua tatizo la maji katika kata yako. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo maswali yetu ni mengi kidogo, kwa hiyo, mniruhusu tuendelee. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, sasa aulize swali lake.

Na. 438

**Kusuasua kwa Ujenzi wa Mradi wa Maji
Bwawani, Makambako**

MHE. DEO K. SANGA aliuliza:-

Mradi wa Maji wa Bwawani umekuwa ukisuasua kujengwa ikiwemo kuzungushiwa uzio:-

Je, ni lini mradi huo utakamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya maji kwenye Mji wa Makambako ulisainiwa tarehe 23/05/2017 kati ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (*IRUWASA*) na Kampuni ya Ujenzi inayoitwa *Building Water and Earth Works Ltd* ya Jijini Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi bilioni 1,568 ikiwa ni pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*). Kazi ya ujenzi ilianza tarehe 08/06/2017 na kwa mujibu wa mkataba, kazi hii ilitakiwa kukamilika tarehe 08/02/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa utekelezaji wa mradi huu kulijitokeza kazi ya ziada ya ujenzi wa uzio kuzunguka chanzo cha maji cha bwawani ili kuzuia uchafuzi unaofanyika kwenye chanzo hicho. Kazi hii imeongeza muda wa kukamilisha kazi zilizopangwa kwa mujibu wa mkataba hadi tarehe 30/06/2019. Kwa sasa uzalishaji wa maji katika chanzo hicho unaendelea na tayari mradi huo unatoa huduma kwa wananchi. Kazi zilizobaki zitaendelea kukamlishwa huku wananchi wakiendelea kupata huduma ya maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, swali la nyongeza.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili. La kwanza, pamoja na mradi huu kutoa maji katika Mji wa Makambako, bado haijakamilika ikiwepo pamoja na kujenga tenki la lita laki 5 ambalo lilikuwepo kwenye mradi, huo uzio wa eneo la chanzo cha maji pamoja na kukamilisha

ofisi ya mamlaka ambayo ilikuwa ndani ya huo mradi. Je, ni lini sasa vitu vyote vitakamilika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa Serikali imetupatia fedha za mkopo nafuu kutoka India kwa ajili ya miradi ile 28 ikiwepo na Makambako, naishukuru sana Serikali, wataalam walishakuja katika Mji wa Makambako wakatembelea na mradi ule umelenga kuhudumia kata tisa ikiwepo Lyamkena na mwisho mpaka Mlowa. Je, ni lini sasa mradi huo utaanza ili wananchi wa Makambako waweze kunufaika na mradi huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kwanza nimpongeze sana Mbunge, mzee wangu Mheshimiwa Deo Sanga lakini ni Mbunge mfuatilaji; siyo mara moja au mara mbili amekuwa akija katika ofisi yetu katika kuhakikisha wananchi wake wa Makambako wanapata huduma hii muhimu hasa ya maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi ule sasa hivi umefikia asilimia 60 ya utekelezaji, nasi tumekuwa wafuatilaji wa karibu sana katika kuhakikisha Mji ule wa Makambako unapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie na tumwagize Mkandarasi aongeze nguvu, nasi kama Wizara hatutokuwa kikwazo katika kudai *certificate* na kumlipa kwa wakati katika kuhakikisha mradi ule haukwami na ukamilike kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la utekelezaji wa mradi wa miji 28, nitumie nafasi hii binafsi nimpongeze Mheshimiwa Waziri wangu lakini pia nimpongeze Katibu Mkuu na wataalam wetu kwa jitihada kubwa zilizofanyika katika kuhakikisha mradi huu unaanza mara moja kwa miji zaidi ya 28 Bara na mradi mmoja utakuwa Zanzibar katika kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ninalotaka kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge, wataalam washauri walishapita huko katika maeneo. Kikubwa katika mpango wetu ni kuhakikisha kwamba mnapofika mwezi wa Tisa Wakandarasi wawepo katika maeneo yote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ndani ya mwezi wa Tisa Wakandarasi watakuwa *s/ite* na utekelezaji utakuwepo, ila la muhimu tunaomba ushirikiano katika kuhakikisha tunashirikiana ili tuweze kutatua tatizo hilo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swalilake.

Na. 439

Vijiji 11 Vinavyohitaji Kujengwa Minara ya Simu

MHE. ALEX R. GASHAZA aliuliza:-

Wakati wa Mkutano wa Bunge wa Bajeti niliwasilisha Orodha ya Vijiji 11 vinavyohitaji kujengewa minara ambavyo ni Chivu, Runzenze, Kigina na Ntoboye Kata ya Ntoboye, Murubanga, Kititiza, Kumubuga Kata ya Nyamagoma, Kijiji cha Mukalinzi Kata ya Muganza na Kijiji cha Ruhuba Kata ya Mbuba:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa minara hiyo ili kurahisisha mawasiliano kwa wananchi wa vijiji hivyo hasa ikizingatiwa kuwa vijiji hivyo viko pembeni mwa Jimbo na hali ya usalama katika maeneo hayo siyo nzuri?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swalilake

Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Kata za Ntoboye, Nyamagoma, Muganza na Mbuba zipo pembezoni mwa Jimbo la Ngara. Katika Kata ya Mbuba, vijiji vya Kumwendo, Mbuba na Kanyinya tayari vimepata mawasiliano. Pia Kata ya Muganza Kijiji cha Mukabu kimepata huduma ya mawasiliano pia. Aidha, Kijiji cha Mukalinzi utekelezaji wa upelekaji mawasiliano utakamilika mwezi Septemba mwaka huu 2019 ambapo ruzuku ilitolewa kwa Kampuni ya *Viettel* au *Halotel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Chivu, Runzenze, Kigina na Ntoboye Kata ya Ntoboye, Murubanga, Kititiza, Kumubuga Kata ya Nyamagoma na Kijiji cha Ruhuba Kata ya Mbuba vitafanyiwa tathmini kwa kuangalia mahitaji halisi na kisha kuingizwa katika orodha ya miradi itakayotekerezwa katika mwaka wa fedha 2019/2020.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza swalii nyongeza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na sasa naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwa kuwa bado kuna vijiji ambavyo havijaweza kupata minara ya mawasiliano kama vile Kijiji cha Kititiza, Kikoi, Mkalinza Kata ya Mabawe na maeneo mengine ya Jimbo la Ngara, ni lini Serikali itaweza kuwezesha ujenzi wa minara katika maeneo hayo yaliyobaki? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, baadhi ya maeneo hususan katika Kata za mipakani kama vile Kata ya Kabanga, Mabawe, Rusumo, Kata ya Kasulu, Kata za Mipakani zinazotokana na nchi ya Burundi na Rwanda, usikivu umekuwa ni hafifu na hata kuwepo na mwingiliano wa mitandao ya nchi jirani. Je, Serikali ina mkakati gani kumaliza tatizo hili la mwingiliano wa mawasiliano? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Gashaza kwa ajinsi anavyofanya bidii kubwa sana kushughulikia wananchi wake kupata mawasiliano. Nikanza na swali lake la kwanza Vijiji vya Mabawe, Kititiza na Kigoi tunategemea kuviingiza kwenye mpango wa vijiji 811 ambavyo tunategemea kuvitangaza hivi karibuni kwa ajili ya kupatiwa huduma ya mawasiliano kabla ya mwezi wa tatu mwakani. Kwa hiyo, namuomba tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira vijiji hivyo vitapatiwa mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili, ni kweli kwamba bado tuna changamoto kubwa kwenye maeneo ya mipakani ambapo mawasiliano yamekuwa yakiingiliana kati ya nchi jirani na nchi yetu. Hata hivyo, tumechukua hatua za dharura kwa kuwaelekeza *T CRA* washirikiane na mamlaka za mawasiliano za nchi jirani kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mwingiliano huo unapunguzwa au kuondolewa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huo umefanyika Mjini Arusha mwezi wa Nne kupitia kikao chao cha *East African Communication (EACO)* ambapo umeshaweka mkakati na kwa kuanzia maeneo ya mikoa ya Moshi na Kagera *Vodacom* wameshaanza kurekebisha mwingiliano wa mawasiliano ili kuhakikisha kwamba kila nchi inapata mawasiliano ambayo anahuksika nayo badala ya kufanya *roaming*.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda.

Na. 440

Kupandisha Hadhi Barabara ya Katoro - Mwingiro

MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi barabara ya Katoro – Busanda – Nyakamwaga – Nyabululo – Kamena - Nyamalimbe – Mwingiro kuwa barabara ya Mkoa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lollesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara, Vijiji na Mijini (*TARURA*) barabara ya wilaya ikiwemo barabara ya Katoro Busanda – Nyakamwanga – Nyabululo – Kamena – Nyanalimbe – Mwingiro kilometra 68 zinahudumiwa na *TARURA* iliyoanzishwa mahususi kwa ajili hiyo. Hivyo zoezi la upandishwaji hadhi barabara kutoka barabara za Wilaya kuwa barabara za Mikoa ikiwemo kukasimu (*designation*) limesimamishwa kwa muda na Serikali kwa nchi nzima ili kuipatia *TARURA* fursa ya kutekeleza jukumu hilo mahususi la kuanzishwa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelekezo hayo, namshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Ofisi ya Rais TAMISEMI na *TARURA* katika kusimamia mipango yao kuhusu barabara hii. Hata hivyo, taratibu za kuomba kupandishwa hadhi barabara imeainishwa kwenye Kanuni Na. 43 na 44 za mwaka 2009 za Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007 ambapo Bodi ya Mkoa ya Barabara (*Regional Roads Board*) huwasilisha maombi kwa Waziri anayehusika

na barabara iwapo barabara tajwa itakuwa imekidhi vigezo vya kupandishwa hadhi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, swali la nyongeza.

MHE. LOLENTA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nampongaza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kwamba *TARURA*sasa inashughulikia barabara hii. Kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana kiuchumi kwenye Wilaya ya Geita na Wilaya ya Nyanghwale, kwa sababu ni kiunganishi kikubwa katika Wilaya ya Nyang'hwale na Geita. Je, Serikali iko tayari kuongeza fedha *TARURA* ili waweze kuikamilisha hiyo barabara kwa kiwango cha changarawe ili wananchi wafanye shughuli zao vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ziko ahadi mbalimbali za Mheshimiwa Rais za muda mrefu sana ikiwemo kilomita 10 za lami Katoro – Guselesele, barabara ya kutoka Katoro kwenda Ushirombo na barabara ya kutoka Geita kuititia Bukori kwenda mpaka Kahama.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuanza kutekeleza barabara hizi kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyofuatilia maendeleo ya Busanda na Geita kwa ujumla, hapa tu ametaja barabara nyingi kweli kwa pamoja na kwa ufundi mkubwa, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nakupongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara hii ya Busanda ambayo inaelekea Nyang'hwale kuiongezea fedha,

kama nilivyojibu siku zilizopita hivi karibuni niseme tu sasa kazi ambayo ilikuwa inafanyika na *TARURA* ipo Kamati maalum inaitwa *National Road Classification Committee*, nilisema hapa kwamba baada ya *TARURA* kufanya kazi nzuri ya kuzitambua barabara zetu na kufanya uchambuzi wa kina ili sasa tuweze kuzipanga upya hizi barabara kulingana na mahitaji yake. Kwa hiyo nitumie nafasi hii tu kwa sababu Kamati hii inamalizia kazi yake iweke kipaumbele na misisitizo mkubwa kuingalia barabara hii tuweze kuitendea haki ili tuweze kuijenga katika kiwango cha changarawe kama Mheshimiwa Mbunge unavyoshauri, mimi hili nitalisimamia ili nione kwamba barabara hii tunaifanyia maboresho makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla kwamba kuwa na chombo hiki *TARURA*, Serikali imedhamiria ili kuhakikisha kwamba barabara zote zinajengwa katika *standard* ambayo inafanana. Siyo kwamba barabara zitakazosimamiwa na *TARURA* zitakuwa tofauti na barabara zinazosimamiwa na *TANROADS*, naomba tuamini hilo, kwamba tutazingatia ubora, tutazingatia weledi, tutazingatia pia kwamba gharama ambazo zinatumika ziwe *reasonable* kiasi kwamba tuweze kuhudumia barabara kwenye mtandao mkubwa, kwa hiyo niwatoe wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi za Mheshimiwa Rais katika ujenzi wa barabara ya eneo hili la Katoro na Buselesele kwa Mheshimiwa Kalemani. kwa sababu Mji wa Buselesele na Katoro umeumana, ziko ahadi za kilomita 10, tulizungumza wa wenzetu upande wa *TAMISEMI* kwamba tutaanza ujenzi pale. Kwa hiyo, tukipata fedha tutaanza ujenzi ili angalau wananchi hawa wa eneo hili ambalo linakuwa kwa kasi waweze kupata huduma vizuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lolesia usiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ipo barabara hii uliyoitaja kutoka Ushirombo kuja Mji wa Katoro kwenda Geita kilomita kama 53 hivi tumeitengea fedha na hivi ninavyozungumza tuko kwenye harakati ya kuanza kujenga

katika kiwango lami. Nikuhakikishie tu kwamba tutakavyoanza kujenga barabara hii tutaweka msisitizo mkubwa ili Mji huu wa Katoro tuweze kuanza katika maeneo haya ili wananchi wawahi kupata huduma muhimu maeneo ambayo pia yana changamoto kubwa, Kwa hiyo nikuhakikishie tutaanza nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umezungumzia pia barabara hii ambayo inatoka Kahama inapita Bulyanhulu, Bukori inakwenda mpaka Geita kilomita 120, Kilomita 51 ziko katika eneo lako Mheshimiwa Mbunge. Nikuhakikishie tu kwamba Mheshimiwa Waziri alikuwa anashughulikia ili tuanze ujenzi wa barabara hii, na Bunge hili limetupitishia fedha ili tuanze kujenga hii barabara muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lolesia nikuhakikishie tu kwamba wakati wowote tunaweza tukaanza ujenzi wa barabara hii muhimu na kwa vile tutakuwa na *lot* mbili, *lot* moja itakuwa katika eneo lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini sasa aulize swalii lake.

Na. 441

Ujenzi wa Bandari Kavu Inyala

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Katika kukabiliana na ushindani na Bandari za nchi jirani, Mamkala za Usimamizi wa Bandari Tanzania ina mpango wa kuanzisha bandari kavu katika eneo la kimkakati la Inyala liliopo Wilaya ya Mbeya:-

- (a) Je, ni lini tathmini ya fidia kwa wananchi itakamilika?

(b) Je, ni lini ujenzi wa Bandari Kavu ya Inyala utaanza;

(c) Je, kuna mkakati wa ujenzi wa reli kuunganisha Bandari Kavu ya Inyala na Bandari ya Itungi (Kyela)?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kuitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*) ina mpango wa kujenga Bandari Kavu katika eneo la kimkakati la Inyara, Mbeya ili kuhudumia wateja wa Zambia, Malawi, DRC na wafanyabiashara wa Tanzania kutoka Nyanda za Juu Kusini ili kukabiliana na ushindani na bandari za nchi jirani. Katika bajeti ya mwaka 2019/2020 *TPA* imepanga kufanya upembusi yakinifu katika eneo lenye ukubwa wa ekari 100 ili kubaini mahitaji halisi na eneo linalofaa kwa ajili ya kujenga Bandari Kavu. Baada ya kukamilisha zoezi hilo, uthamini utafanyika na baada ya kukamilika taratibu za kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi huo zitaanza.

(b) Ili Bandari Kavu itakayojengwa ilete tija, mpango wa Serikali kuitia *TAZARA* ni kufanya upembusi yakinifu kwa lengo la kutandika reli kuelekea kwenye eneo itakapojengwa Bandari Kavu ya Inyala. Mpango huu unatarajiwani kuanza katika mwaka wa fedha 2020/21.

(c) Mkakati uliopo ni kuunganisha Bandari Kavu ya Inyala na Itungi iliyoko Kyela kwa reli ya *TAZARA* ili kuweza kuhudumia nchi jirani za DRC, Zimbabwe, Malawi na Zambia.

Hata hivyo, mkakati huu utaanza kutekelezwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kipande cha reli ya *TAZARA*.

NAIBU SPIKA: Oran Manase Njeza swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali lakini kwa umuhimu wa kipekee wa biashara ya bandari yetu na nchi jirani naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni bandari shindani na bandari yetu ya Dar es Salaam zimekuwa zikiongeza jitihada za kuhakikisha kuwa wanafikisha huduma kwenye maeneo ambayo yalikuwa ni miliki ya bandari yetu ya Dar es Salaam hada DRC Katanga, Zambia na Malawi. Kutokana na ushindani huo biashara yetu ya shehena kwenda maeneo hayo kwa Zambia imepungua mpaka asilimia 25 sasa hivi, na vilevile kwa DRC Katanga nako ni chini ya silimia 25; ni asilimia 21 kutoka asilimia 40. Sasa swali langu nauiliza, pamoja nakuboresha na ujenzi wa Bandari Kavu ya Inyala;

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga sasa barabara ya kutoka Mbalizi – Shigamba – Isongole ambayo inapitia katika eneo la Bonde la Songwe na kwenda mpakani na Malawi?

Ni lini itajenga reli ya *TAZARA* kutoka Tunduma kwenda Bandari za Ziwa Tanganyika kwa ajili ya biashara yetu na DRC Katanga? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Oran Njeza kwa jinsi ambavyo anafuatilia masuala ya kimkakati ya eneo lake. Ni kweli kwamba wananchi wa Mbeya Vijijini wamepata Mbunge jembe ambaye sidhani kama atakuwa na mpinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ametaka kujua mpango wa Serikali wa kuimarisha barabara ya kutoka Mbalizi – Shigamba kwenda Isongelo ambayo itaunganisha na Wilaya ya Illemani ukoje. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kwa mwaka ujao wa fedha tumeshatenga fedha kwa ajili ya kufanya upembezi yakinifu, kisha tutafanya na usanifu wa kina kwa ajili ya kuiimarisha barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Kwa sababu tunajua kwamba kujenga Bandari ya Inyala bila ya kuwa na barabara ambayo ni imara itakuwa haiwezi kusaidia, kwa hiyo tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajenga kipande hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye swali lake la pili anataka kujua kipande cha reli kitakachojengwa kutoka Tunduma hadi Bandari ya Kasanga Ziwa Tanganyika. Ni kweli kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania wanashirikiana na TAZARA kuhakikisha wanaweka miundombinu itakayokuwa wezeshi na rahisi kidogo kufikia Bandari ya Kasanga, Hivyo, kwa sasa wameshaanza upembuzi yakinifu wa kuhakikisha kwamba kipande cha reli kinatandikwa na watakapomaliza upembuzi yakinifu watafanya usanifu wa kina kupata gharama kwa ajili ya kupanga bajeti sasa ya kutekeleza mradi huo. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita sasa aulize swali lake.

Na. 442

Hitaji la Askari wa Kike Kituo cha Polisi Nkome

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA aliuliza:-

Kituo cha Polisi Nkome kina Askari wa kiume pekee hivyo hata huduma kwa akina Mama ikiwemo upekuzi hufanywa na Askari wa kiume:-

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka askari wa kike katika kituo hicho?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vidogo vya Polisi Nkome, Nyamboge, Kakubilo na Nzela ni vituo vilivyo katika maeneo ambayo yanakaribiana na kutokana na changamoto za mazingira magumu na ukosefu wa mazingira rafiki, vituo hivi kwa sasa havina Askari wa Kike ambao wanaishi na kufanya kazi. Hata hivyo, vituo hivi kupata doria maalum kila mara kutoka Kituo Kikuu cha Polisi Wilaya ya Geita ambapo Askari wa Kike na Kiume hufika na kutoa huduma za kiusalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo kuna mtuhumiwa wa kike amekamatwa katika vituo hivi vidogo hufanyika utaratibu wa kumpata mgambo wa kike wa eneo hilo au mwanamke ye yote mtu mzima mwenye busara anayepatikana kwa urahisi katika maeneo hayo kama ambavyo PGO 288 (8), (a) inavyo elekeza, ambapo hufanya upukuzi kwa mtuhumiwa huyo mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kuwa watuhumiwa wa kike hupekuliwa na Askari wa Kiume, Serikali itapeleka Askari wa Kike pindi mazingira ya utendeji kazi hususan makazi yatakapokuwa yameboreshwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Musukuma swalii la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza nisikitike sana kwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri hayaendani kabisa na maeneo ya Jimbo langu la Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri Waziri mhusika Mheshimiwa Kangi Lugola familia yake maana yake Mama yake na Dada zake wanaishi kwenye Jimbo langu, na Mheshimiwa Kangi Lugola mwenyewe ameishi kwenye Jimbo langu anayajua mazingira na majibu yaliyotolewa siyo sahihi. Kwa mfano, ukichukulia kituo cha Nyarugusu, Nyakagwe, Buziku, Bwanga na Chato Vijijini haya yote ni mazingira ambayo karibia tunafanana lakini wenzetu tayari wana Askari wa Kike. Sasa ninataka kujuwa ni lini Serikali itanipatia Askari wa Kike kwa kuwa majibu waliyotoa ni ya uwongo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, *Centre* ya Nkome ni *centre* ya tatu kwenye Mkao wetu wa Geita kwa ukubwa. Kituo kilichopo pale kinaongozwa na Inspekte na nimekjengia mimi kama Mbunge. Tatizo linaloonekana hapa kwamba hakuna makazi ya kuweza kumuweka Askari wa Kike, wajibu wa kujenga makazi bora ya askari ni ya Wizara.

Je, ni lini Serikali itachukua dharura ya kwenda kujenga hiyo nyumba anayotakiwa kukaa Askari wa Kike? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba taratibu hasa zinazohusu upekuzi ni lazima Askari wa Kike ampekuwe mtuhumiwa wa kike. Majibu mazuri kwenye swali la msingi ameyasema Naibu Waziri wangu, kwamba hata pale ambapo kunakuwa na changamoto ya kutokuwepo Askari wa Kike upo utaratibu ama wa kumtumia mgambo wa kike ama kumtumia Mke wa Askari ambaye yuko jirani na mahali ambapo kuna mtuhumiwa. Najua suala la Mheshimiwa

Musukuma nimeshamwagiza tayari Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Geita kupeleka Askari wa Kike kwenye Kituo cha Polisi cha Nkome. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wamekuwa wakiomba tuwapelekee Askari wa Kike kwenye vituo vya Polisi. Ninajua Waheshimiwa Wabunge Askari wa Kike wanapokuwa katika maeneo mbalimbali ni faraja kwa wananchi kwa sababu Askari wa Kike wao wanaruhusiwa hata kuwapekua watuhumiwa wa kiume. Kwa hiyo ninajua kwamba Mheshimiwa Musukuma anatarajia kuona Askari wa Kike katika maeneo mbalimbali ya vituo vya Polisi. Kwa hiyo nimpe faraja kwamba pale ambapo kuna changamoto kama hiyo na juzi tumepata Askari kutoka Chuo chetu cha Polisi Moshi, tutawapelekea Askari wa Kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof/ Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swalii la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini.

Na. 443

Kituo cha Polisi cha Lukumbule

MHE. DAIMU I. MPAKATE aliuliza:-

Kituo cha Polisi Lukumbule kiliungua moto miaka iliyopita na mpaka sasa kituo hicho hakina Askari kimefungwa:-

(a) Je, ni lini Serikali itakirejesha kituo hicho hasa ikizingatiwa kuwa kipo mpakani mwa nchi ya Msambiji?

(b) Je, ni lini Serikali itaweka kituo cha Uhamiaji katika kituo hicho cha Lukumbule?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Lukumbule ambacho kimeishia kwenye lenta baada ya Halmashauri kushindwa kumalizia ujenzi huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Daimu Idd Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Lukumbule kilichomwa moto mwaka 2013 na baadhi ya wananchi wasiotaka kutii sheria katika eneo hilo. Baada ya tukio hilo Jeshi la Polisi kwa kutambua kwamba eneo husika ni la mpakani na nchi ya Msambiji limekuwa likifanya doria za mara kwa mara na pia kushirikisha taasisi nyingine za Serikali ambazo ni wadau wa ulinzi na usalama katika kuimarishe hali ya ulinzi na usalama kwa wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kufungua Kituo cha Uhamiaji Kata ya Lukumbule upo kwenye hatua za mwisho na inatarajiwa kufanguliwa wakati wowote mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuupongeza uongozi wa Halmashauri ya Tunduru kwa ujenzi wa kituo cha Polisi cha Lukumbule ingawa bado ujenzi wake haujakamilika. Hata hivyo, Serikali inatambua umuhimu na uhitaji wa kituo cha Polisi katika eneo hilo. Aidha Serikali kuititia Jeshi la Polisi itafanya tathmini ili kubaini gharama halisi za kukamilisha sehemu ya ujenzi uliobakia na kuona uwezekano wa kukamilisha ujenzi huo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daimu Idd Mpakate swalii la nyongeza.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini chanzo cha kituo kile kuchomwa ni mgogoro wa ugomvi wa usalama barabarani kati ya Askari pamoja na bodaboda, hii ndiyo imekuwa tabia ya Askari wasiokuwa wa usalama barabarani kuwakamata bodaboda na kuwapiga bila kuwaeleza makosa yao.

Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na tabia hiyo ya Askari wasiokuwa wa usalama barabarani kuwakamata bodaboda na kuwapiga bila kuwaeleza makosa yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Jimbo la Tunduru Kusini limepakana na Msumbiji likiwa na Tarafa tatu. Tarafa ya Namasakata tangu imeundwa haijawahi kuwa na Kituo cha Polisi. Je, Serikali haioni haja sasa ya kupeleka Kituo cha Polisi Misechela na Namasakate yenye kwa kituo cha polisi ili kuwahudumia wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini na Tarafa ya Namasakata kwa ujumla.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hatuwezi kuhalalisha jambo lolote na vitendo vya uchomaji vituo vya Polisi, kwa hiyo hata kama kulikuwa kuna matatizo kati ya bodaboda iwe na Askari wa Usalama barabarani ama awe Askari yeoyote basi haihalalishi uchomaji wa kituo cha polisi, hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hoja yake kwamba kuna watu ambao siyo Askari wa Usalama Barabarani wanawapiga bodaboda. Niliwahi kujibu swalii hili siku chache zilizopita na nilieleza kwamba hatujapata taarifa ya kuona Askari Polisi wakipiga bodaboda na kama kuna taarifa hizo basi ni vema tukapatiwa ili tuzifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge amekiri kwamba wanaofanya hivyo siyo Askari wa

Usalama Barabarani, kwa sababu tunaamini askari wa usalama barabarani wamepata mafunzo na weledi wa kutosha katika kutekeleza majukumu yao, Askari wa aina nyingine yoyote ama watu wa aina nyingine yoyote ambao wanafanya vitendo kama hivyo kama wapo kauli ya Serikali ni kwamba ni kinyume na utaratibu hivyo watumie weledi katika kuhakikisha kwamba wanawakamata wanaovunja sheria ikiwemo hawa waendesa bodaboda.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu maeneo hayo mawili aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge ambapo anataka kujua ni lini tutajenga kituo cha polisi. Jibu ni kwamba katika maeneo yote nchini tutajenga kuanzia kwenye wilaya hata ngazi ya kata ikiwemo maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge pale ambapo hali ya kifedha itaruhusu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 444

**Kutokuwepo Kifaa cha Ambu Bag katika
Mkoa wa Katavi**

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Mkoa wa Katavi hauna kifaa cha kumsaidia kupumua mtoto aliye dhaifu (*ambubag*):-

Je, ni lini Serikali itawasaidia wananchi wa Mkoa wa Katavi kifaa hicho?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *ambu bag* na maski ni vifaa vinavyopatia hewa mtoto mchanga aliyezaliwa na tatizo la kushindwa kupumua na ni moja ya afua inayolenga kupunguza vifo vya watoto wachanga nchini. Serikali imeendelea na juhudzi zake za kuhakikisha siyo tu kuna watoa huduma wenye ujuzi, lakini pia dawa na vifaa tiba muhimu vinapati kana katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya hapa nchini. Kwa kipindi cha mwaka 2018, Serikali ilipokea na kusambaza vifaa mbalimbali vya kumsaidla mtoto mchanga mwenye matatizo ya kupumua ikiwemo *ambu bag* na maski 3,735. Vifaa hivyo vilipekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya 3,500 katika Halmashauri 109 za mikoa 16 ya Tanzania Bara. Usambazaji huo ulienda sambamba na mafunzo ya kuwajengea uwezo watoa huduma namna ya kutumia vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inategemea kupokea *ambu bag* na maski nyingine 2,500 ambazo zitasambazwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwenye mikoa ambayo haikupata mgao hapo awali. Utaratibu wa ugawaji wa vifaa hivyo umeandaliwa kuititia Bohari ya Dawa (*MSD*) ambapo Katavi imenorodheshwa katika mgao huo. Nizitake mamlaka husika kuagiza vifaa hivyo kutoka Bohari ya Dawa. Aidha, Bohari ya Dawa itaendelea kuvinunua vifaa hivyo ili vipatikane sambamba na vifaa vingine muhimu kwa ajili ya kuboresha huduma za afya ikiwemo afya ya watoto wachanga.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Taska Mbogo, swali la nyongeza.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa muda wa kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Mkoa wa Katavi unaongoza kwa vifo vyta watoto wachanga. Takwimu tu za mwaka 2018 zinaonesha kwamba Mkoa wa Katavi ulipoteza watoto wachanga 581. Hii ilisababishwa na ukosefu wa vifaa bora wakati akina mama wakijifungua lakini hata vifaa hivyo vikiwepo kwenye vituo hivyo vyta afya haviwezi kufanya kazi kwa sababu havina umeme. Je, Serikali kuitia Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Wilzara ya Afya ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba vituo vile vyta afya ambavyo havina umeme Mkoani Katavi vinapata umeme ili viweze kutumia vifaa vyta kisasa kuokoa vifo vyta mama na motto? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wauguzi wengi Mkoani Katavi hawana mafunzo, Serikali kuitia Wizara ya Afya ina mkakati gani wa kutafuta wadau wa afya ya mama na mtoto ili tuweze kutokomeza vifo hivi Mkoani Katavi? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya katika majibu ya swali lake la msingi. Pia niendeleee kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali kuhusu upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Mkoa wa Katavi baadhi ya vijiji havijaanza kufikiwa na mkandarasi. Nimpe taarifa tu Mheshimiwa Mbunge maeneo yote ambayo ameyauliza Mheshimiwa Mbunge mkandarasi ameshaanza kwenda *site*. Katika Mkoa wa Katavi kuna vijiji 149 vitapelekewa umeme. Sasa hivi mkandarasi ameshawasha Mchakamchaka lakini anaendelea na Kaparara na katika vijiji vingine saba atawasha kuanzia wiki inayokuja. Kwa hiyo,

wananchi wa Katavi wategemee kupata umeme katika maeneo yote. Kesho kutwa watawasha kwenye Mgodi wa Societykwa Mheshimiwa Kapufi. Kwa hiyo, mkandarasi yuko site vijiji vyote vitapatiwa umeme kwenye kipindi hiki cha Julai mpaka Desemba mwaka huu. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ambapo sehemu ya swali la kwanza ameshalijibu Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Niendelee na kipengele kingine ambacho kilikuwa kimebaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba idadi ya vifo vya watoto katika Mkoa wa Katavi ni vingi sana na hili ni kweli lakini halitokani na ukosefu wa huduma za afya kwa watoto wachanga. Mkoa wa Katavi una changamoto kubwa sana ya mimba za utotoni. Wastani wa Kitaifa sasa hivi tuna asilimia 27 ya watoto kati ya miaka 15 mpaka 19 aidha wana watoto au wana mimba. Katika mikoa ambayo inaongoza ndani ya nchi yetu ni pamoja na Katavi, umri wa kupata ujauzito bado ni mdogo sana na kwa kuwa bado hawajafikia ukomavu uliotosha, hili nalo linachangia sana katika vifo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na masuala ya mafunzo, Serikali inaendelea kujipanga na imekuwa inaweka utaratibu wa mafunzo endelevu kwa watoa huduma wake wa afya katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mafunzo kwa ajili ya huduma ya mama na motto. Katika Mkoa wa Katavi, Serikali imekuwa inashirikiana kwa karibu sana na wadau.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Ninja, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 445

Mkakati wa Kukarabati Kambi ya Wazee Fungafunga

MHE. DEVOTHA M. MINJA aliuliza:-

Wazee ni hazina ya Taifa lakini wapo wazee wasiojiweza ambao Serikali imewapa hifadhi katika kambi mbalimbali ikiwemo Kambi ya Fungafunga ya Mjini Morogoro. Hata hivyo, kambi hiyo ni chakavu kwa muda mrefu hali inayosababisha wazee kuendelea kuishi katika mazingira magumu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati kambi hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Ninja, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Morogoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa waliota wazee katika ujenzi wa Taifa hili. Aidha, wazee ni rasilimali muhimu katika ustawi na maendeleo ya nchi. Kwa kutambua hili, Serikali inatoa matunzo kwa wazee wasiojiweza katika kambi 17 nchini ikiwemo makazi ya Fungafunga Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha utoaji wa huduma katika makazi haya, Serikali imefanya tathmini ya hali ya utoaji wa huduma na miundombinu. Taarifa ya tathmini imebainishwa na kuainisha hali ya majengo na miundombinu katika makazi haya ikiwemo makazi ya

Fungafunga na imeweka mkakati wa kuboresha hali ya majengo na miundombinu kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inajali haki na ustawi wa wazee kama ilivyoainishwa katika llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 na itafanya ukarabati wa kambi hizi kwa awamu kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Devotha Ninja, swali la nyongeza.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza majibu ya Serikali na nilitarajia kwa kuwa Serikali hii inakusanya kodi basi ingetilia mkazo katika ujenzi wa nyumba hizi za wazee ambazo nyingi ni chakavu na nyingi zimegeuka kuwa magofu walau wazee hawa nao wajisikie kuwa ni sehemu katika Taifa hili. Swali la kwanza, je, ni upi mkakati thabiti wa Serikali kuhakikisha kuwa nyumba hizi za wazee zinakarabatiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Serikali imekuwa ikitoa maagizo kuwa wazee wote watapata huduma za matibabu bure lakini hali ilivyo hivi sasa wazee wengi hawapati matibabu kama inavyopaswa katika hospitali za Serikali na hata katika vituo vyta afya. Je, ni lini Serikali italeta sheria hapa Bungeni ambayo itasimamia matibabu na maslahi ya wazee hao? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Devotha Ninja kwa maswali yake mazuri na kwa kufuatilia kwa karibu masuala ya wazee hususan katika kambi hii ya Fungafunga pale Morogoro. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi na naomba nitoe maelezo ya awali kwamba Serikali tuna kambi 17 za kuhudumia wazee. Hata hivyo, kwa mujibu wa sera yetu Serikali inachukua wazee pale inapoonekana yule mzee hana watoto wa kumtunza, ndugu na watu katika jamii ambaao wanaweza wakamtunza. Mpaka sasa hivi tuna wazee takribani 500 ambaao tunawahudumia sisi kama Serikali ambapo katika vigezo hivyo vitatu ambavyo nimevisema pale awali wametimiza na ndio maana tunawachukua na sisi kama Serikali tunawatunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa hii miundombinu ya vituo vyetu 17 umeshaanza na vituo ambavyo tumeshavifanya ukarabati ni pamoja na Bukumbi, Mwanzage na Magugu. Aidha, tumejenga tena nyumba mpya pale Kolandoto na tumefanya ukarabati wa bweni pale Kilima. Ndiyo maana nasema tunakwenda awamu kwa awamu kuhakikisha kwamba hizi kambi zote tunaweza kuzifikia na kuzifanya ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na matibabu kwa wazee, Serikali ilitoa agizo kwamba wazee wote ambaao wamefika umri wa zaidi ya miaka 60 wapate vitambulisho ili waweze kupata matibabu bure. Kumekuwa na changamoto kidogo ya kusuasua katika utekelezaji kwenye baadhi ya Halmashauri kutoa vitambulisho. Nitumie fursa hii kuzikumbusha Halmashauri kuzingatia agizo hili la Serikali la kutoa vitambulisho kwa wazee ambaao wamefika miaka 60 na vilevile kutenga madirisha mahsusini kwa ajili ya wazee.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhu ya kudumu ya jambo hili ni hili jambo ambalo tunataka kulifanya kama Serikali kuhakikisha kwamba kila mtu anaingia katika mfumo wa Bima ya Afya ya Wote. Mwezi Septemba tunataka tulete Muswada ambapo utaratibu wa kuwa na bima utawekwa ili kuhakikisha wanapata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tunatambua kwamba kuna magonjwa mahsusini ya wazee

na sisi wataalam tuna kitu kinaitwa *geriatric medicine*. Ndani ya Wizara, tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba haya magonjwa ambayo ni mahsus kwa wazee nayo tunayawekea utaratibu ili wazee waweze kupata matibabu kulingana na magonjwa walijonayo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumalizie Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, sasa aulize swalii lake.

Na. 446

Ujenzi wa Mabwawa ya Umwagiliaji

MHE. MARWA R. CHACHA aliuliza:-

Mabwawa ya Mesaga, Nyamitita na Bugerera katika Wilaya ya Serengeti yalikuwa kwenye mchakato wa kujengwa kwa ajili ya umwagiliaji:-

Je, mchakato umefikia wapi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Jimbo la Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umwagiliaji Mesaga ulisanifiwa mwaka 2004 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na miundombinu ya shambani. Hata hivyo, fedha za ujenzi zilianza kupatikana mwaka 2014 na 2015 ambapo mradi ulipokea shilingi milioni 200 na shilingi milioni 198 mtawalia. Fedha hizo kwa pamoja zilitumika kuanza ujenzi wa utoro wa maji (*spill way*) kwa kuwa hazikutosha kuanza ujenzi wa tuta la bwawa na ujenzi wa mifereji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto ya fidia katika eneo hilo, Serikali imetoe maelekezo kwa uongozi wa wilaya kutatua mgogoro wa fidia kwa kupitia na kuhuisha gharama za mradi huo ili ziendane na wakati. Aidha, Serikali itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kuandaa andiko jipya la mradi kwa ajili ya kutafuta fedha za kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Nyamitita ulitekelezwa mwaka 2013 na unahusisha banio na mifereji ya umwagiliaji. Mradi huo unafanya kazi ingawa haujakamilika kutokana na ufinyu wa bajeti ambapo katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 217 ili kuendeleza ujenzi wa mradi huo na hivyo kuwanufaisha wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umwagiliaji Bugerera unahusisha bwawa dogo la miundombinu inayoweza kumwagilia hekta 5 tu. Mwaka 2010, Serikali ilifanya upimaji na usanifu kwa ajili ya kuongeza ukubwa wa bwawa na kuongeza shamba la umwagiliaji hadi kufikia hekta 80. Aidha, Serikali itaendelea kutafuta fedha ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha mabwawa ya Mesaga, Nyamitita na Bugerera yanajengwa na kuwanufaisha wananchi wa Serengeti na Taifa kwa ujumla.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, swali la nyongeza.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Bwawa la Mesaga liko Kata ya Kenyamonta na ni kata ambayo inaongoza kwa kuwa na watu wengi katika Wilaya ya Serengeti. Bwawa hili lilianza kutengewa fedha ama kutolewa fedha 2014/2015. Tumeona zimeenda shilingi milioni 200 na zikaenda tena shilingi milioni 198, ni fedha nyangi. Hata hivyo, ukiangalia majibu ya Serikali wanasema sijui kuna fidia na ni kama walipeleka waka-dump zile hela wamezitelekeza mpaka leo. Mimi nilitaka kujua, Serikali mlipeleka fedha kwenye eneo lenye mgogoro ambalo halina andiko mradi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nashukuru kwamba Wizara imetenga fedha shilingi milioni 217 kwa ajili ya Bwawa la umwagiliaji la Nyamitita, niombe fedha hizi zitoke. Niseme kwamba pamoja na fedha hizi kutengwa, kumekuwa na *tendency* ya fedha kutokutoka. Naomba fedha hizi zitoke pamoja na za Bwawa la Mesaga, wananchi wanataka kujua ni lini fedha za Bwawa la Mesaga zitatoka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chacha Ryoba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anataka kujua kama eneo hilo lina mgogoro kwa nini Serikali ilipeleka fedha? Eneo lile wakati lilifanyika andiko na hitaji la kujengwa mradi ule hakukuwa na mgogoro na hii ni baada ya kupata taarifa ya kimaandishi kutoka kwa wakulima na viongozi wa Wilaya kwamba wakulima wamekubali eneo lile liendelezwe kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, shida kubwa iliyoko pale na Mheshimiwa Mbunge anajua kwa sababu nimeshafika pale ni kwamba wale wakulima ambapo lile bwawa linajengwa, wale wa sehemu ya juu baada ya hela kupelekwa wanataka wafidiwe na wakulima wenzao waliokuwa upande wa chini. Mgogoro ulioko pale ni wale wakulima wa chini hawataki kuwamegea ardhi wale wakulima wenzao waliopisha bwawa lile kujengwa. Baada ya hali hiyo kutokea na hela tulishapeleka ndiyo maana kama Serikali tumewaelekeza kwanza wakulima wenye wakae na uongozi wa wilaya watatue mgogoro huo. Baada ya utatuzi huo kukamilika na tukipata taarifa kwamba hakuna mgogoro basi hatua zingine za kupeleka fedha zitaweza kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anataka kujua lini sasa Serikali tutapeleka fedha kwenye Bwawa hilo

la Mesaga. Kama nilivyojibu kwenye maelezo yangu ya awali, kutokana na mwongozo tuliokuwa nao sasa hivi wa kuendeleza miradi yote ya umwagilajji, lazima tupate *commitment letter* kutoka kwa wanufaika wenyewe kwamba eneo linalojengwa mradi halina matatizo na wamekubaliana ili tusjepeleka fedha halafu kumbe kuna mgogoro. Kama tunavyofahamu tulipitisha wenyewe sheria hapa, ardhi yoyote haiwezi kutwaliwa bila kwanza kulipwa fidia. Kwa hiyo, wale wanaopisha eneo la ujenzi ule wa bwawa lazima kwanza wafidiwe na wenzao kule eneo la chini na baada ya mgogoro huo tutapeleka fedha.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu wa maswali, nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo siku ya leo, tutaanza na matangazo ya wageni waliotufikia Bungeni.

Kwanza ni wageni 70 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), ambao ni walimu 10 na Wanafunzi 60 kutoka Shule ya Msingi Kikuyu ya Jijini Dodoma, wakiongozwa na Ndg. Dina Mdasha. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 65 wa Mheshimiwa Selemani Jafo, ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Wabunge wote walisoma Shule ya Sekondari Sengerema ambao ni wanafunzi wa zamani wa shule hiyo (*ALUMNAE*). Wakiongozwa na Mwalimu Mkuu wa sasa wa shule hiyo Mwalimu Zacharia Lutambi. Karibuni sana wanafuzi wa zamani wa Shule ya Sekondari Sengerema. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, ambaye ni Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Masiliano kutoka Ushetu Mkoa wa Shinyanga ambao ni watoto wake. Ndg. Ivan Richard, Ndg. Victoria Thadei na Ndg. Julieth Kwandikwa. Karibuni sana watoto wa Mheshimiwa Kwandikwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, ambaye ni Naibu

Waziri wa Maliasili na Utalii. Ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha St. Johns kilichopo Mkoani Dodoma wakiongozwa na Ndg. Nyigana Nyigana. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa Almas Maige ambaao ni wadau wa Lugha ya Kiswahili Tanzania, wakiongozwa na Ndg. Victor Eliah. Karibuni sana wadau wa Kiswahili. (*Makof*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambaao ni Waandishi wa Habari wa Dar Mpya TV kutoka Jijini Dar es Salaam na hawa ni Ndg. Brighton Masalu na pia Ndg. Ezekiel Msese. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 31 wa Mheshimiwa Vedasto Ngombale ambaao ni wakulima 25 wa alizeti kutoka mikoa ya Lindi na Mtwara wakiongozwa na Ndg. John Julius. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni wengine wa Mheshimiwa Ngombale ambaao ni wakulima sita wa *Aga Khan Foundation* wakiongozwa na Ndg. Steven Tumaini. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Mary Chatanda ambaao ni wajasiriamali kutoka Korogwe Mjini wakiongozwa na Ndg. Mage Gabriel. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 17 wa Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ambaao ni kinamama wajasiriamli kutoka Nzega Mjini wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Kata ya Nzega Magharibi, Ndg. Modesta Malema. Karibuni sana kinamama wajasiriamli, naona hawa wako wamejipanga zaidi, wamekuja na sare kabisa, karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Neema Mgaya, ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndg. Hans Chirare. Karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni tuliona nao na wageni wote mnakaribishwa Bungeni.

Lipo tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, anawatangazia Wabunge wote wa Kamati hii ya Kudumu ya Bunge kwamba saa saba kamili mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge mnatakiwa kwenda kwenye kikao bila kukosa kwa ajili ya kujadili na kuchambua Muswada Na. 3, Mwaka 2019. Mwenyekiti anawasihi sana msikose kwenda lakini pia muwahi kufika kwenye chumba chenu cha mikutano.

Waheshimiwa Wabunge lipo pia tangazo kutoka kwa Meneja wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Kadutu, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote matangazo ya michezo iliyochezwa mwishoni wa juma kama ifuatavyo:-

Siku ya Jumamosi tarehe 22 Juni, 2019 lilifanyika Bonza liliodhaminiwa na Benki ya *NMB* na matokeo ya michezo mbalimbali yalikuwa kama ifuatavyo:-

Kuvuta kamba, maarufu kama Simika, wanaume walikuwa washindi wa kwanza, kwa hiyo, *Bunge Sports Club* ilishinda. (*Makofii*)

Pia kuvuta kamba upande wa wanawake, Bunge pia iliibuka kidedea, kwa hivyo, wavuta kamba upande wa *Bunge Sports Club* walishinda kwa upande wa wanaume na wanawake. (*Makofii*)

Pia mpira wa wavyu (*volleyball*), *Bunge Sports Club* waliwashinda NMB kwa seti mbili kwa sifuri. (*Makofii*)

Mpira wa kikapo (*Basketball*) NMB waliwashinda *Bunge Sports Club* kwa magori 53 kwa 52. Hili moja hili nadhani walikatisha kabla ya muda wangekuwa *Bunge Sports Club* wameshinda pia. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge mpira wa pete (*Netball*) *Bunge Queens* waliwafungwa watunza fedha *NMB* magori 26 kwa 18. (*Makofii*)

Pia mpira wa miguu (*Football*) *Ndugai Boys* waliwasambaratisha *NMB* magori manne kwa mawili. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge magori haya yalipatikana kipindi cha *penalty* baada ya kutoka suluhu kwenye dakika 90 za mchezo kwa kufungana gori moja moja.

Pia siku ya Jumapili 23 Juni, 2019 kulikuwa na michezo ya *netball* kati ya *Bunge Queens* na *Combine* ya wanamichezo kutoka Zanzibar, Dar na Dodoma (*MUWAFAKI*), pamoja na mchanganyiko huo bado *Bunge Queens* waliibuka kidedea kwa magori 26 kwa 13. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge mnajulishwa kwamba Mgeni Rasmi kwenye Bonanza hilo alikuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Kadutu anawashukuru sana na anawapongeza sana Wadhamini wa Bonanza la Jumamosi yaani Benki ya *NMB* kwa kufanikisha kwa kiwango kikubwa michezo hiyo, lakini pia anawashukuru Wabunge wote kwa kushiriki na wananchi wote kwa ujumla. (*Makof*)

Tangazo lingine litatoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kuhudhuria sherehe ya ufunguzi wa Tawi jipya la Benki ya Biashara ya *TIB* (*Tanzania Investment Bank*), naambiwa hiki kinachofunguliwa hapa inaitwa *TIB Corporate Bank Limited*, ambayo imekamilisha ujenzi wa tawi na ofisi ndogo ya benki hiyo kwenye jengo la *PSSF* hapa Dodoma. Kwa hiyo, Wabunge wote mnakaribishwa kushiriki kwenye sherehe hizo ambazo zitafanya siku ya leo tarehe 24 Juni, 2019 kwenye viwanja vya jengo hilo lilitopo barabara ya Jakaya Kikwete. Sherehe hizo zitaanza saa saba mchana, ambapo Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge wote mnakaribishwa, lakini katika mwaliko huu wale amabo wanahuksika na

Kamati ya Katiba na Sheria, wao wanashauriwa kuelekea kwenye kamati yao wakati Wabunge wengine tukienda kuhudhuria sherehe hizo za ufunguzi.

Baada ya matangazo hayo Waheshimiwa Wabunge tutaaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mwongozo wa Spika.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mwongozo wa Spika.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haonga!

MHE.PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na nikiwa naamini kabisa wewe ni mwanamichezo na hivyo naamini kabisa suala hili utalismia vizuri liwezen kwenda vizuri. Jana kulikuwa na mechii kati ya *Taifa Stars* pamoja na *Senegal*/na *Taifa Stars* ilifungwa magori mawili kwa sifuri. Hali hii kwa kweli, watanzania walio wengi hasa wanaopenda soka na wanamichezo mbalimbali, kwa kweli wamelala na maumivu makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tetesi ambazo zinaendelea, ambazo zinazungumzwa kwenye mitando ya kijamii na maeneo mbalimbali kwamba Serikali ilisema ingeweza kuwapatia *Taifa Stars* dola 300 kwa siku wakiwa kule Misri. Hata hivyo, habari zilizopo ni kwamba wamepewa kama dola 70 tu, hivyo inaonekana kwamba hawajalipwa sehemu kubwa ya fedha zao ambazo zinatakiwa walipwe kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini wote kwamba, unapoingia kwenye michezo, ili uweze kucheza vizuri lazima uwe na morali nzuri, uwe na *mood* ya kuweza kucheza michezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na hali hii ya kutopewa fedha zao ilipelekea siku moja wachezaji wa *Taifa Stars* kutofanya mazoezi kule Misri. Kwa hiyo, mgomo wa chini chini ni kama unaendelea hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba utusaidie kutuongoza vizuri hapa, kwa nini Serikali haiwapatii fedha zao wale wachezaji wetu ambao wako kule, wachezaji wa timu ya Taifa, badala ya kuwapa dola 300 wanapewa dola 70 kwa siku. Kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwenye hili jambo, hili jambo linakubalika kwa wachezaji wetu kuendelea kuishi kwenye wasiwasi na hali ya kutokuwa vizuri kimchezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu michezo inaendelea kule, kwa hiyo, ili suala hili liweze kwenda vizuri, naomba sasa Serikali iweze kusimama na kuweza kuangalia namna gani ya kuweza kutoa fedha kwa wale wachezaji wetu kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini utatuongoza vizuri katika hili. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe!

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi ili nipate mwongozo wa kiti chako. Siku za karibuni kumekuwa na tabia ambayo inafanywa na magazeti, hasa zaidi magazeti yanayotumika kwa *propaganda* au jambo lingine na niyataje tu, *Gazeti la Tanzanite*, Jamvi la Habari na baadhi ya *Social Media*. Sasa hivi wamekingia mpaka kwenye mhimili wako. Wamekuwa wakiwachafua sana Wabunge pale panapotokea jambo zito ambalo liko mbele, ambalo ni suala la kutifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, magazeti haya siku za karibuni yameandika majina ya Wabunge, wakiwataja kwamba wameshiriki kwenye rushwa ili kufanya baadhi ya

mambo na ni moja kwa moja wanaugusa muhimili, wanagusa kiti chako. Tumeona wameongea kuhusu masuala ya AZAKI, sheria inayotaka sasa kujadiliwa kwamba kuna Wabunge wamepokea rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba kiti chako, kwamba kwa nini isione sasa ni wakati kuwaita wahariri wa magazeti haya mbele ya Kamati ya Maadili ikiwezekana, ili waweze kueleza kinagaubaga hizo rushwa zinazotajwa. Kwa sababu tunatambua kuna baadhi ya magazeti sasa hivi wana kesi mbalimbali ambazo ziko mahakamani, kama mtakumbuka gazeti la *Tanzanite* limeshitakiwa na Mheshimiwa Benard Membe na hii kesi inaendelea huko kwenye mahakama ya kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini na sisi Bunge tusiamue kuchukua hatua dhidi ya hivi vyombo kwa sababu wanaweza kuchafua amani yetu lakini pia wanaudhalilisha muhimili wako, wanataka kuonesha huu muhimili ni dhaifu sana, jambo ambalo siyo sahihi. Kwa hiyo, tuombe kiti chako kitoe maelezo kutokana na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Haonga, akieleza kuhusu jambo lilitotokea jana nchini Misri, kwa upande wa *Taifa Stars* kufungwa na Senegal, ametoa maelezo marefu, akihusisha jambo hilo na pengine kutokupewa fedha kama ambavyo ahadi zimetolewa.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68(7) inataka kiti kitoe mwongozo kwa jambo lilitotokea Bungeni mapema, jambo hili halijatokea hapa Bungeni. Kwa hiyo, utaratibu unaotakiwa kutumika ni ule ambao hautakiwi kuombwa Mwogozo Kiti. Kwa hiyo, kwenye jambo hili kiti hakina mwongozo wowote.

Waheshimiwa Wabunge, pia nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Cecil Mwambe akitoa maelezo marefu kuhusu magazeti ya *Tanzanite* na Jamvi la Habari kwamba haya ni magazeti ya *propaganda* na hivi karibuni yamekuwa yakinjua majina ya Wabunge yakiwahusisha na kuchukua rushwa ama kufanya mambo yasiyopendeza na Mheshimiwa Cecil Mwambe yeze ametoa mapendekezo kwamba pengine magazeti haya wahariri wake wangeitwa kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ili waweze kujeleza ama kuleta ushahidi wa jambo hili ambalo huwa wanaandika na uzuri ameshatoa na yeze mfano kwamba haya magazeti kwa mambo ambayo wameshawahi kuandika huko nyuma wako mahakamani.

Waheshimiwa Wabunge hata jambo hili pia halijatokea hapa Bungeni, lakini hata hivyo Waheshimiwa Wabunge, gazeti linapomwandika Mbunge yeote, sheria inamruhusu yeze ambaye anaona gazeti limemkosea heshima ama limemkosea adabu ama limesema jambo ambalo si la kweli, kama ambavyo tunafahamu magazeti hushitakiwa, anapaswa kwenda mahakamani kwa sababu kule wanavyo vyombo wa kuweza kuchunguza na wao watapata fursa ya kutoa ushahidi kuhusu mambo haya. Wote tunafahamu ile Kamati yetu ya Maadili, inayo mambo ambayo ina nguvu nayo kushughulika nayo na inayo mambo ambayo ni kazi ya mahakama.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote ambao huwa wanatajwa ama magazeti haya yanawakosea heshima wanashauriwa kwenda mahakamani. Kwa maana hiyo, kwenye jambo hili pia mwongozo haupo kwa sababu halijatokea hapa Bungeni, lakini Wabunge ambao wanaguswa na magazeti haya wanashauriwa kwenda mahakamani.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu!

NDG.YONA KIRUMBI-KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge majadiliano yanaendelea, nimeshaletewa majina hapa kwa mujibu wa uwiano wetu kivyama humu ndani. Tutaanza na Mheshimiwa Leah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi ajiandae.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuwa mchangiaji wa kwanza katika siku hii ya leo. Moja kwa moja nikiunga mkono hotuba ya bajeti kuu ya Serikali iliyowasilishwa, nikikubaliana na mapunguzo ya tozo yaliyofanyika na mabadiliko ya kanuni mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono kufutwa kwa kodi ya ongezeko la thamani katika taulo zinazotumiwa na wanawake. Ninaunga mkono kwa sababu, kupungua kwa kodi hii wote tuliona hakukuwa na mabadiliko yoyote katika bei na Serikali ilieleza kwamba, kuondolewa kwa kodi ya ongezeko la thamani, lakini gharama ya uzalishaji iliendelea kuwa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya uzalishaji imeendelea kuwa juu kwa sababu, pamba nyingi tunayozalisha, asilimia 70 ya pamba tunayozalisha Tanzania inaenda nje na asilimia 30 tu ndiyo inayobaki kutumiwa katika nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wale wanaozalisha nchini, ile pamba inakwenda kutengenezwa kwanza kule nje ya nchi na kurudi Tanzania ili iweze kuzalisha pedi, kwa hiyo, moja kwa moja gharama za uzalishaji inakuwa iko juu. Kwa hiyo, ninaunga mkono kufutwa kwa kodi ya ongezeko la thamani katika tauo za kike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya kupunguza kiwango cha kodi ya mapato ya makampuni kutoka asilimia 30 hadi 25 kwa wawekezaji wapya wa kuzalisha tauo za kike. Ninaunga mkono kwa sababu gani, kutawezesha kuvutia wawekezaji, kutaongeza ajira, kutaongeza mapato na hata asilimia kubwa ya pamba yetu tunayozalisha itatumika nchini, pamba yetu itakayotumika nchini, gharama ya uzalishaji itakuwa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema, Mkoa wa Simiyu mapema mwaka 2017, tulipitisha mpango wa uwekezaji katika mkoa. Moja ya uwekezaji ilikuwa nikuwekeza kiwanda cha kuzalisha vifaatiba, vikiwemo *drip* za maji, pamoja na tauo za kike.

Mheshimiwa Naibu Spika,kwa nini Mkoa wa Simiyu, ni kwa sababu tunauhakika wa maji ya kutoka Ziwa Victoria, tuna uhakika wa pamba, kwa sababu asilimia 60 ya pamba inayozalishwa Tanzania inatokea Mkoa wa Simiyu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa kiwanda katika Mkoa wa Simiyu, pamba itazalishwa kwa gharama ndogo kwa sababu pamba hiyo inatokea mkoa huohuo, na nina uhakika kiwanda kitakapotengenezwa kitamudu soko la nchi nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili pia limekuwa likiungwa mkono na Makamu wa Rais, kwamba Simiyu sasa tuanzishe kiwanda cha uzalishaji wa tauo za kike. Ninavyooingea, Mfuko wa Wafanyakazi umeonesha nia ya kujenga kiwanda katika Mkoa wa Simiyu, Mfuko wa Bima ya Afya umeonesha nia ya kuwekeza kiwanda. Ninachoomba ni *commitment* ya Serikali; kwamba watakapokuja kujibu

watupe uhakika ni lini sasa kiwanda hicho kitajengwa ili tuweze kumpnguzia mzigo mwanamke katika bei itokanayo na ununuzi wa taulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pia kwa kuunga mkono Serikali; moja ya kipaumbele katika kuandaa mpango ilikuwa imezingatia umuhimu wa kumaliza miradi inayoendelea ili kupata matarajio tarajiwa. Vilevile naunga mapendekezo ya kurekebisha Kanuni ya 23 ya Kanuni za Sheria za Bajeti ya Mwaka 2015 ambayo inampa mamlaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuongeza muda wa kukamilisha miradi hiyo. Mwanzo fedha ilikuwa ikibaki mwisho wa mwaka anapewa miezi mitatu tu ili fedha hizo zimalizwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono si tu kwa ajili ya kuwepo fedha za kulipa walipaji ambao wanadal hati za madai, lakini hii pia itasaidia katika halmashauri za mitaa kupunguza matumizi mabaya yaliyokuwa yalifanyika kwa fedha iliyobaki. Fedha nyingi sana zimekuwa zikibaki katika Halmashauri. Kwa mfano, fedha iliyopokelewa 2017/2018 katika halmashauri 176, bilioni 783 iliyotumika ni milioni 521 tu; kwa hiyo asilimia 33 ilibaki mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri nyingi zimekuwa zikifukuzana kumaliza fedha mwisho wa mwaka na si kukamilisha miradi kwa ubora. Kwa kumuongezesa muda Mlipaji wa Serikali fedha hizi zitatumika kama zilivyotarajiwa. Naomba kukiri kwamba Waheshimiwa Madiwani walikuwa wakihoji kuhusu matumizi ya fedha wanaambwiwa wakubaliane kwa sababu tusipokubali fedha zitarudi Serikalini; na pale kulikuwa kuna mianya ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Nikiri kwamba Serikali imeona kuongeza muda kwa sababu fedha nyingi zinaletwa mwisho wa mwaka. Kwa kuwa tunatekeleza *cash budget* naomba basi kuwe na *time frame* ya mwisho wa fedha ziletwe angalau mwanzoni mwa mwezi wa sita ili fedha nyingi zisiendelee kubaki maana yake badala yake miradi inatekelezwa kwa ubovu, ubovu, ubovu, ubovu kwa sababu ya kukimbizana kumaliza fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichangie kuhusu mapato yanayokusanya na halmashauri zetu nikiweza kulinganisha na mchanganuo wa matumizi namna jinsi ulivyo ili sasa tuone wapi tunatakiwa tufanye ili ule mgawanyiko uweze kuleta manufaa kama yalivyokusudiwa. Mapato ya halmashauri ambayo ni asilimia 100 mgawanyiko wake bado unaleta uzito katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, asilimia 40 inakwenda kwenye miradi ya maendeleo, asilimia 10 inakwenda kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ile asilimia 50 inayobaki matumizi yake mengine, fedha zake ni mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*), wengine mamlakaa ya maji, kuna likizo na matibabu ya Watumishi, kuna uendeshaji wa Ofisi ya Mkurugenzi. Nasema hivyo kwa sababu gani? natafuta pale kuhusu Mheshimiwa Diwani fungu lake pale liko wapi? kwa kuwa fedha nyngi ziko *allocated* kwa matumizi mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatutaona haja ya kuwasaidia Waheshimiwa Madiwani waletewe angalau posho ile ya madaraka ya mwezi walipwe na Serikali Kuu utekelezaji wa fedha za miradi ya maendeleo hautafanyika, asilimia 10 ya wanawake haitapelekwa, kwa sababu ni vigumu sana utetee asilimia 10 ipelekwe halafu fedha za miradi ya maendeleo ikafanyike wakati wewe Mheshimiwa Diwani maslahi yako hayajalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja nikisema sasa Wizara ya Fedha anTAMISEMI wakae wapiti ile asilimia 10 mgawanyiko wa matumizi yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Mgaya atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, Mheshimiwa Charles Kitwanga ajiandae.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Haki za Bunge

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba.

KUHUSU HAKI ZA BUNGE

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 51(4) inayohusu masuala yanayohusu Haki za Bunge, nitaisoma kwa faida ya wote Kanuni hii, inasema:-

51.- (40) Mambo yanayohusu haki za Bunge yatawasilishwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa katika Kanuni hihi na endapo wakati wa Kikao chochote cha Bunge jambo lolote litazuka ghafla ambalo litaonekana linahusu haki za Bunge, shughuli zitasitishwa kwa madhumuni ya kuliwezesha jambo hili kuwasilishwa na kuamuliwa isipokuwa tu kama wakati huo kura inapigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwambe ameeleza jambo kubwa sana ambalo linahusiana na Bunge lako la Wabunge wako kupewa rushwa ili kuweza ku-lobby ili mabadiliko ya Sheria Ndogo yaliyoletwa katika Bunge lako tukufu ziweze kupitishwa kwa namna ambayo Wabunge hao wanaona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Bunge lako liliita Wabunge wachache takribani 40 ili kupewa uelewa wa namna sheria zinazoletwa kwa hati ya dharura zinataka nini, ila kilichotokea na alichokieleza Mheshimiwa Mwambe ndicho kimenishtua zaidi kwa sababu kwenye vyombo vyahabari na magazeti mbalimbali ilionekana Wabunge wale wamepewa rushwa ili kushinikiza kupitishwa kwa sheria hizo. Jambo hili ni aibu kubwa na magazeti aliyoyataja Mheshimiwa Mwambe nimepitia kwa haraka yametaja na *social media* zinazungusha habari kwamba Wabunge wako wamepewa pesa ili kupitisha Miswada hiyo.

Sasa jambo hili limekuwa kutokea mara kwa mara Bunge lako kujaribiwa, naomba busara ya Kiti chako iweze kuwajibisha kupitia Kamati yetu ya Maadili hawa Waandishi wa Habari na Magazeti haya walete uthibitisho wa namna gani Wabunge wako walioheshimiwa na kupewa ridhaa ya kusimamia mambo ya kisheria wamepewa rushwa na namna gani wana-lobby na kushinikiza kupitishwa kwa miswada hii ili hii iwe fundisho kwa magazeti mengine yote ambayo yanatumia nafasi yao vibaya kulidhalilisha Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nitoe hoja ili shughuli za Bunge zisitishwe tuweze kujadili suala hili. naomba mniunge mkono Waheshimiwa Wabunge wenzangu.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, naomba mkae.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Salome Makamba kwa mujibu wa Kanuni ya 51(4) akitoa maelezo ambayo sikusudii kuyerejea ambayo kwa mujibu wa maelezo yake yanaashiria kwamba kuna Haki za Bunge ambazo jambo hili limezuka ghafla hapa na ndiyo maana maneno ghafla yametumika hapo na kwamba Mheshimiwa Salome angependa kutoa hoja ili Bunge hili liahirishe shughuli hi tunayoifanya ili tuweze kujadili hilo jambo ambalo amelieleza.

Katika maelezo yake Mheshimiwa Salome Makamba anasema siku ya jana Bunge liliita semina ama liliita Wabunge wachache takribani 40 kwa ajili ya kupewa uelewa kuhusu muswada huu wa sheria ambao unakusudia kuleta mabadiliko mbalimbali katika sheria mbalimbali.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nianze kwa habari ya kuonesha kana kwamba hili jambo; amelihuisha pia na jambo alilolisema Mheshimiwa Mwambe la kuhusu magazeti kuandika kuhusu Wabunge kupewa rushwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nianze la kwake yeye akiacha hilo la kuhisisha na alilolisema Mheshimiwa Mwambe, kuhusu Bunge kuwaita Wabunge jana ili kupewa uelewa.

Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Bunge haina taarifa hiyo, hakuna taarifa hiyo ya kwamba kuna barua mahali kwa sababu lazima mfahamu namna Kamati za Bunge zinavyofanyakazi zinafanyakazi kwa maandishi. Hakuna mtu anaruhusisha kuitisha semina labda njie ya hapa na pia awe hajaihusisha ofisi wala haongei mambo ya ofisi. Ukiitisha watu huko kwingine huo ni mukutanoo siyo unaohusu Bunge, kwa hiyo hivyo hivyo kwa kuwa hakuna kibali cha Spika cha kuitisha mukutano uliofanyika jana na mimi nasamikia yeye na ofisi mimi ndiyo niko hapa sasa hatuna hiyo taarifa ya kuita mtu ye yote kuja kutoa uelewa kuhusu muswada huu. Kwa hiyo, kikao hicho kama kilikuwepo ama ilikuwa vipi, chochote kilichoendelea huko ofisi haina taarifa na mukutano huo.

La pili kuhusu Wabunge kutajwa na magazeti mbalimbali na kwa namna moja ama nyngine kuileta hoja hiyo kana kwamba ni ya Bunge zima sasa, kwa hiyo ni haki za Bunge hili, hapana. Sheria tumetunga sisi wenyewe kama Bunge ya kutoa fursa kwa Mbunge ye yote anayeona chombo cha habari kinamsema kwa namna ya kumshushia hadhi, ama kwa namna ya kumdhalilisha, ama kwa namna ambayo chombo cha habari kimechapisha habari ambazo si za kweli kuhusu Mbunge huyo anapaswa kwenda Mahakmani; ndicho chombo kilichopewa mamlaka na sheria tulizotunga sisi ili aweze kupata haki yake huko.

Kwa hiyo yote hayo mawili Waheshimiwa Wabunge nimeyatolea maelezo na maelezo ndiyo hayo. Hakuna haki yoyote ya Bunge katika matukio yote haya mawili ambayo inaweza kutusababisha tuache kufanya shughuli za Bunge halafu tujadili hayo.

Mheshimiwa Neema Mgaya.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ya kuweza kusimama ndani ya Bunge hili Tukufu na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wka kazi kubwa anayoifanya ya kutekeleza miradi mikubwa ambayo itakuja kuleta tija na kujenga uchumi endelevu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara hii ya Fedha kwa kuona umuhimu wa kutumia malighafi za kilimo, mifugo, uvuvi, madini katika kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa ajili ya soko la ndani ya nchi yetu na ziada kwa ajili soko la nje na vilevile na kuongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, dira yetu ni ya kujenga nchi ya viwanda; ni vyema basi tukajenga viwanda ambavyo vitatumia malighafi inayopatikana ndani ya nchi yetu kama hizo malighafi za kilimo, mifugo, uvuvi, madini n.k.

Mheshimiwa naibu Spika, nchi yetu imejaaliwa sana kuwa na malighafi hizi ndani ya maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Ukiangalia kule Ludewa, nchi yetu imejaaliwa kuwa na madini ya chuma katika mradi wa Liganga na Mchuchuma. Kule kwenye mradi wa Liganga na Mchuchuma kuna takribani tani 128 za chuma ambazo zimechanganyika na madini mengine. Haya madini yanaweza kutusaidia kujenga uchumi wetu kama tukiamua kuyachimba na kuyatumia katika viwanda vya kutengeneza nondo, mabati, viwanda vya kutengeneza vifaa vya ujenzi wa madaraja na reli. Kwa kuweza kuzalisha chuma hiki tutaweza kuokoa pesa bilioni 640 kila mwaka kwa muda wa miaka 30 ya uhai wa mgodi huu wa Liganga na Mchuchuma, sambamba na

kutengeneza ajira 35,000 zitakazotokana na mgodi huu wa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la malighafi ya misitu. Mkao wa Njombe, Songwe, Mbeya, Iringa, Katavi, Rukwa, Tanga na mingineyo ndani ya nchi yetu ya Tanzania ina malighafi nyingi sana za misitu lakini vilevile misitu hii tuna kila aina ya mbao; tuna *soft wood*, tuna *hard wood*, tuna mianzi tuna mpaka nta ya kuweza kutengenezea *furniture*. Nilikuwa naiomba Serikali ihamasishé wawekezaji ambao watatumia malighafi hizi za mbao kuwekeza katika viwanda vya kutengeneza karatasi kwa wingi. Kwa kufanya hivi tutakwenda kutumia karatasi zetu za ndani ya Nchi bila kuagiza nje ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niishauri Serikali ihamasishé wawekezaji wa viwanda vya *furniture* ili waweze kuwekeza kwa wingi ndani ya nchi yetu na tuendelee kununua *furniture* ambazo zitakuwa zinatengenezwa ndani ya nchi yetu ambazo zina ubora zaidi ukilinganisha na zile ambazo zinatoka nje ya nchi. nyingi ambazo zinatoka nje ya nchi zinakuwani mavumbi tu ya mbao, siyo mbao halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni wakati muafaka wa kujuliza hivi kwa nini Serikali inaendelea kununua samani nje ya nchi ilhali tuna JKT, tuna Magareza, tuna viwanda vya watu binafsi ambavyo vinatengeneza mbao ndani ya nchi yetu. Na kwa hili niiombe sana Serikali iangalie namna bora ya kusaidia viwanda hivi vya *furniture* ambavyo viko ndani ya nchi yetu lakini vilevile na kuhamasisha zaidi wawekezaji wapya wa kuweza kuwekeza katika vianda hivi vya *furniture* na kuwatolea tozo na kodi ambazo si za lazima katika ufanisi wa viwanda hivi vya *furniture*. Vilevile wawaondolee kodi katika vle vifaa ambavyo vinatumika kurembea *furniture* zetu. Kwa mfano, vitasa, kuna vle vimishikio, msasa, *vanish*, vyote hivyo viondolewe kodi ili kuweza kuhamasisha ufunguaji wa viwanda vingi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikuwa naiomba Serikali iongeze kodi kwa *furniture* zile ambazo zinatoka nje

ya nchi ili kuweza kulinda viwanda vya furnitures ambavyo viko ndani ya nchi na ambavyo vitakavyoendelea kufunguliwa ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa bado katika suala zima la utengenezwaji wa samani bado kuna hii mlaighafi ya ngozi. Naminikabisa Tanzania tuna malighafi nyingi ya ngozi, tukiachilia mbali kutengeneza tu mikoba na viatu tuangalie namna bora ya kuweza kuwekeza zaidi katika viwanda vitakavyoweza kutumia malighafi ya ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Ethiopia wenzetu wameingia mkataba na Kampuni ya Mercedes Benz. Nchi ya Ethiopia ina-supply ngozi ambayo inatengeneza viti ambavyo vinatumika katika magari ya Mercedes Benz. Nilikuwanaishauri Serikali ifanye utafiti na uwezekano wa kuingia mikataba kama hiyo ambayo Ethiopia wenzetu wameingia ili kuweza kutumia malighafi ya ngozi yetu lakini vilevile na kuweza kuongeza uchumi wa taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitoridhika kama nitamaliza kuchangia hotuba hii bila kuzungumzia malighafi ya mazao ya kilimo na hususani katika zao la parachichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Njombe, Songwe, Rukwa, Mbeya, Iringa na Mikoa mingine ndani ya Tanzania inalima sana parachichi; na tunaishukuru Serikali kwa mikakati mbalimbali ambayo imefanya ya kuweza kuwasaidia wakulim wa parachichi kusafirisha nje ya nchi parachichi hiyo ikiwa ghafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo bado, Serikali itafute namna ya kuhakikisha kwamba inahamasisha wawekezaji ambao watakuja kutumia malighafi hii ya parachichi ndani ya nchi yetu kuweza kufungua viwanda mbalimbali ambavyo vitatumia malighafi ya parachichi hii vikiwemo viwanda vya cosmetics kama mafuta ya nywele, lotion, conditioner kwa ajili ya nywele. Vile vile malighafi hii ya parachichi tunaweza kufungua viwanda vya kutengeneza asali pamoja na dawa ambazo zinatokana na majani ya

parachichi. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kukuza uchumi wa nchi yetu na kuweza kuendelea mbele. (*Makofii*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuishauri Serikali, kule bandarini nilikuwa naishauri Serikali iweze kuanzisha, iweke ile *single receiving point* ya mafuta. Kwa kuweka *single receiving point* ya mafuta, faida kubwa itasaidia katika kupunguza zile *demurrage charges* ambazo zinakwenda kumsaidia mfanyakiareshara wa mafuta kumpunguzia mzigo. Halikadhalika itaenda ku...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pilii ilishagonga. Shukrani sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimewita Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Kitwanga na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma ajiandae. (*Makofii*)

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii, nami niweze kusema machache kuhusu hoja iliyo mbele yetu. Nina masuala matano tu ya kugusia kwa ufupi yanayohusu mwenendo wa bajeti yetu na itakavyoenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza naomba Wizara husika au Serikali ichukue ni juu ya umuhimu wa kuwa na soko katika kukuza uchumi wetu. Tunazalisha malighafi mbalimbali, kwa bahati mbaya malighafi hizi kama ni kutoka kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi au Misitu, tuna shida katika *value chain* yetu, haiko vizuri, usindikaji wa mazao haya hauko vizuri ambao ni *competitive* Kimataifa au pia katika kuvutia soko la ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu sana wa kuangalia masoko katika Sekta mbalimbali zinazogusa

Wizara au Taasisi husika na Wizara yenyewe au Wizara ya Viwanda na Biashara kutafuta masoko ya ndani, kuboresha soko la ndani, *kuji-advertise* nchi yetu kwa masoko ya nje ili tuwe na uhakika pale tunapozalisha, basi kile tunachozalisha kiweze kutuletea tija na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona mifano mbalimbali katika Sekta ya Mifugo, tuna shida katika ngozi, tumeona katika Sekta ya Mifugo, hivyo hivyo kuna shida katika uzalishaji wa maziwa. Tuna-*import* zaidi kuliko ku-*export*. Kwa hiyo, nafikiri ni wakati muafaka wa kujitathmini kwa upya na kuweka msisitizo mkubwa katika kuangalia soko linafanyaje kazi nchini ili kukuza uchumi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili nataka niligusie ni kufungamanisha viwanda na sekta nydingine na malighafi ambazo zina-*feed in* kwenye hivyo viwanda na masuala mazima ya elimu. Tunataka nchi yetu iendeshwe na Sera ya Viwanda lakini viwanda hivi vina changamoto nydingi. Kwa hiyo, naomba kuishauri Serikali, Wizara husika, Viwanda na Biashara, uwekezaji, Wizara ya Fedha na Mipango hebu iangalie ina-*connect* vipi na Wizara nydingine husika ambazo zina *feed in* kwenye viwanda? Naomba sera iangaliwe kwa upya ili tuweze kuvii marisha viwanda vyetu siyo kinadharia, bali sasa tuanze kufanya hivi kivitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu nataka niligusie ni umuhimu wa mazingira na jinsi mazingira yanavyoweza yaka-*shape* maendeleo ya nchi kiuchumi na katika jamii yake kiafya. Nilikuwa nimepitia kitabu hiki cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika Mwaka 2018 ukurasa wa 112 kwenda 113 sura ya nane inaongelea kuhusu mazingira na hali ya mazingira nchini illivo. Ninaomba tu ninukuu baadhi ya aya kutoka aya ya 161 na 162, inasema kwamba, "mwaka 2018 Serikali iliendelea kusimamia mazingira kwa lengo la kupunguza athari za uharibifu wa mazingira kwa binadamu ikiwa ni pamoa na kudhibiti athari za matumizi ya Zebaki (*Mercury*) katika uchimbaji mdogo mdogo."

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ni mbaya sana kwa sababu asilimia kubwa ya Zebaki inatumika katika wachimbaji wadogo na asilimia kubwa ya hawa wachimbaji inayozidi asilimia 30 wameshaathirika. Hapa hatuangalii tu athari ya hawa wachimbaji wadogo wanavyotumia madini haya ya Zebaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini haya yana athari kubwa sana. Huu ni mfano tu mmoja wa uhalibifu wa mazingira katika mazingira yenye na katika afya ya wahusika, kwa kuwa ikishaingia katika mfumo wa mazingira, madini haya siyo rahisi kutoka na yanaendelewa kurithiwa kizazi kwa kizazi kwa wanyamapori, samaki, mifumo ya maji na binadamu wenyewe; inaenda kuharibu kizazi na afya ya yule ambaye ameathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hii, mazingira ndiyo uchumi, mazingira ndiyo maendeleo, lakini kwa bahati mbaya hatuiangalii kwa jicho hilo kama Serikali ili kutuvusha hapa tulipo. Hii ipo *reflected* hata kwenye bajeti yenye ya mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa naibu Spika, tumetengeneza Mfuko wa Mazingira hapa nchini, lakini mfuko huu badi haujawezeshwa kufanya kazi ile inayotakiwa, umenyimwa fedha tangu uanze. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kuangalia mazingira na tuanze sasa *ku-link* mazingira na shughuli za uchumi wetu. Unapoharibu mazingira, unaharibu vyanzo vya maji, unapoharibu maliasili ina maana utaenda kugharamia zaidi katika kuboresha yale mazingira yawe katika hali ya uzalishaji. Kwa hiyo, naomba tuiangalie kwa mantiki hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipo hapo kwa mazingira kwa umuhimu wake aya ya 162 inasema, "mwaka 2018 Serikali iliendelea kudhibiti uharibifu wa ardhi ikiwa ni pamoja na kukamilisha tathmini ya hali ya uharibidu wa ardhi nchini, Tathmini hiyo inaonesha kuwa takribani asilimia 75% ya ardhi yetu hapa Tanzania inakabiliwa na upungufu wa rutuba na uharibifu wa ardhi."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, uzalishaji wowote wa kiuchumi katika ardhi unaenda kuharibiwa unakuwa wa chini. Utalima lakini utatumia nguvu nyingi kupata mavuno yanayotakiwa kwa sababu tayari ile ardhi haina rutuba na haina hali ya kukuwezesha wewe kuzalisha kile unachokitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuangalie kwa jicho la ziada kuwezesha mazingira nchini kutunzwa, kwa hiyo, iwe *reflected* katika bajeti kuwekea hela katika kudhibiti ili mazingira haya yaweze kutulea sisi. Kwa hali iliyopo sasa hivi ni tete sana na tutatumia gharama kubwa katika kuirejesha ardhi hii au mazingira yetu ili yaweze kutuzalishia bidhaa mbalimbali na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la nne ambalo nataka niligusie kwa ufupi ni umuhimu wa utafiti na *data*. Any informed decision lazima iwe na *backup* na tafiti na *data* fulani. Kwa hiyo, naona jambo hili bado halijapewa kipaumbele katika Serikali yetu ili kuweza kuboresha bajeti yetu iweze kujiendesha yenyewe. Tunaweza tukafanya *decision* fulani lakini haina *backup* ya *data* nzuri, yaani lazima kuwe na takwimu nzuri ili iweze kukuelekeza kwamba mikakati yako uipangaje au *priorities* zako ziendaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwenendo huo basi, ninaiomba *National Bureau of Statistics* iwezeshwe kwa rasilimali watu na kiuchumi iweze ku-coordinate kama ndiyo *Bureau* yetu ya *Statistics* na taasisi mbalimbali kama *COSTECH* ziwezeshwe ku-collect *data* na kuzihifadhi ili tuweze ku-make sound decisions.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho naomba niligusie, tuweze kujiuliza wote kwamba hii bajeti ilioletwa mbele yetu *is it gender sensitive?* Je ime-accommodate matabaka mbalimbali katika kukuza uchumi wetu? Naomba nisemee hilo kwa kutoa tu mfano kwa suala zima la taulo za kike wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 38 na 39 unaozungumzia kuhusu Sheria ya Kodi ya Mapato, inasema

kwamba inaenda kupunguza kiwango cha kodi ya mapato kwenye makampuni ambayo yanaenda kuzalisha taulo za kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali la kujiuliza je, hii *movie* ya Serikali inaweza kwenda kuwasaidia watoto wa kike kuwa na uwezo wa kupata hizi taulo za kike ambayo ni muhimu sana katika afya yao na katika kujenga uchumi wa nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, najua maongezi hayo, majadiliano tunafanya pamoja na Kamati ya Bajeti, lakini ningependa tu kuweka msisitizo ijitafakari kwa upya ni nini Serikali ifanye ili taulo hizi za kike ambayo ni muhimu sana kwa afya, ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi kwa tabaka hili wa jinsia ya 'Ke' waweze kuangaliwa; kwa wale ambao hawako mashulenii wanaipataje kwa bei ambayo ni rafiki na ni rahisi kupata? Wale walio mashulenii, watoto wa kike wanawezaje kupata hizi taulo za kike?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo, ahsante sana kwa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Kitwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma na Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa sababu mimi naongea pole pole, nimeomba wakubwa zangu waniongezee dakika kidogo. Naomba nizungumzie bajeti hii ambayo ni nzuri sana inayoendana hasa na ile *vision* yetu ya 2025. *Vision 2025* ndiyo *the plan. That is the plan*, lakini hii *vision* imekuwa *cascaded into strategic plan* za miaka mitano. Tumeanza na kujenga misingi. Sasa hivi tunajenga uchumi wa viwanda ili tuende kwenye uchumi wa kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapo jenga uchumi wa kati *we must sacrifices*, kwa sababu hapo unachukua *decision* nzito na kubwa zinazokuwezesha kumlisha ng'ombe

ili baadaye uanze kumkamua. Watu tunaanza kulalamika kwa sababu tulikuwa tumezoea ule uchumi tunaotaka kuondokana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, ana *long vision and wide*. Nawaomba sisi ambaao tumepewa nafasi za kumsaidia tuelewe anachofanya, nasi tuwe na *long vision and wide* ili tumsaidie sasa kuhakikisha kwamba tunafika kwenye huu uchumi wa kati. Hizi *strategic plans* za miaka mitano zinakuwa *again cascaded into yearly operation plan*. Hizi *operation plans* ndizo *plans* tunazoletewa sisi hapa kuziangalia. Hizi *yearly operation plans* ndiyo zinatuwezesha kutengeneza bajeti. Hii bajeti ina-*support* sasa kuweza kutekeleza hii miradi tuliyo nayo. Nafurahi sana kuona jinsi ambavyo tunakuwa na *big project*. Hizi *big projects* zimelenga kuhakikisha kwamba huu ndiyo ulishaji wa ng'ombe ili anenepe tuweze kupata maziwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mafanikio makubwa ambayo tumeyapata na hii sasa nianze kutoa ushauri kwa Serikali yangu. Cha kwanza, naishauri Serikali yangu iendelee kutoa elimu bure na kuwalipia wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu ambaao wanapata sasa hivi mikopo yao bila matatizo. *That is how you think big* na unatekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mafanikio hatuyaoni, tunapiga kelele tu, lakini mafanikio ni makubwa sana kwa sababu hii ni mojawapo ya *pillar* ambayo inatuwezesha kwenye *education* tuwe na wanafunzi, tuwe na watendaji watakaokuwa ni wa kwetu tuliowajenga kwenye vyuo vyetu. Tumetoa hela zetu kwa ajili ya watakaokuja sasa kufanya kazi kwenye viwanda vyetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, anasimamia vizuri na hapo kwa kweli siwezi kusema sana pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko kwenye umeme; niseme ukweli, hata kama wasio na macho wanaona, mabadiliko ni makubwa sana. Maendeleo ambayo

yamepatikana kwa kuweka umeme vijjini yanaonekana, watu wote wanaona. Watu ambao sasa hivi wamekuwa *active* na wamekuwa *knowledgeable* kwa kutazama hata *TV* tu hizi ndogo, wanachomelea, wanaendelea kujipatia kipato kutokana na umeme kufika vijjini, lakini wengi wetu ambao tumekuwa na *narrow mind* na *short vision* hatuyaoni hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye *health*. Wananchi wetu wakiwa na afya kwanza watafanya kazi lakini zitakuwa ni *resources* za kununua *product* zetu ambazo sisi tunazizalisha. Ukiwa na wananchi wenye afya njema, wanafanya kazi, wanajipatia kipato, utawezza kuzalisha katika viwanda vyako na wananchi wataweza kuwa na vipato hivyo waweze kununua hizo mali na uchumi utakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba ndugu zangu ushauri tu wa *health* pamoja na vituo vya afya vizuri tunavyovijenga, *dispensaries*, hospitali zetu za Wilaya ambazo zinaonekana, Hospitali za Rufaa katika mikoa yetu ambazo zinaonekana, sasa tujikite kuwa na wataalam waliobobea na kuweka mfumo mzuri hao wataalam waliobobea waungane na utafiti wa wagonjwa. Pale mgonjwa anapoingia hospitalini isichukue muda mrefu kupimwa na kujua afya yake na kumwezesha aweze kutibiwa ili atoke haraka hospitalini aende kuendelea kuchapa kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Watanzania wenzangu, niliseme hili linalotusumbua sana. Huko nyuma tulizoea sana kupata hela za magumashi, sasa hivi fanya kazi ndipo upate hela, bila kazi huwezi kupata hela. Ndiyo sababu imeandikwa hata kwenye vitabu vyetu vya dini, asiyefanya kazi na asifanye nini? Asile. Tufanyeni kazi, mambo ni mazuri, yanaendelea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije la mwisho sasa katika ushauri wangu, *good governance*. Hili ni eneo ambalo kwa kweli tunahitaji kuongeza nguvu, ndilo linalotusababisha tusi-perform katika baadhi ya sekta. Tunahitaji tuhakikishe

kwamba kila usimamizi, kila senti inayopatikana, ni senti ambayo inaenda kuzalisha au kutumika kama ilivyokuwa imepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upatikanaji wa *resources* hizi za pesa, ziko za aina mbili; pesa zetu na pesa za misaada. Pesa zetu zipo za aina mbili; zile tunazokusanya kodi na zile tunazokopa. Tunapokopa pesa ni za kwetu, maana mbeleni tutazilipa kwa kutumia zile tulizokusanya. Kwa hiyo, tunapopata mkopo tuhakikishe ule mkopo tunautumia vizuri, tusiwe na hali ya kwamba tunawekewa masharti, unajikuta zile pesa nyngi zinarudi tena kwa yule aliyetukopesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mzuri tu kwa ndugu zangu wa Wizara ya Maji. Pale Wizara ya Maji kuna matatizo, maana kutokea Awamu ya Nne Kulikuwa na mradi wa kutoa maji Ruvu kwenda Kimara. Kulikuwa na mradi wa Ukerewe, sasa hivi tuna mradi wa kutoa maji Shinyanga kwenda Nzega, Igunga na Tabora; na sasa hivi tuna mradi huu unaoitwa wa Wilaya 29, una matatizo. Kwa sababu pale kuna Mhandisi Mshauri ambaye kwa miradi yote niliyoisema ameshiriki na kushiriki kwake hakina tija sana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba, nitakuletea makaratasi ambayo yanazidi kiasi hiki uipelekee Serikali ijue kwamba Watanzania wanajua, wanaelewa; na nini kinachoendelea. Maana mimi nilifikia hatua maana mimi nilifikia hatua nikaenda nikatafuta, huyu Mhandisi Mshauri, ofisi zake ziko wapi?

Ukiona mahali ofisi zake zilipo ndipo hapo itabidi ofisi yake iwasiliane na Serikali, hatutakuwa na muda tena wa kuona tunafanya yale yaliyotokea wakati wa *Symbion*, wakati wa Lugumi, wakati wa *IPTL*, haya yatakuwa mabaya zaidi kwa jinsi nilivyoona na nilivyoysoma. Nitakuletea hayo makaratasi uyasome pamoja na Serikali itayarishie kwamba hapo mambo siyo mazuri maana tuna umeme, tuna nguvu

kazi, tutawezaje kuwa na viwanda vinyavyofanya kazi kama havipatiwi maji? Maji ni *resource* kubwa sana katika uendeshaji wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunivumilia, naunga hoja hii mkono asilimia 100. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Asha Abdullah Juma atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mheshimiwa Mohamed Mcengerwa ajiandae.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya bajeti. Naanza kwanza kwa kuunga mkono hoja hii, nachukua nafasi hii kupongeza juhudzi zinazoendelea kufanywa juu ya utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi chini ya Kiongozi wetu mahiri Dkt. John Pombe Magufuli, akisaidiwa na viongozi Waandamizi wake, Mama Samia Suluhu, Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Watendaji wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Philip Mpango, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Ashatu na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha walioweza kufanya kazi nzuri hii leo inatuweka hapa ambayo ndiyo roho ya Taifa letu, Wizara ya Fedha ndiyo roho, wakaweza kuwasilisha bajeti shirikishi na kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Esther ananikera. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu ujikite zaidi katika hii sekta ya uchumi, ukurasa wa sita hali ya uchumi. Kukua kwa uchumi ni jambo zuri kwa Tanzania. Pato la Taifa tumeona limekua kwa asilimia 7.0 kutoka asilimia 6.8 ya mwaka 2017. Namuuliza Waziri Je, uchumi huu na ukuaji huu ni shirikishi, yaani *inclusive*? Ambao umezingatia umaskini kwa kina? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji mkubwa umerekodiwa katika sekta ya sanaa ambayo tumeona hapa ni 13.7 ukililinganisha na sekta ya kilimo umepata kukua asilimia 5.3 ambao hautoshi. Kama tunavyotambua sekta hii ya kilimo ina watu wengi wanaoitegemea kwa ajira, kuzalisha chakula, biashara, mazao, kwa ajili ya viwanda. Kwa maoni yangu, sekta hii ya kilimo ndiyo inauhitaji mkubwa kukua zaidi, ili iweze kuongeza, uzalishaji zaidi (*productivity*) ili iweze kulima kisasa, (*modern agriculture*) na kupanua wigo kwa kuongeza malighafi. Mheshimiwa Waziri tuangalie kwa jicho la ziada namna gani ya kuongeza bajeti kwenye hii sekta ya kilimo na je, tunaona kwa hii tuliyopangia sasa hivi inaweza kukidhi kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kwamba, sekta ya sanaa tumeona imebeba ajira kwa vijana wengi, lakini naamini sekta ya kilimo villevile ikifanyiwa ubora zaidi, hasa kwenye mambo ya *organ, research*, pamoja na kuongeza malighafi itaweza kuajiri, kupanua wigo kwa vijana zaidi watavutiwa hasa tukitia hiki kitu wanaita *agri-business*. Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mpango, ninataka kufahamu kwamba, hii asilimia Saba ya ukuaji uchumi Kitaifa kwamba, je, imeoanisha na takwimu za Zanzibar za ukuaji uchumi, maana imesema Taifa? Sasa Taifa hili ni Taifa Tanzania au Taifa upande gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri uchumi ni mkubwa. Nataka niulize huu uchumi mkubwa ambao umeanza kukua kwa zaidi kwa kasi kubwa, je, unaushikaje mkono uchumi mdogo wa Zanzibar? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri kwamba kutayarishwe mkakati wa pamoja (*strategic growth*), baina ya Tanzania Bara na Zanzibar ili kuweza kuangalia mambo haya. Katika hali ya uchumi wa Taifa ya mwaka 2018, ukurasa wa 118 kitabu kimeonesha viwango vya umaskini Tanzania Bara kwamba umepungua, mapato na matumizi 2017/2018 *basic needs property survey* imeonesha kutoka 28.2 hadi kufikia 26. Kwa sasa, kama mnavyojuwa tunatekeleza malengo endelevu ya *SDG 2030* na agenda ya *2063 Afrika*.

Mheshimiwa Naibu Spika, umasikini kupungua ni hali nzuri. Tunataka tuchukue hatua, ili umasikini huu uweze kupungua zaidi. Tunaweka mikakati ipi madhubuti ya kuongeza tija kwenye kilimo tuweze kutumia bahari yetu kikamilifu, tuendeleze kujenga miundombinu, tuendeleze *human development*, kustawisha elimu na afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba taarifa hizi za ofisi zetu za takwimu ziweze kufanywa pamoja baina ya Zanzibar na Tanzania bara. Kama vile tunavyofanya kwa sensa ya watu kwa vile taarifa hizi zinatumika kwa pamoja na zikiwa zimefanywa kwa pamoja zitaleta *picture* yenye faida zaidi. Nafahamu pia kwamba, tunakwenda kuwasilisha *report* ya hiyari ya utekelezaji wa *SDG UN* mwezi Julai. Pande mbili najua zinashiriki katika matayarisho, nasisitiza uanishwaji wa *data* na taarifa muhimu za uchumi na umasikini, napendekeza bajeti *survey* ifanywe mwaka mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu mikopo nafuu, ukurasa wa 10 makadirio na mapato. Natambua kwamba, Serikali inatayarisha mwongozo wa ushirikiano baina ya Tanzania na washirika wa maendeleo. Katika kufuatilia kwangu nimefahamu Zanzibar imeshiriki kikamilifu katika matayarisho ya mfumo, *frame work*, ingawa katika utekelezaji kumekumbwa na changamoto na nina imani kubwa Serikali hii inafanya kazi changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Zanzibar ina miradi ambayo kwa utaratibu inapitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mpaka sasa iko miradi kadhaa ambayo imekwama ikiwemo miradi ya maji, barabara, kwa mfano Barabara ya Wete – Chake, Hospitali ya Mnazi Mmoja, Uwanja wa Ndege wa Zanzibar na Bandari ya Mpigaduri, mingine imekwama kutokana na vipengele vyaa misamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii barabara na hospitali ilitarajiwa kupata mkopo wa *Saudi Fund*. Kadhaa kubwa ni hii ya mradi wa Zanzibar *Airport*, mkopo kutoka

Exim Bank, mradi huu umekwama muda mrefu sana na kipingamizi kikubwa kwa maendeleo na ustawi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba mazungumzo yaendelezwe kwa *speed* na yakamilishwe kwa manufaa ya pande zote mbili ili Zanzibar nayo iweze kufaidi na kutumia *Airports* zake maana upo vivu wa maendeleo kwa sababu *Airport* ya huku Dar-es-Salaam imekamilika na hii yetu iliyoanza mwanzo haikukamilika, tunachukua kwamba, Zanzibar ni kisiwa na uchumi wa kisiwa unategemea zaidi bandari na uwanja wa ndege. Sasa tunaomba kwamba jithada za ziada zichukuliwe baina ya Serikali zetu hizi mbili ili hili jambo liweze kukwamuka. Sekta hizi mbili, bandari na uwanja wa ndege, ndiyo sekta kiongozi kwa uchumi wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo nafuu na misaada. Misaada ya kibajeti, mifuko ya kisekta, miradi ya maendeleo, ningependa kujua katika jedwali hili kwenye ukurasa wa 103, Zanzibar imepata kiasi gani? Pendekezo kwa mbele ni bora itakuwa vizuri kui-*desegregate* na kuchanganua takwimu za Tanzania Zanzibar na Bara zioneshwe waziwazi, ili tuweze kujua kila mtu anapata nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Asante sana. Mheshimiwa Jesca Kishoa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mheshimiwa Fakharia Shomari ajiandae.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuwa tunazungumzia maendeleo ya kiuchumi hatuwezi kuacha kuzungumzia suala zima la ubora wa watu, yapo matatizo mengi ambayo yamesababishwa kwa kiwango kikubwa siyo na sera au mfumo, lakini yamesababishwa pia na tatizo la ubora wa watu, kwa maana ya maarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mdogo sana, ukiangalia Serikali inakusanya kwa mwezi bilioni 1,300. Katika kila bilioni 1,300 bilioni 580 inatumika kulipa wafanyakazi, kama sawasawa na kama asilimia 45. Sasa unaweza ukaona kwamba, asilimia 45 hii ni *portion* kubwa sana, lakini inaoneka ni kubwa kwa sababu ya uzalishaji ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumzia uchumi wa viwanda. Kama Taifa tulishapiga hatua kubwa sana kwenye suala la uchumi wa viwanda toka miaka ya sabini, sabini na tano, cha ajabu tukapiga--*reverse big time* ukilinganisha uchumi wa viwanda wa sasa na uchumi wa viwanda wa miaka ya 1970 ni vitu viwili tofauti. Kwa mambo kama haya, hata ikitokea Baba wa Taifa Julius Kambarage Nyerere akafufuka leo, atakufa kwa *stress ambazo zipo* katika Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumzia uchumi wa viwanda tunaambiwa vyerehani, tunaambiwa vyanzo vya mapato ni mawigi. Dunia kwenye *Force Industrial Revolution*, wanazungumzia *artificial intelligence*, asimame Waziri ye yeyote hapa aseme kama kwenye Wizara yake ameshafanya *research* akaangalia ni kwa kiwango gani *artificial intelligence* inakwenda kuathiri sekta yake au kwa kiwango gani inakwenda kunufaisha sekta yake, hakuna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema tuka-*invest* bila kuogopa kwenye ubora wa watu. Ni mambo ya ajabu sana tunazungumzia uchumi wa viwanda na wakati hatu-*invest* vya kutosha upande wa watu. Ninaomba kipindi cha zamani tulikuwa tunaangalia kwenye soko la ajira tulikuwa tunapambana sana na Wakenya, lakini sasahivi tunakwenda kupambana na ma-*robot* kwa sababu, ya uwezo tulionao na nguvu tuliyotumia kuwekeza kwenye ubora wa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia *Google* wamejenga centerkubwa sana ya *artificial intelligence* pale Accra, Ghana, mwaka jana na wamealika nchi tisa kwenye

timu hiyo kuhakikisha kwamba wanapata *knowledge* ya namna gani *artificial intelligence* inaenda kunufaisha katika Mataifa yao, kwa upande wa *East Africa* wamechukua Rwanda peke yake. Kwa hiyo, ni bora wakati tunafikiria uchumi wa viwanda, lakini tukawekeza kwa nguvu kubwa sana kwenye ubora wa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigosie pia suala la Deni la Taifa. Kwa muda mrefu sana tumekuwa tukipigia kelele suala la Deni la Taifa, mwaka 2016 nilileta maelezo binafsi humu ndani kuelezea ni kwa namna gani Deni la Taifa linakua kwa kasi kubwa sana, lakini mpaka leo Deni la Taifa limeendelea kuwa ni habari ambayo haina majibu ya kutosha. Badala ya kuendelea sasa kuangalia ukubwa wa Deni la Taifa ni muhimu sasa tukajielekeza kuangalia uhalali wa deni hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango atakapokuja hapa nimtaké wakati anahitimisha kwa kutumia *Audit Report* ya Madeni kwa sababu najua Serikali mnakagua madeni, atuambie uhalali wa deni ambalo tunalilipa la bomba la gesi ambapo inaonekana kwa kiwango kikubwa deni hili limekuwa na kizungumkuti kikubwa. Tutaendelea kukamata wauza kahawa na wafanyabiashara wadogo kwa ajili ya kulipa madeni ambayo hayaeleweki watu wallingia katika utaratibu gani? Ninaomba Mheshimiwa Mpango afanye hivyo, atuambie gharama halisi ya gharama ambayo ilitumika kujenga bomba la gesi na atuambie tunalipa kiasi gani kila mwezi kufidia gharama hiyo ya bomba la gesi? Na kama hatafanya hivyo, nakusudia kuleta hoja binafsi Bunge lijalo, kutaka Serikali iunde Tume kwa ajili ya kuchunguza suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia, nigosie kwenye suala zima la *TRA*. Imekuwa ni kama utaratibu fulani hivi kwamba nchi nyingi ambazo ni za kimasikini zimekuwa na utaratibu wa kutengeneza muundo mkubwa sana wa Serikali na *kuu-feed* kwa gharama kubwa sana. Hii inaonesha ni kwa kiwango gani ambavyo tunakuwa tunakosa *trust* na *private sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mataifa ambayo yameonesha *trust* kwa *private sector* kiwango cha kuzipa *private sector* mamlaka ya kutengeneza Mahakama. Kwa mfano kama Marekani, lakini sisi imefikia hatua kwa mfano *TRA* tunashindwa nini kutengeneza mfumo ambao utatusaidia kukusanya kodi kiurahisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kupeleka *ma-agency* maeneo mbalimbali kama ambavyo mabenki yanafanya. Tunakuwa tuna ma-*agency* *balimbali* maeneo yote nchini ambayo inarahisisha zaidi ukusanyaji wa kodi. Ni vema tukawa tunakuwa *innovative* kuhakikisha kwamba, tunakusanya mapato na kuhakikisha kwamba tunafanya vizuri kwenye sekta ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mpelekee maji ya kunywa Mheshimiwa Jesca Kishoa. Waheshimiwa Wabunge Katibu, hebu mtunzie dakika zake, kama atajisikia vizuri baada ya muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa Philip Mulugo ajiandae.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa mambo machache kusema kwamba, Tanzania *is a sovereign state*. Tanzania ni nchi huru na Taifa lolote kuwa huru kuna mambo mawili lazima yatimie, jambo la kwanza ni Taifa hilo kuwa huru kutunga sheria zake za ndani na kufanya maamuzi ya ndani bila kuingiliwa na Taifa lolote. Jambo la pili, Taifa lolote kuwa huru ni kuamua kufanya siasa za nje bila kuingiliwa na Taifa lolote. Ndiyo maana tunasema Tanzania *is a sovereign state*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeamua nianze kusema haya kwa sababu miezi michache iliyopita tuliona *clip* iliyokuwa inasambaa kutoka kule Ujeruman ikiwaonesha Wabunge wa kutoka Ujeruman wakituambia Watanzania tusimamishe utekelezaji wa mradi wa *Stiegler's Gorge*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni upungufu wa fikra tuseme na pengine wenzetu wanapaswa kutambua kwamba, Taifa lolote linapokuwa huru, linakuwa huru kutunga mambo yake na kufanya mambo yake bila kuingiliwa na Taifa lolote. Kwa namna hiyo katika *clip* ile inawaonesha Wabunge wa Ujerumani wakisema kwamba, wao ni koloni la Tanzania wakiamini kwamba bado ni koloni lao. Niiombe Serikali kufanya maamuzi yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Serikali ifanye tathmini ya athari za ukoloni hapa nchini, ukoloni ulituathiri nchi yetu kwa kiwango gani? Wakati huo tunatambua kwamba Ulaya imejengwa na Afrika kupitia *raw materials* zilizotoka hapa Tanzania na nchi nydingine za Afrika. Tuombe Serikali ifanye tathmini ya athari za ukoloni, lakini baada ya kufanya tathmini ya athari za ukoloni Serikali ifungue kesi katika Mahakama ya Kimataifa kudai fidia zinazotokana na ukoloni. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kufanya hivyo, Kenya imefanya hivyo na Mahakama za Kimataifa zimeamuru wenzetu waweze kulipwa fidia kutokana na athari za ukoloni, niliona nianze hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya vita ya Dunia Tanzania tuliachwa chini ya *League of Nations*, tuliachwa chini ya Waingereza, lakini tunatambua kwamba, Waingereza hawakufanya lolote kwa Taifa letu, walitufanya Tanzania tuendelee kudumaa kiuchumi. Serikali pia, ikiwezekana ifanye tathmini ya athari zozote zilizofanywa na Taifa la Uingereza ili tuweze kufungua mashtaka kwenye Mahakama ya Kimataifa ya kudai fidia zilizotokana na athari hizi za ukoloni ambazo zimefanywa na wenzetu hawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi lazima niipongeze sana Serikali lakini pili nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kudhamiria kutekeleza Mradi wa *Stiegler's Gorge*. Mradi huu ni nembo (*symbol*) ya Taifa letu. Mwalimu Nyerere mwaka

1956 wakati wa kupigania uhuru, wakati ule alivyokuwa akija Rufiji alidhamiria kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa. Wamepita viongozi wengi wa nchi hii, Marais wengi wamepita, maamuzi yaliyofanywa na Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ni maamuzi magumu na ya kizalendo ya kwenda kutekeleza mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unakwenda kuongeza pato la Watanzania. Tukiweza kuzalisha umeme *megawatts* 2,100 inamaanisha kwamba viwanda vyetu vyote vitaweza kupata umeme wa kutosha. Tutambue kwamba umeme kutokana na mradi huu utakwenda kuuzwa kwa bei ya chini kabisa. Ni kiongozi gani ambaye anaweza kukubali kufanya maamuzi haya magumu, ni Rais peke yake aliyedhamiria kuwakomboa Watanzania. Kwa hyo, sisi tunaipongeza sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami lazima niseme sisi watu wa Rufiji tumetunza vyanzo vile kwa muda mrefu sana. Kupitia kwa Mbunge wao Mchengerwa, mara kadhaa nimeleta hoja hapa kabla hata Serikali kuamua kufanya maamuzi haya. Lazima tukiri kwamba huu ni utekelezaji wa llani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba wakati Serikali inakwenda kutekeleza mradi huu, tuwakumbuke watu wa Rufiji kwa sababu zipo kelele za wananchi wetu wa Rufiji kwamba kwenye ajira hawajachukuliwa wengi. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri kwamba wakati sasa tunakwenda kutekeleza mradi huu, kipaumbele cha kwanza kabisa cha ajira kiwe ni kwa wananchi wetu wa kutoka Rufiji kwa sababu ndiyo wameutunza mradi huu kwa miaka mingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mradi huu kutengenezwa utaendelea kubaki Rufiji na ndiyo maana tunasema kwamba Warufiji tuwaangalie kwanza kwa sababu wao ndiyo wanautunza mradi huu lakini kupitia Mbunge wao, ndiyo tulileta hoja hapa kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa. Yako maeneo yatahitaji uboreshaji

wa miundombinu kuptitia kwenye mradi huu, tunaipongeza sana Serikali imejenga barabara na madaraja. Tunaomba sasa barabara hizi ambazo zimejengwa na Serikali zijengwe kwa kiwango cha lami. Ili mradi huu utekelezwe kwa miaka mitatu anayoitaka Mheshimiwa Rais, kipande cha kutoka Kibiti - Mkongo ni kibovu sana, tunaiomba Serikali kuhakikisha kwamba eneo hilo linaboreshwu vizuri sana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutoa mchango wa namna gani tunaweza kuongeza kodi, ipo kodi inasahaulika. Pengine Mheshimiwa Waziri wa Fedha akisimama hapa atuambie ipo kodi ambayo kimsingi inawekwa kwa ajili ya *ku-discourage consumption*. Kodi hii mara nyingi tunaita *excise duty au sin tax*. Kodi ambayo inatakiwa itozwe kwenye sigara na pombe lakini kodi hii imesahaulika kwa muda mrefu. Serikali inatumia mabilioni ya fedha kutibu watu *TB* lakini haijafanya nyongeza yoyote ya kodi kwenye sigara. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwhi kuandika andiko moja 20 iliyopita kuhusiana na makusanyo ya kodi ya *sin tax*. Tuombe Mheshimiwa Waziri aangalie Watanzania wanaathirika sana na sigara, Serikali inapaswa *ku-discourage consumption* kwa kuongeza kodi hii ili Watanzania waache kutumia sigara. Pia hata kodi kwenye pombe Serikali iangalie uwezekano ili iweze kuongeza mapato lakini pia *ku-discourage consumption* ya vitu hivi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa tumekuwa tukiangalia sana madini ya dhahabu lakini yapo madini mengine ambayo yanatumika kwenye viwanda, Serikali imesahau sana. Tumuombe Waziri wa Fedha atakaposimama hapa atuambie Serikali imefikia hatua gani kuhusu kuimarisha na kuboresha mchakato wa matumizi ya madini ya *soda ash* ambayo yanapatikana kule Arusha.

Mheshimiwa Nailbu Spika, madini haya yana fedha nyingi sana kuliko hata dhahabu lakini Serikali imekaa kimya, haizungumzia jambo lolote kwenye eneo hili. Tunatambua

kwamba Wajapan walitoa fedha nydingi sana na fedha hizi walipewa watu wa *NDC*. Waziri wa Fedha akisimama hapa atuambie fedha hizi zimekwenda wapi na kama kuna wanaohusika kuzila fedha hizi, basi Serikali ichukue hatua kali kwa wahusika wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua madini haya (*industrial minerals*) ndiyo yananufaisha nchi nydingi sana. Bajeti ya Marekani inategemea madini ya viwandani. Kwa hiyo, niombe Serikali kuzingatia hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa asilimia 100, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Fakharia Shomar atafuatiwa na Mheshimiwa Phillipo Mulugo na Mheshimiwa Selemani Bungara almaarufu Bwege ajiandae.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi adhimu ili nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Wakuu. Wizara hii viongozi wa juu wamo Wazanzibari, kwa hiyo, naiangalia kama ni sehemu ya Muungano, naipongeza Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyowajali Watanzania katika bajeti yake kwa kuwaondolea tozo, ushuru wa forodha na VAT. Hapa tunaiona Serikali inavyowajali raia wake na kuwapunguzia ukali wa maisha katika utendaji na ufanyaji kazi wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutoa misamaha kwa viwanda vyetu vya ndani. Hili ni jambo adhimu na kubwa la kuvisaidia viwanda vyetu vya ndani

kupata mapato na kuwezesha Serikali kupata mapato lakini kuwanufaisha Watanzania kwa kuyatumia mapato yao wanayochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushuru wa forodha naomba uwakilishi uwe wa pande zote za Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Pia kinachopatikana kiwe ni kwa faida ya pande zote mbili. Kwa kufanya hivyo itasaidia kuonesha jambo hili linafanya kazi kwa mujibu wa makubaliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia taulo za kina mama. Sipingi maelezo yaliyotolewa kwenye kitabu hiki na Mheshimiwa Waziri, yapo sahihi na tunayakubali lakini bado Wizara izidi kuliangalia tena suala hili kwa sababu vijana wetu hawana uwezo. Wizara itafute mbinu ili taulo za watoto ifikie Sh.300 mwisho Sh.500 kwa *box illi* mtoto aweze kulinunua au hata mzazi maskini aweze kumnunulia mtoto wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, kuna matangazo ya dawa ya mswaki *Colgate*, wanaambiana vijana/watoto wadogo Sh.300 tu unaweza ukununua na meno yako yakakaa sawa. Sasa vitu kama hivyo ukiviangalia na ukivisaidia itapendeza na itawasaidia vijana wetu wawewe kujikimu lakini maelezo uliyoyatoa nayakubali na hayana matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulizungumzia suala la Bandari ya Mpiga Duri. Zanzibar inategemea bandari iliyopo Malindi na bandari ile tayari imeshazidiwa maana ni ya toka ukoloni. Sasa hivi tumeamua kuanzisha Bandari ya Mpiga Duri lakini nguvu zetu sisi bado zipo chini ya dhamana na mikono yako Waziri. Naomba hili Waziri uliangalie tena kwa jicho la huruma na imani maana hivi sasa baadhi ya makontena tumeyatoa Malindi kule tumeweka Darajani lakini kwa mazingira haijapendeza na hayajakaa sawa na ile sehemu si nzuri ukiweka makontena maana kuna vijana wanayavamia, wanakwenda kufanya ufuska pale, haipendezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa kwa huruma na busara zako Waziri utaweka mkono na kutufanikisha bandari ile ikaweza kujengwa utakuwa umeisaidia Zanzibar katika uchumi wake. Uchumi wa Zanzibar ukukua tayari Tanzania itafaidika, itakuwa tayari Zanzibar inaweza kujitegemea na Zanzibar ikaweza kutekeleza majukumu yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Phillipo Mulugo atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Bungara na Mheshimiwa Livingstone Lusinde ajiandae.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia Wizara hii kubwa namna tunavyoendesha nchi yetu kwa sababu hapa ndiyo penyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka mwaka jana kama siyo mwaka juzi, nilichangia hapa mifumo ya Serikali tunavyoendesha hasa katika ugawaji wa rasilimali. Nililalamika sana hapa Mheshimiwa Mpango ulinisikia lakini napenda kushukuru kwamba baada ya malalamiko yale, naweza sasa leo nikajidai hapa nikasema sasa Songwe tuna hospitali na kila kitu ambacho nilikilalamikia pale ikiwemo miradi ya maji. Kwa haya yote, nikupongeze sana kwa namna ulivyonisikia na namna ulivyotekeleza mambo kwenye Mkoa wetu wa Songwe na Jimboni kwetu. Naishukuru sana Serikali ya Awamu hii ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa mambo yote yanayoendelea kutekelezwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kikao alichokifanya cha wafanyabiashara *two weeks ago* pale Dar es Salaam. Kwa kweli kikao kile kimetupa dira na kimeleta mwelekeo mzuri wa wafanyabiashara Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge tumekuwa tukilalamika sana humu ndani na Waheshimiwa Wabunge mtaniambia, mengi ambayo tumekuwa tukiongea sasa ndiyo yaleyale ambayo aliongea na wafanyabiashara lakini Mawaziri wetu ni kama vile mna-*ignore* Wabunge. Tukiongea sisi hata wale watumishi wenu wanasema aah wameongea tu wanasiasa, ni siasa tu, lakini tumeongea sana humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka hata Mheshimiwa Musukuma alivyoongea pale aliongea yaleyale ambayo kila siku anaongea humu ndani na sisi tunaongea hayohayo. Hata hivyo, kwa sababu kilikuwa ni kikao *special ameitisha* Mheshimiwa Rais yakachukuliwa kama vile ndiyo mambo ambayo ni makubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango na sisi Wabunge tukiongea mambo hapa undeni Tume ya kufuatilia yale ambayo tunakuwa tumeyaongea, mtapata faida nyngi. Tusingefikia pale kama mngekuwa mnachukua michango ya Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba Mkoa wa Songwe kule Jimboni kwangu, hivi ninavyoongea kuna kampuni moja inaitwa *Heritage Rukwa Tanzania Ltd* wale Wazungu wameenda kwao kwa sababu hawa jaelewana na *TPDC*. Hawajaelewana nao kwa sababu hawa watu wa kampuni ya *Heritage* walikuja kufanya utafiti wa kuchimba mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni hii ndiyo iliyofanya utafiti wa kupata mafuta kule Uganda ambapo sasa hivi *pipeline* inaendelea kutengenezwa kufika Tanzania. Ni kampuni kubwa ambapo tungeweza kunufaika nayo sana. Wamefika Jimboni kwangu Kijiji cha Maleza, wameanza kufanya utafiti wao, wamechimba na wameyakuta mafuta. Baada ya pale wamerudi Serikalini kufanya *negotiations* katika sheria zetu ambazo zimebadilika mwaka juzi kuhusiana

na masuala ya mafuta na madini. Mpaka hivi ninavyozungumza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wale watu wameondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifuatilie ule mgogoro ni nini hasa? Maana yake mpaka sasa hivi wameshatumia *million 3.6 USD*; wameshajenga madaraja na wameshafanya kila kitu. Ukiiongea nao unaweza ukatoa na machozi lakini kuna watu wapo pale Shirika la Petroli sijui wamefanya nini na wale Wazungu. Naomba Serikali hebu lichukueni hili kama ni *serious issue*. Mheshimiwa Rais akija Songwe nitamwambia na nitamfikisha sehemu ile. Sasa kabla Mheshimiwa Rais hajafika Songwe, naomba Serikali na nyie mkae na watu wa *Heritage Tanzania* wapo pale Dar es Salaam muone tatizo ni nini. Hii inatupotezea umaarufu mkubwa sana wa kujipatia fedha kwa ajili ya masuala ya mafuta. Wenzetu Uganda walikubali na wamefanya na sasa hivi mafuta yamepatikana kule Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, yule *RAS* ambaye Mheshimiwa Rais ametupa Songwe ni *very creative* yule kijana anaitwa David Kafulila. David Kafulila ameshawishi Mkoa wetu kupitia *RCC* tumeanzisha kampuni inaitwa *Songwe Business Company Ltd*. Wakurugenzi wa Halmashauri ndiyo wadau na ndiyo *board directors* kwenye kampuni ile. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni hii tayari TAMISEMI walishaturuhusu na imeshaanza kufanya kazi. Naomba kila Halmashauri au kila mkoa kama wangeweza kupitisha kwenye *RCC* zao tuwe na kampuni kama hizo ambazo zinamilikiwa na *RAS* pale mkoani, inafanya biashara kuliko kutekeleza kule Halmashauri ambako kuna *bureaucracy* nyingi sana. Ni jambo zuri na mtakuja kuona faida yake. Sisi baada ya miaka mitano tunaweza tusiwe tunaomba hela Serikali Kuu, *RAS* wetu Kafulila anafanya kazi kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kitu ni kikubwa sana, siku moja Waheshimiwa Wabunge nitawaletea ile *Memorandum of Understanding* ya *RCC* ya Songwe, ni jambo

kubwa sana Mheshimiwa Mama Mbene anaweza akani-*support* hapa. Kwa hiyo, naomba hata Halmashauri zingine ziweze kufanya hivyo, hii kampuni inamiliikiwa na Halmashauri zote tano za Mkoa wa Songwe na Ma-*DED* ndiyo *board members* wa kuendesha miradi ya kibashara kwenye Halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nilichangie ni kuhusu suala la *EPICA*, kuna kitu kinaitwa *EPICA* kwenye mfumo wa fedha. Nataka niseme kabisa kwa machozi makubwa, hii *EPICA, of course* sisi siyo wataalam wa kujua *EPICA* ni nini lakini angalau mimi najua. *EPICA* hii inasumbua sana baada ya kupitisha bajeti hii, tarehe 30 Juni, 2019 kesho kutwa baada ya bajeti kupitishwa hapa, fedha zote za kwenye Halmashauri zinafungwa. Kuanzia tarehe 1 Julai, 2019 mpaka ije ifike tarehe 30 Julai, 2019 kule kwenye Halmashauri kunakuwa hakuna mfumo kabisa wa namna ya ku-access fedha za Serikali mpaka tarehe 1 Agosti au mpaka Septemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mwaka jana mpaka Halmashauri wananiuliza Mbunge tuna mfanyabiashara gani mkubwa hapa tunaweza kumkopa fedha tuweze kukamilisha labda mahitaji ya Halmashauri. Naomba tutafute mfumo mwengine ambao unaweza ukasaidia ili baada ya bajeti kupita, angalau tarehe 15 au hata baada ya wiki mbili Serikali ifungue mifumo yake ya fedha. Nini maana ya kujenga mkongo wa Serikali kwa Halmashauri? Kwa hiyo, mifumo ya kompyuta ifunguke mara moja ndani ya wiki mbili Halmashauri ziweze ku-access fedha ili tuweze kutumia. Najua Waheshimiwa Wabunge wenye Majimbo mtakuwa mnahangaika sana na mifumo ya fedha kuanzia Julai na Agosti kwenye Halmashauri zetu, kwa kweli mimi kule kwangu inasumbua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi mchango wangu leo ilikuwa ni hayo, hasa mfumo wa *EPICA* na *Heritage Company*, watu wa *TPDC* waweze kukaa na Serikali na wale Wazungu ili mambo yaweze kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Selemani Bungara atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Willy Qambalo ajiandae.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya kuongea leo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninachoifurahia Serikali ya CCM kwa kutoa tozo za ng'ombe au wafugaji. Hata hivyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, katika sekta ambazo umeisahahu ni Sekta ya Uvubi. Sisi wavuvi; mimi mvuvi, ndiyo; sisi wavuvi kuna tozo moja tunatozwa dola 1.5 *royalty levy*, ni shillingi 3,300 kwa kilo ya dagaa. Na alivyokuja Waziri Kilwa na wavuvi wa Kilwa tuliomba sana hii tozo ipungue, kwa sababu unapoteza dola 1.5 sawasawa na kila kilo moja ya dagaa shilingi 3,500 mvuvi atakuwa hapati bei nzuri na wala hatuwezi kuuza nje ya nchi hawa dagaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sababu kubwa kule Ziwa Victoria dagaa hao hao wanatozwa 0.16, shillingi 300 kwa kilo. Kwa hiyo dagaa wa Pwani shilingi 3,600 kwa kilo, dagaa wa Victoria shilingi 300 kwa kilo. Ina maana kwamba dagaa wa Pwani hawatakuwa tena na soko kwa sabbau hawatakwenda nje. Tunaomba sana kwamba hii tozo ibadilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha pili, wavuvi wa Kilwa wamechomewa nyavu zao. Walikata leseni, wana vyombo vyao halali, nyavu zao ni milimita nane, za halali za kisheria, na mtu ukikata leseni ina maana kwamba mtego wako umekaguliwa na ni halali kuvulia. Sasa cha ajabu zaidi ni kwamba tuliomba Serikali kwamba hizi nyavu zisichomwe mpaka hiyo kanuni ya milimita nane ipitishwe; Waziri akakubali kwamba nyavu zisubiri. Alivytoka pale Kivinje kufika Dar es Salaam tu siku ya pili nyavu zikachomwa. Zile

nyavu milimita nane zikachomwa halafu mwezi wa tano zikaruhusiwa tena milimita nane zivue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naona ajabu, halafu mnasema Serikali hii ya wanyonge. Kwamba milimita nane tuliomba zivumiliwe Waziri akasema zisichomwe mpaka sheria irekebishwe na alituhidi kwamba itarekebisha mwezi wa tano. Akitoka pale Kivinje anavyotuahidi akifika Dar es Salaam tu kachoma. Alivyochoma mwezi wa tano anaziruhusu zilezile nyavu alizochoma zivue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana kwa kuwa wavuvi walikuwa na leseni zao, vyombo vyao halali na nyavu zao zilezile zilikuwa halali, naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango ongeza katika bajeti fedha za kuwalipa fidia milioni 900. Ongeza warudishiwe hela zao kwa sababu mmewaonea, naiomba Serikali wavuvi warudishiwe hela zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu chako ukurasa wa 79 anasema kiongozi achaguliwe anayetoka katika ndani ya chama cha siasa kinachotetea maslahi ya haki ya wanyonge na chama hicho ni CCM. Sifa za wagombea, chakushangaza mna sifa gani ninyi CCM kwamba wanyonge ndio mnawatetea ninyi!

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mnasema kwamba wafanyakazi wasiongezewe mishahara kwa sababu kuna miradi mitatu mikubwa ya kiuchumi. Wakati mnawaambia wafanyakazi wasiongezewe mishahara sisi Wabunge posho yetu ya siku 30 ni mishahara ya miaka miwili na miezi sita ya mfanyakazi. Tuseme wafanyakazi wadogo wangojee sisi Wabunge tuna mishahara mikubwa na miposho mikubwa wao wangojee. Wanyonge hao, wanyonge mnawanyonga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge leo hata tukikaa miaka mia hatuongezewi mishahara wala hatuna taabu; tunakunywa maji safi na salama, tunasomesha watoto wetu, lakini wanyonge, wafanyakazi wasiokuwa na mishahara

mizuri mnazuia kuongeza mishahara mnasema eti mngojee mpaka... hii CCM hii, naomba sana...

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bungara, kuna taarifa; Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

TAARIFA

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Selemani, maarufu Bwege, kwamba alikuwepo wapi mpaka sasa hivi anaona hana nafasi ya kupata katika uchaguzi ujao anasema kwamba mshahara ni mkubwa; alikuwa wapi tangu alipoinga humu Bungeni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bungara, endelea na mchango wako.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muda wangu uzingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wala simuelewi anachokisema, naona kababaishababaaisha maneno tu. Ninachosema Serikali ya CCM mnasema mchaguliwe kwa sababu mnawatetea wanyonge, wanyonge ni watu ambao wanapokea mishahara midogo...

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: ...posho yetu sisi Wabunge...

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Taarifa juu ya taarifa, mimi najibu taarifa hii kwanza. Kwa hiyo...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bungara, kuna taarifa; Mheshimiwa Agness Marwa.

TAARIFA

MHE. AGNESS M. MARWA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa taarifa kwa muongeaji anayeongea kwamba Serikali imesema kwamba wafanyakazi wasiongezewe mishahara kwamba Mbunge haruhusiwi kuongea uwongo Bungeni, atuelezee kwamba ni nani aliyetamka hayo matamko.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, aliyetamka ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na *clip* tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo katika Nchi za *SADC* tulikubaliana kwamba kilimo kisipate chini ya asilimia 10 ya bajeti. Leo mkulima mnyonge mnampangia asilimia 1.5, eti Serikali ya CCM ya wanyonge. Serikali ya CCM leo watu wanatekwa, wanapigwa risasi, wanyonge, hawafikishwi mahakamani, na wanaopigwa risasi wanakufa, eti Serikali ya wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mkulima wa korosho kalima korosho zake mpaka leo hajalipwa, Serikali ya wanyonge. Leo wavuvi wanachomewa nyavu zao ilihali ... Serikali ya wanyonge; mnyonge gani? Leo wafanyabiashara wadogowadogo wanalipishwa shilingi 20,000 kila mtu, Serikali ya wanyonge; wanyonge gani? Nashangaa sana ninyi mtapitaje katika uchaguzi huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wanalia, wavuvi wanalia, wakulima wanalia, wafanyakazi wanalia; Serikali ya wanyonge mtapita wapi? Tunajua mnataka kupita ninyi kwa kutumia rungu yenu ya dola, polisi, wanajeshi wasimamie uchaguzi ili mshinde, lakini kwa wanyonge wa

nchi hii kuichagua CCM, *ng'ooo!* Mnyonge gani! Leo tunakula tunaomba sana Serikali ya CCM siyo ya wanyonge, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, mnyonge hapati haki mpaka mwenye nguvu atake, wenye nguvu ndio ninyi Serikali ya CCM, manawaonea wanyonge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kimechanwa kitabu juzi hapa kwa kuwa sijui kitabu cha wanyonge mmeacha tu; mikutano ya hadhara inazuiliwa kwa sababu sisi wanyonge, acheni bwana. Naomba sana Serikali ya CCM ijirekebishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge posho yake ya mwezi mmoja mishahara ya miaka miwili na nusu ya mnyonge. Soko hilo hilo, shule hizo hizo, anaposoma mtoto wa mnyonge na mtoto wa Mbunge hapohapo; soko la mnyonge na soko la Mbunge hilohilo lakini mshahara 350,000. 350,000 kwa mwezi sisi posho siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania Nyerere alisema, mwisho nasema, kasema mtu mmoja hapa eti nchi yetu ina uhuru, Nyerere alisema nchi yoyote isiyoweza kujitegemea haiwezi kuwa huru. Ndiyo maana tulisema ujamaa na kujitegemea, kama hukujitegemea ujamaa hautekelezeki na tutakuwa chini ya mabeberu mpaka kiama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutwa ombaomba tu na mtu anayeombaomba hawi huru, kwa hiyo, sisi hatupo huru tuna uhuru wa bendera tu. Naomba sana...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: ...naomba sana, naona kasimama mama pale.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bungara kuna taarifa. Mheshimiwa Jenista, naona kengele yake imegonga hapo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimesimama kabla kengele hajagonga.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge huyu ndio Waziri mwenye dhamana ya ajira, kwa hiyo Mheshimiwa Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Bungara. Amesema kwamba nchi yoyote ambayo inataka kujitawala ni lazima ijenge uchumi wake yenye, na ame-quote maneno ya Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Bungara, na ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Dkt. John Pombe Magufuli imeamua kubeba *concept* ya Baba wa Taifa kuhakikisha inakuja na miradi mikubwa ya kimkakati ili kuhakikisha nchi yetu inajenga uchumi wa ndani na uchumi ule wa ndani ndiyo utakaomaliza kero nyingi za wananchi wanyonge wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huohuo, tukiendelea na miradi mikubwa ya kimkakati, miradi ile ya kuwanufaisha wanyonge kama ujenzi wa zahanati, ujenzi wa vituo vya afya, elimu bure kwa wanafunzi, hayo yote yameshakwenda kwa wananchi wanyonge. Mheshimiwa Bungara anajua hati wananchi wa jimbo lake wanapata elimu bure na kitu hicho hakikuwepo katika muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninataka kumpa taarifa Mheshimiwa Bungara.

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake kwanza ni nzuri sana.

NAIBU SPIKA: Muda ulishaisha Mheshimiwa Bungara. Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka...

(Hapa Mheshimiwa Selemani Bungara alikuwa akipiga kelele)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bungara tafadhalii!

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kuna wakati taarifa za kifedha zikiwekwa wazi huwa kuna watu wanalamika hivi. Iakini maneno kama haya yakizungumzwa pengine ni muhimu watu wafahamu ni fedha kiasi gani Wabunge wanapata ili irahishe wananchi huko nje kuona uhalisia wa mambo haya. Kwa sababu mtu anaweza akasema jambo halafu akitoka hapo nje anadaiwa 50,000 miezi sita mtu hajalipa wakati analipwa hela ambayo ni posho ya siku moja mtu analipwa mshahara.

Kwa hiyo pengine ni muhimu Waheshimiwa Wabunge kama mnakubaliana na Mheshimiwa Spika, atangaze Wabunge tunapata kiasi gani inaweza ikarahisisha mchango wa Mheshimiwa Bungara ili wananchi wafahamu, inaweza kutusaidia kidogo maana naona Wabunge walikuwa wananiangalia hapa kama ni kweli ama viyi.

Waheshimiwa Wabunge tuendelee na wachangiaji niliokuwa nimeshawataja; Mheshimiwa Livingstone Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Willy Qambalo, Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo ajiandae.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai na afya ili niweze kuchangia katika mchango unaoendelea sasa wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja na dada yangu, Mheshimiwa Dkt. Ashatu ambaye ni Mbunge wa Mkoa huu wa Dodoma, wanafanya kazi nzuri sana, kazi yao ni njema na tumeona Mheshimiwa Rais akionesha njia

kwa kukutana na wafanyabiashara pale Dar es Salaam watano toka kila wilaya na wafanyabiashara wakamwambia mambo mengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika wakuu wa mikoa na Waziri mwenye dhamana ya Wizara hiyo watakuwa wamepata mwongozo kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa namna ya kukutana zaidi na wafanyabiashara wengine wengi zaidi, isiishie pale tu alipoishia Rais, Rais ye ye ameonesha njia wao sasa wachukue nafasi hiyo kuendeleza ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango kinaonesha uchumi unakuwa takribani kwa asilimia saba. Na kila siku nimekwa nikisisitiza sana kwamba hesabu hizi wakati mwingine tuwe tunazihusisha na maisha ya kawaida ya raia wa nchi yetu, tukifanya hivyo tutauona uchumi namna unavyokuwa. Tuwe tuna *sample* ya pengine wilaya iliyokuwa maskini mwaka jana au mwaka juzi hali yao kwa sasa ikoje, tukifanya hivyo tunaweza tukapata picha ya moja kwa moja namna ambavyo uchumi wa nchi yetu unakuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona safari hii *TRA* wakiondoa kodi kwa biashara mpya. Kitendo hiki kitachagiza sana wafanyabiashara hawa kuweza kujua katika miezi sita amezalisha kiasi gani na anaweza kutozwa kodi kiasi gani. Mwanzoni yalikuwa ni maajabu kabisa, unamkamua ng'ombe halifu ndiyo unakwenda kumlisha, yaani biashara inaanza leo na kodi unaanza sasa. Kwa kweli pale haikuwa sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndiyo maana nikawa natafakari, wakati mwingine maafisa wetu wa kutoza kodi hawa ingekuwa kama zamani ambapo viongozi tulikuwa tunasisitizwa unapotaka kuhamisha kilimo na wewe uwe na heka yako moja ya kilimo, kwa hiyo, unaweza ukawaonesha wananchi kwa vitendo kwamba wewe unalimaje na unfuataje taratibu za kilimo. Na maafisa wetu watoza kodi hawa na wao wangekuwa walau na biashara,

walau duka, anaiza ili na yeze tuje tumuone katika miezi sita atakuwa amepata faida kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua ukitaka kupima adha anazopata mlemavu wa macho hebu funga kitambaa cheusi halafu nenda sokoni, ukikoswa na bodaboda ya kwanza tu utakitoa kile kitambaa. Kwa hiyo, kwa kweli wakati mwingine tunafanya vitu kwa sababu sisi hatuishi maisha hayo. Kwa hiyo, rai yangu kwa watu wa *TRA* ni yaleyale maelekezo ya Mkuu wa Nchi kwamba wawe rafiki na wafanyabiashara badala ya kuleta lugha ambazo zitakuwa zinaudhi baadhi ya wafanyabiashara na kuwakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nachangia vitabu vyote viwili; kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango na kitabu cha Kambi Rasmi ya Upinzani. Na kwa kweli sikusudii kukichana hata kidogo, labda pengine ntakichana kwa hoja tu. Kuna watu wanajaribu kuzalisha hoja kwamba Serikali, Mawaziri, sijui wanahofia maelezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani, si kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikinukuu katika hotuba yao ukurasa wa kwanza anasema, namnukuu Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani:-

"Mheshimiwa Spika, kama mkakati ndiyo huo wa kudhoofisha Upinzani Bungeni kwa kuwafukuza Wabunge wa Upinzani. Napenda kulithibitishia Bunge lako kwamba mkakati huo umeshindwa kabla hata haujaanza kutekelezwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iko imara zaidi leo kuliko jana ndiyo maana kila wakati tunapowasilisha maoni yetu hapa Serikali yote inahaha kutujibu". (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno si ya kweli nataka nieleze hapa kwamba kama ikitokea Mwalimu Nyerere akarudi hapa akiwa na rafiki yake Bob Makani, hawa watu wawili wote watakuwa na mshangao mkubwa sana. Mwalimu Nyerere kuna mambo yatamshangaza na Bob Makani kuna mambo yatamshangaza. Bob Makani alikuwa Mwasisi wa CHADEMA, Mwalimu Nyerere Mwasisi wa CCM, hawa wawili wanatashangaa!

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mwalimu akifika Lumumba atashangaa kukuta ofisi ya ghorofa ambayo hakuiacha, Bob Makani atashangaa kukuta ule mgahawa bado upo pale. Yaani nataka niwaambie hawa watu watashangaa sana. Bob Makani kila atakapojaribu kwenda Kinondoni atakuta hata rangi zilizopakwa za CHADEMA bado ni zilezile, hazijawekwa mpya, atashangaa sana Bob Makani, kwamba hawa watu ndio walikuwa wa maendeleo hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi Mwalimu atakapokuja atakwenda Chimwaga akidhani ndiyo Ukumbu wa CCM, ataambiwa ni chuo kikuu, atashangaa Mwalimu kwamba hii kazi imefanywa. Atapotea atakuwa anakwenda Kizota anafikiri bado tunafanyia mikutano Kizota, ataambiwa hapana, shuka hapo katikati kwenye daraja, Mwalimu atashangaa sana, atakuta mabadiliko ni makubwa ambayo Bob Mnyanga Makani hatayaona CHADEMA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bob Makani kuna kitu atataka kujuliza, atasema labda niende sasa kwenye demokrasia maana ndiyo jina la chama chetu, hebu niulize demokrasia inatendekaje ndani ya CHADEMA, atakuta Mwenyekiti ni yuleyule, atashangaa sana Bob Makani. Hawa watu ndiyo mnasema eti sisi tunawahofia, hawa, ambao hata Bob akija leo atawashangaa. Atauliza Mwenyekiti wa chama nani, ataambiwa yuleyule uliyemuacha, wakati huku Mwalimu ataambiwa Mkapa alimaliza, akaja kijana wako Kikwete kamaliza sasa yuko Magufuli, Mwalimu atashangaa kukuta demokrasia inatekelezwa ndani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme kweli kwamba hawa jamani hata mzee wa paka huwa anapokea, hawa ndio mnasema tuwaogope? Hatuwezi kuwaogopa hawa. Mwalimu Nyerere atauliza chama changu vipi mfumo wake wa Viti Maalum unafanya kazi, ataambiwa wapo, Wabunge wa Viti Maalum wapo. Bob Makani akiuliza CHADEMA atasema wapo lakinwanapangishwa chama, milioni moja na laki tano kila mwezi wanalipia chama. Kwa

hiyo atashangaa sana, hawa watu siyo wa kututisha sie. Pia kila atakapokuwa akiuliza, ataambiwa basi chama kingine ataambiwa, cha Cheyo Mwenyekiti bado Cheyo; cha Mrema, Mwenyekiti bado Mrema, NCCR Mageuzi ataambiwa bado Mbatia; hawa ndio waje watutishe sisi? Hawa? Akiuliza ataambiwa na Dovutwa bado anaendelea, akiuliza ataambiwa na Lipumba naye ni Mwenyekiti; kwa kweli Mwalimu atashangaa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka niwasihii Watanzania kwamba sisi hatuko hapa kwa ajili ya kushughulika na hawa, hawa wameshajifia jamani, hakuna upinzani nchi hii, wamejifia wao wenywewe kutokana na tabia zao na maisha yao, wamefika mahali wamejua wamegonga ukuta. Kwa hiyo tuisumbuke kabisa na watu hawa na wala viongozi wa Serikali msihangaike na watu hawa, wameshajiu. Mtu kama anakufa kwa asali huna sababu ya kumtilia sumu jamani, unamuacha tu anajifia mwenywewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vichaa walikuwa wamekubaliana watoroke hospitali. Wakakubaliana kwamba wafike getini wamnyonge mlinzi halafu watoroke. Vichaa wale walipofika getini wamkakuta mlinzi hayupo wakasema dili limeharibika turudi; dili limeharibika turudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona namna ambavyo tunafanya siasa za ajabu. Tumeona Serikali ya Awamu ya Tano ikifanya kazi kubwa; inajenga hospitali kila wilaya inajenga vituo vya afya kila jimbo; Wizara ya Maji imeboresha mfumo wake tunaona maji yanapatikana. Kazi yetu sisi ni kuwatieni moyo tu ili muendeleee. Migogoro ya ardhi sasa hivi ukifika kila kona ya nchi yetu inaondolewa. Mimi nasema hivi hakuna sababu ya kuwavunja moyo Waheshimiwa Mawaziri pigeni kazi; Dkt. Mpango pamoja na mwenzako pigeni kazi ili uchumi wa nchi hii uweze kukua na wananchi wapate maendeleo. Hizi rabsha rabsha chache mnazoziskia hizi zisiwapotzee muda; hawa Wabunge mnaowaona humu ndani wamepangishwa chama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwneye hili nataka nimwambie Dkt. Mpango, kuna kodi mpya hutozi hapa, hapa lazima *TRA* watoze kodi mpya. Ni kwamba, Wabunge wa Viti Maalum wa CHADEMA wanalipishwa kodi ya upangaji kwenye chama 1,500,000 kila Mbunge kwa mwezi, kasoro Wabunge wateule wachache tu kama wawili, watatu ambaao nao wakiniudhi nitawataja siku moja hapa, hao hawalipi na sababu mimi nazijua, nao nawaweka kiporo; lakini wengine wote ni wapangaji hawa, wamepanga kwenye chama, wanalipishwa kodi hawa na wasipolipa wanafukuzwa chama. Wabishe si wako hapa mimi naongea vitu vya ukweli, hawa ni wapangaji. Hapa hatuna Wabunge; hapa tunawapangaji wamepangishwa, sasa na sisi tutoze kodi mpya ya mapato ambayo aliywewapangisha anapata ili walipie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Willy Qambalo atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi ajiandae

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Takwimu zinaonesha kwamba nchi hii takriban asilimia 65 ya wakazi wake wanajihuisha na shughuli ya kilimo wengi wao wakiwa maeneo ya vijijiini ukillinganisha na karibu asilimia 97 ambazo tulikuwa nazo miaka ile tunapata uhuru wetu. Sasa hii inatuambia nini, hii inatuambia kwamba kila mwaka asilimia ya watu wanaojihuisha na kilimo inazidi kupungua na matokeo yake tutafika mahali kama ambapo wenzetu *USA* wamefika asilimia mbili ya wakazi wake ndiyo wanaojihuisha na kilimo na masuala ya ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii 65% ya Watanzania inazalisha chakula kwa ajili yake lakini pia inabidi izalishe chakula kwa ile 35% iliyobakia. Pia hii asilimia 65 inatakiwa izalishe mazao ambayo tunataka yaende viwandani. Vilevile hii asilimia 65 inatakiwa izalishe kwa ajili ya mazao ya kuuza nje ili tuweze kupata fedha za kigeni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri ni muhimu sasa tuijulize swali, hii asilimia 65, je, itaweza kufanya haya yote ambayo tunakusudia iende ikayafanye? Takwimu za Serikali bado zinaonesha kuwa asilimia 53 ya Watanzania inalima kwa kutumia jembe la mkono, asilimia 20 ndiyo inayotumia matrekta, asilimia 27 ndiyo inayotumia wanyama kazi. Kwa hiyo utaona ni dhahiri kwamba kwa asilimia hizi jinsi zilivyo kwa sasa ni vigumu sana kufikia hicho ambacho tunakitaka. Ni wazi kwa kutumia jembe la mkono hatutatoka hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa nataka kuishauri Serikali hii, kwamba kama kweli inajali wananchi wake wananchi wake hawa ambao asilimia kubwa wameajiriwa na sekta ya kilimo ni lazima ifanye mapinduzi kwenye kilimo hiki ili basi wazalishe kile ambacho tunatarajia wazalishe. Leo katika nchi hii hakuna mkulima anafuraha; wakulima wa korosho wamenuna, wakulima wa alizeti wamenuna, wa kahawa walikwisha kununa wa mahindi ndiyo hivyo halikadhalika. Kwa hiyo ili mazingira haya ya kilimo yaweze kuvutia ni sharti wakulima wapate kile ambacho kitawasaidia ili waweze kwenda kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado bei ya mazao ya wakulima hali ni mbaya sana. Hebu Serikali tuishauri ikubali kuwaunganisha wakulima na masoko ili waweze kupata fedha ambazo zitawasaidia katika mambo yao lakini pia kuchangia kwenye uchumi wa taifa. Hapo nyuma tulikuwa na mikopo ya matreka kupitia Shirika la SUMA JKT, lakini mikopo ile sasa imefutwa, ukitaka trekta inabidi ulipe *cash* milioni 48, milioni 50. Hivi ni Watanzania wangapi wa vijiji wanauwezo wa wa kulipa shilingi milioni 48 ili waweze kumiliki trekta? Mheshimiwa Mpango wewe ni mkopaji mzuri sana, unakopa nje na unakopa ndani na ndiyo maana Deni la Taifa hadi sasa ni triliioni 51.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba na tunashauri wakulima wakopeshwe matrekta ili wakazalishe vizuri. Kwa majembe yetu ya mikono na kwa kutumia wanyama kazi hatuwezi kutoka hapa ambapo tumefika

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala zima la madeni ya Serikali, kama ambavyo nimesema hapa mbele. Walimu, kada ambayo inafanya kazi katika mazingira magumu sana wanaidai Serikali shilingi bilioni 61. Hizo hela za walimu wapewe. Tunafahamu mazingira ya kazi ni magumu miundombinu na kazi ya ni kidogo, tunaomba Serikali ilipe hela za walimu ili walimu wakafanye kazi na wazalishe elimu ya watoto wetu. Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, dakika tano. Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, atafatiwa na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ajiandae.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya makadirio ya Serikali ya mwaka wa fedha mwaka 2019/2020

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ya nne ya Serikali ya Awamu ya Tano, imeonesha msimamo madhubuti wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wetu Rais John Pombe Magufuli kwa kuendeleza miundombinu ya msingi ili kuwezesha uchumi imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana wakati nachangia Bajeti Kuu ya Serikali nilizungumzia umuhimu wa kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya vijana kujiajiri. Nimefurahishwa sana na uamuzi wa Serikali wa kuamua kufuta kodi kwa muda wa miezi sita; suala hili litapelekea vijana kupata chachu kubwa ya kuweza kujiajiri. Natoa wito kwa vijana wote nchini kuchukua fursa hii; Serikali ina mifuko mbalimbali inayosaidia vijana kutoa mitaji. Mpaka sasa Serikali kuitia vikundi vinavyoendeleza vijana vikundi 775

vimeshapewa mitaji jumla ya bilioni 4.2, kwa hiyo naipongeza sana Serikali yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakuomba kwa unyenyekevu mkubwa; nimesema mara kadhaa hapa Bungeni kwamba Mkao wa Kagera ndio mkoa pekee unaopakana na nchi nyingi Afrika Mashariki. Mkao wa Kagera unapakana nan chi za Uganda, Rwanda pamoja na Burundi. Vilevile kuitia Ziwa Victoria Mkao wa Kagera unaifikia Kenya. Nilikuwa naiomba Serikali yangu sikivu ije na mkakati wa makusudi wa kuufanya Mkao wa Kagera kuwa kituo kikubwa cha biashara. Najua sasa hivi Serikali inatekeleza miradi mikubwa kama barabara, reli na umeme, lakini pia hili la biashara ni kubwa kwa sababu itapelekea nchi yetu kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudhi anazozifanya kutokana na kupinga suala zima la rushwa. Hapo zamani tulipata kusikia kwamba kuna kipindi bajeti ya Serikali asilimia 30 ilipotea kuitia manunuvi. Kwa sasahivi hadithi hii haipo fedha zikipangwa kwenda kwenye shughuli za umma zinafika kwenye shughuli za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa hadithi moja, hii hadithi inasikika sana TBC, nadhani wengi wetu tunajua. Kwamba kulikuwa kuna binti mfalme yupo kilimani kunahitajika mchumba kwenda kumuoa, na sharti lilikuwa, utakapokuwa unakwenda chochote utakachokisikia usigeuke nyuma, pembeni wala nyuma. Kwa hiyo watu wakawa wanapita wakifika katikati wanaskia woowoowoo akigeuka kushoto, kulia anageuka jiwe, kushoto kulia anageuka jiwe. Sasa kuna kijana mmoja ambaye alikuwa jasiri yeche hakugeuka nyuma alitembea moja kwa moja mpaka kule kilimani akamfikia huyo binti mfalme.

Waheshimiwa Wabunge nataka niwaambie kiongozi bora ni yule anayesimamia anachokiamini. Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli huu ni mwaka wa

nne sasa amesimamia kwenye miradi mikubwa anayoitengeneza. Hajatikisa na kelele za ndani wala za nje, ye ye amesimama imara anaelekea kule kukamilisha miradi yake mikubwa, anaenda kumfata binti mfalme, binti mfalme huyo ndiye Tanzania ya viwanda; kwamba atakapokamilisha miradi hii Tanzania ya viwanda itakuwepo. Kwa hiyo naomba sana kumpongeza Mheshimiwa Rais na aendelee na msimamo wake huo na nina wapongeza Mawaziri wote wanaomuwezesha ye ye kufikisha lengo hilo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi atafuatiwa na Mheshimiwa, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Dkt John Pallangyo, Mheshimiwa Angelina Malembeka ajiandae.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hii hotuba ya bajeti ya Waziri Mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na timu yake kwa ujumla; kusema kweli wanafanyakazi nzuri na ni kazi yenye kutukuka. Mimi nikucombe tu Waziri Mpango kwamba mnapoona kule upande wa pili wanajaribu kubeza haya mafanikio wanabeza tu kwa sababu ni utaratibu kwamba lazima wazungumze. Kusema kweli kazi ambayo mnaifanya ni kazi nzuri ni kazi ambayo inawapa matumaini makubwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda mimi ninachowea kusema katika mchango wangu; ni kweli kwamba pamoja na maendeleo yote ambayo yanafanyika lakini Watanzania wangependa kuona huko kukua kwa uchumi kukiwa kunaonekana katika maisha ya kawaida ya watu. Kama hivyo ndivyo labda mimi nichangie tu katika maeneo machache ambayo tunaweza kuyafanya katika mpango wa

muda mfupi, mengine tukaweka kwenye mpango wa muda wa kati, na mengine tukayaweka kwenye mpango wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na mpango wa elimu, nakumbuka mwezi uliopita Mheshimiwa Rais alienda Malawi, akaenda Afrika Kusini, akaenda pamoja na Namibia. Pamoja na mambo mengine aliyokuwa anayazungumzia lakini alikuwa anasisitiza zaidi kuona namna ya kuboresha au Kiswahili kuwa lugha ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Waziri unaweza ukatenga kiasi kidogo cha fedha na kiasi hicho ukakipeleka kwenye ofisi zetu za Ubalozi zile ofisi za Ubalozi zile tukatengeneza tu *crash program* kwa ajili ya walimu wanaofundisha Kiswahili wakawa na vyumba pale kwenye Ubalozi wetu. Kiswahili ambacho nchi zetu za Afrika wanahitaji kufundishwa ni kile cha kujua kusoma na kuandika. Sasa hii *crash program* inaweza ikawa inaanza asubuhi mpaka jioni. Kwa hiyo utajikuta kwamba yale mataifa mengine wanaotaka kujifunza Kiswahili wanajiandikisha pale ubalozini, na walimu wetu wako pale na wanawafundisha. Kwa hiyo tutajikuta kwamba mambo mawili tutayafanikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, tutakuwa tumepata ajira kwa ajili ya walimu wetu kwa ajili ya mpango wa muda mfupi, lakini la pili tutakuwa tumepata mapato. Hilo nalisema; leo ukienda pale *British Council*/pale Posta pale, unakuta unakuta pale Serikali ya Uingereza imeanzisha mfumo huo na kila siku zaidi ya wanafunzi 200 wanapata pale elimu na kwamba wale wanaotaka kujifunza Kiingereza wanajifunza, lakini vile vile Serikali yao inapata kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunadhani kwamba pamoja na mpango wa muda mrefu, lakini naamini kwamba huo ni mpango wa muda mfupi ambao Mheshimiwa Mpango ukuuamua leo tayari ndani ya miezi miwili ni zoezi linaloweza kufanyika na tayari watu wetu wakapata maisha, na mambo yakaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nilipenda nichangie, katika kukuza ajira; maana mojawapo ya kazi yoyote ile ya Serikali, pamoja na mambo mengine lakini ni pamoja na ku-create ajira kwa wananchi wake. Leo ukiangalia tunao vijana wengi wa Kitanzania hawana ajira. Sasa kwenye upande wa kilimo kinaweza kikachukua watu wengi zaidi katika kuwasaidia wakajipatia ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo mojawapo Serikali imeanzisha mpango mzuri wa kuchukua vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kipindi cha miaka miwili. Hivi sasa kuna *in-take* ambayo sasa nadhani kama sikosei huu inaelekeea mwaka wa tatu. Mimi ushauri wangu ni kwamba, wale vijana pamoja na kazi zingine wajikite zaidi kwenye uzalishaji wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili suala la JKT kwanza ni vizuri likawepo katika kila mkoa, na kulekule wakachagua mazao. Pia tusikalie tu yale mazao ambayo tunasubiri soko la dunia liseme, yako mazao ambayo tunaweza kuyauzia katika nchi zetu hizi za Afrika. Kwa mfano leo tukilima zao kama la mpunga tunaweza kuza Kenya, Uganda Rwanda na Zambia. Kwa hiyo basi kama hivyo ndivyo hawa vijana hawa, badala ya kuwaingiza JKT miaka miwili halafu tukawaondoa ni vizuri wakatumia muda mwinge wakazalisha na wakapata mtaji na kwa hiyo tunapowaondoa wawe wamejifunza maisha ya kijeshi lakini vile vile sasa tuwape mitaji ili wakaendelee na maisha yao. Kwa hiyo nadhani hii ni nafasi nzuri ya kuwatumia wale vijana ili waweze kujipatia ajira lakini vile vile waweze kujipatia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi hata leo ukija kwenye mifugo; katika nchi hii tunayo mapori mengi tena ni *ranch* za Serikali. Kwenye zile *ranch* leo ukienda ni miti tu inakua kiasi kwamba hata mifugo haiwezi kuchungwa. Kwa hiyo zile *ranch* zile tukizitumia vizuri; na tunaweza kuzitumia vizuri kwa maana ya kuzikodisha; na katika kuzikodisha leo Watanzania wengi wanayo mifugo, wengi wanafuga lakini hawana mahala pa kufugia. Kwa hiyo zile *ranch* zile tukizikatakata vipande na Serikali

ikawakodishia wananchi, watanenepesha mifugo yao humo na baada ya kunenepesha ile mifugo, tunayo masoko makubwa; kule Comoro kuna soko kubwa sana la mifugo, kule Uarabuni nako soko ni kubwa. Shida moja tu ni kwamba Watanzania wengi hawana mahala pa kufugia mifugo yao, kwa maana ya kunenepesha ili waweze kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ndiyo maana wakati mwininge tunalalamika au watu wetu wanalalamika wanasema uchumi mgumu kwa sababu tu kwamba kuna maeneo ambayo yangeweza kuwachukua *to accommodate* watu wengi lakini hizo fursa wanashindwa kuzipata. Kwa hiyo, naamini kwamba tukitumia na hiyo nayo itawasaidia sana Watanzania wengi kuweza kujipatia uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni eneo la uvuvi, ambalo nalo; leo ukiangalia samaki kama sato wanatakiwa kila mahali lakini uwezo wetu wa *ku-supply* ni mdogo. Kwa hiyo nadhani kwamba haya ni baadhi ya maeneo ambayo leo tukiyasimamia vizuri, yataleta matokeo ya haraka. Baada ya kusema hayo, nakushukuru sana naunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pallangyo tutamalizia na Mheshimiwa Angelina Malembeka.

MHE. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kidogo kwenye hii hoja iliyoko mezani. Nitangulie kwanza kumshukuru Mungu, Baba yetu wa Mbinguni ambaye ndiye ametuamsha salama na kutukutanisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mpango. Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana pamoja na Naibu wako na Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mnafanya, pia kwa bajeti nzuri ambayo mmetuleta ambayo naweza nikai-*brand* kwamba ni *reconciliatory budget*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imegusa miyo ya wananchi wengi ambayo ilikuwa imeinama kwa kukumbana na kero nyingi katika kufanya shughuli zao kwa kuondoa tozo 54 na kuweka *checks and balances* kwenye kodi, kwa kweli bajeti ni nzuri na inastahili kuungwa mkono *hundred percent.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukiona Wizara inafanya vizuri, ina mila ya utendaji wa mamlaka iliyoko juu. Kwa maana hiyo, nasema nampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ambaye amekuwa ni msukumo mkubwa kwenye utekelezaji wa mradi na mambo mengi mazuri ambayo yanaendelea hapa nchini. Amekuwa anatekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa umahiri mkubwa, amekuwa anasukuma utekelezaji wa miradi mikubwa ambayo mwisho siku itaacha historia kubwa sana hapa nchini kwetu; *Stiegler's Gorge, SGR*na ununuzi wa ndege *Air Tanzania.* Haya mambo siyo madogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napata shida kidogo nilipokuwa nasikia Waheshimiwa wengine wanasema kwamba haya ni maendeleo ya vitu badala ya watu. Nikajiuiza, hivi mtu ukijenga nyumba yako nzuri utasema ni maendeleo ya nyumba au ya nani? Nadhani kuna haja ya kujitathmini kidogo kwenye haya mambo kabla hatujasema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo juu ya kilimo. Kilimo bado ni mwajiri mkubwa kwa Watanzania, lakini mpaka sasa sidhani kama tumeweka nguvu ya kutosha. Tumekuwa tunategemea hali ya hewa na hali ya hewa inabadilika mara kwa mara. Matunda yake, wananchi wetu wanalima, wanapata mavuno kidogo. Basi niseme kwamba wakati umefika sasa hivi wa kuweka programu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya mwisho kufanyika ilikuwa ni pragramu ya Kilimo Kwanza. Nadhani wakati umefika sasa wa kuanza pragramu ya *Irrigation Kwanza*, Kilimo cha Umwagiliaji, tuache kutazama mawingu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine llani ya Uchuguzi ya mwaka 2015 ililenga katika kukuza soko la ajira. Katika hilo ilikuwa ni kulinda taasisi zetu. Wizara hii ya fedha ina taasisi nyingi. Nilikuwa napitia makabrasha hapa nikakuta taasisi ya mamlaka ya bima (*TIRA*). Kazi yake hii ni kukuza soko la bima na kulinda migongano ndani ya walengwa na ndani ya wadau. Nimeshuhudia siku za karibuni na taasisi hii *players* wake ni mashirika ya bima, *brokers, loss adjusters* na mawakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibu nimeona kwamba hii taasisi, *TIRA* wanatoa leseni za u-*broker* kwa mabeki. Hii nikaona kama syo sawa, kwa sababu mabenki watafuta ma-*bocker*. Mabenki hawawezi wakashauri wateja kwamba ni bima ya namna gani ambayo inatakiwa ichukuliwe. Kwa ajili hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri *regulations* ziangaliwe ili benki ziwe *restricted* wasipewe u-*broker*, waishie kwenye u-*agent* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza, naomba, kuna somo ndani ya Biblia linamhusu mtoto mpotevu, aliomba haki yake kwa baba yake akapewa akaondoka, akaenda kuzurura mjini, akatumia ile haki yake akamaliza akafilisika, akapata shida, mwisho akaanza kushiriki chakula na nguruwe, akaamua kurudi kwa baba yake kwenda kuomba msamaha; na siku amefika alipokelewa na baba yake vizuri akachinjiwa kondoo na ng'ombe mnono sana akafanyiwa sherehe kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu kule Arumeru Mashariki kwa muda mrefu sana barabara zake hazijatengenezwa, hazipati matengenezo stahiki na ya wakati. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba yake sasa hivi hazipitiki. Naomba unipe ruhusa nimwombe Waziri wa Fedha aangalie namna atakavyomwezesha Waziri wa Ujenzi na TAMISEMI ili ifanyike programu ya barabara, opesheni barabara kule Arumeru Mashariki barabara zile zibadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanajisikia vibaya wakitoka pale Kibaoni King'ori wakifika

Bomang'ombe kuna barabara lami inakwenda milimani, wakifika kwa Sadala kuna barabara ya lami, inakwenda milimani; wakifika Machame kuna barabara ya lami inakwenda milimani; wakija Kibosho kuna barabara ya lami inakwenda milimani; pale Meru hakuna barabara ya lami. Mheshimiwa Mpango nakuomba, nakusihii lile Jimbo sasa hivi ni Jimbo mkakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba kibali unipe nizungumzie hilo kwa sababu nimetoka kwenye lile Jimbo na ninajua hali yake ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba kuunga hoja mkono kwa *percent* mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Angelina Malembeka.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika bajeti hii. Kwanza nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha na timu yake yote. Sambamba hilo, nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anayoifanya hasa ikionyesha wazi kwamba ana nia njema ya kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi kwa manufaa ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Pamoja nakuunga mkono hoja, nataka nimtoe wasiwasi Waziri wa Fedha na timu yake kwamba ndugu zangu tumewazoea, watasema pale, baada ya dakika mbili watgeuka watakuja huku huku, watapita kwa Mawaziri, watawanong'oneza, Jimboni kwangu hakuna maji, Jimboni kwangu nataka shule, Jimboni nataka barabara, wanakuja huku huku. Mimi nakaa hapa hapa wanawaona. Mara wameenda kwa Waziri wa Fedha, mara Waziri wa Ardhi, mara Waziri wa Maji, mara wa TAMISEMI, mimi niko hapa

hana nawatazama; lakini wakipewa fursa ya kuchangia, wao ni hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapana hizi ifike sehemu na sisi tujirekebishe, tusiwe tunapenda mno anaposema hapana tunamlazimisha kumpa kitu. Hii ni bajeti ya nne katika Awamu hii ya Tano. Mara ya kwanza tunesema hapana, tumefanya kazi nchi nzima bila ubaguzi Majimbo yote, kazi imeonekana. Hakuna Jimbo lolote ambalo litasema halina shule ya msingi, halina shule ya sekondari, halina kituo cha afya, hana mwalimu, hana nesi, hana mtendaji, hana mkurugenzi. Hawa wote bajeti yao inapita hapa na tunachangia. Juu ya hilo

TAARIFA

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Angelina Malembeka, kuna taarifa Mheshimiwa Yosepher Komba.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimpe taarifa mama yangu mzungumzaji kwamba maendeleo ambayo yanatokana na bajeti ya humu ndani siyo kwamba ni hisani ya Wabunge na hawapewi Wabunge, bali wanapewa wananchi kutokana na kodi zao. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Angelina Malembeka endelea na mchango wako.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee ila nikukumbushe, kuna wakati tunaingia Bungeni, niliomba Wabunge tukapimwe akili. Matokeo yake tukaletewa semina hapa ya matumizi sijui ya bangi, matumizi ya pombe, matumizi ya sigara, tukaonyeshwa udhaifu wake. Umbali kutoka hapa mpaka kwenda pale kwenye kituo cha wagonjwa wa akili kupima, siyo mbali. Hivi tunapata shida gani kwenda kupimwa akili

sisi Wabunge? Kwa sababu inafika sehemu mtu anaongea lingine, anakupa mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa, hebu nendeni Majimboni kwenu kwanza halafu tuone kama utekelezaji wa ilani haufanyika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuchangia kama ifuatavyo:-

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Angelina Malembaka kuna kanuni inavunjwa. Mheshimiwa Selasini.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa mujibu wa Kkanuni ya 64 (1) (g). Mheshimiwa anasema Wabunge waende kupimwa akili. Sasa hii siyo akili nzuri. Kama ye ye anajisikia akili yake ina matatizo, akapime. Sisi wengine hususan mimi, akili yangu ni nzuri kabisa ni timamu sihitaji kwenda kupima akili Milembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ama afute kauli yake au usaidie afute kauli yake kwa sababu Bunge zima litaonekana kwamba sisi ni vichaa. Au athibitishe kwamba kuna Wabunge humu amba wana akili ambazo siyo nzuri. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Selasini amesimama kuoneshwa kwamba kanuni ya 64 (1) (g) imefunjwa na Mheshimiwa Malembaka kwa kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge akili.

Waheshimiwa Wabunge, ningetamani kama ambavyo huwa nasisitiza siku zote; moja, kuzingatia kanuni zetu; lakini la pili, ni uvumilivu. Haya mambo ya kupimwa akili, kuna wakati kuna Mbunge alishapata kusema

Watanzania wote inabidi wakapimwe akili. Wakati huo haikuonekana kama ni jambo la ajabu Watanzania kuambiwa wakapime akili.

Wakati huo huo sisi Wabunge hapa ni Wawakilishi wa hao wananchi ambao tunawatumia ili wakapime akili. Sasa nakuwa sielewi ni wakati gani kipimo tayari kinakuwa kimeshajulikana kabla hatujaenda.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tuwe tunafuatilia sisi wenyewe michango yetu na maneno tunayoyatumia. Maneno yale ambayo siyo lugha ya Kibunge, hayo yatakuwa yanaondolewa kila wakati. Yale ambayo matumizi yake huwa tunayatumia sisi wenyewe, basi tuwe wavumilivu hata vile ambavyo huwa yanatoka sehemu nytingine.

Mheshimiwa Malembeka, endelea na mchango wako. (*Makof*)

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, tunaendelea kusisitizana kupima afya zetu ikiwemo Malaria, UKIMWI, *TB*, vyote tukapime. Nasi Wabunge ni binadamu kama wengine, lazima tukacheki afya zetu kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama nilivyosema mwanzo, wao mara zote wanachangia, wanakataa, wakishamaliza, wanakuja huku kuomba. Sasa hilo nanyi mliweke sawa, kwamba isifike sehemu sisi ambao tunakuja tunatetea hoja zetu, tunatete kauli zetu na yule ambaye kila siku anapinga, tena anapinga kwa uwazi, halafu tunaonekana wote tupo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo Majimbo ambayo watu kila siku wanasmama hapa wanapiga kelele, lakini Majimbo yao hayajafanyiwa kazi.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Kuna wengine kila kitu wanakataa, lakini wanafanyiwa kazi. Mimi lengo langu kubwa ni kwamba kwa kuwa llani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa nchi nzima, sasa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Malembeka, kuna taarifa.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Sasa wasiwe kila kitu wanakataa. Vile ambavyo wamefanyiwa, wawe wanakubali kuwa...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Malembeka, kuna taarifa. Mheshimiwa Khatib.

TAARIFA

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nampa taarifa mwongeaji kwamba Wabunge wanapowafuata Mawaziri kuomba ni haki yao kwa sababu ni Serikali yao na kodi zinajumlisha Majimbo yao. Hivi ni nani bora...

NAIBU SPIKA: Taarifa ni moja Mheshimiwa Khatib.

MHE. CECIL D. MWAMBE: (*Aliongea nje ya microphone*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil, taarifa ni moja Mheshimiwa Khatib. Mheshimiwa Malembeka, endelea na mchango wako.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kesho ni siku ya kupiga kura na Watanzania wapo wanatuona. Hizo taarifa, taarifa zao wanazotaka kunivuruga ili nisimalize ninayosema, nitayasema mpaka dakika ya mwisho.

MHE. CECIL D. MWAMBE: (*Aliongea nje ya microphone*)

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nilindie muda wangu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Malembeka naomba unyamaze kidogo.

Mheshimiwa Cecil Mwambe, Michango ya harusi sasa hivi inahusikaje? Hebu kuwa mtu mzima kidogo, tafadhali. Hebu kuwa mtu mzima kidogo *for once* tafadhali. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Angelina Malembeka endelea kuchangia na harusi ni wewe unapanga namna ulivyoona; na watu tulio kuchangia tumenyamaza, wanaopiga kelele hata hawakukuchangia.

Mheshimiwa Mbunge, endelea la mchango wako.

MBUNGE FULANI: Rudisha hela wewe mamaa!

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza, siwezi kuchanganyikiwa na kelele ya mtu ye yote kwa sababu havinihusu. Mimi ninaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono moja kwa moja mapendekezo ya Hotuba ya Waziri wa Fedha kwa sababu za kwanza zifuatazo:-

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza katika hotuba yao ya mapendelezo wameelezea kwamba wana nia nzuri ya kupanua wigo wa kodi na usajili wa walipa kodi. Pili, wameelezea nia yao ya dhati kuwekeza kwenye maeneo ambayo Serikali inaweza kupata mapato zaidi ikiwemo katika Sekta ya Uvuvi, ndani ya bahari kuu na ujenzi wa bahari za uvuvi lakini pia katika ununuzi wa meli za uvuvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika mapendekezo hayo nimeona wamelezea ni jinsi gani ambavyo wanaweza wakaongeza ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji wa kodi za ndani. Pamoja na hayo, wameonyesha kwamba wana nia ya dhati kabisa ya kuimarisha uwezo wa ufautiliaji na udhibiti wa uhamishaji wa faida na unaofanywa na makapuni ya nje. Pamoja na hilo, wameelezea nia yao ya dhati kuimarisha mifumo ya ufautiliaji na katika taasisi za Serikali ambazo zinatakiwa zitoe makato yao katika Mfuko Mkuu kwa muda muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wameahidi na wameelezea kwamba wako tayari sasa hivi kuimarisha usimamizi wa misamaha ya kodi ambayo mapato yake yataenda katika miradi ambayo imekusudiwa. Mheshimiwa Waziri, mimi nataka niseme kidogo kwamba katika suala la killimo yamezungumziwa mazao mengi ya mkakati. Naomba niwakumbushe, katika mazao ya mkakati, lipo zao la minazi ambalo wengi hawajalizungumzia. Zao lile ni zao ambalo lipo katika mikoa ya Pwani na limekuwa na faida nyingi sana ikiwemo masuala ya mapambo, mafuta yenye, urembo, dawa na kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi ambao wanavuna minazi sasa ni ile ambayo ilipandwa na mababu zao. Haijaoneshwa msimamo wakati sasa hivi kuonyesha na kuhamisha zao la minazi lipandwe nalo liingie katika biashara kama ilivyo mawese na mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala la Wakandarasi. Wengi wana madeni na tulikuwa tunasisitiza Wakandarasi wa ndani wapewe fursa ya kuwekeza ndani, lakini madeni yale yamekuwa yanawakatisha tamaa. Utakuta wanadai miaka miwili mpaka mitatu. Naomba katika bajeti hii wawaangalie Wakandarasi waweze kulipwa fedha zao ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala zima la taulo za kike. Mimi naunga mkono kwamba kwa kuwa huku zinaingizwa kodi, halafu upande wa pili wawekezaji wa

ndani wanapunguziwa kodi ili waweze kutengeneza taulo za kike, ni vizuri kwa sababu pamoja na kupunguza hizo gharama kwa wanafunzi na akina mama, lakini suala kubwa hapo kuangalia lisiwe kwenye suala la taulo tu tuangalie uwezekano wa kupata maji katika maeneo yao. Kwa sababu hata kama watapewa mataulo, hata kama kodi itapunguzwa, lakini ikiwa maji hamna katika maeneo yale, bado tutakuwa tuna hangaika. Kwa hiyo, suala la maji naomba liwekewe umuhimu sana katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la reli ya kisasa, wapo wanaolalamika kwamba ujenzi wa reli ya kisasa kwamba tunasaidia nchi nyininge badala ya kunufaika sisi Watanzania. Ninaamini kabisa, ujenzi wa reli ya kisasa utatoa ajira kwa Watanzania, lakini pia itatusaidia katika usafiri na katika kuinua uchumi wa nchi yetu. Hili Jambo zuri na kubwa lazima lipongezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie suala la Madiwani. Tunao Madiwani ambao tunafanya nao kazi muda mrefu. Posho zao bado zimeendelea kuwa chini. Naomba katika bajeti hii tungalie Madiwani ili nao waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja tunakutana kesho. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge niwataje Waheshimiwa Wabunge ambao tutaanza nao mchana kati ya hao ambao watakaotajwa sasa hivi. Tunaye Mheshimiwa

Yosepher Komba, tunaye Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Alex Gashaza, Mheshimiwa Rhoda Kunchelwa na Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi. Tutaanza na yeote kati ya hao.

Waheshimiwa Wabunge, nachukua fursa hii kuwaomba radhi, umeme namna unavyokuja na kutoka ni kwa sababu tunahitaji umeme mkubwa sana humu ndani. Sasa kikitokea kidogo shida upande wa *TANESCO* ndiyo tunapata changamoto. Kwa hiyo, nawaomba radhi Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kipindi hicho cha giza kidogo, kwa sababu pitcha zitakuwa hazikuonekana vizuri.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

(Saa 7.10 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Yosepher Komba atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe Mheshimiwa Aida Khenani, ajiandae.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niunge hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani taarifa au hotuba yao ambayo wameitoa hapa wakiwa wanaishauri Serikali kwa mambo mengi na naomba ieleweweke kwamba Kambi ya Upinzani haipingi miradi ambayo inaanizishwa ndani ya nchi hii lakini Kambi ya Upinzani imekuwa ikishauri namna bora ya kutekeleza miradi hiyo.
(Makofu)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Kama Kambi ya Upinzani hatupingi kwa sababu tunaamini miradi ikisimamiwa

vizuri itakuwa na manufaa kwa wananchi wote, kwa hiyo wale ambao wanadhani tunapingga, hatupingi tunashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze na sura ya bajeti, nimesoma Kitabu cha Waziri kwenye ukurasa wake wa 86 ukiangalia sura ya bajeti ina vyanzo mbalimbali ambavyo vinaweza kutengeneza trillioni 33.11 kwanza kuna mapato ya kodi ambayo kwa mwaka jana ilikuwa ni trillioni 17 vyanzo vya ndani vya kodi, mwaka huu imefika trillioni 16.1 lakini tuna mapato yasiyo ya Kodi ambayo ni trillioni 3.18. Tuna mapato yanatokana na Halmashauri ambayo ni bilioni 765.5 kuna mikopo ya masharti nafuu, kuna misaada kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tumekuwa tukisema humu ziko bajeti ambazo zinalenga watu na ziko bajeti ambazo zinalenga vitu, nimechambua kidogo kwenye Bajeti ya Maendeleo, nimeangalia sekta ambazo zinaajiri au zina watu wengi sana zaidi ya asilimia 70, sekta ya afya, elimu, viwanda, kilimo, maji, mifugo na uvuvi. Hizi ni sekta ambazo Watanzania zaidi ya asilimia 70 wanapatikana humo, sekta ya afya imetengewa bilioni 500 sawa na asilimia Nne ya bajeti yote ya maendeleo, elimu imetengewa bilioni 663 sawa na asilimia Saba, lakini viwanda imetengewa bilioni 51.5 sawa na asilimia 0.4, Kilimo imetengewa bilioni 143 sawa na asilimia 1.2 kuna maji na mifugo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijumlisha hizi Wizara ambazo ndizo zenye watu wengi unakuta ina jumla ya trillioni 2.1 ambayo ni sawa na asilimia 17 tu ya Bajeti yote ya Maendeleo, lakini hizi Wizara ambazo zina miradi ile mikubwa zina zaidi ya asilimia 55. Kwa hiyo, tunaposema bajeti ilenge maendeleo ya watu na siyo maendeleo ya vitu hatupingi miradi ambayo inaanizishwa lakini hatuwezi ku-*compromise* afya za wananchi kwa sababu tunajenga *Stiegler's*, hatuwezi ku-*compromise* elimu za Watanzania kwa sababu tunajenga *SGR*. Hivi ni vitu ambavyo vinatakiwa viende sambasamba tunaambiwa tufunge mikanda wananchi wajikaze mazuri

yanakuja, kufunga mikanda tulianza kufunga tangu mwaka 1976 kipindi cha vita ya Uganda, Mwalimu Nyerere alituambia tufunge mikanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba Waziri akija *ku-wind* aniambie vyanzo viyi mmeviandaa vyta kodi ambavyo vita-*push* kodi za ndani kutoka trillioni 17 ambayo mwaka jana mliikusanya kwa mbinde kwa wafanyabiashara kwa nguvu kwa mitutu na hekaheka mpaka kufika trillioni 19, mmeandaa vyanzo gani rafiki kwa wafanyabiashara ambavyo mtakusanya kodi bila kuwasumbua, ambavyo hamtawa-*discourage* katika kufanya zao ili muweze kufikia lengo la trillioni 19. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu suala la Pedi, yamezungumzwa mengi mwaka jana tulishangilia sana, Serikali ilipotoa *VAT* mwaka huu yamerudi tena *VAT* imerudishwa, niseme jambo moja, wakati Serikali inatoa *VAT* kwenye pedi wafanyabiashara wa jumla au *importers* wakubwa walishusha bei, ambao hawakushusha ni wafanyabiashara wa rejareja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Serikali hamkutimiza wajibu wenu katika hili, kama wafanyabiashara wakubwa na *importers* wakubwa walishusha bei, rejareja ndio hawakushusha bei, naamini kwa sababu rejareja ukifuatilia mnyororo wao wa thamani wao wana zaidi ya *profit margin* asilimia 40 na hata wakishuka asilimia 20 ya *profit margin* au 25 bado hawapati hasara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba Serikali Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itoe bei elekezi hamna haja ya kutoa *VAT* kwenye hili suala, watoto wetu wa kike wanapata shida tuendelee kuwasaidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itoe bei elekezi, halafu tuone huyo mfanyabiashara ambaye atakiuka hiyo bei ambayo imetangazwa na Serikali, lakini kitu kingine hili suala, siyo suala la kiuchumi ni suala la kutoa tamko, kama nchi tunaona watoto wetu wanapata shida, wanakosa raha,

wanakosa masomo tuwape nafasi, Serikali itoe tamko hapa. Naomba VAT itolewe kama ilivyotolewa mwaka jana wananchi wetu wafurahie. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Anna Lupembe atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Alex Gashaza ajiandae.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuzungumzia Bajeti yetu ya Taifa kwa siku hii ya leo. Kwanza kabisa ninaomba nimshukuru Mungu aliyetuumba ametupa uzima na uhai leo tunazungumzia bajeti yetu ya Nne kwa ajili ya Awamu ya Tano. Namshukuru sana Mungu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niipongeze sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa sana ambayo imeifanya mpaka leo kupitia miradi mbalimbali ambayo Watanzania wanaona miradi inayoteklezwa na Serikali ya Awamu ya Tano kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ile ya manufaa ya wananchi wa Tanzania kwa sababu inaonekana na pesa ambazo zinapelekwa kwenye miradi ile na ile miradi inaonekana siyo kusema labda haionekani, inaonekana sasa ndio maana watu wanahangaika sana kwa ajili ya hiyo miradi, kwa sababu italeta mafanikio makubwa sana katika nchi yetu na Watanzania watanufaika sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Mtanzania yejote ambaye anafunga mkanda Watanzania wote wameridhika wanafanya kazi zao kwa sababu wamejua wanatakiwa wafanye kazi ili Tanzania iweze kwenda juu na tumeona kabisa jinsi gani Serikali imefanya kazi kubwa na leo hii uchumi wetu umepanda asilimia 7.1. Hongereni sana Serikali msirudishwe nyuma songeni mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu wako, mnafanya kazi nzuri sana na kazi mnayoifanya tunaiona na jitihada mnazozifanya tunaziona na mmekuwa wasikivu tunavyowaelekeza ndiyo mnavyofanya, hongereni sana endeleeni kuwa wasikivu nchi yetu itasonga mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Awamu zote Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ilisema itaunganisha Mikoa kwa ajili ya uchumi, Mkoa kwa Mkoa lazima barabara za lami ziweze kufunguka kwa ajili ya uchumi wa Watanzania, ni jambo zuri na imefanyika tumeona kila sehemu barabara za lami zimejengwa na watu wanafanya shughuli zao za maendeleo, ombi langu katika Mkoa wa Katavi, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi, Mkoa wa Rukwa na Katavi haujaungana kwa lami, kuna kipande kama kilomita 90 hivi bado hakijawekewa lami, nayo ilitakiwa iwekewe lami lakini sasa kuna tatizo kwa sababu ni Mbuga ya Wanyama ya Katavi, sasa katika ile Mbuga yetu, ina barabara mbili kuna barabara iko juu na barabara nyingine iko chini, kuna barabara ambayo inatoka Kizi kwenda Stalike na nyingine ya chini Kibaoni kwenda Stalike.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hapa wanyama wanazaliana sana, lakini tukiangalia upande wa chini huku Kibaoni Stalike ndiko mazalia ya wanyama wanakozaliana na kuna mabwawa mengi na kuna uchumi mkubwa sana kwa ajili ya hiyo barabara, barabara ya kutoka Kizi kwenda Stalike Wanyama ni wachache sana, tunaiomba Serikali kuititia uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Katavi Mkoa wa Katavi, tunaomba katika barabara hiyo moja au ya Kizi - Stalike iwekwe lami ili Mkoa ule uweze kufunguka kwa ajili ya mchumi na kwa sababu sasa hivi Mheshimiwa Waziri nimeona katika vitabu vyako unaelekeza kujenga bandari katika eneo letu la Kalema ili uchumi Mkoa wa Katavi uweze kukua zaidi, naomba ili basi Mkoa wa Katavi uweze kufunguka tuwekewe barabara ya lami kutoka Kizi mpaka Stalike.

Mhesimiwa Naibu Spika, vilevile tuwekewe barabara ya lami kwa sababu hata *Standard Gauge* inakwenda Kalema na bandari inajengwa Kalema na tunashukuru tunaipongeza Serikali gati lile limekwisha na kwenye vitabu vyako Mhesimiwa Waziri umeandika gati limekwisha, sasa hivi ni mwendelezo wa kujenda bandari, kwa sababu ya mazao yote ambayo yanaenda katika nchi yetu ya jirani ya DRC. Naomba tujenge barabara ya lami kutoka Mpanda mpaka Kalema ili *Standard Gauge* itakapofika inakuta barabara ya lami tayari imeshajengwa basi yale mazao ambayo yanatarajwa kwenda kwenye bandari au vifaa mbalimbali vinavyoenda kwenye bandari yetu ya Kalema viweze kwenda.

Mhesimiwa Naibu Spika, vilevile hii barabara kwa nini tunaomba ili uchumi ufunguke kwa sababu bandari ya Kalema ikijengwa mazao yote ambayo yanahitajika kwenda Congo yatapita na barabara ya lami ambayo tayari tutakuwa tumeshaunganisha kile kipande cha Kizi, ambako barabara sasa ya lami itakuwa imeungana ile ya Rukwa Kizi Kibaoni, Kizi Stalike itakuwa imeshakamilika kwa kiwango cha lami, uchumi utakuwa mkubwa sana ndani ya Mkoa wetu wa Katavi ninaomba sana Waziri.

Mhesimiwa Naibu Spika, vilevile tulikuwa tunajua barabara ya lami imeishia Vikunge, tunaomba ili tuweze kufika Kigoma kile kipande cha Vikunge kwenda Uvinza nacho tuwekewe barabara ya lami ili sasa tuunganishe Mkoa wa Katavi pamoja na Mkoa wa Kigoma ili uchumi ndani ya Mkoa wa Katavi uendelee kukua zaidi. (*Makofî*)

Mhesimiwa Naibu Spika, kuhusu mazao ya kibiashara kama tumbaku, pamba, korosho, kahawa ndani ya Mkoa wetu wa Katavi tunalima sana Tumbaku, ninaomba zao hili ndani ya Mkoa wetu wa Katavi limeshuka sana katika na wengine watu wa Tabora wamesema tunaomba Serikali sasa kwa sababu zao hili lilikuwa zao la kibiashara wananchi wa Katavi walikuwa wanalitegemea sana kwa ajili ya uchumi, naomba tuweze kulipangia mkakati

mzuri ambao wananchi wote wanaolima zao hili la Tumbaku waweze kufaidika na kunufaika ili uchumi wa wananchi wa Tanzania wale wanaolima tumbaku waweze kurudisha uchumi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi, hili kila mwaka ninalisemea, tuna Ziwa Tanganyika, kwa wananchi Katavi matatizo ya maji mkitusaidia kama wenzetu wa Ziwa Victoria ambao walipata maji katika Mkoa wa Mwanza, Shinyanga, sasa maji yale yanaenda mpaka Tabora, naomba sana Ziwa hili la Tanganyika nasi watu wa Mkoa wa Katavi litatusaidia sana matatizo ya maji yakaisha kabisa tunaomba tutolewe maji kwenye Ziwa Tanganyika kuletewa ndani ya maeneo yetu ya Mkoa wetu wa Katavi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la *scheme*, tunalima sana na sasa hivi mvua zetu hazitabiriki lakini tuna mabonde mengi makubwa na Awamu zote zilijaribu kutengeneza *scheme* mbalimbali, kuna *scheme* ambazo zilitengenezwa zikatoa manufaa makubwa sana, naomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ijkite kwenye *scheme* ili kilimo cha umwagiliaji kiweze kufuatiiliwa kwa undani zaidi, kitaleta manufaa makubwa na tija ndani ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Serikali yangu sikivu, umwagiliaji sasa ndiyo utatutoa, utaleta tija kwa sababu katika mabonde yetu tayari kuna unyevunyevu na mvuke mvuke, ule mvuke utatusaidia na kuweka utaalami mkubwa kwenye ulimaji wa mazao mbalimbali kuititia mabonde yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mabonde yetu Mkoa wa Katavi tuna mabonde mengi tunaona jinsi gani wananchi wanajitahidi kuititia hayo maji ya kuchotelea kwenye vikopo wakamwagilia lakini wanatoa mazao. Serikali ikiingiza nguvu yake katika *scheme* mbalimbali katika nchi yetu nafikiri tutapata manufaa makubwa sana na ukombozi wa Kilimo katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna tatizo *TRA*, leo hii kuna ndugu yangu mmoja ameenda *TRA* amehangahishwa kupata *TIN* amefungua kampuni mpya ili apate *TIN*, leo siku ya saba kupata *TIN*, huko *TRA* kuna tatizo gani, *TIN* inatolewa siku moja na ana kila kitu kafungua Kampuni ana vigezo vyote lakini leo anakwenda siku ya saba anaambiwa bado sijui hujaleta sijui hiki, hujaleta hiki, sasa kwa nini siku ya kwanza wasimwambie, wasimwandikie vitu vyote *TRA*? Imeshakuwa usumbufu *TRA* mpaka yule Dada akaanza kuwafokea watu wa *TRA* anasema ninyi Vijana ndiyo mnaowafanya hawa watu wakubwa wanatumbuliwa kila siku kwa ajili yenu ninyi. Ninaomba bado huyu Kamishna mpya bado ana kazi kwa sababu bado Vijana wako hawajaelewa somo. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Aida Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Alex Gashaza, Mheshimiwa Rhoda Kunchela ajiandae.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ninamshukuru Mungu nami kupata nafasi kuchangia bajeti muhimu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yoyote makini ina kipaumbele, Serikali yoyote makini kipaumbele chake ni kipaumbele cha wananchi wake. Tunapozungumza hapa bajeti iliyopita na bajeti hii tunawatazama Watanzania ambao wametupa dhamana leo tunazungumzia hali ya uchumi kwenye vitabu kila siku inaonekana uchumi unakua lakini ukienda kwenye uhalsia hali ya Watanzania inazidi kuwa mbaya hasa katika hii Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali ni vizuri takwimu hizi zinazoongezeka kwenye vitabu zipelekwe kwenye uhalsia wa maisha ya Watanzania na baada ya

kupeleka huko na haya mambo yote itaonekana kama yana ufanisi endapo utawala bora utazingatia Sheria ndani ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo watakaosema kwamba Serikali imefanya nini Watanzania kuititia Wawakilishi. Kwa mujibu wa Katiba tuna haki ya kufanya mikutano kuwaeleza Watanzania nini kinaendelea kwenye nchi hii. Mikutano imezuiliwa, kwa hiyo ninyi mtatengeneza wenyewe na mtakuja kujisifia wenyewe, lengo letu ni moja kuijenga nchi yetu, pelekeni takwimu hizi ziende kwenye uhalsia kwa Watanzania, maisha ya Watanzania bado ni magumu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosababisha uchumi wa nchi hii uonekane bado ni butu, ni kero zinazoendelea kuhusu tozo na ushuru ambaao unakuwepo kuanzia kwenye bandari na maeneo mbalimbali. Nitolee mfano mmoja tu, leo ukiagiza gari kwa milioni kumi na moja, mpaka ukaichukue pale bandarini bei yake inafanana na ile ulioagizia.

MBUNGE FULANI: Kweli. (*Makof*)

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nini tunafanya? Ukiangalia kero ambazo wafanyabiashara walienda kuzungumza ikulu kwa Mheshimiwa Rais inaonesha ni jinsi gani Wabunge tumeshindwa kutimiza wajibu wetu. Zile ni kero ambazo wanazipata Wafanyabiashara na kama unataka kukuza uchumi wa nchi yetu lazima tuangalie watu ambaao wanaweza kukuza uchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza wanazungumzia kilimo ambacho ndiyo kinaajiri vijana wengi na watu wengi kwenye Taifa letu, tumejipangaje kwenye kilimo chetu. Serikali ya Awamu ya Tano ilikuja na *slogan* ya Serikali ya Viwanda, tumejipangaje kwenda kwenye viwanda, ni lazima tuboreshe kilimo nchini. Leo tunapozungumzia kilimo hali ni ngumu sana kulingana na pembejeo ambazo wakulima hawawezi gharama bado ni kubwa sana, kama

slogan ni Serikali ya Viwanda lazima tuwekeze kwenye viwanda, viwanda hivyo vikijengwa nchini vitapunguza gharama za pembejeo ambazo zitawaidia Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama pembejeo bado ni ghali kwa wakulima hawa lakini rudi kwenye hali halisi ya soko ambayo ni wajibu wa Serikali kuhakikisha inatafuta masoko kwa hawa wakulima, bado Serikali haijajikita kutafuta masoko. Ushauri wangu, tunatumiae Muungano wetu wana Umoja wa Afrika Mashariki kuweza kuuza mazao yetu ambayo wanaweza kuyalima Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilliona kwenye hotuba kuna tozo zimeondolewa lakini ukitazama sekta ya uvuvi halijaguswa kabisa. Hawa wavuvi wanapata leseni kutoka Serikalini na wanalipa kodi inakuwaje wao wasiguswe na wana kero nyingi sana kwenye nchi hii? Tusijivunie kukusanya kodi bali tujivunie kutengeneza mazingira rafiki kwa wavuvi na wakulima wetu, hapo ndiyo tutazungumzia ukuaji wa uchumi ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa napozungumza leo ziwa tunalotumia sisi la Ziwa Tanganyika suala la usafirishaji ni mgumu. Nategemea Serikali itakuja ituambie hapa suala la MV Liemba mmeefikia wapi mpaka sasa ambapo ni usafiri ambao utatusaidia kwenda kuuza mazao yetu Burundi, Congo na maeneo mengine, hiyo mtakuwa mmetusaidia kama Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini tumejipanga sisi kukusanya kodi kwa hawa wavuvi badala ya kujipanga kuwatafutia masoko kwanza. Hawa Watanzania leo kama mkulima na mvuvi analia, huo uchumi unakua kutoka wapi? Ni vizuri Serikali ikaangalia Watanzania hawa, kama tunataka kukusanya kodi na wao waone faida ya kodi wanazozitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Alex Gashaza atafuatiwa na Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Flatei Massay ajiandae

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti kuu ya Serikali na hali ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kuwapongeza viongozi wetu; Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mipango, Naibu Waziri, Dkt. Ashatu Kijaji, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Mlinga alipokuwa akichangia alijaribu kuonyesha jinsi ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano inavyofanya kazi katika kutekeleza llani. Wenzetu walijinasibu kwamba hiyo ni llani yao lakini naomba niwarejeshe kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi, kuanzia ukurasa ule wa 36 – 80, kwa maana ya Sura ya Tatu inaeleza jinsi ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaenda kuboresha huduma na miundombinu ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara, reli, kuimarisha huduma za usafiri wa anga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inatekeleza llani ya Uchaguzi. Kama walivyosema kwamba walichokifanya ilikuwa ni ku-copyna ku-paste mtakumbuka wakati wa uzinduzi wa kampeni mwaka 2015, walisema kwamba llani yao wananchi wataikuta kwenye website, hawakuwa na llani mezani. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata
utaratibu)*

MHE. ALEX R. GASHAZA: Kwa hiyo, nimeona hili niliweke wazi ili kujua kwamba tunatekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2015-2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha kwamba ifikapo 2025 tunafikia uchumi wa kati. Ili tuweze kufikia uchumi wa kati, ni lazima kujikita kuwekeza katika sekta nyeti ambazo zitatufanya tuweze kutoa ajira kwa wingi pia tuweze kukuza kipato cha Taifa na cha mtu mmoja mmoja. Lazima tuwekeze kwenye sekta ya kilimo kwa sababu hakuna namna ambavyo tunaweza tukawa na uchumi wa viwanda kama hatujawa na uwekezaji mzuri kwenye sekta ya kilimo, hatujatengeneza mazingira rafiki ya kufanya biashara, hatujaweza kuwa na vyanzo vyta mitaji kwa maana ya kuwa na mikopo ya bei nafuu. Kwa hiyo, nipongeze Serikali kwamba katika mpango wake wa bajeti hii ya 2019/2020 wamejaribu kuangalia maeneo yote hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba katika sekta ya kilimo tumefanya vizuri kwa maana ya kwamba ni miongoni mwa sekta ambazo zimechangia kwenye pato la Taifa kwa asilimia 28.2 lakini bado unaweza ukaona kwamba tuna fursa kubwa ya kuongeza pato la Taifa kupitia sekta hii ya kilimo kwa sababu yapo maeneo ambayo tulitakiwa tuweze kuyafanya kazi hususani eneo la umwagiliaji ni asilimia isiyozidi 6 tu kwenye maeneo yanayofaa kwa ajili ya umwagiliaji ambayo tumeweza kufanya. Kwa hiyo, bado tunayo nafasi, ukizingatia kwamba kuna mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanaathiri hali ya upatikanaji wa mvua na hali ya ardhi ni vizuri sasa tukajikita kwenye kilimo cha umwagiliaji ili maeneo haya yaliyobaki takribani hekta karibu 20,000 zinazofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji tujikite huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuendelea lazima pia tuwe na Taifa ambalo limeendelea na ili tuweze kuendelea lazima tuwekeze kwenye elimu, hususani elimu ile ambayo itamwezesha pia mtu mmoja mmoja kuweza kujiajiri. Leo tunaona jinsi ambavyo vijana wanamaliza chuo kikuu na kushindwa kujiajiri. Najua kwamba katika michepuo tunayoenda nayo sasa ya masomo ya sayansi, kilimo na biashara lakini nishauri kwamba katika kuboresha elimu tujikite pia katika *vocational training* kwa maana ya kuboresha na kupanua wigo wa kuwa na vyuo vyta *VETA*. Pamoja na

kwamba Serikali imeweza kuonyesha jitihada na kuboresha vyuo vya *FDC*'skwa maana ya vyuo vya maendeleo ya Taifa takribani 54 lakini bado havitoshelezi. Kwa hiyo, nashauri kwamba tuendelee kupanua wigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata katika masomo yale ya kawaida kwenye zile taasisi ambazo ni za sanaa na sayansi, kwa sababu tunalenga kutengeneza elimu ambayo itamfanya mwananchi au vijana wetu waweze kujiajiri basi tuone uwezekano wa kuingiza somo la *entrepreneurship* katika kila tahasusi. Kwa mfano, badala ya masomo ya sanaa kwa maana ya HGL, HGK unaweza ukasema HEL au HEG, hizi tahasusi zipo katika nchi za *East Africa Community* kwa mfano Rwanda, Uganda na Kenya. Masomo haya yanawasaidia angalau anayemaliza kidato cha nne, kidato cha sita hata chuo kikuu kuwa na *basic* ya somo la *entrepreneurship* ambalo litamfanya aweze kupambana na hali yake anapokuwa akisubiri suala la ajira anaweza akajajiri mwenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye upande wa miundombinu, miundombinu ya barabara na reli ni muhimu sana kwa ajili ya kuongeza au kuinua uchumi wa Tanzania. Nipongeze kwa jitihada za kuanza ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* ambayo itatoka Dar es Salaam kuja Isaka na matawi yake kwenda Tabora - Msongati - Mwanza pia kwenda Keza - Kigali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, reli hii ni muhimu hususani katika eneo la Ngara ambapo kuna *deposit* kubwa *nickel*, kama reli hii ikijengwa na mgodi wa *Nickel*/ukaweza kuanza utaweza kufanya reli hii iwe na tija kwa sababu mzigo utakaosafirishwa ni mkubwa na ambao unaweza ukasaidia katika kuhakikisha kwamba deni ambalo tunakuwa tumekopa kwa ajili ya ujenzi wa reli hii basi liweze kurudishwa kwa haraka kutohana na biashara ambayo tutakuwa tukiifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye upande wa *feeder roads* ambazo ziko chini ya *TARURA*, barabara hizi ni

muhimu. Tunajua kwamba tunapowekeza kwenye kilimo, maeneo ya kilimo yako vijiji na ambako tunahitaji barabara safi na bora kwa ajili ya usafirishaji wa mazao kuyapeleka sokoni. Kwa hiyo, niombe kwamba katika maeneo ya Halmashauri zetu *TARURA* iweze kusimamia na kuangalia barabara ambazo ni za kipaumbele kwa kushirikiana na Halmashauri zetu ili kusudi barabara hizi ziweze kuboreshwa na hatimaye wananchi waweze kunufaika na uwekezaji katika barabara hizi kwa ajili ya kusafirisha mazao yao kupeleka sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata soko la mazao yao yameanzishwa masoko ya mipakani. Ngara ni mionganini mwa Wilaya ambayo iko mpakani mwa Rwanda na Burundi na lipo soko ambalo lilianzishwa la mpakani la Nzaza tangu mwaka 2013 liliipoanzishwa mpaka leo bado halijakamiliika. Tunaomba miradi hii ambayo imeanzishwa kimkakati kwa lengo la kutengeneza masoko ya ndani basi iweze kukamilika ili wananchi waweze kupata maeneo ya kuweza kuuza biashara zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Rhoda Kunchela atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Massay na Mheshimiwa Muhammed Amour ajiandae.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda mbali zaidi, nilitaka nifahamu kupitia bajeti hii uamuzi wa Serikali kutangaza safari za ndege za *ATCL* na kuanzisha safari za kwenda South Africa wakati tulitegemea ili kukuza masuala ya utalii kwenye sekta hii mngeweza kuweka vipaumbele katika nchi ambazo zinaingiza watalii wengi. Tukiangalia South Africa ni nchi ya 8 katil ya nchi 15 duniani, sasa kupeleka ndege kwenye nchi ya 8 na kuacha nchi kama Kenya,

Marekani, Burundi jambo hili nilitaka nifahamu kwa kina Serikali ilikuwa inapanga kukuza sekta gani kama siyo kukuza sekta ya utalii kuititia huu uboreshaji wa masuala ya ndege kwenye Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la vitambulisho ambalo Wabunge wameliongelea kwa upana wake linawaumiza sana Watanzania. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha ili tufahamu, kwa sababu huku mikoani kumekuwa na kero kubwa, akinamama wanateseka sana kwa sababu Serikali bado haijatoa mwongozo wa moja kwa moja kuonyesha nani mhusika anatakiwa hicho kitambulisho cha Sh.20,000. Akinamama wanamwagiwa samaki, hata hawa Mgambo badala ya kuwaelimisha akina mama wengine wamekuwa wanapigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wangu wa Katavi ukienda Kasokola, Kakese, Mpanda Vijijini, Ikola, Inyonga na maeneo mengine watu wanalazimishwa vitambulisho, imekuwa ni kero akinamama wanashindwa kwenda kwenye masoko yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa hivi ukienda kwenye masoko ya Mpanda Hoteli, soko kuu, Mishano akina mama wanashindwa kupeleka biashara zao. Mkuu wa Mkoa sasa amekuwa ndiyo kero, ndiyo kama mfalme pale, kulazimisha akina mama kuchukua vitambulisho. Watu wanatishiwa na Wanajeshi na Polisi, Serikali mna mpango gani kusaidia hili kundi ambalo mnasema ni la wanyonge? Mheshimiwa Waziri, mwalimu wangu, atakapokuja kuhitimisha atueleze maana amekuwa na matamko ambayo hayaeleweki, hususani sasa ni nani mlengwa wa hivi vitambulisho vya ujasiriamali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la bodaboda na bajaj, nataka kufahamu kwenye ulipaji wa *TRA* kwa sababu kwa Mpanda wanalipa *TRA* lakin wamelazimishwa kuwa vitambulisho. Nataka nifahamu ni bodaboda na bajaji nchi nzima wanatakiwa kulipa *TRA* au ni wa Mpanda Mjini

tu? Nataka kufahamu kwenye masuala ya makusanyo ya kodi jambo hili liko nchi nzima au ni Mkoa wa Katavi peke yake kwa kuwalenga hawa madereva wa bajaji pamoja na bodaboda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tumbaku ambalo kimsingi Mkoa wa Katavi ni wakulima wa tumbaku na ukiangalia kwenye Jimbo la Katavi, Mpanda Mjini na Tanganyika ni maeneo ambayo yanajikita zaidi katika zao la tumbaku. Wakulima hawa 2016/2017 na 2017/2018 kumekuwa na malalamiko mengi kwenye hivi vyama vyaa ushirika hususani katika Chama cha Msingi cha Ukonongo Kilichopo katika Jimbo la Katavi na Chama cha Msingi cha Mpanda Kati. Wakulima hawa wamekuwa na malalamiko mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kufahamu kwa sababu watu hawa ni kundi kubwa na wanapoteza pesa nyingi sana kwenye masuala ya urasimu katika mauzo ya tumbaku. Kuna shilingi milioni 315 zimeibiwa na hiki Chama cha Mpanda Kati lakini mpaka sasa haijulikani ziko wapi. Hiki kikundi cha hawa wanachama wa Chama cha Msingi Mpanda Kati wamekuwa wakihangaika kwa muda mrefu. Ofisi ya Waziri Mkuu ina taarifa ya wizi huu wa zaidi ya shilingi milioni 315 lakini kuna wizi wa fedha zaidi ya shilingi milioni 400 kwenye Chama cha Msingi Ukonongo katika Jimbo la Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashindwa kuendelea mbele kwa sababu kila tukitoa mbinu ya kutatua changamoto hizi kwa wakulima na wananchi ambao Serikali hii inajinadi kwamba inasaidia wanyonge hatuoni mrejesho wa moja kwa moja kuwasaidia hawa wakulima ambao ndiyo kundi kubwa. Naomba mambo haya yazingatiwe pia tuone namna gani tunawasadia hawa wakulima, wafanyabiashara wadogo ambao ndiyo walipa kodi na mpunguze tozo ambazo zinawanyima usingizi Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Flatei Massay atafuatiwa na Mheshimiwa Muhammed Amour na Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi ajiandae.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kushukuru Mungu kupata nafasi hii lakini pili nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu ambaye kimsingi anatenda vizuri sana na Waheshimiwa Mawaziri wake hasa Waziri Mpango na Naibu wake, mtani wangu, Naibu Waziri wa Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, usiposema ukweli hautajulikana. Miradi hii ambayo nimeisoma hapa katika hali hii ya uchumi na imeelezwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri. Naomba tu leo nisome mistari ya Biblia kutoka Yohana 20:27, inasema: "Kisha akamwambia Tomaso, leta hapa kidole chako; uitazame mikono yangu; ulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu, wala usiwe asiyeamini, bali aaminiye". Haya ni maneno ya Yesu mwenyewe wakati anawaeleza Mitume wake ambao hawakuamini mambo ambayo yalikuwa yanatendeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Dkt. Mpango maneno haya yampe faraja huko anakoelekea maana ni vigumu sana kwa wengine kueleza habari ya *Stigler's, SGR* au ndege. Hii ni miradi ya kimkakati ambayo imesemwa na nchi hii ili kuipeleka nchi yetu kwenye uchumi wa kati, hali hii isipokuwepo namna gani tutaendelea? Kwa hiyo, mimi nikupongeze naendelea hivyo hivyo. Najua wengine watakwambia acha hii, watabeza sana lakini maneno haya ya Biblia kutoka Yohana yaendelee kukutia moyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukupa moyo sasa nijielekeze kwenye kilimo. Kwa kweli nipongeze walau kwa namna fulani mwaka huu imeonyeshwa jinsi ambavyo tutaelekea kwenye eneo hili la kilimo. Asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania wanategemea sana kilimo na

ukiangalia imeanza kupanda kutoka asilimia tatu kwenda asilimia nne. Sasa basi ni vyema tukaelekeza mipangilio yetu katika eneo hili la kilimo kwa sababu ukiangalia ipo miradi mingi ambayo inatekelezwa hasa masuala ya mabwawa ambapo mengine yamefanya kazi lakini mengine bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kulingana na nchi yetu hatuna mvua za kila mara, mvua zetu zinahesabika ni wakati wa masika, tukiwekeza katika mabwawa kilimo chetu kitakuwa na uhakika kwa sababu tutanyeshea wakati mvua hakuna. Kwa maana hiyo basi, Serikali ikijielekeza katika kujenga mabwawa mengi ni wazi kwamba baadaye wakulima wetu wanaweza kuendelea kulima kilimo cha kumwagilia ambacho kina uhakika wa kupata maji na hivyo tukaweza kusonga mbele zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule jimboni nina bwawa moja ambalo kimsingi lina shilingi bilioni moja lakini bado halijakamilika linahitaji shilingi milioni mia nne (400) tu. Kwa msingi huu, kama Serikali ikijielekeza moja kwa moja katika eneo hili la mabwawa ikamalizia mabwawa yote ambayo imeshaamua kuyajenga basi asilimia tatu kwenda nne itakuwa tano kwenda sita. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ijielekeze upande huu kwa sababu ndiyo maeneo ambayo ukigusa utakuwa umesaidia pia katika eneo hili la kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nishukuru sana Serikali na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa eneo hili la afya. Kwa eneo la afya mambo yameenda vizuri hata kama siyo kwa asilimia 100, vituo vya afya na hospitali zimejengwa lakini niombe sasa tujielekeze katika vifaa tiba. Tukishapata vifaa tiba Tanzania itakuwa imesaidika sana kwani Watanzania watapata afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, tuongeze pia watumishi, wafanyakazi wakishapatikana kwenye maeneo haya basi Tanzania tutasonga mbele. Sehemu ambayo ina mkosi yaani inasababisha kushuka kwa uchumi wa kawaida

wa mtu mmoja kule vijiji ni habari ya afya kwa sababu ni ghali lakini tukijielekeza kwenye vifaa tiba na watumishi Tanzania itakwenda mbele sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka kusemea habari ya miradi ya maji, tunajua wazi kwamba miradi ya maji tumeiahidi kwenye ilani ya Uchaguzi na kwa maeneo mengi imetekelezwa lakini yako maeneo machache ambayo kimsingi utakumbuka wakati wa kampeni tulisema tunamtua mama ndoo kichwani. Hii inawezekana ikiwa tu pale ambako miradi hii itatembelewa kwa ukaribu sana na Watendaji wa Serikali. Iko miradi mingine imekaa kwa muda mrefu na hata kwenye jumbo langu lipo na iko mingi lakini tukielekeza maeneo haya tukaweka usimamizi wa kutosha ni wazi miradi hii itakwisha na Tanzania wananchi watapata maji na asilimia ambayo inaonekana hapa itaongezeka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalopenda kusema ni habari ya mgawanyo wa *TARURA* na *TANROADS* kwa 30% kwa 70%. Niombe, ipandisheni asilimia hii kutoka 30 kwenda hata 40% au 50% ili walau barabara za vijiji zikaweza kupitika na baadaye malighafi kwa sababu inatoka vijiji iweze kufika mjini. Tukifanya hivyo basi ni wazi kwamba uchumi wa Tanzania utapanda na hali kadhalika barabara zetu zitakwenda mbele. Mheshimiwa Mpango nikuombe sasa, kuna barabara ya Mbulu – Haydom – Sibiti; hii kwa kweli mara nyingi nimejaribu kuisema nimeomba kweli kweli, nimeona mambo yameshakuwa mazuri, imeshafanyiwa upembuzi yakinifu, imeanza kuwekewa fedha, mwaka huu nikuombe ioneokane walau kwenye mipango yako basi. Ikiwekewa fedha na katika hali hiyo ukituwekea fedha bwana utakuwa umefufua eneo ambalo kwa kweli kwa uchumi wa Kanda yetu kule utakuwa umefungua sana na nina hakika katika hali hiyo mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ajili ya elimu bure. Eneo hili la elimu bure hata kama hauoni kwa macho hakika sasa hivi ukiangalia wanafunzi au watoto wengi wameandikishwa shulenii wengi

sana. Hebu fikiri kama Mheshimiwa Rais asinge *support* hii elimu kuwa bure watoto wangapi wangebaki kule vijiji ni hawana namna ya kujitosa katika elimu. Kwa hiyo ukialgangalia kiwango kile cha watoto waliojiandikisha mwaka wa awali, ni wazi kwamba tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa sababu amefanya kazi kubwa sana. Na hii ndugu zangu wapendwa kama hamuoni mtaona wapi? Ni vema tukawapongeza pia Serikali hii, kwa kweli Rais huyu ameamua kufanya kweli na hii kweli yake tumpe *big up* sana na iko katika llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa kweli nielezee habari ya *REA*, ukweli ni kwamba Serikali inafanya vizuri kwa upande wa *REA*. Kwa kweli katika hali hii Tanzania itakwenda mbele, sisi vijiji ni sasa hivi tunapata umeme ni wazi kwamba tuipongeze na kuisaidia Serikali yetu iweze kwenda mbele zaidi. Zipo changamoto chache, kuna maeneo machache tu ambako *REA* haikufika wakandarasi wanakosa fedha, kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango elekeza mipango hii pale ili *REA* nao iende mbele zaidi vijiji viwe vingi na hatimaye pawe na kile kinachoitwa ujazilizo katika maeneo yetu. Maana yake maeneo ya vijiji ni sasa hivi kwa bahati mbaya sana imefika kwenye maeneo ya Kata tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri pamoja na mipango hii ikielekea na namna hii kufika mwaka 2020/2021 tutakuwa tumefika maeneo mengi sana na wananchi watakuwa wamepata umeme. Leo hii *Television* zinaonekana vijiji jambo ambalo kwa miaka iliyopita ilikuwa hakuna, kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais nakuombea Mungu akubariki sana uendelee mbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana ahsante sana kwa mchango naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mohammed Amour atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Lucia Mlowe ajiandae.

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakushukuru kunipatia fursa ya kuchangia bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/2020. Kwanza nitoe pongezi kwa hotuba nzuri sana kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni jinsi ilivyosheheni ushauri mzuri sana kwa Serikali. Pia kabla sijaendelea na mchango wangu naomba niikumbushe Serikali ile ahadi tulyotoa kwamba tutawapatia wana vijiji wetu milioni 50 kila kijiji katika Tanzania hii ule wakati wa kutoa ndiyo huu. Watanzania wana msemu wao wanasesma, ahadi ni deni kwa muungwana na muungwana ni kitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo nianze rasmi, kwanza nitaanza na elimu, elimu ndiyo mwanzo kuliko kila kitu na hapa nataka kuzungumzia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na ucheleweshwaji mkubwa sana wanaopatiwa vijana wetu hawa wanaoanza chuo. Wale vijana wanaomba mikopo baada ya kuomba na kupata uhakika wa kuijunga na vyuo. Wanapoombaa mikopo kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu nao wanaarifiwa kwamba mkopo umepata lakini inafika wakati wanaenda chuo ile mikopo bado hawajapata. Wanaka wiki tatu, mwezi mmoja; sasa je, muda ule wote watapata wapi fedha ya kujikimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari kwa maslahi ya hao vijana wetu, mimi niiombe Serikali kwa heshima zote ifikirie tena wale vijana *once wakiripoti tu pale chuoni basi siku ya kwanza, ya pili, sana sana ya siku ya tatu basi zile akaunti zao ziseme*. Ile mikopo yao wapewe ili waweze kuwa na utulivu wasome vizuri pale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia vizuri sana kitabu cha bajeti lakini bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano siyo *sensitive* kwa Zanzibar, haitaji kabisa Zanzibar. Naomba uniongeze dakika mbili, tatu labda turudi kwenye historia tuangalie kwani hii Tanzania ni nini? Na Tanzania ni akina nani hasa? Kwa kipindi kirefu hakukuwa na Taifa linaloitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni *two Independent Sovereign States* endizo zilizokuja kwenye shirkisho

zikaunda *Tanzania United Republic* of Jamhuri ya watu wa Tanganyika na Jamhuri ya watu wa Tanganyika wakaungana pamoja wakatengeneza Jamhuri ya watu wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mbele ya hii Jamhuri ya watu wa Tanzania kuna Mamlaka tatu hapa *separately*. Kwanza Zanzibar na Tanganyika walikubali kusalimisha baadhi ya mamlaka yao wakayaweka pamoja wakasema haya ndiyo mambo tutakayoshirikiana katika Muungano, Nataka kuzungumzia haya. Pia kuna mambo mengine yakabaki Tanganyika, wao watafanya peke yao lakini *still* yatasimamiwa na Serikali ya Muungano, hayo ni ya kwao peke yao Tanganyika. Kwa upande wa Zanzibar wao watasimamia yale mambo yaliyokuwa si ya Muungano kwa upande wa Zanzibar yatasimamiwa na SMZ. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kuzungumza hiki kikapu cha pamoja hiki, hapa ndiyo bajeti haiku *sensitive* na Zanzibar. Ukienda bandarini pale Zanzibar, nianzie hapa Dar es Salaam kwanza, ukienda pale kuna maboresho mengi sana kabisa ya bandari yanafanywa, ni *Union meter* ile. Ni jambo jema, zuri nalipongeza kwa kweli, tulikuwa tunapendelea tuone kwamba na Zanzibar mambo kama yale yanafanywa. Ukienda uwanja wa ndege Dar es Salaam *the reserve hall room*, ukienda uwanja wa ndege Zanzibar umeachwa kama kwamba wenyewe hawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wapi tunakwenda watanzania, Baba wa Taifa alisema hapa, umoja na nguvu na utengano ni udhaifu. Kwa hivyo mnatutenga, narudia kusema hapa miradi mingi sana ya kimaendeleo hata yale ya Muungano yanafanywa upande mmoja tu wa muungano na upande wa pili unaachwa kama kwamba wao siyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tu Waziri wa fedha kule Zanzibar anawasilisha bajeti yake kwenye Baraza la Wawakilishi kalitamka hili, kwamba wenzetu wametukalia

pabaya kwenye uchumi, tunapotaka kuomba mikopo wanakataa kutupa *loan guarantee*. Juzi hapa kuna Mbunge mmoja alichangia akakuletea hii *document* ambayo Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mpango alikataa kusaini na akamwambia yule mjumbe hapa, Mheshimiwa Dkt. Mpango una roho mbaya sana alimwambia hivyo. Sasa siweze kusema hivyo lakini kama utaratibu utakuwa ndiyo huu na nyingine tunayo hapa kama hiyo ya mwaka 2014. Wakati ule sijui Waziri wa Fedha alikuwa nani, naye alikataa kusaini, sasa kama *trend* itakuwa ndiyo hii hata ile sifa ya kuambiwa Waziri Mpango una roho mbaya itakuwa haikutoshi, labda tufikirie msamiati mwingine tukupatie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo niseme naiomba Serikali kwa heshima zote, kwa heshima zote, kwa heshima zote. Najua Mheshimia Waziri Dkt. Mpango wala huna roho mbaya ni mtu mzuri, kule Zanzibar kuna ndugu zako kule na wewe unelewa hilo. Kwa hivyo nikuombe ukae na Waziri mwenzako wa SMZ mfikirie namna gani itapatikana mikopo ya namna kama hii mnakaa pamoja, mnazungumza ili ile mikopo Zanzibar nayo ipate. Au mtataka wale watu kule wafe? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende 4.5 ambayo Zanzibar inapata kutoka Serikali ya Muungano. Wakati *East Africa Currency Board* inavunjika Zanzibar ilikuwa inachangia karibu asilimia 11, tukatengeneza BoT, BoT kule sisi kuna mitaji wetu Zanzibar, tukakubaliana tupewe 4.5 siyo mbaya. Kwa hiyo, wakati ule ilikuwa inatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa *demand* ni kubwa sana, *population* inaongezeka kwa kiasi kikubwa sana kule Zanzibar nadhani na hata huku Bara viwanda vya kutengeneza watoto Alhamdulillah. Sasa watu wanaongezeka kwa kiasi kikubwa sana sana kabisa. Kwa hivyo 4.5 haitoshe kwa mahitaji hayo ya sasa ya Zanzibar. Sasa niiombe Serikali kwa heshima zote kabisa, mkae tena mjadili angalau tutoke kwenye 4.5% tuende 9% angalau Zanzibar nayo ikaweze kujitutumua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kauli ya Serikali kwamba uchumi wa Taifa umepanda kwa asilimia 7. Hapa napa pana matatizo kidogo ila sitaki kupingana na Serikali wala sitaki niishutumu vibaya Serikali kwa sababu wao ndiyo wenye *mandate* ya kuweka hizi data na kuzitangaza kwa watu wote nchini. Hii 7.5 tunaweza kui-*transform* vipi hii from the digital form kwenye paper in to our everyday life, hili swal sasa, how we can verify this? Siyo tunasema tu kwamba 7.1%, Je, tunajenga Standard Gauge? Ukiangalia uchumi katika nchi yetu sasa katika yearly practice ni vigumu mtanzania wa kawaida kukubali hili hakubali kirahisi. Mifuko kidogo imetoboka, korosho ndiyo hivyo Nchi is going a stun

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda uwekezaji umeshuka nearly 40%, uzalishaji nao mtihani mtupu, wafanyakazi na watumishi wengine Serikalini hawaongezwi mishahara. Sasa kama uchumi umepanda, wapi unasema? Kwa sababu inabidi mfanye mipango tuone maana yake ni kweli huu uchumi umepanda really practice. Kuna watu wakati fulani walikuwa wanaishi kwa milo miwili, hivi sasa hata huo mmoja kidogo ni mtihani. Sasa niombe sana sana sana kwa heshima zote, Serikali jaribuni ku-*transform* hii data 7.1 muilette in to our everyday life tuone kwamba ni kweli uchumi sasa umepanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nije kwenye Mfuko wa Jimbo, hapa kwa kweli kuna matatizo makubwa. Nia njema ya Serikali kutoa Mfuko wa Jimbo kwa Wabunge wote wa Majimbo Tanzania is a good approach, kwa kweli naipongeza. Sasa swal langu liko hapa; mnapohakiki, mnafanya uhakiki, mnahakikisha vipi kwamba hii fedha imewakuta walengwa na wameitumia kama vile inavyotakiwa. Naheshimu uwepo wa Waziri Kiongozi wa zamani wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mheshimiwa Shams Vuai Nahodha na naheshimu uwepo wa Waziri Mkuu ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amour Kengele ya pili imeshagonga, ahsante sana shukrani sana. Ahsante Mheshimiwa. (Kicheko)

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika mbili naomba.

NAIBU SPIKA: Dakika moja!

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge wako sijapata Mfuko wa Jimbo wa mwaka uliopita. Sasa kama Serikali kuna watu mliwapa waje watupe, mimi bado. Ni hilo sasa, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Amour hili la kwako la mwisho la kutokupata Mfuko wa Jimbo nadhani unaweza kuiona ofisi inayohusika ili iwe rahisi kwako. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Amina Makilagi atafuatiwa na Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga ajiandae. Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge mnapochangia muongee na kiti kuliko kuongea na Waziri moja kwa moja kwa sababu mwisho wa haya hata yeye pamoja na kwamba ni Waziri wa Fedha na madongo yote unamfuata hata yeye ni mwanadamu. Hata yeye ni mwanadamu kama sisi kwa hiyo ukimpelekea maneno kama hayo moja kwa moja nadhani tumuache Mheshimiwa jamani apumue kidogo. (*Kicheko*)

Kwa hiyo Mheshimiwa Amina Makilagi atafuatiwa na Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga ajiandae.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia lakini vilevile nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mungu muweza wa yote aliyenipa fursa hii ya kuweza kusimama na kuweza kuzungumza jioni hii katika Bunge lako Tukufu. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu hoja ambayo ni muhimu kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono na sababu ninazo. Sababu ya kwanza Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wote na timu yake yote ya Wizara ya Fedha na Watendaji wote na Mawaziri na Serikali chini ya uongozi wa mpendwa wetu Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli wamefanya kazi nzuri katika bajeti iliyopita. Nimejaribu kupitia vitabu vyote hivi, nimeanzia na kitabu cha hotuba ya Waziri, nimepitia Taarifa ya Hali ya Uchumi katika Taifa, nimepitia kitabu cha Mpango wa Utekelezaji wa Bajeti, wanyonge wanyongeni haki yao wapewe kazi wamefanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono bajeti hii kwa sababu hata bajeti iliyopita kwa kiwango kikubwa ilijielekeza katika miradi ya kufufua uchumi wa Taifa letu. Huwezi kusema unataka kufikia uchumi wa kati bila kuwa na reli yenye viwango vya kimataifa, huwezi kusema unafikia uchumi wa kimataifa bila kuwa na ndege za kutosha kwa ajili ya utalii na kwa ajili ya uchumi. Huwezi kufikia viwango vya kimataifa bila kuwa na umeme wa uhakika, bila kuwa na kilimo chenye tija, hizo ndizo sababu zangu za kuunga mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono kwa sababu Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/2020, umelenga kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi na umelenga kwenda kutekeleza malengo endelevu. Katika yale malengo endelevu yote Serikali ya Tanzania imeweka vipaumbele tisa na vyote viro katika mpango, sina kila sababu ya kuunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono kwa sababu kero zote zilizokuwa ni kero kwa ajili ya uchumi wa Taifa letu zimeondolewa, Mungu atupe nini, ninaunga mkono. Ninaunga mkono bajeti hii kwa sababu vipaumbele vyote vilivywerekwa vinalenga utashi wa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tazania. Ukienda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 16 umejieleza vema, Mheshimiwa Rais alipoingia alituonesha kabisa anataka

kuingia kwenye uchumi wa kati na bajeti hii imezingatia matakwa ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya utangulizi huo, naomba sasa nijielekeze katika mambo machache na leo nimechagua kwa sababu Wabunge wengi wameshaongea kabisa wiki nzima hii mengi wameshayagusia. Leo nimeona nijielekeze katika maeneo yanayogusa wananchi walinchagua na si wengine ni wanawake wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao kwa kweli katika kuchangia pato la Taifa wao ndiyo wanaoongoza katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo taarifa zinaonesha uchumi wa Taifa letu kwa kiwango kikubwa pia unategemea kilimo. Wazalishaji kati ya asilimia 65 wanawake ni zaidi ya asilimia 80 wanalima na kwa bahati mbaya wanalima kwa kilimo cha mkono. Wanawake wa Tanzania ndiyo tunaotegemea katika kilimo hata akina baba watanisapoti, ukipita huko vijiji watu unaowakuta kwenye mashamba ni wanawake na watoto wao wa kike. Akina baba walio wengi wanalima lakini si kwa kiwango cha wanawake. Nikitolea Mkoa wetu wa Mara na hasa walaya ninayotoka wanawake ndiyo wanaolisha hata familia, wanawake ndiyo wanaolea familia, wanawake ndiyo wanaoleta uchumi wa Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo nimeona nijielekeze kuwasemea katika kilimo na hapa ndipo waliponituma. Kilimo chao bado kinategemea jembe la mkono, kilimo chao bado kinategemea kilimo kisichokuwa na utaalalm, kilimo chao bado kinategemea kutokuwa na pembejeo za kutosha, kilimo chao bado hata kupata fursa zenyewe za kupata mikopo kwa ajili ya kununua pembejeo bado, kilimo chao hata mazao wanayolima bado kuwa na uhakika wa masoko bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona leo nije niishauri Serikali, kama kweli tunataka kufika uchumi wa viwanda na

kuipeleka Tanzania katika uchumi wa kati ninaishauri Serikali yangu tukufu hebu tuwekeze kwenye kilimo. Hapa ninatoa ushauri kwamba ni lazima Serikali katika bajeti hii na hata katika bajeti zijazo tujielekeze kuimarisha kilimo chetu na katika vipaumbele vyetu kama ambavyo bajeti imesema, tuongeze wigo wa kilimo cha umwagiliaji. Tanzania ina hekta nydingi sana za kilimo, zaidi ya 4,000 lakini zinazofanyiwa kilimo ni chache sana. Mpango wa Wizara ya Maji kwa mwaka uliopita walielekeza wanataka tufikie hekta 1,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba Serikali iharakishe hii mipango ili twende kwenye kilimo cha umwagiliaji. Hatuwezi kujikomboa kiuchumi kama bado tunaendelea kutegemea kilimo cha mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya mikoa, kwa mfano hii Kanda ya Kati ya Dodoma hata ufanyeje, kuna Wilaya kama ya Kongwa hata ukilima mazao kama ya mahindi hayaoti. Ukienda Mkoani kwetu Mara sasahivi ardhi imechoka. Sasa tunayo maziwa, mito, maji ya mvua na mpaka hatuna hata mabwawa. Ninaishauri Serikali hebu sasa tutafute fedha kwa ajili ya kuwekeza katika kilimo ili sasa uchumi wetu huu tunaouzungumza kwamba umekuwa kwa kiwango cha asilimia 7.5 sasa uende hata kumnufaisha mwananchi ili naye aone matokeo ya kukua kwa uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee uwezeshaji wa wanawake kiuhumi. Ninaipongeza Seriakli yetu ya Chama cha Mapinduzi, imekuwa mstari wa mbele kuwawezesha wanawake. Kama ambavyo nimetangulia kusema, mwanamke ndiye kila kitu, ukimuwezesha mwanamke ni sawasawa na kuliwezesha taifa. Ni ukweli usiopingika kwamba mapato anayoyapata mwanamke kwa kiwango cha asilimia zaidi ya 90 kinakwenda kwenye familia. Ninaposema hivi ninao ushahidi kwa sababu akina baba matumizi yao ni mengi, lakini hakuna mama anayeweza akaishi vizuri bila kuhakikisha mtoto wake anasoma bila kuhakikisha malezi ya mtoto. Hawa akina baba wakipata hela zinakuwa na matumizi mengi lakini akina mama

akikipata vyote vinakwenda kwenye familia. Kwa hiyo ninashauri hapa, hebu tuwawezeshe wanawake kiuchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mwaka wa fedha uliopita 2016/2017 tulitengeneza hapa sheria ambayo inaitaka Serikali kila palipo na jambo lolote la manunuzi, kila mahali ambapo wanatengeneza *tender*, iwe ni kujenga barabara, reli na kufanya kila kitu katika miradi ya maendeleo asilimia 70 wanaopata hiyo kazi au wanaopata hiyo zabuni au wanaopata hiyo *tender* wawe ni wanawake. Ninafurahia mpango huo na ninaipongeza sana Serikali yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kufanya utafiti, baadi ya taasisi zetu za Serikali hazitekelezi. KKwa hiyo ningependa kujua Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa hebu tuamble, tangu tumepitisha sheria hii mpaka sasa ni wanawake wangapi wananaufaika? Na kama hawanufaiki Serikali ina mkakati gani? Kwa sababu baadhi ya miradi ni mikubwa, kwa mfano mradi wa ujenzi wa *Stiegler's Gorge*, mradi wa reli na miradi mingine hata ya kununua ndege wanawake wananaufaikaje? Tujue! Hata hivyo, hata huko kwenye kilimo hata kwenye miradi mingine ya ujenzi wa madarasa, n.k tujue wanawake wananaufaikaje. Tunapoagiza vitu kutoka nje ya nchi wanawake kwenye asilimia 30 wananaufaikaje. Hapa nitaomba Mheshimiwa Waziri utakapokujaj hebu tusaidie kuainisha ili baadaye sisi kama Bunge tupime, isije baadaye sheria hiyo nayo ikaja ikaondolewa kwa sababu tumeshindwa kusimamia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naona wenzangu walikuwa wanapiga kelele juu ya mambo ya taulo za kike. Taulo za kike tulijichelewesha wenyewe, tulifanya uzembe, sisi wenyewe Wabunge hatukuwa *serious*, matokeo yake mpaka imeondoka. Sasa na kwenye hili naomba tusiwe wazembe, hii asilimia 30 tunasemaje katika kuhakikisha inanufaisha wanawake?...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

MHE. AMINA S. MAKILAGI: Nitaleta kwa maandishi ikiwemo pamoja na taulo za kike nimetoa ushauri wangu, nimezungumzia juu ya asilimia tano ya wanawake, vijana na walemavu na nimezungumzia pia utaratibu wa utoaji wa uboreshaji wa mapato ya kodi. Nitaleta kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lucia Mlowe, atafuatiwa na Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mheshimiwa Zainab Bakari ajiandae.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti hii. Awali ya yote naomba niunge mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina vitu kadhaa ambavyo nitachangia. Kitu cha kwanza ni suala la vitambulisho vya wajasiriamali. Suala la vitambulisho vya wajasiriamali limeleta mkanganyiko takribani nchi nzima. Jana huko Njombe wamesomewa barua makanisani, kwamba watu wote wanatakiwa kuwa na vitambulisho vya ujasirimali. Kwa mfano akina mama ntilie ambao wameajiri wafanyakazi kuwasaidia, kuosha vyombo na shughuli zingine ndogo ndogo wameambiwa wanatakiwa wawe na vitambulisho vya wajasiriamali. Watu wanaofanya kazi kwenye bustani wanatakiwa wawe na vitambulisho vya ujasiriamali, mafundi ujenzi wanatakiwa wawe na vitambulisho vya ujasiriamali. Ninaomba kujua, hivi kodi ya kichwa imerudi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inasikitisha kwa sababu wananchi hawa wamechanganyikiwa. Wamenipigia simu mimi asubuhi wanaongea kwa masikitiko makubwa sana wamechanganyikiwa. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atupatие basi ufanuzi na

mwongozo kuwa ni watu gani wanaotakiwa kuwa na vitambulisho hivi vya mjasiriamali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili naomba niongelee mradi wa Liganga na Mchuchuma. Juma lillopita nilikuwa nimeuliza swalii; kwa kweli wananchi wa Mkoa wa Njombe, ingawa haya madini ni ya Taifa zima lakini kwa kweli tunasikitika; kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Njombe wamejiandaa kwa muda mrefu, wametafuta maeneo karibu na mradi, wamewekeza wanajиandaa tayari mradi uanze lakini mradi hauanzi. Kuna watu walilima mazao kama mboga mboga, matunda wakidhani kwamba sasa watapata soko, lakini mradi uko kimya; na nimeangalia katika kitabu hiki sijaona mahali popote kuhusu mradi wa Liganga na Mchuchuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni fidia. Wananchi wanalia na fidia, hawajafidiwa. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie hao wananchi watalipwa lini fidia, kwa sababu hii kwa kweli inakatisha tamaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine naomba niongelee juu ya mashine za *EFD*; mashine za *EFD* kwa kweli ni mbovu. Nina watu kadhaa ambao wamenionesha zile mashine na zile mashine inaonekana kila inapoharibika anatakiwa kutengeneza kwa 150,000. Kwa hiyo unaweza kukuta imetengenezwa wiki hii, wiki ijayo tena inaharibika, anatakiwa atoe 150,000. Ni kwa nini Serikali isitafute kampuni ambayo inatengeneza hizi mashine imara? Nitaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja basi atuelekeze, atutolee ufanuzi kama kuna uwezekano wa kutafuta kampuni nyingine inayoweza kutengeneza mashine imara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine naomba niongelee suala la taulo za kike. Mwaka jana baada ya kupata msamaha wa kodi kwa taulo za kike kwa kweli wananchi walifurahi sana, hususan wanawake; lakini mwaka huu tena imerudi. Ninaomba Waziri atakapokuja atueleze ni namna gani hawa akina mama tutaenda kuwafariji? Kwa

sababu mpaka sasahivi watu wameshachanganyikiwa tena, kwamba kwa nini hizo kodi zimerudi ilhali viwanda vyatutengeneza taulo hizo bado havipo?. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Bakari, Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ajandae.

MHE. DKT. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya bajeti kuu ya Serikali ya mwaka huu 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kasi kubwa ambayo sote tunaishuhudia, tunaiona ya ukuaji wa uchumi wa taifa letu la Tanzania; nampongeza sana. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, yeye pamoja na Naibu wake; na nipongeze timu nzima ya wafanyakazi wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya pale. Tumeona safari hii wametujia na bajeti ya triliioni 33.11 ikiwa ni ongezeko la takriban asilimia 1.9 kutoka kwa bajeti ya mwaka jana ya triliioni 32.48; nawapongeza sana kwa kazi kubwa hiyo mliyofanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo mimi nianze kabisa kwa kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Mipango ambayo imeletwa mbele yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzijadili kwa kina Bajeti za Wizara mbalimbali na tukazipitisha, leo tunajadili Bajeti Kuu. Bajeti Kuu ambayo ndiyo muunganiko wa bajeti zote za Wizara zote ambazo tulizipitisha hapa siku za hapa karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulismewa taarifa na Waziri wa Mipango kwamba wanajipanga vipi kukusanya hizi trilioni 33.11 zitakazokwenda kukidhi haja ya bajeti ya Wizara zote kwa mwaka huu 2019/2020. Mimi kwa upande wangu naunga mkono hatua zote na njia zote ambazo zimependekezwa. Tumeshuhudia kuna maeneo kodi zimetolewa, tumeshuhudia kuna maeneo tozo zimetolewa lakini kuna maeneo pia zimeongezwa kiutaalam na kukidhi haja, ya kwamba bajeti hii ikawe kweli ni bajeti ya mfanyakazi wa chini hapa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nongoose sana miradi mikubwa ya Serikali ambayo imewekwa kama kipaumbele. Mradi wa *SGR*, *SGR* ni ujenzi wa reli ya kisasa, mwendo wa kasi, yenye uwezo wa kufanya kazi kubwa ya kubeba mizigo ambayo itapungua matumizi ya barabara zetu ambazo zimekuwa zilharibika kwa kubeba mizigo mikubwa sana. Nongoose sana kwa sababu usafiri ni kitu muhimu sana katika kuleta maendeleo ya nchi yoyote ile. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana mradi wa *Stiegler's Gorge*, kwa maana ya kupata umeme. Tunapozungumzia kutaka kuivusha nchi yetu kutoka katika uchumi wa chini hadi uchumi wa kati hakuna namna na namna ambayo sisi tumeichagua ni kuitia viwanda. Viwanda bila umeme tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Tunahitaji umeme mwangi na nafuu ili viwanda vyetu viweze kuzalisha bidhaa ambazo zina bei inayoweza kuchukulika na mfanyakazi wa kiwango cha chini hapa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba tunazihitaji fedha kwa ujumla wake ili tuweze kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hapa nchini. Tunahitaji fedha ili tuweze kutekeleza miradi ya *REA*. Wamezungumza wengi humu ndani kwamba *REA* imeonesha dhahiri kwamba ni eneo ambalo limemnufaisha Mtanzania wa kawaida. Umeme umefika vijiji maeneo mengi ya nchi yetu hadi kufikia sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba ya *REA* si nzuri, inasuasua kwa kiasi kikubwa sana. Tunahitaji tupate pesa ili Serikali ilekeze pesa hizi kwenye maeneo ambayo bado *REA* haijafika ikafike ili angalau kulingana na mpango wetu kufika 2021 vijiji vyote na vitongoji vyote nchi hii viwe vimeshapata umeme. Naogopa kwa kasi hii tuliyonayo sasa huenda hilo lisitimie, lakini naomba sana; nawaamini sana, Dkt. Mpango kwa mipango yako mikubwa unayoiweka hapa basi suala la *REA* liangalie kwa macho ya karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nizungumzie barabara. Barabara kwa maana ya *TARURA* kwa maana ya *TANROADS*, mgao wa fedha kati ya *TANROADS* na *TARURA* wengi wamezungumza hapa; na mimi niwe mmoja wapo wa kuzungumza. Nakuomba tuangalie namna ya kuweza kuwaongezea angalau kidogo *TARURA* kutoka asilimia 30 wanazopipata sasa angalau wapate asilimia 40 ili nao waweze kufanya kazi inayotegemewa kwa ajili ya kuwaletaa maendeleo wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* wanabeba eneo kubwa sana la barabara hapa Tanzania, tena barabara ambazo ni za udongo, barabara ambazo kila mvua ikinyesha zinaharibika, barabara ambazo kila mwaka lazima zifanyiwe matengenezo; tofauti hata na *TANROADS*, *TANROADS* wanashughulikia barabara kubwa ambazo kwa kiasi kikubwa zimeshatengenezwa kwa umakini mkubwa, zina lami haziharibiki mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara iliangalie hilo kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji fedha ili tuweze kutekeleza miradi ya kilimo. Wengi wamezungumza hapa ndani kwamba ili tuweze kuivusha nchi na jinsi tulivyojipangia sisi wenyewe, kwamba tunataka kuivusha nchi toka uchumi wa chini hadi uchumi wa kati kupitia viwanda vinavyotegemea kilimo. Tutegemee kilimo, tukizungumzia kilimo cha kutegemea mvua hapa tutakuwa

tunajidanganya. Tunahitaji kuzungumzia kilimo cha umwagiliaji, chenye uhakika hivyo tunahitaji mabwawa ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza baadhi ya watu waliopita kwamba maeneo mengi ya Tanzania hasa haya ya katika mvua si za uhakika sana, lakini ardhi yetu ni bora, nzuri na ina rutiba ya kutosha, shida ni maji; lakini maeneo haya haya tunayoyazungumza maji yapo karibu; tunaweza kutengeneza mabwawa na kuchimba visima. Kwa hiyo niombe sana fedha zipatikane ili suala zima la kilimo cha umwagiliaji lipewe umuhimu wake kama tunavyolizungumza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji; tunahitaji fedha tupeleke kwenye miradi ya maji; maji safi na salama. Watanzania tunahitaji tumtue ndoo mwanamke, mambo ya kutembea kilometra na kilometra; na kwenye vijiji vyetu kuna maeneo; mimi kuna kijiji cha Nzali wananchi wa Kitongoji cha Mapinduzi akina mama kazi yao ni kuondoka alfajiri kurudi saa 9 hadi saa 10; hii sio. Pamoja na kwamba kuna mambo mengine yanachengesha; tumekwenda mara mbili tunawachimbia visima pale hatupati maji; sasa wenyewe wanasema kwamba kuna wazee hawataki maji yapatikane. Sasa hilo nalo ni jambo lingine lakini kwa hakika tunahitaji kumtua ndoo mwanamke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo nizungumzie kuhusu miradi ya elimu. Tunahitaji watoto wetu waende shule ili taifa letu liweze kwenda huko kwenye uchumi wa katika, tunahitaji liende kwenye uchumi wa katika likiwa na wananchi wenye kuelimika. Watoto wetu waende shule, madarasa yapatikane, maabara zipatikane na nyumba za walimu zipatikane; zote hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji miradi ya afya pia iweze kutekelezeka. Tupate zahanati kila kijiji, vituo vya afya kila kata na hospitali za wilaya ili wananchi tuweze kuwa na afya njema ili tuweze kuifanya kazi ya kuweza kuvusha nchi kutoka hapa tulipo kwenda uchumi wa katika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono tena hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Bakari, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, Mheshimiwa Venance Mwamoto ajiandae.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda nikushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi. Pili naunga mkono hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwa hadithi moja ambayo inasema: "*alamatu-l- munafiq thalatha; idha hadatha kadhaba, waidha'waada akhlafa, waidha'atumina khana;*" alama za mtu mnafiki ni tatu, akizungumza husema uongo, akiweka ahadi hatimizi na anapoaminwi hufanya hiana. Hapo hapo kuna msemo kwamba ahadi ni deni na deni hilo utakwenda kulilipa mpaka mbele ya Allah (*Subhanahu Wataala*). (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza kwa maneno hayo kwa sababu zifuatazo; napenda kuzungumzia, kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano iliweka ahadi kujenga *border post* katika Bandari ya Wete mpaka sasa Bandari hiyo haina *Border Post*. Namtaka Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango akija aje atuambie, kuna kikwazo gani kilichosababisha kutojengwa kwa *border post* katika Bandari ya Wete? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitazungumzia tena juu ya masuala ya miradi mitatu ya Zanzibar. Huu ni Muungano na tulikubali wenyewe kuungana na kuna ahadi ambazo tuliwekeana kwamba tutatimiza kote kote bila upendeleo. Sasa, sijui katika hadithi hii kama Serikali ya Muungano itakuwa salama na itakwenda kujibu nini mbele ya haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mradi wa barabara ya Wete-Chakechake, hili ni suala ambalo lipo zamani.

Nashangaa, kipindi cha Waziri wa Fedha ambaye amepita, nadhani ni Marehemu, Mheshimiwa Mgimwa, alitia saini mkataba huu wa barabara ya Wete. Sijui kuna chokochoko gani na figisufigisu gani mpaka sasa hivi umekwamisha mradi huu usitekelezwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hili kwa sababu, tunajifanya kwamba watu wa Tanzania Bara na watu wa Zanzibar ni ndugu wa damu. Ni damu gani ambayo inapenda kuangamiza wenziwe? Udugu huu wa makopa hatuutaki wala hatuutamani. Udugu wa kukutana kwenye madishi, huu siyo udugu. Udugu ni kufaana. Tujengeeni barabara hiyo ili mtimize ahadi zenu, siyo kila siku mnasema uongo. Mtu mwongo anajua mahali pake pa kwenda kuishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza hili kwa uchungu sana. Barabara takribani kilomita 40 tu zinashindwa kujengwa. Ninyi huku Tanzania Bara mnajenga barabara hata kilomita 1,500 na kuendelea; hivi hamwonii huku ni kuwanyanyasa Wazanzibari? Wazanzibari wamewakosea nini? Wazanzibari mmewafanya, mme, aaah, sijui hata nitumie neno gani! Huku ni ninyi Serikali ya Muungano mnaingia katika alama za watu wanafiki ambazo ni tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuzungumzia suala la mradi wa *airport* ya Zanzibar. Dar es Salaam mnajenga *airport*, mmemaliza; *terminals* zinafika sijui *foursijui* ngapi? Kule Zanzibar, mnakuona sijui kama kichaka gani? Mpaka leo *terminal three* imeshindwa kumalizika kutokana na kwamba hamtaki kutia saini. Sijui roho hiyo mbaya mnaipata wapi? Sijui kwa nini mnataka Wazanzibar wasiukatae huu Muungano. Tukisema hivyo tunaambiwa ni wachochazi. (*Makofii*)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni suala ambalo halikubaliki.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga, sijui nani kasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Getere kengele ilikuwa imeshagonga ya muda wake kwisha.

Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, atafuatiwa na Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika ajiandae.

MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi name niweze kuchangia mapendekezo ya bajeti kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Nami nianze kwa kuunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuisimamia Serikali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kutengeneza mapendekezo haya ambayo kwa kiasi kikubwa yanakwenda kuipeleka Tanzania mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa usikivu, kwa kusikiliza maoni ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na maelekezo yao pamoja na maoni yaliyokuwa yanayotolewa kwenye Kamati za kisekta, maoni ambayo yalikuwa yanakusudia kujenga Tanzania kwenye mwelekeo wa kiuchumi unaofaa. Bajeti hii imeonyesha kupokea kwa kiwango kikubwa maoni hayo na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Serikali ilikuwa haijachelewa kupokea maoni haya kwa sababu tungeshangaa sana kama Serikali isingejipa muda wa kuyatafakari na kutathmini kabla ya kuyapokea. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali yetu kwa kazi kubwa waliyoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii iko karibu sana na wafanyabishara wakubwa, lakini ipo karibu sana na wafanyabiashara wa kat, pamoja na wafanyabiashara wadogo na hata wajasilimali. Hii ni bajeti ambayo inakwenda kusukuma mbele mapinduzi ya viwanda na kujenga msingi wa kwenda vizuri kwenye Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu wa Sita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wanaosema Sera yetu ya Viwanda haitekelezeki kwa sababu pengine eti hatuna malighafi za kutosha. Hili siyo suala la kweli hata kidogo. Ukiangalia malighafi ambazo zipo katika Sekta ya Kilimo tu, ni nyangi na toshelevu kuliko uwezo wa viwanda vyetu vya ndani wa kuzichakata malighafi hizo. Ukiacha katika maeneo mengine, lakini tuna tumbaku ya kutosha. Je, tunao uwezo wa kusindika tumbaku yetu yote? Tunalima korosho, tunavuna korosho zaidi ya tani 250,000, hatuna uwezo hata wa kuchakata robo ya korosho tunayovuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi ya sita Afrika katika kilimo cha muhogo. Inakadiriwa kwamba tunavuna muhogo zaidi ya *metric* tani tano kwa mwaka. Ni kiasi gani cha muhogo tunakichakata katika viwanda vyetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya huku nikiwa na uhakika kwamba Tanzania tunalima sana nazi, lakini ni kwa kiwango gani mazao yanayotokana na nazi tumeweza kuyachakata kwenye viwanda vyetu? Hii ina maana kwamba, tuko vizuri katika malighafi, lakini pia tuna fursa pana bado ya kuendeleza Sekta ya Viwanda. Hata hivyo, hakuna nchi ambayo inajitosheleza katika malighafi zake zote, ndiyo maana tuna-*export* na tuna-*import* malighafi na kuzipeleka pia nje kwa ajili ya kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maoni ambayo pengine yakichanganya na maoni mengine ya Bunge yaliyotolewa katika kuimarisha Sekta ya Viwanda basi tunaweza tukapiga hatua. Maoni haya yanaweza yakaongeza pato la Taifa, lakini pia yanaweza kuongoze ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo nadhani ni jambo muhimu, ni kuendelea kukaa chini na kuondoa changamoto zote za kikodi na kitoto ambazo zinaonekana kuwakwaza wawekezaji. Hili ni jambo la msingi sana. Tunaona Serikali imepiga hatua, kwanza kwa kutuletea mapendekezo yaliyopo kwenye mapendekezo ya bajeti, lakini pia mpango wake wa kutengeneza mazingira wezeshi ambaao unapangwa sasa kupitia *blue print*, nina imani tunakwenda vizuri katika kuhakikisha kwamba tunasonga mbele kwenye uchumi wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu, ni lazima kuwe na mkakati unaotekelozeka wa kufanya uwekezaji katika maeneo ambayo tayari kama nchi na mikoa mingine yote imeitikia wito kwa kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Tunazo kanda za kiuchumi, lakini pia tunayo maeneo ya EPZA ambayo kimsingi bado uwekezaji haujafanyika kwa kiwango kinachoridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika Mikoa ya Kusini, kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Mtwara, utaona kuna eneo kubwa limetengwa kwa ajili ya uwekezaji na wananchi wameshalipwa fidia zao, lakini uwekezaji bado haujafanyika. Hivyo, kuna jitihada za makusudi zinazohitajika kufanya na Serikali ili uwekezaji katika eneo la viwanda uendelee kufanyika katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kuna ushauri mwingine, hebu tuangalie ni kwa kiwango gani Sera yetu ya Viwanda kama nchi inafungamana na kuchangamana na sera za viwanda za nchi nyiningine ambazo ni jumuiya za kiuchuni. Ni namna gani sera yetu ya viwanda inachangamana na kufungamana na sera ya viwanda katika

nchi za Afrika ya Mashariki; katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara; nchi za *SADC*; katika Kanda za Kimataifa na hata nje ya Bara la Afrika? Ni namna gani sera yetu ya viwanda inafungamana na sera za nchi hizo? Hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lingine, hebu tuone ni namna gani Serikali inasimamia kikamilifu namna ambavyo soko la ndani na soko la nje la bidhaa zetu zitakuwa ni za kiushindani ili tuweze kuza bidhaa zetu nje na katika jumuiya hizo nilizozitaja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lingine, nalo ni jambo muhimu sana katika kuliangalia. Ni vema Serikali ikaendelea kusimamia matumizi ya teknolojia ya kisasa katika viwanda vyetu. Hili nalo linaweza likawa ni changamoto kubwa. Ili tuendelee kuimarisha Sekta ya Viwanda na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine haya yakifanyika, ninayo imani kwamba tutasonga mbele katika suala letu la kusukuma maendeleo ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, ni muhimu kuangalia pia namna nyingine tunavyoweza kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Katika upwa wa Pwani ya Bahari ya Hindi, hususan katika Mkoa wa Mtwara na hata katika Mkoa wa Lindi, hatuna hata kiwanda kimoja ambacho kinachakata mazao ya bahari, tungependa uwekezaji uliangalie eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Mkoa wa Mtwara tuna gesi na mionganoni mwa mazao ya gesi ni mbolea inayoweza kutengenezwa. Tungependa Serikali ione ni namna gani sasa tunaweza kujenga kiwanda cha mbolea katika Mkoa wa Mtwara ili kusukuma mbele maendeleo na mapinduzi ya kilimo kwa kuongeza uzalishaji wa mbolea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendelekezo ya bajeti yameeleza pia namna mabavyo Serikali imefanya kazi ya kuhakikisha inalipa madeni na malimbikizo au madai na malimbikizo katika mapendelekezo yaliyopendekezwa na Serikali. Katika bajeti iliopita, Waziri ameonyesha ni namna gani madai hayo pamoja na malimbikizo yamekuwa yakilipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015/2016 kuna wafanyabiashara walisambaza pembejeo. Kama ikiwa pembejeo walizosambaza zimeshahakikiwa, basi tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango achukue hatua ya kuwalipa wafanyabiashara hawa. Ni miaka minne sasa, uhakiki unaendelea. Kwa kweli inasikitisha sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017/2018 wajasiriamali wadogo wadogo walipewa majukumu ya kuzalisha miche kwa ajili ya kusambaza kwa wakulima wa korosho. Wajasiriamali hawa wengi walikopa benki na wengine walikopa hata kwenye Halmashauri yangu ili kuhakikisha kwamba wanapata fedha na kutengeneza vitalu vya kusambaza miche. Mpaka leo tunavyozungmza, watu hawa bado hawajalipwa. Ni nini kinachosababisha wasilipwe? Watahakikiwa mpaka lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema kama mtu hata kama alizalisha mche mmoja, alipwe kwa haki yake, lakini alipwe kitu ambacho kwa kweli anastahili kulipwa. Wananchi hawa wana malalamiko makuwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda. Uchumi wa viwanda tunaokwenda nao ni lazima kusukuma mbele uzalishaji wa umeme. Tunaipongeza Serikali, kwa mradi mkubwa wa kielelezo wa *Stiegler's Gorge*, lakini kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengine, sisi pia tuna mategemeo makubwa katika maeneo yetu kuhusu usambazaji wa umeme wa REA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kubwa la kasi ya usambazaji wa umeme huu. Nilichangia katika Wizara ya Nishati na leo narudia, nazungumza kwamba, katika mikoa ambayo ina vijiji vingi havijafikiwa na umeme, ni Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Lindi. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Venance Mwamoto, atafuatiwa na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika na Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma ajiandae.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa mambo makubwa ambayo ameyafanya. Baada ya hapo nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake. Mimi niseme, imenitia moyo sana baada ya kuona upande mwингine unapigwa madongo. Ukiiona upande mwингile ule unasifiwa ujue kazi huwezi. Sasa maana yake kazi yako ni nzuri, wewe endelea kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo amefanya katika kubadilisha baadhi ya Watendaji wa TRA ambako muda mrefu kumekuwa kukilalamikiwa. Sasa hivi mmeboresha, kuna mabadiliko makubwa ambayo tunayaona sisi ambao tuna macho, yanaendelea kufanyika. Kilio cha watu ambacho walikuwa wanalia cha jinsi ya *style* ya ukusanyaji bila kutumia mfumo imeanza kupungua na malalamiko ya watu yamepunguza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana utakuta fedha ambazo zitakusanya mwezi huu zitakuwa zimeongezeka kiasi kikubwa sana. Hata ushauri aliompa Mheshimiwa Rais

akutane na wafanyabishara, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, utamsaidia sana. Kwa sababu walikuwa wanakosa sehemu ya kwenda kuzungumza shida zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, kuna Wizara ambazo zimefanya vizuri hasa tukienda kwenye nchi ya viwanda. Mimi nianze na Wizara ya Ardhi. Niseme Wizara ya Ardhi, wamefanya kazi kubwa sana, kwa sababu ukisema unataka maendeleo, unaanzia kwanza kwenye ardhi. Kesi, malalamiko kwenye Wizara ile sasa hivi yamepungua. Watu wamepewa hati na zimeonyesha thamani, wanaweza kukopa na kuzungusha fedha ambazo baadaye zinarudi kwenye mzunguko wa uchumi. Wizara ya Madini baada ya kukutana na Rais, kuna mabadiliko makubwa yameonekana na kodi sasa zinakwenda kukusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuwa na nishati ya uhakika siyo rahisi pato la Taifa likaongezeka. Tumeona wenyewe, kama tunalalamika, basi ni vijiji vichache ambavyo havijafikiwa. Kikubwa zaidi naomba tu kwaMheshimiwa Waziri wa Fedha, ukizungumza nishati unazungumza habari ya usambazaji umeme vijijini na unazungumza habari ya nguzo; na ukizungumza habari ya nguzo ujue asilimia 45 zinatoka Wilaya ya Kilolo ambako barabara zake ni mbovu. Kwa hiyo, namwachia Mheshimiwa Waziri, tutaongea maana yake leo hatuji kuomba fedha, tutajua jinsi ya kuzungumza naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu ambavyo inabidi tuzungumze, kama nilivyosema, ukiwa na ardhi, umeme, watumishi, maji na usafirishaji, unazungumza habari ya kuinua uchumi. Nimesema Wizara ya Ardhi inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa umeme, bwawa la maji tunajenga, litaongezea nguvu kule. Tutakuwa tunaongeza nguvu kwenye umeme, lakini kwenye umwagiliaji. Kwa upande wa maji, naishukuru Serikali na Bunge letu kwa kuamua kuunda Wakala. Tukipata Wakala wakawa na bodi yao wamejitegemea kama ilivyo *TANROAD*, tutafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika usafirishaji, kama ambavyo tumeona *standard gauge* na ndege, kazi inaendelea. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii, niwapongeze sana timu yetu ya Taifa amba jana wamefungwa kule Misri. Ukiangalia tathmini, walicheza na timu ya *Senegal*. Timu ya *Senegal*, thamani ya timu ile kwa wachezaji ni *pound* milioni 380. Timu yetu thamani yake ni *pound*/milioni 14. Sasa unaona tofauti yake. Maana yake timu ya *Senegal*/thamani ukizipeleka kwenye fedha za Kitanzania ni trioni 1.1, wakati thamani ya timu yetu ni bilioni 44. Hii inakuja vipi?

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe.

TAARIFA

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimpe taarifa msemaji kwamba kama haya tuliyajua, sasa kwa nini tuliamua kupeleka timu yetu badala ya kujipanga na sisi tukafikia hapo walipotaka wengine? (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwambe, ungemwacha amalize hoja yake ili uelewé. Sasa hajamaliza hata hoja, naamini hujamwelewa ndiyo maana unampa taarifa.

Mheshimiwa Mwamoto, endelea na mchango wako.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nitampa na nauli ili aende akaione kule. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, nilichokuwa nazungumza ni kwamba tusitake kufurahia kwenda Peponi wakati tunaogopa kufa. Maana yangu nini? Maandalizi, matayarisho

ya timu yetu bado. Tunatakiwa sasa tukae tujipange, kwa sababu hawa wamewekeza; hawa wa-Senegal wamewekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, timu nzima ile ya Taifa wachezaji wanacheza nje ya nchi yao, kwa hiyo kwa sababu wamewekeza, fedha zile ambazo zinapatikana sasa thamani yake inarudi kwenye uchumi wa nchi yao na kuongeza pato la nchi. Wachezaji wetu wanne tu ambao ndiyo wanacheza nje ya nchi na thamani yao ndiyo ile ambayo mmeiona. Kwa hiyo, ninachotaka kusema sisi ndiyo Wabunge wa kuishauri Serikali tufanyeje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, kwa kuwa uwezekano wa kujenga *academy* kwa nchi yetu siyo rahisi, basi tuwatumie wachezaji aidha wa riadha, ngumi, mpira ambao walifika *rank* ya Kitaifa kuwasambaza kwenye Shule zote Tanzania hata kwa kuwalipa posho kufundisha michezo baada ya miaka mitatu tutaona nchi nzima itabadilika tutakuwa sawa na wenzenetu wengine badala ya kuendelea kulalamika. Kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa ulisikie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia niwaombe suala la kukuza michezo ya nchi yetu siyo la Serikali peke yake, wadau, *TFF* na Serikali kama vile ambavyo Mkoa wa Mwanza juzi wamezindua uwanja mzuri ambao Mwenyekiti alikuwa Mzee Kitwanga hapa. Kwa hiyo, haya ndiyo mambo ambayo yanatakiwa yafanyike badala ya kuendelea kulalamika, tuisitake tufanye vizuri wakati hatuchangii pia *TFF* wajikite katika kupanga ratiba vizuri ili mambo yaende vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba awe ni Waziri Mkuu au Rais tena akutane na wadau wa maliasili na utalii. Utalii ni sehemu ambayo tunaweza tukapata fedha nyngi sana lakini tumepasahau kidogo. Kwa mfano, juzi kuna Wabunge wamekwenda kuangalia michezo kule, nilitegemea tungewapa hata vipeperushi (*brochures*), wakaenda navyo wakavisambaza kwa watu kule ili

kutangaza utalii wetu, nami tarehe 26 nitakuwa mmojawapo ambae nitakwenda, niombe Waziri husika kama upo kama ni kilo 20 au 30 nibebeshe nitakwenda kufanyakazi hiyo ya kuvisambaza kwa niaba ya nchi yangu ya Tanzania kwa sababu naipenda.(*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ilikuwa ni nafasi pekee ya wawekezaji, dawati la wawekezaji wangekwenda kutumia fursa hiyo, zile ni fursa kwenda kutafuta wawekezaji kule, dawati likaenda kule lingeweza kutuletea watu kule wa kwenda kupanda Kilimanjaro, Serengeti, Manyara na sehemu nyingine ndiyo fursa zenyewe na sasa hivi ninavyozungumza kuna mechi zinaendelea hapa Tanzania, timu za walemvu za Afrika Mashariki zinapambana pale Dar es Salaam kwa kutumia nembo ya Tembo *worriers* sasa hizo ni fursa kwamba hata ukichukua wale walemvu ukawapeleka Kilimanjaro wakapanda Kimataifa tunaonekana na watu wanavutiwa kuja kuona mbuga zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nichukue nafasi hii niipongeze Serikali kwa kuwa wametujengea hospitali nzuri sana pale Wilaya ya Kilolo, hospitali ambayo ni ya mfano wa kuigwa ambayo Mheshimiwa Rais huenda akafungua kwa niaba ya nyingine zote. Kwa hiyo, niiombe Serikali muendelee kukusanya mapato kwa kutumia mfumo ambao utakuwa ni mzuri.(*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika suala la mwisho kabisa niombe kwenye zile mashine za *EFD*, zile mashine zinazofanyakazi ni chache sana. Ukitanya hesabu, kafanye hesabu ni ngapi unazo na ngapi mabao zinaingia kwenye mfumo wako, utashangaa ni fedha kiasi gani zinapotea nami niko tayari kukupa baadhi ya *documents* ukihitaji ili uone ambavyo fedha zinapotea. Kwa hiyo ninakuomba huu ni mfumo mzuri kwa sababu kwanza Watanzania sifa yetu kubwa ya Mtanzania ilikuwa ni kukwepa kulipa kodi lakini sasa hivi siyo ujanja. Ujanja mzuri ni kulipa kodi na kuokoka ndiyo ujanja ambao unaafaa.(*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge wawakilishi wetu waliokwenda kuitia moyo timu naona sura nydingi zimerudi humu, hebu wasimame kidogo tuwaone, wale waliotuletea....

(*Hapa Waheshimiwa Wabunge walioenda Misri kwa ajili ya AFCON kuishangilia timu ya Taifa ya mpira wa miguu walismama*)

NAIBU SPIKA: Karibuni sana, na tunawashukuru kwa kazi nzuri kwa sababu magoli mawili siyo sawa na hamsa kwa hiyo kidogo mambo yamekwenda vizuri na nina uhakika mchango wenu umeonekana huko. Ahsanteni sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika atafuatiwa na Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma na Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib ajiandae.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na leo hii kusimama hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya jambo la busara sana kukutana na wafanyabiashara ili kuwasikiliza kero zao, alizikuta kero zao ni kodi ya *TRA* kuwapandishia kwa muda mrefu na wafanyabiashara hao wakashindwa kulipa kodi hizo na wakafunga biashara zao na wengine wakaondoka katika nchi, Waziri siku zote hizo alikuwa hajalionna. Sasa hivi kasema biashara isifungwe mpaka apewe kibali, haya mapato ya Serikali yameshapotea kwa wingi ndiyo leo tunaamka na siku zote Wapinzani walikuwa wakisema neno hilo lakini ilikuwa bado hamjatafakari, kupotea njia ndiyo kujua njia. Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii kwa kweli bado haijampenda mnyonge, kwa sababu Rais wa Muungano anasema yeye ni Rais wa wanyonge lakini hii haijawapenda wanyonge. Nitazungumzia kuhusu nguo za mitumba. Nchi yetu asilimia 80 wavaa mitumba hawawezi kuvala nguo mpya kwa unyonge wao, leo mnawapandishia kodi kutokea asilimia 25 mpaka 35 kwa nini? Waziri nakuomba chondechonde hizi asilimia 10 uziondoe ili wanyonge wapate kuvala nguo za mitumba ili wasitirike, nakuomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu Dodoma. Serikali yetu imeipandisha hadhi Dodoma inakuwa Jiji la Dodoma na ndiyo Makao Makuu lakini bado ilikuwa hajajipanga vizuri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mgeni weka vizuri hiyo *Microphone* yako ili kumbukumbu zisiklike vizuri, hapo nimezima nakuelekeza wewe uiweke vizuri isimame karibu na kinywa chako.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali hajajipanga kwa sababu haiwezekani Makao Makuu ya nchi mpaka leo hii ikawa bado hawajaweka mtambo wa kuchapishia magazeti. Magazeti mpaka yatoke Dar es Salaam ndiyo yafike hapa ni kwa nini? Kwa hivyo jipangeni mkianza kufanya mambo ili mambo yote yaendane kwa sababu hapa ndiyo kitovu cha nchi, panapotungwa sheria, kwa hiyo leo mpaka gazeti litoke Dar es salaam lije hapa? (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka kuzungumzia ni kuhusu Zanzibar. Serikali ya Muungano ni pamoja na Serikali ya Zanzibar ndiyo ikaitwa Muungano. Sehemu ya Serikali ya Muungano ni pamoja na Zanzibar ndiyo ikaitwa Muungano ni sawa lakini bado Muungano haujaitendea haki Zanzibar. Kwa sababu haiwezekani Kitabu cha Bajeti kuanzia ukurasa wa 25 mpaka 35 zote zinajenga Tanzania Bara wakati Tanzania Visiwani nayo inayo haki katika Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Waziri wa Fedha wa Zanzibar alipohitimisha bajeti yake ya fedha alisema kuwa kuna miradi mitatu imeshindwa kutekelezeka kwa sababu Serikali ya Muungano hawajaweka saini na miradi mitatu hiyo kwanza ni barabara inayotoka Mkoani kwenda Chakechake, kilometra 40, vilevile akazungumzia kuhusu gati ya Mpigaduri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar uchumi wetu ni bandari, uchumi wetu ni biashara *Airport* leo bandari ile ni nyembamba sana ikiingia meli moja tu inaweza kupakua mizigo kwa muda wa wiki nne haiwezi kuingia meli nyingine. Meli nyingine zinakuja inabidi zipindishe zikateremshe mizigo katika nchi jirani ya Kenya bandari ya Mombasa. Kwa hivyo, tukasema tutengenezeeni bandari ya Mpigaduri ili tuweze kufanikiwa lakini wameshindwa kutia saini, ni kwa nini? Hapo kweli Muungano mnautendea haki? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia *Airport* ya Chakechake sasa ni mwaka mzima, mashine ya ukaguzi haifanyikazi. Haifanyi kazi ukipita pale mizigo inabopabopa kama mafenesi au wewe mwenyewe, mpaka madawa ya kulevyta yanaweza yakapitishwa kwa sababu hapana usalama katika *Airport* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine nazungumzie kuhusu Bandari ya Wete. Juzi niliuliza swalii nikaambwa pesa zimetengwa, itatengenezwa na mwenzangu amezungumzia hapa lakini hakuna kinachoendelea, kwa hivyo tunaiomba Zanzibar siyo wana wa kambo, tupo nasi katika sehemu ya Muungano, yaliyo ya Muungano tuyaaingize kwenye Muungano, yasiyokuwa ya Muungano basi tutafanya wenyewe lakini isiwe kutuonea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bandari ya Wete...

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib na Mheshimiwa Ramo Mataala Makani ajiandae.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, pia naomba nimshukuru sana Mungu kwa kuendelea kunipa afya njema ili niendele kutoa michango yangu katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitoe salamu za pongezi kwa Serikali. Naomba kuanza kwa kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo wameweza kuleta upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza, tumeuona watu wote tumekuwa tukisafiri na tunaona uwanja wa ndege wa Mwanza kwa hali ambayo ulikuwa nayo lakini Serikali imewekeza pesa pale na kuweza kufanya upanuzi wa uwanja ule wa ndege wa Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Seriakli kwa sababu imeweza kuwalipa fidia wananchi ambaao walikuwa wana migogoro na Jeshi katika maeneo ya Lukobe na maeneo mengine ambayo walikuwa na migogoro katika Mkoa wa Mwanza. Tunaipongeza sana Serikali kwa sababu tumekuwa tukiiomba sana kuwalipa fidia wananchi hawa ambaao wamekuwa wakiingia kwenye migogoro na Jeshi. Pia naomba kuiomba Serikali waendelee kutusaidia kuwalipa fidia wananchi ambaao wapo katika uwanja wa ndege ambaao unapanuliwa. Wawalipe fidia wananchi hawa ili kuweza kuepusha migogoro inayoendelea katika upanuzi ule wa uwanja wa ndege na kutufanya, kama wananchi wa Mkoa wa Mwanza au Wabunge wa Mkoa wa Mwanza kupunguza kura zetu. Ninaamini kwamba Serikali ni sikivu na itaweza kulisikia hilo na kulifanyiakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa salamu hizo za pongezi, naomba sasa kuendelea kuipongeza Serikali

kuhusiana na suala la hoja iliyoko mbele yetu ya Bajeti Kuu ya Serikali. Bajeti hii kama hatutatoa pongezi kwa Serikali kwa namna ambavyo imejitahdii kuhakikisha kwamba inazifanya kazi changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikitolewa mara kadhaa katika Bunge hili na Wabunge wa Bunge hili tutakuwa hatujaitendea haki Serikali. Wanasesma 'mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni' name sina budi kuipongeza Serikali kwa sababu bajeti hii ambayo iko mbele yetu tunaijadili siku hii ya leo imezitatua changamoto mbalimbali za kodi lakini pamoja na tozo mbalimbali ambazo zimekuwa ni kero pamoja na yote wameendelea kuhakikisha kwamba wanaweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara wote walio wakubwa, wa kati pamoja na wafanyabiashara wadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siipongezi tu hivi mtu anaweza akadhani ninapongeza pasipokuwa na *evidence*. Ukiangalia Serikali imeweza kufanya marekebisho ya ulipaji wa kodi mbalimbali. Wamepunguza ulipaji wa kodi kutoka kiwango cha shilingi 150,000 hadi shilingi 100,000 lakini pia wamepunguza malipo ya kodi kutoa 318,000 hadi 135,000. Waheshimiwa Wabunge mkiangalia ukurasa wa 41 hadi ukurasa wa 42 mtaona ni namna gani Serikali imeweza kuingatia ushauri ambao umekuwa ukitolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, siishii hapo; katika miaka mitatu mfululizo ndani ya Bunge hili nimekuwa nikiishauri Serikali mara kwa mara kuhakikisha kwamba wale wafanyabiashara ambao wanaanza biashara zao wasitozwe kodi kabla hawajaanza biashara. Kwa nini nisilipongeze Serikali kama imeweza kuyachukua maoni yale na kuweza kuyafanyiakazi kwa kufanya marekebisho ya Sheria na kuhakikisha wkamba inatoa *tax holiday* kwa wale wafanyabiashara ndani ya miezi sita kama unaanza biashara yako unapewa unafuu wa kutokulipa kodi hadi baada ya miezi sita ina maana kwamba baada ya miezi sita ukiwa kama mfanya biashara unaweza kuwa umekwishakufahamu kuwa biashara yako ina mtiririko gani, unapata faida ama unapata hasara, pamoja na hapo utaweza kukadiriwa kodi

vizuri na hiyo itasababisha wafanyabiashara wengi kulipa kodi kwa hiari bila kukwepa kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuipongeza bajeti hii ya Serikali, tumekuwa na changamoto mbalimbali pia ambazo zinatokea. Bajeti hii ina changamoto kubwa moja ambayo inawagusa Wanawake wa Tanzania. Nikiwa kama Mbunge ambae nawakilisha Wanawake wa Tanzania nitakuwa sijawatendea haki wale ambao ninawawakilisha hawana uwezo wa kuja kuyasema haya ndani ya Bunge hili bali wametuma wawakilishi wao, kama sitawasema nitakuwa sijawatendea haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imeonesha kutokuwa na *gender responsive*, kwa sababu gani nasema hivyo? Kuna suala la Serikali ukiangalia pale katika ukurasa wa 34 wamefuta msamaha wa kodi la ongezeko la thamani katika taulo za kike. Suala la kufuta msamaha huu kwa kweli kama Wanawake wawakilishi ndani ya Bunge hili hatujalelewa suala hili, ni kwa nini Serikali imekuja na wazo hili, walikaa wakafikiria nini. Ukiangalia suala la taulo hizi za kike hazitumiwi tu na watoto au wanafunzi ambao wako mashulen i bali zinatumia na asilimia kubwa sana ya Watanzania ambao ni wanawake. Wanatumia watoto wa kike, wanatumia akinamama ambao wametoka kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujifungua mwanamama anahitaji kutumia taulo za kike ndani ya siku 14 au zaidi kwa hiyo Serikali ilipokuwa imetoea msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani katika taulo hizi za kike walitarajia na walikuwa wana nia njema na tuliwapongeza kwamba walikuwa wana nia njema ya kuhakikisha kwamba kunakuwa kuna unafuu wa gharama katika kununua taulo hizi za kile lakini kwa bahari mbaya sana suala ambalo Serikali na wananchi tulilitarajia halikutokea lakini Serikali imekuja na kusema kwamba wanaondoa tena ule msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge nimekuwa nikijiuliza, Serikali ina mkono mrefu. Wajibu

mmojawapo wa Serikali ni kuhakikisha kwamba wana-regulate bei ya bidhaa zinapokuwa zipo sokoni. Kama Serikali inaweza leo hii sukari ikapanda bei Serikali ikatia mkono wake, ikatoa kauli yake, kutoa bei elekezi ya sukari ili kila mwananchi aweze ku-afford kununua sukari, vipi kuhusiana na tauo za kike suala ambalo linawagusa wananchi karibu asilimia 50 ambaao ni wanawake?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali baada ya kuwa wametoa ule msamaha, wameshindwa vipi kuhakikisha kwamba wana-monitor suala la ongezeko au pungozo la bei? Serikali imeshindwa vipi kukaa na wafanyabiashara hawa kuwaambia kwamba tumetoa msamaha wa kodi tunaomba mpunguze bei na kuwapa bei elekezi kuwa kiasi kadhaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi tauo hizi za kike zinanunuliwa kwa gharama ya Sh.2000 hadi Sh.3500, hiyo ni gharama kubwa sana. Kwa Mtanzania tu wa hali ya kawaida hawezi kununua tauo hizi za kike. Ndiyo maana tukaitaka Serikali kutusaidia na ndiyo maana na wenyewe wakatoa msamaha huo wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali irudi tena mezani iangalie suala hili linawezekana kwa sababu limekuwa likiwezekana kwenye bidhaa zingine kama vile petroli, sukari, Serikali imekuwa ikiweka mkono wake, kwa nini Serikali isitusaidie sisi wanawake? Mnataka mpaka wanawake wote wa Bunge hili tugome pamoja na wanaume naamini watanisaidia kwa sababu wao ndiyo wanunuvi wa tauo hizi za kike. Hatuzinunui sisi wenyewe, akina baba hawa ndiyo wanaozinunua hizo tauo za kike. Ina maana mwanaume kama yupo ndani ya nyumba ana mke wake ambaye ndio mama, watoto wa kike watano, ndugu, jamaa na marafiki anaishi nao mule ndani ya nyumba ambaao ni wanawake, mwanaume si ndiye anayenunua? Kwa hiyo, leo nikisema wanawake tuanzishe mgomo kwa ajili ya suala hili, naamini wanaume watatuunga mkono na tutaweza kufanikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutaki kufika huko kwa sababu tunaamini kwamba Serikali hii ni sikivu. Kama imekuwa ikiyasikia maoni mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge na kuyatafakari na kuyafanyia kazi, naamini hata hili haliwashindi wanaweza wakalitafakari na wakalifanyia kazi. Huo ndiyo ushauri wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutoa ushauri huo, pia naomba niishauri Serikali kwamba viro viwanda vyetu, kwa mfano kuna Kiwanda cha cha MSD, Mkao wa Pwani, pia kuna kiwanda kingine cha madawa Mkoani Simiyu, naishauri Serikali ivielekeze viwanda hivi kuanzisha *production line* ya hizi taulo za kike. Hiyo itasaidia taulo hizi kupatikana ndani ya nchi na hivyo kuleta unafuu wa bei na wananchi wanaweza wakazifikia kwa urahisi zaidi. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib atafuatiwa na Mheshimiwa Ramo Mataala Makani na Mheshimiwa Mary Chatanda ajiandae.

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi nataka nianze na hadithi ndogo tu. Kuna kijana mmoja kule Zanzibar alifunga safari na kaka yake kwenda Mwanza. Alipofika Morogoro akamuuliza hatujafika, akamwambia bado. Walipofika Singida akaamuliza hatujafika, akamwambia bado. Akasema eeh, kumbe hawa wenzetu wa Bara wana roho mbaya sana yaani kumbe nchi yao ni kubwa kiasi hiki lakini wana *hasada na visiwa* *vyetu vidogo hivi kama chawa tu, kama pua, akaambiwa hiyo ndugu yangu ndiyo ilivyo.* [**Maneno haya siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**]

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi niseme tu kwamba Wazanzibar tunapaswa kupewa pole sana kwa

kuwa katika Muungano huu maana *tumeungana na watu ambao wana hasada*. *Binadamu si vibaya kuwa na choyo lakini binadamu mbaya ni yule mwenye hasada. Mwenye hasada hata akawa na malikiasi gani lakini...* **[Maneno haya siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mohammed Khatib, kuna kanuni inavunjwa, Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe jambo la utaratibu mchangiaji aliyepondo kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(f) na (g).

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha nyingine zinazoongelewa humu ndani hazina ladha ya lugha za Kibunge na ulishatoa utaratibu. Sasa husuda hiyo watu wa Bara tuliyonayo ni husuda gani?

MBUNGE FULANI: Hasada.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Hasada. Kwa kweli mchangiaji atoe hoja, lakini lugha nyingine zinaudhi. Sisi wa Bara na Wazanzibari ni wamoja lakini anazo hoja zake na uhuru wa kibunge achangie kwa kutumia uhuru wa Kibunge wa kuzungumza lakini lugha nyingine kwa kweli, hapana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Jenista kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(f) na (g) akieleza kuhusu lugha ya mchangiaji aliyepondo kwa maneno

anayoyatumia katika kuonesha kwamba upande mmoja wa Muungano una namna unavyoutazama upande mwingine wa Muungano.

Waheshimiwa Wabunge, jana nilisema na nirudie tena kuwakumbusha matumizi ya maneno. Nilikuwa nimekusudia kuzungumza baada ya michango yote ikiwa imekwisha na wakati mwingine inasikitisha kidogo Waheshimiwa Wabunge wanapopiga meza kuashiria kukubaliana na jambo ambalo kama lingetokea upande ambao siyo wangelikataa sana. Kwa mfano, maneno aliyokuwa anayatumia Mheshimiwa aliyekuwa anachangia sasa hivi kazungumza kwa kinywa chake kwamba visiwa vile ni vidogo kama chawa, angezungumza mtu mwingine hapa ndani sasa hivi pangekuwa hali ni mbaya lakini anasimama Mbunge anazungumza kuita sehemu ya Zanzibar kwamba visiwa vile ni vidogo kama chawa. Maneno kama haya angeyatumbia Mbunge mwingine sisi humu ndani tungeona kuna shida na hata pia wenzetu ambao wapo nje ya Bunge hili wangeona kuna shida kwa nini Zanzibar inaonekana imewekwa kama chawa. Kwa hiyo, maneno kama haya ambayo yanaleta uchochezi usio na maana yoyote tusiyatumie Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa namna hiyo hiyo, tunavyotumia vitabu vyetu vya dini kuhalalisha tunayotaka kuyasema, hii si sehemu ya mahubiri na kwa sababu hatuna sehemu ya kuanza kuelezea muktadha wa dini fulani ilipotumia maneno fulani ilimaanisha nini, hata hayo Waheshimiwa Wabunge tuyaepuke. Nilitoa maelezo jana kwamba unapochukua vitabu vya dini kueleza jambo liliilo jema basi ni vizuri lakini unapochukua mstari wa kitabu cha dini kueleza ubaya wa mtu mwingine unaleta jambo ambalo linaleta tafsiri isiyio njema. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, jana mtu alichukua mistari kadhaa kwenye Biblia ambayo kimsingi kile alichotaka kusema kingeweza kuhalalisha watu kuitwa mkia ama watu kuitwa mikia kwa muktadha aliyokuwa anazungumza yeye, nikayakataa maneno yale. Leo Mbunge mwingine

anasimama akitumia maneno ya dini kuonesha kwamba kuna watu wanawenza kuhalalishwa kuitwa wanafiki. Sasa Waheshimiwa Wabunge tunaenda mbele tunarudi nyumba na wote tunahudhuria humu ndani, tujifunze kutokutumia vitabu vya dini ambavyo tutatumia hivyo hivyo mwininge atataka kusimama na kuona dini yake imedhalilishwa.

Waheshimiwa Wabunge, si jambo zuri sisi humu tuna utaratibu ndiyo maana tumeweka Kanuni. Huu si mkutano wa hadhara kwamba unaweza kutumia maneno yoyote utakavyo, hapana. Yakizungumzwa maneno humu namna yanavyochukuliwa ni kwamba ni kiongozi kasema, sasa kama viongozi tuchukue dhamana hiyo.

Mheshimiwa Mohammed Khatib maneno ya kuita Zanzibar ni visiwa vidogo kama chawa si lugha ya Kibunge na hairuhuswi. Zanzibar si ndogo kama chawa. Pia kuonesha kana kwamba pengine upande mmoja wa Muungano una hasadi ama maneno yoyote yanayoweza kutumika kuonesha ubaya fulani si sawasawa, wote tupo humu ndani hakuna mtu aliyejaribu kuonesha kwamba pengine yeye kwa haki yake ya kuzungumza anatazamwa kwa udogo wake ama kwa ukubwa wake.

Waheshimiwa Wabunge, kwa namna hiyo, natarajia kadri tunavyoendelea na tunavyojifunza haya tusirudi nyuma tena kwa sababu sisi wote naamini tunaelewana tukipewa miongozo ya namna hii.

Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib endelea na mchango wako, hayo maneno uliyokuwa umeyatumia mwanzo yanaondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napokea hayo maelekezo yako lakini niseme kwamba hasada si neno la kidini. *Hasada ni neno linalotumiwa na Waswahili lenye asili ya Kiarabu maana yake ni kwamba ni mtu aliye na choyo iliyopitiliza. [Maneno haya siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

NAIBU SPIKA: Sasa huyo mwenye choyo ni nani? Sasa hapo unataka kusema upande wa Tanzania Bara ndio wenye choyo dhidi ya Zanzibar? Mchoyo yuko wapi hapo sasa? Mheshimiwa Mohammed Khatib tusiende huko, hilo neno limeondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge endelea na mchango wako. (*Makofii*)

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya yanatia uchungu sana kwa kweli, haiwezekani hata siku moja wenzetu huku ninyi mnajenga barabara maelfu ya kilomita lakini sisi kwa mfano barabara iliyotajwa ya Chake - Wete wengine wanasema hapa kwamba ni kilomita 40 haifiki, ni kilomita 25. Sasa ikiwa ni watu ambao wanajinasibu kwamba asili ya Muungano huu ni undugu kama ilivyozungumzwa hapa lakini wengine wanajenga barabara ndefu kiasi hicho wakati wengine barabara ya kilomita 25 inazuiwa. Wengine wanajenga *Airport* kubwa mikoa mingi tu lakini wengine *Airport* yao moja tu inazuiwa.

TAARIFA

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib, kuna taarifa, Mheshimiwa kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba Sera ya Taifa letu nchi yetu ni mikoa yote kuunganishwa kwa barabara za lami lakini sisi na Morogoro haijunganishwa na mimi kwenye Jimbo langu toka Liwale - Nachingwea, Liwale - Nangurukuru hakuna barabara ya lami. Kwa hiyo, inapokosekana barabara Pemba haina maana kwamba kuna ubaguzi ipo mikoa ya Tanzania Bara haijapata lami kama ilivyo Pemba hana lami. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib.

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, barabara moja tu ya Dar es Salaam - Moshi inaweza kujenga barabara zote za Unguja na Pemba moja tu. Sasa kama wewe Mheshimiwa Kuchauka hujajengewa nadhani ni tatizo lako mwenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Wabunge hapa wamemlaumu Mheshimiwa Dkt. Mpango lakini mimi namtetea hili si suala la Mheshimiwa Dkt. Mpango ni la Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi hakiko tayari kuona kwamba Zanzibar inaendelea na eti siku hizi wana vikao wanajiliza kwa nini Zanzibar siku zote kwenye uchaguzi tunashindwa na hasa Pemba kwa nini hatupati hata Jimbo moja? Eti wanafikiria mipango ya uchaguzi huu 2020 unaokuja wafanye dawa ya kushinda lakini nawaambieni kwamba haya ndiyo mambo yanayowafanya Wazanzibar wakainyima kura CCM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kama ingekuwa Wazanzibar wanaikubali CCM wanaipa kura ni sahihi kabisa kusema kwamba akili zako siyo sawasawa kwa sababu huwezi kumbagua mtu kiasi hiki halafu akaenda kukupa kura, haiwezekani. Kwa hiyo, niwahakikishieni kwamba CCM hata

...

TAARIFA

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib, kuna taarifa, Mheshimiwa Mattar.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe taarifa mzungumzaji, Zanzibar CCM wapo na Chama cha Mapinduzi kwa upande Zanzibar kinashinda vizuri na kura tunapata vizuri na hakuna suala la ubaguzi, tunafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, nimwambie kaka yangu na mzee wangu

anapoongea aweke maelezo mazuri, kwa utaratibu tuliokuwa nao katika Kisiwa chetu Zanzibar Chama cha Mapinduzi kinashinda vizuri na tunafanya kazi vizuri na CCM, *inshalaah*, kila mwaka inaendelea kushinda, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mohammed Khatib, malizia muda wako.

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo yanayothibitisha kwamba CCM Zanzibar haikuchaguliwa na nikasema si kosa la Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa sababu juzi Mheshimiwa Waziri wa Fedha pale Zanzibar alivyokuwa anawasilisha bajeti kwenye Baraza la Wawakilishi, tena niseme kwamba lile Baraza la Wawakilishi 100 juu ya 100 ni CCM, lakini walilalamika kwamba Serikali ya Muungano inakataa kusaini mikataba ya barabara, bandari na ujenzi wa *airport*. CCM wenyewe wamesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Zanzibar CCM haiwezi kuchaguliwa na sababu ni wao wenyewe. Kwa sababu Mheshimiwa Makamu wa Rais ndiye anayeongoza vikao vinavyojadili kero za Muungano lakini kero za Muungano kila siku zinaimarika na ye ye yupo na wala hakuna mafanikio yoyote yanayopatikana. Hiyo ni kuonesha wazi kwamba wenzetu wengine wako huku kwa sababu ya maslahi yao lakini hawaitetei Zanzibar. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khatib, muda wako umekwisha lakini hapo mwisho wakati ukimalizia unaongea habari ya Makamu wa Rais kwamba amepewa hiyo ofisi ya kushughulikia Muungano na hashughulikii kero za Muungano. Waheshimiwa Wabunge, hayo mambo huzungumzwa humu ndani kila siku kwamba katika zilizokuwa kero zimebaki ngapi na tunakoendelea sisi ni binadamu huenda kutakuwepo na nyingine lakini isionekane kwamba kuna kazi haifanyiki, si

sawasawa. Wote tunazo hizo taarifa kwamba ni mambo mangapi yameshafanyiwa kazi.

Tunaendelea na Mheshimiwa Ramo Matala Makani atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Chatanda na Mheshimiwa Josephine Genzabuke ajiandae.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuwa mionganoni mwa wachangiaji jioni ya leo. Nimshukuru kwa namna ya pekee kabisa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya afya na uzima alionipatia na kuweza kusimama hapa leo. Mchango wangu mimi ni kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza bajeti ya mwaka 2019/2020 tunayojadili inakwenda kutekeleza mpango wa mwaka mmoja wa mwaka 2019/2020 huo huo. Huo mpango wa mwaka mmoja tunaoujadili ni sehemu ya mpango wa miaka mitano unaoendelea ambaao unaisha mwaka 2020/2021 ambaao na wenyewe pia ni sehemu ya Dira ya Taifa tuliojiwekea tangu mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira ya Taifa ambayo inaendelea kudumu kwa muda wa miaka 25, mipango yetu ya miaka mitano na mpango mwaka mmoja mmoja kwa miaka mitano yote tulipitisha wote kidemokrasia. Kwa kuwa tulipanga wote basi hata kutekeleza tutekeleze wote kila mmoja akiwa amesimama kwenye nafasi yake. Ikiwa katika utekelezaji tunakutana na mafanikio basi tutajipongeza na pale ambapo tutakuwa hatuwezi kufikia malengo basi tutafute sababu kwa nini hatujafikia malengo na tutatue tatizo hili. Kukaa pemberi na kulalamika haitasaidia mtu mmoja mmoja wala haiwezi kusaidia Taifa, tuweze kuangalia namna bora zaidi ya kuweza kutekeleza mipango tuliojiwekea wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Dira, nataka niishauri Serikali ijaribu kuangalia kipindi ambacho Dira inadumu kwa sababu nimeangalia ya Kenya nimeona wao Dira yao ilioko sasa inaishia mwaka 2030, Uganda inaishia

mwaka 2040, Rwanda ya kwanza inaisha mwaka 2020 lakini ya kwao ina miaka 20 wakati ya kwetu ni ya miaka 25, Kenya ni miaka 22, Uganda miaka 32. Halafu hao wa Rwanda wanayo tayari kwenye mpangilio dira mpya, wanazo mbili tayari; itakayoishia mwaka 35 na itakayoishia kwama 2050, hizi ni za vipindi vifupi vifupi nya miaka 15. Je, ni vizuri kupanga Dira ya muda mrefu sana au muda mfupi au muda wa katii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natazama pia hata malengo ya kidunia, nimeziangalia *MDG's* zinadumua miaka 15, hata *the Sustainable Development Goals* na zenyewe pia ni miaka 15, sasa sisi Dira yetu ilikuwa ni miaka 25, hebu tujaribu kuona hapo nini kinaweza kufanya pengine kuna namna bora zaidi ya kufanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni suala la ufuatiliaji na tathmini, naipongeza Serikali sana kwa sababu kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti safari hii ukurasa wa 33 Serikali imizingatia sana suala hili na imeliweka vizuri kwa sababu, taarifa za huko nyuma za kina za kupitia utekelezaji wa mipango iliyotangulia zilizungumza suala hili kwamba, lilikuwa ni suala ambalo lilikuwa ni *gape*. Kama muda ungetosha ningeweza kusoma hiki kipengele kimoja kwenye *Comprehensive Review Report for Tanzania Five Years Development Plan* ile ya kwanza ya 2011/2012 mpaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa, muda hautoshi siwezi kwenda kusoma kunukuu, lakini kifupi ilikuwa inaonesha kabisa kwamba, kukosa kufanya ufuatiliaji na tathmini ni mojawapo ya changamoto kubwa ambazo zilikuwa zikirudisha nyuma katika kutekeleza mipango yetu. Kwa hiyo, naipongeza Serikali hatua ambayo imeichukua sasa hivi ya kuweza kuhakikisha kwamba, sasa haturidii au tumerekebisha makosa yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili kwenye uchangiaji, hili ninataka tu kurejea mchango ambao ulitolewa humu ndani na mmojawapo wa wachangiaji akiwa anazungumzia mradi mmojawapo katii ya miradi ya

kimkakati, mradi wa reli ya kati ambayo inaboreshwu kwenye kiwango cha *Standard Gauge*. Alisema mchangiaji mmoja kwamba, hakuna jipya, mbona hii nchi ina *Standard Gauge Railway* tangu mwaka 75/76 na ambayo ilijengwa na Nyerere na kaunda. Kwa kifupi alionesha kabisa kutothamini, ni kama kuudharau mradi huu wa *Standard Gauge Railway*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu niwafahamishe wale ambaao hawafahamu kwamba, kukamilika kwa mradi wa *SGR* huu tunaokwenda kuujenga sasa hivi kunakwenda kuifanya Tanzania kuingia kwenye kundi la nchi ya pili kuwa na *speed train* katika Afrika. Tuna treni moja tu ambayo inakwenda kwa kilometra 320 kwa saa, iko Morocco, lakini baada ya hiyo zinazofuata zote ni *160 kilometres per hour* ambayo ndio sisi tunakwenda kuifikia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mradi huu ni mradi mzuri, ni bora na ni muhimu. Na kifupi tu ni kwamba, uchukue tu mfano kwamba, maana yke, tafsiri yake ni nini ya haraka ni kwamba, watu wanaweza kutoka Dar-es-Salaam na kufika hapa Dodoma ndani ya saa pungufu ya tatu au wakichelewa sana saa tatu. Ni sawasawa na mtu atakayekuwa anasafiri kutoka mojawapo ya vitongoji vya Dar-es-Salaam kwenda katikati ya mji kwenda kufanya kazi kwa siku. Maana yake utaokoa muda kwa hiyo, utaongeza tija katika uzalishaji kwa sababu watu watakuwa wanakwenda kwa haraka. Kwa hiyo, naishauri Serikali iendelee kuongeza kasi ya kutekeleza mradi huu kwa haraka kwa sababu ni mradi wa manufaa sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jabo langu la pili la kuchangia ni nafasi ya lugha ya Kiswahili katika kutekeleza miradi ya maendeleo au katika kuharakisha maendeleo ya nchi. Historia ya nchi hii inatuambia wazi kabisa kwamba, hata tulipokuwa tunatafuta uhuru mojawapo ya silaha ambayo inatamkwa waziwazi kabisa kwamba, ilitumika na ikasababisha tukapata uhuru kirahisi na pengine mapema sana ni lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba, ni vema kwenda na Kiswahili pia, hata katika hatua ya

kutafuta maendeleo, umefanya vita ya kutafuta uhuru, sasa fanya vita ya kutafuta maendeleo kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu gani, Kiswahili kinaelimisha, Kiswahili kitarahisisha kutoa taarifa kwa watu, kitaunganisha watu pamoja na pengine niweze kunukuu tu msemo mmoja wa Kingereza unasema, *if you want to go fast go alone but if you want to go far go together*, maana yake wengi kwa pamoja ndio mnawenza mkafanya jambo la kudumu, *sustainability*. Sasa kama unataka kufanya jambo la kudumu lazima ushirikishe watu wengi. Watu wengi mnawezaje kuweza kuwasiliana vizuri, ni kwa kutumia lugha ambayo kila mmoja atailewa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa, kengele ya pili hiyo. Asante sana, Mheshimiwa Mary Chatanda atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Saul Amon Henry ajiandae.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi nipate kuchangia. nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kutengeneza na kuandaa bajeti hii ambayo tumepewa na tumeisoma, tumeisoma, tumeipitia, ni bajeti nzuri ambayo Wananchi wetu wengi walioko huko kwenye maeneo yetu wanaipongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Waziri wa Fedha kuipongeza Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya ya kumsaidia Waziri, kumshauri, kuhakikisha kwamba, anaandaa kitabu hiki ambacho cha bajeti ambacho kimekuwa na maneno mazuri na maandalizi

mazuri ambayo yanaeleweka. Nilikuwa naomba tu labda ninukuu maneno ambayo aliyasema Mheshimiwa Waziri, ili kusudi Spika nae aweze kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema kwamba, Kamati hii ya Bajeti imetoa mchango mkubwa sana katika kuboresha sera za uchumi na bajeti kuliko Watanzania wengi wanavyofahamu. Amesema, kusema kweli wanastahili kutambulika kipekee, kama kuna nishani na au tunzo ya Spika kwa kamati hii ya Bunge inayojitanabahisha kwa utumishi uliotukuka basi, kama itakupendeza Mheshimiwa Spika napendekeza iwe kamati ya kwanza kutunukiwa heshima hiyo. Hajapata kutokea katika bajeti zote tulipoanza toka 2015 huyu Mheshimiwa Waziri kuzungumza maneno haya maana yake kamati hii imefanya kazi kubwa mno ya kumsaidia kwa hiyo, ni vizuri Spika nae sasa akaliona hili basi akalifanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Waziri amezungumzia hapa katika ukurasa wa 16 mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano katika utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2015. Amezungumza pale, ukiangalia na nimewasikia wenzangu wanasema kwamba, habari ya kwamba, bajeti hii ni ya vitu sio watu, lakini ukiangalia alivyoandika katika utekelezaji huu ambao amefanya katika kipindi kilichopita anasema ujenzi wa reli ya kati kiwango cha *Standard Gauge* maana yake unafanyika; hii maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, si ya vitu tu ni pamoja na ya watu kwa sababu watapanda watu. Amezungumzia suala la ufufuaji wa shirika la ndege ambapo sasa tuna ndege *Bombadier*, wanapanda watu. Amezungumzia ujenzi wa jengo la tatu, *terminal three*, miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Julius Nyerere kimekamilika, kinatumiwa na watu. Amezungumzia barabara kuu za mikoa kiwango cha lami, kwenye barabara anapita nani? Si wanapita watu kwa hiyo, ni vitu vya ajabu watu wanapozungumzia kwamba, hii ni bajeti ya vitu sio

watu. Ni bajeti ya vitu na watu, nilikuwa naomba sana tafsiri yake basi wenzetu wawe wanaielewa kwamba, bajeti hii ni ya vitu pamoja na watu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Serikali yangu kwa umeme wa *REA*. Kwamba, nchi nzima sasa hivi namsikia Waziri anakimbizana huku na huku anazungumzia masuala ya umeme wa *REA*. Kwa hiyo, niombe Serikali sasa kwa kuwa, tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda kwa maana pale Korogwe nina wawekezaji wa viwanda kama wawili wanapata tatizo la kupata umeme. Gharama za umeme wanazotajiwa ni kubwa kiasi kwamba, inawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kiwanda cha matunda ambacho kinatakiwa kuanzishwa pale wameandika kuomba umeme, gharama waliyopelekewa yaani yule mzungu amebaki sasa anashangaa. Ni vizuri viwango vyta umeme kama wanaomba wawekezaji wawekewe kiwango ambacho akishaweka maana yake si atakuwa ananunua huo umeme, tuisiwakatishe tamaa. Kwa hiyo, tunahitaji kuwa na viwanda, lakini vilevile tunahitaji kuwa na umeme ambao wananchi wetu hawa wawekezaji wakiwekewa unaifuwanawenza wakawekeza na sisi tunahitaji hivyo viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali yangu kwamba, bajeti hii, mpango huu wa bajeti ambao umeweke maeneo ya vipaumbele wa 2019/20 niombe basi Serikali yangu sasa angalau kwa mwaka huu mnaonaje kama fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya hivi vipaumbele tulivyoviweka tukahakikisha kwamba, fedha yote inapatikana itakapokuwa imekusanywa ikapelekwa kwenye hivi vipaumbele, ili tuweze kuijipima katika mwaka mzima kwamba, tumeweke vipaumbele hivi je, tumefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuliko tunavyofanya kipindi hiki cha miaka mitatu huku nyuma tumetenga bajeti haifiki kile kiwango ambacho tumejiwekea. Nilikuwa naomba ili

tuweze kujipima basi bajeti ambayo tumetenga kwenye hivi
vipaumbele itolewe yote ili sasa tuweze kujipima kwamba,
sasa tumejfikia wapi katika mpango mzima wa vipaumbele
ambavyo tutakuwa tumejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru tena kwa
kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. Asante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Asante sana. Mheshimiwa Josephine
Genzabuke, atafuatiwa na Mheshimiwa Sauli Amon,
Mheshimiwa George Simbachawene ajiandae

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu
Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ili nami niweze
kuchangia bajeti hii. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi
Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama jioni hii katika Bunge
lako Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa
kuunga hoja mkono bajeti hii ya Wizara ya Fedha na
Mipango. Naomba nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Dkt.
Philip Mpango, maarufu kama chambo kwa lugha la kiha,
Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Katibu Mkuu
Dotto, Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri
wanayoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu
nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa
kuweza kukubali kukutana na wafanyabiashara wanaotoka
katika maeneo yote ya nchi ya Tanzania. Walikuwepo watu
watano-watano kutoka katika wilaya, alikubali kupokea
ushauri wao, akawaruhusu kutoa mawazo yao na akakubali
kuwaruhusu kuweza kutoa kero zao. Kwa niaba ya
wanawake wa Mkoa wa Kigoma ambao ni
wafanyabiashara na wanawake wote wa Tanzania
ninamshukuru sana Rais kwa kuwaweza kutenga muda wake
wa kukubali kukutana na wafanyabiashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee
kuishukuru sana Serikali kwa kuondoa tozo mbalimbali

kwenye biashara mbalimbali, hatua hii itaendelea kuhamasisha wawekezaji kuweza kuendelea kuwekeza katika nchi yetu. Hii itasaidia sana kurudisha biashara maeneo mbalimbali ya nchi, ili wafanyabiashara waweze kufanya biashara yao bila kuwa na wasiwasi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara nyingi zilifungwa kwa ajili ya kutokuwa na imani na watu wa *TRA* kutokana na wingi wa kodi na jinsi walivyokuwa wanatoza kodi kwa manyanyaso makubwa, lakini kwa hatua hii sasa wafanyabiashara wataweza kuwa na imani na Serikali yao na wataweza kufanya biashara kwa uhakika zaidi na bila usumbu wowote. Kwa kweli, wafanyabiashara walienda kukata tama. Natokea Mkoa wa Kigoma, wengi walikuwa wanafunga biashara wanahangaika kukimbia huku na huku, ili labda waweze kutafuta sehemu ambayo hawawezi kupata manyanyaso, lakini kwa hatua hii nina amini na nina imani wafanyabiashara wataweza kuwa na hali ya utulivu na kuendelea kufanya shughuli zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba niungane na Wabunge wenzangu kama walivyosema na ninaomba nichangie katika maeneo matatu. La kwanza lilikuwa katika kodi, lakini la pili naomba kuzungumzia viwanda na malighafi inayotakiwa kutumika viwandani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa viwanda kama vile walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni lazima kuhakikisha tunahamasisha matumizi ya malighafi zinazotokana na na mazao ya kilimo kama vile mchikichi, kahawa, pamba, tumbaku, chai, korosho, n.k. Tukijenga viwanda vya namna hii wananchi wetu wataweza kupata soko na uhakika wa soko kwa hiyo, wataweza kuzalisha kwa wingi kwa sababu watakuwa sasa wanajua wakizalisha watapeleka bidhaa zao wapi, lakini ajira itapatikana kutokana na viwanda vitakavyokuwa vimejengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kama ifuatavyo kwa mfano, katika Mkoa wa Kigoma lipo zao la mchikichi. Mkoa wa Kigoma lipo zao la mchikichi ambalo

zao hilo linapatikana katika Mkoa wa Kigoma na viwanda vinavyotumia mahitaji ya zao la mchikichi vitazalisha bidhaa kama vile mafuta, sabuni, mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo, n.k. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa ya mafuta, sabuni na mashudu zitatumika kwa ajili ya Wananchi wa Kigoma na Wananchi wa Tanzania, kwa ujumla. Kwa hiyo, tukizalisha kwa wingi hatutaweza tena kutumia pesa zetu za kigeni kwenda kununua bidhaa nje, tutaweza kununua bidhaa zetu za ndani ya nchi. Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba Serikali kwa vile sasa Kigoma inaanza kuzalisha mchikichi na kwa sababu sasa hivi wananchi wameshakuwa tayari sasa kuweza kuanza kulima kilimo cha mchikichi, ninaiomba Serikali iweze kusaidia mbegu, ili wananchi waweze kulima kilimo chenyetija. Kwa sasa mbegu ni tatizo...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga, ahsante sana.

Mheshimiwa Saul Amon, tutamalizia na Mheshimiwa George Simbachawene.

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia mpango wa bajeti ya mwaka 2019/2020. Kwanza kabisa naanza na pongezi kwa sababu nilisikiliza Mheshimiwa Dkt. Mpango alivyoisoma mwanzo hadi mwisho, alinikuna sana kwa ufupi, kabla ya yote, naunga mkono bajeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili matatu ya kuchangia kwa sababu ya muda naomba sijaona vizuri juu ya wafanyabiashara, kwanza tunaanza na hoteli. Watu wamelalamika, lakini watu wafanyabiashara wanatakiwa walipe *hotel levy*, wanatakiwa walipe *sales levy*, wanatakiwa kukusanya VAT, TARA imo ndani ya hoteli, kwa kweli ni mzigo mkubwa sana. Naomba hilo liangaliwe ni namna gani

wafanyabiashara hawa wanaweza kutengenezewa utaratibu wa kodi. Nilidhani mimi kama mimi kwamba, kama mtu anayekusanya VAT, hao watu wa Manispaa na Halmashauri za Miji wasikusanye hiyo *hotel levy* kwa sababu inamkandamiza sana mfanyabiashara, hilo naomba liangaliwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili sheria hapa zimetungwa na zinatungwa vizuri sana, tatizo ni wale wanaokwenda kutengeneza hizo kanuni za kutumia hizo sheria. Nitatoa tu mfano mdogo, Serikali haiwajibiki kumkinga mfanyabiashara au kumuwekea kifua kwamba, nitoe mfano mfanyabiashara ameingia mkataba na kampuni fulani huko nje alete mzigo hapa Tanzania, lakini kuna baadhi ya kanuni zinamkingia kifua huyo mfanyabiashara alete hizo biashara peke yake hapa Tanzania; hiyo haikubaliki na haiwezi kuleta ushindani ulio sawasawa, kwa nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haitaleta ushindani ulio sawasawa kwa sababu huyu atakuwa anapanga yeye mwenyewe bei, yeye mwenyewe ataweka bei ya juu na Serikali itakosa mapato kwa sababu mzigo atakuwa anaingiza yeye peke yake. Nitatoa mfano, hapo nyuma kulikuwa na uingizaji wa maziwa ya watoto yanaitwa *Info Care*, lakini ukienda kwenye maduka yote *South Africa* inauza shilingi 3,000 ambapo mtu angweza kuleta angeuza 7,000/ 8,000 lakini ka sababu Serikali imemkingia mtu kifua maziwa hayohayo yanauzwa elfu 20 hapa Tanzania kwa sababu, anaruhusiwa kuleta mtu mmoja. Biashara ya ushindani haiwezi kwenda na Serikali haiwezi kupata mapato kwa sababu anayeruhusiwa kuingiza ni mtu mmoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninaomba hilo lizingatiwe waliangalie watunga kanuni. Mtu akiingia mkataba na kampuni, kati ya kampuni na kampuni, mfanyabiashara na mfanyabiashara, Serikali inaingiaje? Acha kila mtu alete hizo bidhaa hapa na kila mtu aweze kuuza kadiri anavyotaka, mlaji ndio aamue na soko liamuliwe na bei itakayouzwa na mlaji. Hilo nimeliona na muliangalie vizuri sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikuwa nazungumza kwenye upande wa kilimo kuna kilimo ambacho kimeingia na kimepamba moto na kilimo chenye tija sana cha maparachichi, lakini bei ya miche ni kubwa mno. Naomba Mheshimiwa utusaidie kupitia Waziri wa kilimo watutengenezee miche mingi, bei ya 3,000 Wananchi wengi wanashindwa kukianza hicho kilimo, lakini muitikio ni mkubwa kwa Tanzania nzima, naomba huo msaada mtusaidie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa ni hayo matatu. Na vilevile l nne ni kwamba, kuna hili suala la ukaguzi wa mizigo wa *TBS* huko nje ya nchi, najiuliza hivi ukaguzi unavyofanywa nje ya nchi ni kwa faida ya nani kwa sababu, tunalipa nje, kwa nini tusileté mizigo hapa, tulipie *certificate* tuwenazo hapa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano unapokwenda kununua sukari unajua kiwanda ni... (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana, lakini naamini Mheshimiwa Mpango na Naibu Waziri wameshailewa hoja yako hii ya mwisho. Mheshimiwa Geogre Simbachawene.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi ya mwisho kwa leo hii na bila shaka ndiye mchangiaji wa mwisho kwa maana ya wachangiaji wa kawaida katika bajeti ya Serikali. Nianze kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu na Viongozi wa Taasisi zote na Idara zote zilizoko chini ya Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya ya kuhakikisha kwamba, tunakuza uchumi wa nchi yetu, ili tuweze kupata matunza tunayoyataka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza nianze kupongeza kwa Serikali kutekeleza kwa vitendo ahadi ya kuhamishia Serikali Dodoma kama Makao Makuu ya nchi. Ni jambo kubwa ambalo lilahidiwa kwa muda mrefu, lakini limetekelizwa na tunaona kasi yake ambavyo Dodoma inabadilika na mimi kama Mwanadodoma kwa niaba ya Wananchi wa Dodoma niseme jambo hili limetufurahisha. Tunaona namna ambavyo tumepata faida ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja na imebadilisha maisha ya watu wetu. Serikali imelifanya jambo hili bila kutumia gharama kubwa, lakini lina tija kubwa sana kwa Wananchi wa Dodoma na sisi tunaoishi Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na niseme tu na nilitaka niwataarifu Wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwamba, kwa bajeti ya mwaka huu jumla ya pesa itakayoingia Dodoma kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya barabara tu ni bilioni 175. Bilioni 175 zitapitia *TANROADS*, zitapitia Halmashauri ya Jiji ya Dodoma na zitapitia kwenye Fungu lile la miradi ya Miji ya Kimkakati, ukijumlisha zote ni kwamba, bilioni 170 na ushee zinaingia Dodoma kwa ajili ya kutengeneza barabara ikiwepo barabara ya mzunguko. Hili si jambo dogo, ni jambo kubwa na tunaipongeza sana Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, limezungumzwa jambo hapa liliokuwa linahusianisha maendeleo ya watu dhidi ya maendeleo ya vitu na jambo hili limetafsiriwa vizivyo likinukuu Kauli ya Mwalimu Nyerere na ni upotoshaji mkubwa. Na kama kungekuwa kuna Profesa anasahihisha mtihani kwa watu waliokuwa wanachangia wakienda na mtizamo wa hoja hiyo wote wangepata sifuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, alichokisema Mwalimu ni kwamba, maendeleo ni lazima yawe yale yanayotambua pia hali ya usawa, haki na utu kwa maana ya dhana ya usawa, haki na utu kwa sababu ya *element* za kikoloni zilizokuwepo wakati huo wakati wakoloni wanatuambia tutawafanyia hiki, tutawafanyia hiki, hamna haja ya kudai uhuru kwa sababu, tutawafanyia kila kitu. Akasema hapana,

lazima utu wetu, haki, viwepo ndipo tuone uzuri wa maendeleo. Leo kilichotafsiriwa hapa ni kama vile usijenge barabara, lakini uvae nguo nzuri, usijenge nyumba, lakini upulizie *perfume*, ndicho wanachozungumzia, hiyo sio hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa Shivji alipokuwa anaongea katika mdahalo wa Kigoda cha Mwalimu Nyerere tarehe 25 Machi, 2017 aliondoa utata wa jambo hili. Na katika maeneo aliyosema, alisema namnukuu, "*Hakuna kitu kinachoitwa maendeleo ya vitu kutokana na ukweli kwamba, vitu havijiendezi.*" (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alipokuwa anahitimisha akasema, uhuru bila maendeleo ni ulaghai uliosukwa na walionacho. Uhuru bila maendeleo ni ulaghai uliosukwa na walionacho kwa hilo, ili uweze kuitafsiri vizuri kati ya maendeleo ya watu na maendeleo ya vitu katika falsafa za kisasa za mendeleo kwa maana ya maendeleo huwezi ukatenganisha hivi vitu viwili. Na ukatenganisha utapata tatizo maana tunajenga miradi mikubwa kwa ajili ya kujenga msingi wa uchumi wa nchi yetu. Tunajenga *Airport* ili tupate kuingiza fedha zaidi kila kinachofanyika, tunajenga barabara, tunajenga madaraja, tunajenga mradi wa kuzalisha umeme, ili hivi vijenge msingi wa uchumi wetu, uchumi wetu bado ni mdogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Serikali iende kwenye kuzalisha chuma la Liganga, ili tuweze ku-export chuma tupate fedha nyingi. Hii yote ni katika kujenga msingi wa uchumi maana uchumi wetu ni mdogo, lakini hapa mtu anasema eti kwa nini hamuongezi mishahara? Uchumi huu mdogo unaongezaje mshahara?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima uanze kujenga uchumi wa nchi kwanza, msingi wake wa uchumi ndio uongeze mshahara, utaongeza hewa tu. Hapa sasa hivi ninyi Waheshimiwa Wabunge na wengi wetu tumeajiri wafanyakazi wa ndani, tumwambie Mheshimiwa Dkt. Mpango hapa aweke kima cha chini shilingi milioni moja

kama tutaweza kulipa kwa uchumi tulionao, uchumi wetu hauwezi kubeba. Kwa hiyo, Rais anaposema nipewe muda tuweke mambo sawasawa halafu tutaongeza mshahara kwa kiwango kizuri, lazima tuelewe msingi wake ni nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo wangu ninaamini Serikali inafanya vizuri. Mheshimiwa Dkt. Mpango endeleeni tukamilishe miradi hii mikubwa, ili tuweze kutatua tatizo la msingi na baadaye uchumi wetu uweze kukua, tulionao uchumi wa sasa ni mdogo mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa mahali hapa na kupata nafsi hii muhimu kabisa ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/2020. Hotuba hii inakwenda kuhitimisha bajeti kuu ya Serikali katika mipango mbalimbali na mikakati, aidha, bajeti hii inakwenda kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyoelekeza. Halikadhalika nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kuipongeza Serikali kwa kuandaa hotuba nzuri, inayokwenda kutupatia mwelekeo wenye tija kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kutoa pongezi nyingi kwa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa ya kusimamia wanyonge kupinga ujisadi kuhakikisha maliasili zote zinainufaisha nchi na watu wake ili kuleta maendeleo kwa Taifa, katika bajeti ya mwaka 2018/2019, Serikali imetuambia ilitarajia kupata jumla ya shilingi trilioni 32.48 kutoka katika vyanzo vyote vya ndani na nje. Aidha, mchanganuo wa mapato yaliyopatikana hadi Aprili, 2019 ikilinganishwa na lengo la kipindi hicho ni kama Serikali ilivyoainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi trillioni 2.04 sawa na asilimia 122 ya lengo. Mapato yasiyo ya kodi yalivuka lengo kutokana na kuimarika kwa matumizi ya teknolojia katika ukusanyaji wa maduhuli kwenye taasisi za Serikali kupitia mfumo wa kielektroniki wa Serikali wa ukusanyaji wa mapato (*Government electronic payment Gateway –GEPG*); mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 529.25, sawa na asilimia 72 ya lengo; misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilifikia shilingi trillioni 1.70 sawa na asilimia 86 ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya ndani ikijumuisha mikopo ya kulipia dhamana za Serikali zilizoiva ilifikia shilingi trillioni 3.3, sawa na asilimia 57.4 ya lengo; na mikopo ya masharti ya kibiashara ya nje ilifikia shilingi bilioni 692.3, hizi ni hatua nzuri zilizofikiwa na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuhakikisha kila lengo lilllopangwa linatimla kwa wakati na kulifanya Taifa lisonge mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika Serikali imetueleza namna ilivyoshindwa kwa baadhi ya maeneo kutofikiwa kwa malengo ya mapato ya kodi kulitokana na sababu mbalimbali zikiwemo ugumu wa kutoza kodi sekta isiyo rasmi, kuendelea kuwepo kwa upotevu wa mapato kunakosababishwa na tatizo la magendo hususani kupitia bandari bubu kwenye mwambao mrefu wa Bahari ya Hindi na mwamko mdogo wa wananchi kudai risiti za kieletroniki wanapofanya manunuzi au baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kutotoa risiti wanapofanya mauzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali katika changamoto hii, kutotoa risiti ama kwa wananchi kutokudai risiti ni jambo ambalo linahitaji muda kuweza kulitattua. Kwanza elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi ili wajue ni wajibu wao kudai risiti, wasipodai risiti wanapoteza mapato ya Serikali na hivyo kupelekea kwa baadhi ya miradi ya maendeleo kutokukamilika hasa katika huduma za kijamii ambazo zinawagusa wananchi moja kwa moja. Vilevile Serikali ianzishe sasa kutoka elimu ya wajibu wa kulipa kodi tangu shule za msingi ili kutengeneza kizazi

kijacho chenye kutambua umuhimu wa ulipaji kodi, msingi huu utasaidia sana kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Watumishi wa *TRA* wana wajibu wa kutoa elimu kwa walipa kodi na kutokutumia vitisho pale wanapokusanya kodi. Imejengeka hali ya uoga na vitisho kati ya mlipakodi na mkusanya kodi kwa baadhi ya watumishi hawa kujenga mianya ya rushwa na kupelekea kwa baadhi ya wafanyabiashara kufunga hata biashara zao kwa kuona kodi wanazodaiwa ni kubwa kuzidi mitaji ya biashara zao. Vilevile naishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuzirasimisha bandari bubu ili sasa zitambulike na kukomesha uhalifu unaofanyika huko, kuzirasimisha bandari hizo kutasaidia Serikali kupata kodi ambayo sasa wanaikosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto ya muda mrefu ya malimbikizo ya madai mbalimbali ya Wazabuni, Watumishi wa Serikali na kadhalika kuidai Serikali. Changamoto hiyo pia imewakumba baadhi ya watumishi wa Serikali Jimboni Kibaha Vijiji hasa katika Sekta ya Elimu kuwa na madai ya muda mrefu, lakini Mheshimiwa Waziri ametuambia Serikali imeendelea kuhakiki na kulipa madeni ya wazabuni, makandarasi na watumishi ambapo hadi Mei, 2019 kiasi cha shilingi bilioni 598.4 kimelipwa kati ya bajeti iliyotengwa ya shilingi bilioni 600.0 kwa mwaka 2018/2019. Kati ya kiasi kilicholipwa shilingi bilioni 300.5 ni kwa ajili ya Wakandarasi, shilingi bilioni 232.9 ni kwa ajili ya watoa huduma na shilingi bilioni 65.0 ni kwa ajili ya Watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha tumeelezwa kuwa, Serikali imelipa malimbikizo ya kimshahara ya Watumishi 790 waliostaafu kabla hawajalipwa, ambapo hadi Aprili, 2019, jumla ya shilingi bilioni 3.10 zililipwa, ni hatua nzuri sana, lakini bado changamoto ipo ukillinganisha na hali halisi, malimbikizo haya yanapolipwa ama kwa wazabuni, watumishi basi yanakwenda kusaidia sana katika kukuza uchumi wa watu kwani fedha hizo zinakwenda kuingia kwenye mzunguko na hivyo kusaidia hali ya uchumi wa chini, kati kuwa katika hali nafuu. Naishauri Serikali kuongeza

kiwango cha kulipa malimbikizo hayo ili kuleta nafuu kwa wadai na wategemezi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wanaouza kwa rejereja bidhaa mbalimbali baada ya kufanikisha kuzinunua kwa wazalishaji wakubwa kwa maana ya viwanda wamekuwa wakitozwa kodi, ni jambo jema sana kwani kodi ndio msingi wa maendeleo katika Taifa lolote lile duniani, lakini sasa naomba kuishauri Serikali kuanza kutumia aina tofauti ya ukusanyaji wa mapato ambayo kwa kiasi kikubwa itawaondolea wenzetu wa TRA usumbufu wanaoupata katika kukusanya kodi kwa wafanyabiashara wa mwisho, kwa maana wale wanaouza kwa rejareja, Serikali iweke mfumo maalum wa TRA wa kukusanya mapato kwa pamoja hasa katika vyanzo vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali, mfano Viwanda vya Mabati, Nondo, Saruji, Vinywaji mbalimbali, Viwanda vya Sukari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huo uwe unakata kodi zote mpaka ya mfanyabiashara wa mwisho kwa maana ya wale wanaofanya kwa rejareja, kwa maana hiyo mfanyabiashara huyu wa rejareja anapokwenda kuchukua bidhaa kwa mzalishaji mkubwa (Kiwanda) anauziwa bidhaa anazohitaji kwa bei ambayo itakuwa imejumuisha kodi zote pamoja na kodi ambayo kwa sasa wafanyabiashara wa mwisho wanakatwa. Hatua hii itakwenda kusaidia zaidi watu wa TRA kwa kupata kodi yao kwa uhakika bila kusumbuana kama ilivyo sasa, tunaona namna ukusanyaji wa kodi kwa wafanyabiashara wa mwisho (rejareja) unavyosuasua kwa namna ya elimu ama wengine kutokutoa risiti kwa kila bidhaa wanayoiiza. Vilevile hatua hii itapunguza nguvu kubwa inayotumia Serikali katika kukusanya kodi kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine kwa Serikali, ni kuanzisha mikoa ya kikodi kwa Sekta nzima ya Maliasili na Utalii, mikoa hiyo ya kikodi kazi yake ni kukusanya kodi zote husika zinazotokana na maliasili na utalii, mfano katika sekta nzima ya utalii, kuna mahotelii, vivutio vya utalii na mambo mengine mbalimbali yanayohusiana

na sekta nzima ya utalii, Serikali ikifanya hivyo itakwenda kusaidia sana ukusanyaji wa kodi katika sekta nzima ya utalii na kuepusha ukwepaji wowote ambao kwa namna moja au nyininge kwa baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu wamekuwa wakikwepa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wetu wa kukusanya kodi ni mzuri sana, napenda kuipongeza tena Serikali kwa jitihada inazofanya katika kukusanya kodi, lakini tuna changamoto moja na muda mrefu ambayo imekuwa ikilalamikiwa na Watanzania walio wengi, ni tozo kubwa za kodi zinazotozwa bandari kwa vifaa mbalimbali, mfano, vyombo kama magari, bei ya kununulia nje ya nchi kama Dubai, Japan na kwingineko ni kiasi cha wastani, lakini ukileta hapa nchini, tozo ya kodi ya kutolea gari hiyo inakuwa mara tatu na bei ya chombo halisi, haileti maana hasa ukizingatia bei ya chombo husika iko wazi na inajulikana, najuliza kwa nini tozo inakuwa kubwa kuliko bei halisi ya manunu? Naishauri Serikali kuanza utozaji mkubwa wa tozo za kodi kwa bidhaa ambazo zinazalishwa hapa nchini kwa maana viwanda vyake viwo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kuagiza nje ya nchi bidhaa zinazozalishwa nchini ni kuua viwanda vya ndani, kufanya hivyo kutasaidia sana kuviinua viwanda vyetu vya ndani, aidha kwa bidhaa zozote ambazo hazizalishwi hapa nchini, basi Serikali naiomba ichukue ushauri wangu wa kupunguza kodi ili sasa Watanzania waweze kumudu kuagiza vitu mbalimbali, hasa magari kwani ndio tozo zake zimekuwa zikilalamikiwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na kukua kwa miji mbalimbali hapa nchini kwetu, hali hiyo imetupata pia watu wa Kibaha Vijijini, kwani sasa mji unazidi kukua kwa kasi sana na huduma mbalimbali muhimu zinapatikana, idara mbalimbali nazo zinapatikana, mfano Idara ya Maji, tuna ofisi ya Halmashauri pamoja na Jeshi letu la Polisi kwa kituo chetu kupandishwa hadhi, naiomba Serikali sasa kutokana na hayo yote niliyoyataja na mengine mengi yenye kutupa hadhi wana Kibaha Vijijini kuwa na sifa zote, Serikali

sasa ni wakati wa kuja kufungua Ofisi za *TRA*, Kibaha Vijijini, kufunguliwa kwa Ofisi ya *TRA* kutasaidia kwa kiasi kikubwa kusogea kwa huduma hiyo karibu na wananchi, na pia kutasaidia kwa Serikali kukusanya kodi zake kwa urahisi na kugundua changamoto mbalimbali na kuzifanyia kazi kwa uboreshaji zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua ya kufuta ada hiyo, ilikuwa kero kubwa kwa wananchi illinganishwa na hali halisi ya uhaba wa maji na changamoto mbalimbali katika sekta ya maji ambazo ni za muda mrefu. Changamoto hizo zimepelekea wananchi kwa gharama zao wenyewe kuamua kujichimbia visima vyao ili kupata maji kwa matumizi ya nyumbani, lakini wakakumbana na kikwazo cha kulipia kodi, kikwazo hicho sasa kimeondolewa, pongezi tena kwa Serikali, hivyo nawasihi wananchi mbalimbali wenyewe uwezo kuendelea kuchimba visima kwa kufuata taratibu zilizopo kisheria na kujipatia maji. Hata hivyo, nazishauri Bodi za Maji za Mabonde kuendelea kufuatialia visima vyote ili kuwa na idadi kamili na kuepuka uchimbaji holela unaoweza kujitokeza kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa hatua kubwa ya mageuzi ya kiuchumi na kijamii ambayo yameushangaza ulimwengu kwa kipindi hiki cha miaka mitatu na nusu tu chini ya uongozi wa Awamu ya Tano. Pia, niwapongeze Waziri wa Fedha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na taasisi zake zote kwa kazi nzuri walizofanya kwa kipindi chote. Mwenyezi Mungu azidi kuwaongoza vema katika utendaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Tanzania kwa uzalendo mkubwa, upendo wake kwa Watanzania na nchi yake, kwa kuchukua hatua mbalimbali ambazo zinasaidia nchi yetu kusonga mbele kimaendeleo.

Mheshimiwa Rais wetu amekuwa jasiri, hodari na mbunifu mkubwa hasa kwa mambo ambayo yalishindikana kwa awamu zote za utawala wa nchi yetu. Ni Rais ambaye atakumbukwa na vizazi nya sasa na vizazi vijavyo, Mwenyezi Mungu azidi kumlinda na amjalie afya njema na neema tele.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, nina maoni/ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo; Serikali ijenge maghala ya kisasa na vihenge nya kuhifadhi chakula ili kuzuia uharibifu wa mazao ya wakulima ambayo mengi yanaharibika kwa kukosa hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko; kuwe na kitengo maalum cha kutafuta masoko nje ya nchi ya mazao mbalimbali na kipewe bajeti ya kutosha. Ukizingatia kuwa biashara ya mazao yetu ni lazima tuitangaze huko duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutenga maeneo makubwa ya kilimo; Serikali ichukue hatua ya makusudi ya kutenga maeneo makubwa ya kilimo na kuyatangaza ndani na nje ya nchi ili wawekezaji ambao wako tayari au wana nia ya kuwekeza kwenye kilimo, wachukue fursa hii. Watanzania pia washirikiane na wageni katika kuwekeza kwenye kilimo cha kisasa cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao ya viungo; mazao kama karafuu, hiliki, pilipili manga, mdalasini, *vanilla*, mchaichai na viungo vingine. Mazao haya hayana utaratibu mzuri wa masoko, wakulima wa mazao haya wanahitaji mafunzo maalum ya jinsi ya kuendeleza kilimo chao na fursa ya mikopo kabla na baada ya mavuno ya mazao yao. Kwa mfano bei ya hiliki, karafuu, pilipili manga ni kati ya Sh.20,000 mpaka Sh.40,000, lakini walanguzi huenda kununua mti mmoja wa pilipili manga kwa Sh.50,000 ambapo mti mmoja hutoa kilogram 50. Hali hiyo inawanyonya wakulima wa viungo hapa nchini, tatizo ni kukosa huduma ya fedha kwa mazao ya muda mrefu, mazao haya yana soko kubwa nje

ya nchi. Maeneo ya Morogoro, Muheza, Mbeya, Kigoma na kadhalika ndiyo kunakolimwa mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha bajeti vizuri na yenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali chini ya Rais wetu mpenzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wenye maslahi mapana ya nchi wa kusitisha mchakato wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo. Ni ukweli usio na shaka mkataba ule haukuwa na maslahi na nchi yetu na ulikuwa unaelekea kuifilisi nchi. Hata hivyo, ujenzi wa bandari umuhimu wake bado upo pale pale, nichukue fursa hii kuiomba Serikali yangu sikivu ama kujadiliana upya na wawekezaji hawa au kutafuta wawekezaji wengine kwani kimsingi ujenzi wa reli ya kisasa *SGR* unategemea zaidi bandari kubwa kama ya Bagamoyo kusafirisha mizigo ili kuwezesha reli yetu ya kisasa kuweza kulipa gharama za mwekezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kielelezo wa ufuaji wa umeme wa nguvu za maji wa *Stiegler's Gorge* ni mradi mzuri na naipongeza Serikali yangu kwa kutekeleza mradi huu uliobuniwa na Hayati Mwalimu Julius Nyerere. Sambamba na mradi, nashauri Serikali yangu kuanza utekelezaji wa skimu ya kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Rufiji. Ni muhimu sana mradi huu ukaanza sanjari na ujenzi wa bwawa la kufua umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni mapato yatokanayo na watalii; hapa nazungumzia utalii katika Kisiwa cha Mafia. Kwa mujibu wa takwimu rasmi za Serikali, Kisiwa cha Mafia kinapokea watalii zaidi ya 5,000 kwa mwaka. Kwa kuzingatia ukweli na ukweli miundombinu ya usafiri ya kuingia na kutoka. Mafia haipitiki kirahisi ikiwemo upatikanaji wa boti ya kisasa na uwezekano wa Shirika la Ndege la *ATCL* kuanza

safari zake katika Kisiwa cha Mafia. Naliletä hili ili Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na Wizara ya Kisekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano washirikiane ili kuweza kutatua changamoto hizi na Kisiwa cha Mafia kiweze kufikika kirahisi na watalii wakaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvuvi katika bahari kuu umesimama kwa takribani miaka mitatu sasa kutokana na changamoto ya tozo (*royalty*) ya dola 0.4 kwa kila kilo moja ya samaki aina ya Jodari (*Tuna*). Kwa kuwa meli hizi haziji kuvua na Serikali inakosa mapato kutokana na tozo ya kukata leseni, naishauri Serikali yangu kulitafutia ufumbuzi haraka sana jambo hili kwani samaki wanahama, wanazaliana na kufa. Kitendo cha kutovuna mazao haya ni hasara kwa Taifa na hatunufaiki na chochote kwa siku zijazo kwa kutovuna mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Philip Mpango, kuwa Mafia tuna chanzo cha mapato kitokanacho na watalii wanaoingia katika hifadhi ya bahari. Tunaomba chanzo hiki kikusanywe na *TRA* Mafia badala ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji; Katibu Mkuu na Wizara yote ya Fedha kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kutumikia na kutekeleza llani ya Uchaguzi ya CCM 2015 - 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kufuta kodi ya ongezeko la thamani kwa taulo za kike kwani hata mimi ni shuhuda wakati nanunua taulo hizo wakati napeleka shulenii, nilinunua kwa bei ya juu sana mwezi Agosti, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kutoza ushuru wa nywele za kike ambazo zinatoka nje ya nchi na viwanda vya ndani pia. Ushuhuda wangu ni kwamba,

nywele za nje huuzwa mpaka Sh.600,000 hasa za maharusi. Kwa nywele za viwanda vya ndani huuzwa mpaka Sh.30,000 kwa moja, niombe Serikali isirudi nyuma kwa mipango mizuri 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* Dodoma ifuatilie maduka ya jumla, vituo vya mafuta ukusanyaji wake uko chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, afya; niombe Serikali ujenzi wa vituo vya afya vikikamilika ni vema vifaa tiba vipelekwe kwa wakati na watumishi wa afya wapelekwe haraka kwa kutengewa fedha.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Fedha na Mipango wakati wa majumuisho afikirie mambo yafuatayo:-

(a) Kupunguza *SDL* ili kurahisisha ufanyaji wa biashara nchini;

(b) Kupunguza matumizi ya Wizara Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuleta mpango wa kujenga nyumba za Ofisi za Balozi zetu kwa mkopo na benki kwa dhamana. Nyumba zitakazojengwa ndani ya miaka 10 tutamaliza madeni na kuwa na nyumba zetu;

(c) Serikali ifikirie kuirudisha *VETA* kuwa chini ya Wizara ya Kazi na Ajira katika Ofisi ya Waziri Mkuu ili waajiri wanaochangia zaidi ya shilingi bilioni tisa kwa mwezi waone faida yake iliyokusudiwa hapo awali ya kuongeza ujuzi wa wafanyakazi. Waajiri hawaoni mantiki ya *VETA* kuwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na

(d) Suala la *REA* haliendeshwi vizuri katika vijiji vya Jimbo langu la Tabora Kaskazini lenye vijiji 87 na *REA* III (/) nimepangiwa vijiji 18. Mpaka sasa ni vijiji vitatu tu ndio vimewashwa, Waziri wa Nishati aje na maelezo kwa nini mradi huu unaendeshwa bila uwiano katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha pamoja na kielelezo cha nafuu ya *SDL* kwa nia ya kuongeza mapato kwa Serikali.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii nami niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti. Kwa mtazamo wangu bajeti hii siyo *Gender Responsive Budget* bali ni bajeti ambayo inamkandamizi mwanamke. Kwa nini nasema hivyo? Ni kwa sababu Serikali imerudisha ushuru kwa upande wa taulo za kike (Pedi). Hii ni kumfanya mwanamke huyu ambaye suala hili la hedhi ni la kimaumbile na lazimishi, kwa nini nitozwe kwa sababu hii ya kupata hedhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuishauri Serikali iweke ruzuku na bei elekezi kwa wafanyabiashara wa pedi kwani bila kufanya hivi wafanyabiashara hawa kila mtu ajipangie bei yake itakuwa shida kwani pakiti moja ya pedi inauzwa Sh.1,500/=, ukiongeza hili ongezeko la thamani ambalo ni Sh.1,646.7 ambayo ni $1,647 \times 18\% \text{ ya } VAT/100 = 296.406$ or 297.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo $1,500 + 297 = 1,797$ kwa kila pedi moja ya bei ya chini ambayo ni $1,500/=$. Hii ni bei ya zamani tukiongeza ongezeko la thamani ya sasa pedi moja itauzwa kwa bei ya Sh.1,797.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za maendeleo, kilimo ni uti wa mgongo kwa nchi yetu. Zaidi ya 75% ya Watanzania ni wakulima na katika hiyo 75% wanawake ndio wanaojihusisha na kilimo lakini cha kushangaza fedha za maendeleo tunazotenga kila mwaka kwa mwaka 2018/2019 zimetengwa shilingi bilioni 98, hii ni aibu kwa nchi na Taifa kwa ujumla ukichukulia hii ni awamu ya Serikali ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii ya kumkandamizi mkulima huyu kwani fedha zilizopelekwa ni 0.143% 41 bilioni, kwa kiwango hiki wanategemea watapata wapi malighafi wakati unaikandamiza sekta hii na badala yake wanawekeza kwenye vitu mfano, barabara, ndege,

Stiegler's George, tunaona ni kwa jinsi gani wanachukua hadi fedha za ziada za kwenye Kilimo, Afya, Elimu naomba itambulike kuwa watu ni kilimo, watu ni afya, watu ni elimu, watu ni maji. Mfano mzuri ni wa Abraham Lincoln alisema *if you think education is expensive try ignorant* kwa maana kama unafikiri elimu ni gharama jaribu ujinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii imekuwa haiwekezi kwenye elimu ndio maana tunapata changamoto nyingi kwani hakuna wabobezi wa kutatua changamoto hizi. Nipende kuishauri Serikali tuwekeze kwenye elimu ya kilimo bora chenye tija pia tuwekeze kuwatafutia wakulima masoko yenye uhakika na bei ya kutomkandamizi mkulima ili mkulima huyu afurahie kazi yake ya ukulima.

MHE. ZAINABU M. AMIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu ya kila siku katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni; fedha zinazopitishwa na Bunge katika kila Wizara kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hazifiki kwa wakati na pia fedha zitolewazo hazipelekwi zote na hazitoshelezikuweza kuendeleza miradi hiyo. Naishauri Serikali katika kila Wizara fedha zinazopitishwa na Bunge ziwe zinaakisi hali halisi ya kuweza kuitekeleza miradi ya maendeleo katika Wizara husika na pia fedha hizo zitolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulipaji wa malimbikizo ya madai; katika hotuba ya Waziri, ulipaji wa madai umeelezewa katika ukurasa wa 15-16 kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri. Kuna madai ambayo ndani ya hotuba hii hayajatolewa maelezo kabisa. Wamiliki wa Viwanda ambao wanatumia sukari ya viwandani, takriban miaka minne wanaidai Serikali bilioni 45 na ni kiasi kidogo sana ambacho Serikali imewalipa shilingi bilioni sita tu ndizo zilizotolewa. Hii hudhoofisha mustakabali mzima wa kuelekea Tanzania ya

viwanda, maana wafanyabiashara hawa wanaidai Serikali na kukwamishiwa mitaji yao na kupunguza uzalishaji katika viwanda vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuchelewa kurejesha kwa ushuru wa forodha 15% (*Refundable Import Duty 15%*) katika sukari ya viwandani. Serikali imeleta changamoto kwa wahusika jambo lililopelekea kiasi cha mitaji ya wazalishaji wetu kushikiliwa na Serikali na kuwapunguzia mitaji yao. Nashauri fedha hizo zilipwe ili wamiliki wa viwanda hivyo waweze kufanya kazi ya kuzalisha bidhaa zao bila kusuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2019/2020, ambapo katika kitabu cha hotuba ya Waziri, kuhusu kipaumbele cha viwanda na killimo, kwa upande wangu sijaona sehemu yoyote katika hotuba hii inayozungumzia kuhusu jitihada za Serikali katika kuchukua hatua za kisheria kwa vile viwanda vilivyobinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iunde Tume Maalum ya kufuatilia viwanda vyote vilivyobinafsishwa ili kujionea hali halisi ya utendaji wake maana kuna baadhi vimekiuka kabisa ili dhana na masharti waliyopewa wakati wa zoezi hilo la ubinafsishaji matumizi ya eneo lililobinafsishwa. Hivyo kipitia Tume, hiyo Serikali ivibainishe na kuvichukua viwanda vyote ambavyo havijaendelezwa na kuwapa wawekezaji wengine ili kufikia lengo la Serikali kuelekea Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, kuondoa tozo za kuhifadhi Maiti katika Hospitali zetu za Serikali maana imekuwa kero kwa wafiwa na wakati mwingine hushindwa kulipa na kupelekea Serikali kuchukua jukumu la kuzika. Hivyo naishauri Serikali huduma ya kuhifadhi maiti katika hospitali zetu za Serikali iwe bila gharama (bure).

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali, igawe taulo za kike bure katika shule za msingi na sekondari na pia

kurudisha *Corporate Income Tax* kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato na kubakia 30%, ile ile na kusimamia muuzaji wa mwisho kupunguza bei ya taulo hizo ili kila mwanamke kuanzia mijini na vijijini wawe na uwezo wa kununua na kutumia, kuepusha kutumia bidhaa zisizofaa katika kujisitiri wakati wa hedhi na hii njia huleta maambukizi ya magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, namwomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema na umri mrefu Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake ili waweze kuyatekeleza majukumu yao ya kila siku.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wilaya kwa kazi nzuri na yenye matumani. Nawatia moyo wasikatishwe tama, wakaze moyo ila watende haki na Mungu atakuwa nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri; katika umeme Wilaya ya Bukoba Vijijini kuna maeneo mengi sana hawajapatiwa umeme na Serikali inasema ifikapo mwaka 2020 vijiji vyote vitakuwa vimeingiziwa umeme wa *REA III*. Kutokana na utekelezaji wa utaratibu kwa mradi inaweza ikamalizika bila umeme kufika, kwa hivyo ni vigumu viwanda kufanya kama wanavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo; nashauri kuna wakulima wadogo wadogo wa miwa lakini wanangu'unika malipo wanayolipwa katika Kiwanda cha Kagera *Sugar* ni kidogo sana, kuwepo na mfumo maalum wa kuwatetea waweze kulipwa malipo ya haki sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji; Mkoa wa Kagera Ziwa Victoria limechukua sehemu kubwa karibu wilaya zote, lakini ni manispaa pekee ndio haina shida ya maji, wilaya zilizobaki maji ya Victoria wanayaona tu, Serikali ijithahidi wilaya zote zisambaziwe maji kwa sababu ziko katika mkoa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine; Sheria ya Kodi, Sura 332; kodi ya tauo za kike zitolewe bure kusudi wanafunzi wa shule za msingi na sekondari waweze kujihifadhi pindi wawapo kwenye hedhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawatakia kazi njema katika kazi zao na Mungu awaongoze tena vizuri.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia. Napenda kuipongeza hotuba ya Kambi ya Upinzani; mategemeo yangu Serikali itachukua ushauri uliotolewa na kuufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya Awamu ya Tano imekuwa ikijigamba ni Serikali ya kutetea wanyonge. Mchango wangu utakua kwa maswali zaidi. Je bajeti hii ni rafiki kwa wanyonge wanaosema wanawatetea? Je itawasaidia kiuchumi? Wanasema uchumi umekua kwa asilimia saba (7%) lakini wananchi huko nje hali ni mbaya sana, uchumi huu umekuwa mwenye makaratasu tu lakini siyo kwa mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea tunahitaji siasa safi, watu na ardhi. Je siasa za nchi hii ni rafiki kwa maendeleo? Je, sheria zetu ni rafiki kwa maendeleo? Je, bajeti hii imewasaidia sekta binafsi kwa kiasi gani? Je, tozo zilizopungua kwa kiasi gani zinawasaidia wafanyabiashara ambaao hawakufunga biashara zao? Je, mfumo wetu wa kodi ni rafiki kwa wafanyabiashara, hawaoni ni wakati muafaka wa kubadili sheria za kodi? Je, mifumo yetu ya benki ni rafiki kwa wafanyabiashara wakati wanakopa sababu riba zipo juu sana 18-22%? Je, mfumo wa masoko kwa wakulima wetu ambaao ni zaidi ya 70% ya wananchi ni wakulima Serikali inawasaidiaje kupata masoko? Unakuta mkulima analima mwenyewe, panda, nunua mbegu, mbolea, dawa, anavuna ikifika wakati wa kuyaiza mazao yake mfano mahindi inabidi apate kibali kutoka Serikali. Je, Serikali inamwezesha je mkulima huyu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haipo kabisa *serious* kumsaidia mkulima mfano fedha za maendeleo ambazo zingetumika hata kuzalisha mbegu bora kupata Maafisa Ugani wengi, kuendeleza kilimo cha umwagiliaji wakulima waachane na biashara ya kutegemea lini wingu linajaa uanze kilimo? Bado bajeti kwa ajili ya maendeleo haitoki ya kutosha, mfano mwaka 2018/2019 ziliidhinishwa bilioni 98 lakini zinatoka bilioni 41 tu. Sasa kichekesho mwaka huu 2019/2020 wameidhinisha bilioni 143.5, hivi kama mwaka jana hazijatoka mwaka huu zitapatikana wapi? Naomba Waziri anipe jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tujuavyo magonjwa yasiyoambukiza yanakuja kwa kasi kubwa lakini tunaweza kuyazuia kwa kufanya mazoezi, lakini barabara zetu siyo rafiki kwa watembea kwa miguu, mitaro ya maji takia ipo wazi ni mategemeo yangu kutengwa bajeti ili mitaro ifunikwe na watu wafanye mazoezi kuititia huko na hii itaipunguzia Serikali kutibu watu kwa magonjwa yenye kuweza kukingika sababu na hili Hospitali yetu ya Kanda ya Kaskazini *KCMC* wamejitahidi na kuanzisha kitengo cha *treatment* ya Saratani, tayari wamepata machines za kuchoma mionzi lakini vifaa hivi lazima viwekwe kwenye chumba maalum (*Banker*). Ni vizuri Serikali ikajenga chumba hicho sababu hii itasaidia sana kuondoa msongamano kwenye hospitali ya *Ocean Road*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii ni kati ya sekta zinazochangia katika pato la Taifa zaidi ya 17%, lakini bado Serikali haijawekeza ipasavyo katika sekta hii, mfano, tunazo fukwe nydingi, Dar es Salaam, Bagamoyo, Tanga, Mtwara. Je Serikali ina mpago gani na utalii wa fukwe? Mfano Sadan *National Park* bado hapajawekezwa vizuri, shirikisheni sekta binafsi wajenge hoteli, kuwe na *bank*, *Curio Shop* na kadhalika.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa jitihada kubwa ya kuendeleza nchi yetu. Hongereni Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa wanunuzi wa tumbaku wanaendelea kununua kwa kujadiliana jinsi ya kutatua suala la VAT? Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa mbolea inafika nchini kabla ya mwezi Agosti?

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuchangia machache kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia jambo moja ambalo sikuweza kulichangia kwa kuongea wakati wa mchango wangu kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja wa ndege wa Morogoro. Nashukuru Serikali kwa kutupatia Meneja wa Kiwanja cha Ndege Morogoro Ms Esta Mwigune. Morogoro ni Mkao ulio katikati mwa Jiji la Dar es Salaam pamoja na Jiji la Dodoma. Kwa sababu hiyo na sababu nyinginezo, Manispaa ya Morogoro inakua kwa haraka sana. Tunashukuru kwa Serikali kwa kuliona hilo na kuutambua Uwanja wa Ndege Morogoro.

Pili, Mkao wa Morogoro tuna sehemu za utalii ikiwepo Mikumi, Selou pamoja na Udzungwa. Kwa kuutambua na kuujenga uwanja wa ndege wa Morogoro, kutaongeza kuja kwa watalii wengi, hivyo kuinua uchumi wa nchi yetu

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linalojitokeza sikuona fedha ye yote iliyotengwa ya kutengeneza/kujenga/kukarabati uwanja wa ndege Morogoro, ingawaje tumeanza kupata wafanyakazi kama Meneja na wengineo. Ombi langu, naomba na kushauri uwanja huu wa ndege ukatengenezwe kwani ni wa manufaa kwa nchi yetu na hasa kufuatana na kukuza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha ndege cha Selou tulishaambiwa kuwa kitajengwa. Je, ni lini kiwanja hiki kitajengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, nategemea nitajibiwa, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nimpongeze Waziri wa Fedha, Dkt. Mpango, Naibu Waziri Dkt Kijaji, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kuwasilisha bajeti na taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijatenda haki kama nitakuwa sijampongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana. Kwa kipindi kifupi ameweza kusimamia ukamilishwaji wa miradi mikubwa sana ya maendeleo. Pia kwa kikao kizuri sana alichokifanya tarehe 7/6/2019 Ikulu na wawekezaji na wafanyakazi nchini. Mheshimiwa Rais ameonyesha jinsi anavyoweka kipaumbele katika kuchochea uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze Serikali pia kwa kuona umuhimu wa kusikiliza kero na kuondoa tozo 54 za kodi mbalimbali, lakini pia Serikali iangalie mwingiliano wa majukumu ya taasisi au mamlaka za udhibiti kama *TBS*, *TFDA* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie kuhusu madai ya watoa huduma kwa Serikali yanachukua muda mrefu kulipwa wakati wazabuni hao pia wanatakiwa kulipa kodi zao Serikalini kwa wakati.

(i) Kwa nini kusiwepo na utaratibu wa kubadilishana madeni, yaani Serikali ichukue kodi yake inayodai wazabuni kutoka kwenye deni inayodaiwa na mzabuni, hivyo kupunguza mzigo wa kulipa pesa ambayo mzabuni bado hajalipwa.

(ii) Mtoa huduma anapotoa huduma kwa taasisi zikiwemo zile za Serikali anatakiwa aambatanishe *invoice* yake ya madai na *receipt* ya *EFD* hii ikiwa na kuwa analipa kodi ya VAT hata kabla ya kupata malipo husika. Kwa nini

EFD isitolewe pale tu malipo ya huduma yanapofanyika na si wakati wa madai yanapowasilishwa ikiwa na maana ni kwa malipo ya huduma kwa yanayochelewa kulipwa? Hivyo huathiri mitaji ya mfanyaabiashara na kuanguka kwa biashara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo miradi ambayo ni ya kimkakati lakini Serikali inachelewesha kupeleka pesa na kusababisha għarama za miradi kuongezeaka kwa kiasi kikubwa sana mfano, katika Mkao wa Iringa upo mradi wa machinjio ya kisasa, mradi huo una zaidi ya miaka 10 toka uanzishwe na mradi huu kama ungekamilika kwa wakati ungeweza kuwa ni chanzo kizuri sana cha mapato katika Halmashauri yetu na ni mradi ambaeo ungetengeneza ajira zaidi ya 200 kwa wananchi wa Iringa. Ni kwa nini Serikali isifanye upembuzi yakinifu wa miradi kama hii nchi nzima na kuipatia fedha ili halmashauri zetu ziweze kujlendesha?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelekeea katika uchumi wa viwanda nchini lakini barabara nyngi bado wakati wa kipindi cha masika hazipitiki kabisa. Ni kwa nini Serikali isifanye upembuzi yakinifu wa barabara zote za kiuchumi ili itoe kipaumbele kutokana na bajeti finyu ya *TARURA* zihudumiwe na *TANROAD*. Kwa mfano, Mkao wetu wa Iringa karibu barabara zote wakati wa masika hazipitiki kabisa na kusababisha magari makubwa yanayobeba mazao ya misitu kukwama karibu siku tano mpaka saba au zaidi na kuleta athari kubwa sana za kiuchumi. Pia mkao wetu unategemewa hata kuwa na malighafi za viwanda na wakulima wanashindwa kufikisha sokoni mazao kama njegere, mahindi, vitunguu, nyanya, viazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti kuu ya Serikali. Nianze kwa kusema kuwa, natambua zipo sekta mbalimbali zinazochangia katika ukuaji wa uchumi wa wananchi na pato la Taifa, zikiwemo sekta za madini, mawasiliano, fedha, kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya kilimo ndio inachangia kwa asilimia kubwa na kutoa ajira kwa wananchi kwa wingi na hivyo kuondoa hali ya umaskini kwa wananchi. Hivyo basi, ni vyema Serikali ikawekeza kwenye kilimo kwa kutenga bajeti ya kutosha, bajeti ikiwa ni kubwa, mambo yafuatayo yataweza kutekelezwa:-

- (a) Kufanya tafiti ya ardhi gani inafaa kwa zao lipi katika kila mkoa;
- (b) Kufanya tafiti ya mbegu bora ili kuongeza uzalishaji ulio bora;
- (c) Kuajiri Maafisa Ugani ili watoe elimu kwa wakulima ili walime mazao yenyе viwango vya juu kwa ajili ya *export* na viwanda vya ndani; na
- (d) Kuwekeza kwenye Taasisi ya Zana za Kilimo - *CAMARTEC* ili kukuza kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kuwekeza kwenye kilimo ndipo viwanda na sekta zingine zitakua.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya bajeti 2019/2020 na naipongeza Serikali katika utekelezaji wa Ilani ya CCM, 2015 kwa kiwango kinachoridhisha. Katika uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji katika Wilaya ya Malinyi kuna fursa kubwa za uvezeshaji wa biashara ya kilimo cha mazao ya nafaka (mpunga, ufuta, mahindi) kupitia miradi ya *SACGOT, FEED THE FUTURE, FOMAGATA* (Miradi ya Kitaifa). Miradi hii ya kilimo cha biashara ili iweze kufanikisha ni muhimu kuwepo na uboreshaji wa miundombinu ya barabara kuu inayopita katika Ukanda huo wa *SACGOT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mikumi – Ifaraka – Malinyi – Londo – Songea. Barabara hiyo ni muhimu sana kujengwa katika kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii utatengeneza mazingira ya kushawishi na kuvutia

wawekezaji kwa kuwa, eneo hilo linalopita katika Bonde la Mto Kilombero ambalo linafaa sana kama litatumika kikamilifu linawenza kutatua tatizo lote la upungufu wa chakula katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa muda mrefu imekuwa ikitoa ahadi ya ujenzi wa barabara hivyo, kiwango cha lami (Mikumi – Ifakara – Malawi – Londo – Songea), lakini ahadi hizo hazitekelezwi hivyo, kuathiri sana ushawishi na kuvutia wawekezaji wa kilimo cha biashara na viwanda katika maeneo ya Bonde la Kilombero kutokana na changamoto ya ubovu mkubwa wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuruhusu Baadhi ya Miji kufanya Biashara Saa 24; nafahamu ni suala la biashara kwa maana ya leseni inaeleza muda wa kufanya biashara, Hata hivyo, kama tunataka mapato (kupanua wigo) Wizara iongeze (*take lead*) kuhakikisha kuwa, baadhi ya miji kama vile Mikumi, Ruaha Mbuyuni, Ilulu, Mafinga, Makambako, Igawa na kadhalika iwe *designated* kama miji ya kibashara saa 24 sambamba na miji mikubwa kama Dar-es-Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na miji ya mipakani yote kufanya biashara saa 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la *DRC Congo* hasa kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kuna soko kubwa la mazao Kongo Mashariki. Hata hivyo, ili kunufaika na soko hilo lazima upitishe bidhaa kwa njia mbili:-

- (i) Tunduma – Kasulambesa – Lubumbashi
- (ii) Dar-es-Salaam – Rusumo – Kigali – Bukavu mpaka Kigoma

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018 wakulima wa Njombe walipoteza tani 600,000 za mahindi na mchele baada ya Zambia kuleta vikwazo maana na wao

wanategemea Soko la *DRC* Mashariki. Hivyo, njia sahihi na isiyo na vikwazo ni kutumia Bandari ya Karema ambayo upande wa pili ni Momba au Kigoma – Kalamie na kuna soko kubwa mno, hivyo tukiimarisha bandari zetu tutaongeza tija na *trade volume* itaongezeka maradufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, yapo ya kufanyika kwa mfano kuititia *JPC* – *Joint Permanent Commission* ambayo haijafanyika *since 2002*. Kuititia *JPC* au mikutano ya ujirani mwema itafanikisha kuondolewa kwa vikwazo kadhaa. Kwa mfano, suala la *visa* ambayo ni dola 50 kwa dola 200, *visa* ya kibia shara, lakini pia *SUMATRA* kwa sheria na kanuni hairuhusu meli kubeba mizigo na abiria, lakini kwa *DRC* – *Congo* kutokana na hali yao meli za mizigo zinaruhusiwa na abiria, sasa wakivuka *Lake Tanganyika* wanapigwa faini dola 500, *next week* hawaji. Kwa mujibu wa *World Bank*, mwaka 2017 wafanyabiashara wadogo waliuza mchele *DRC* wa thamani ya dola 1.5m *almost Tshs 3.5b*. Hivyo, kuna fursa ya kuongeza *trade volume* kati ya Tanzania na *DRC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Sukari; pamoja na mchango huu naambatanisha mawazo haya japo ni ya 2016. Kipo cha kujifunza, ili kuondokana na uhaba wa sukari hapa nchini.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, hoja hii ya Bajeti ya Serikali. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Serikali kwa kazi nzuri na ngumu wanazofanya kuhakikisha nchi yetu inaenda vizuri. Bajeti ya Serikali ili yosomwa ni nzuri sana na imegusa maeneo mbalimbali, lakini pia, kuondoa tozo ambazo zilikuwa kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Bajeti ya Serikali kwa jinsi ilivyowasilishwa pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa na utekelezaji wake kama inavyoonesha katika ukurasa 138. Kwa kweli, mambo mengi yaliyopo katika mpango yamefanikiwa kwa kiasi kukubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu kwa upande wa biashara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi kwa Serikali kwa kutoa muda wa miezi sita kwa wafanyabisahara wanaoanza biashara na kulipa kodi kwa muda huo. Kwa kweli, hii ilikuwa ni shida kubwa kwa wafanyabiashara wenye mitaji midogo. Shukrani sana kwa kulitekeleza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba kwanza kuweka maslahi yangu wazi kuwa, mimi ni mdau wa sekta ya mafuta. Tatizo kubwa la wawekezaji wa mafuta na gesi na hata wawekezaji wengine ni vibali vyya kuanzisha ujenzi wa biashara ambavyo, lazima ufile *EWURA, NEMC, OSHA*, Bodi ya Majengo, Bodi ya *Architect, TRA*, Halmashauri/ Manispaa, Ardhi, Bonde la Mto/Visima. Kwa kweli kazi hiyo ni kubwa sana mara nyingine unatamani kuacha kuwekeza. Ushauri wangu, kwenye *One Stop Centre* ya uwekezaji kuwepo na wahusika hao wote ili wananchi wanapotaka kuanzisha biashara wanawaona. Ni bora kulipa gharama kubwa wakati mmoja kuliko usumbufu usiokuwa na mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, biashara ya mafuta kwa maoni yangu naona ilikuwa imekaa vizuri, tatizo ni wale mawakala ambaao wanalipwa Sh.2,830,000/= kwa mwaka, lakini mashine zinapoharibiwa wanakuwa wazito kuja kurekebisha, ndio tatizo. Kwa maoni yangu naona mfumo wa *EFD* za vituo vyya mafuta ukiboreshwala hali itakuwa nzuri zaidi kwa kuwa, sekta ya mafuta ilikuwa na ubabaishaji mkubwa sana, lakini kwa kutumia mashine hizi Serikali imepata kodi zake na hali imezoleleka tusibadilishe kwa haraka mfumo uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari; naungana na Serikali kwa kuruhusu watu kuingia bandarini kutoa mizigo yao, lakini ulinzi uboreshwala kwa kuwa, mizigo ni mingi. Tukiingia wote inaweza kuwa ni vurumai ndani ya bandari japo kwa upande mwengine wataamsha na kuleta uhai wa bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa kupongeza Serikali kwa kudhibiti mfumo wa bei na hasa katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Naziliuzwa mpaka 500/= na vitu vyote bei ilishuka ghafla na kuwa chini, hajawahi kutokea kwa miaka zaidi ya 10, sijawahi kuona hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa kukupongeza sana wewe na Naibu wako kwa kazi kubwa na nzuri. Baada ya pongezi nijikite kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo; hakuna Mtanzania mzalendo atakayeacha kuchangia sekta hii kwa ustawi wa Taifa letu na ustawi wa mtu mmoja mmoja. Umuhimu wa kilimo usipokuwa *reflected* na bajeti hii kutakuwa na tatizo kwa kuwa, ni sekta inayotegemewa na watu wengi na tegemeo kwa malighafi ya viwanda vyetu. Tunaambowiwa sasa hivi Pato la Taifa limepandishwa na sekta ya madini na utalii, ombi langu kwa Serikali, tusibweteke na hali hii tuhakikishe sekta ya kilimo inaboreshw. Kwa sasa uzalishaji unashuka. Serikali ifanye utafiti wa mazao ya wakulima wadogo, wa kati na wakubwa ili kutatua changamoto zao ambazo kwa kweli hazifanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba pia, kwa kuwa wakulima wetu hamasa kubwa ni soko la uhakika la mazao yao, naomba wakulima waruhusiwe kuuza mazao yao nje au popote wanapopata soko. Viwanda vyetu vikiimarika tutazuia uuzaji nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wangu wa Manyara hauhitaji hata mafunzo kwa wakulima kwa sababu kilimo ni sehemu ya maisha yao. Wakiptata soko la mahindi, mbaazi, maharage, vitunguu, basi kilimo kitapanuliwa na kuboreshwa maradufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo. Nikiri kabisa kuwa sekta hii ya mifugo haijapewa kipaumbele kinachostahili na wafugaji pia wapewe fursa ya kuuza mazao yatokanayo na mifugo. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na mifugo mingi, lakini hatuna viwanda vyta kusindika ngozi, hatuna soko la kuuza ngozi ndani ya nchi. Naiomba Serikali iruhusu uuzwaji wa ngozi ghafi nje ya nchi na pia ipunguze tozo mbalimbali zinazotozwa katika suala la uuzaji wa ngozi, hasa *export levy* iondolewe au ipunguzwe sana. Ufike wakati sasa Serikali nayo ione namna ya kuwaboreshea maisha wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sanaa na burudani. Inaongoza kwa kasi ya kukua – 13.7%, lakini inachangia kidogo sana 0.3%. Tuongeze uwekezaji katika Sekta hii. Ikijumuishwa na utamaduni tuboreshe mchango katika utalii *especially* katika eneo la program ya urithi wa ukombozi wa Afrika elimu ya UNESCO yaani – *The African Liberation Heritage Programme*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi mikubwa (kielelezo na kimkakati). Tuboreshe manufaa ya kukamilika kwa miradi, *improve project completion benefits e.g technology transfer* kwa wanafunzi na wataalam wachanga, nafasi za ajira, *local materials, maintenance - for rest of the project life*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa *diaspora*, haujajitokeza vyema katika mpango na bajeti 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya kodi kupungua; mojawapo ya sababu ni biashara ya magendo katika ufukwe. Ufukwe una urefu wa kilometra 900 kutoka Tanga hadi Mtwara. Eneo la ufukwe litumike kama fursa kwa utalii wa fukwe. Mipango ipo hasa katika *FYDP's* lakini ni vyema tukatafsiri kwa vitendo, iwekwe mionganoni mwa vipaumbele kukamilika, Sekta Binafsi ni njia bora na rafiki zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la korosho; mchango wa kilimo 28.3% ndiyo unaongoza katika Pato la Taifa. Mchango wa kilimo cha mazao ndiyo unaongoza mionganoni mwa nyinginezo ndani ya kilimo. Korosho inaongoza mazao yote, hivyo kuboresha uzalishaji, masoko na uongezaji thamani ni muhimu. Suala la malipo ya mkulima wa korosho lishughulikiwe kama darura, hiyo itasaidia.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo hii kuweza kuijadili bajeti ya nne kwa Awamu hii ya Tano – 2019, chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Mpango; Naibu wake, Mheshimiwa Ashatu Kijaji pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa umakini wao kwenye kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka huu imegusa kila sekta katika nchi yetu na kuelekea kwamba hali ya uchumi itazidi kuwa nzuri kwa wananchi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umeme wa Maji, Bonde la Rufiji (*Stiegler's Gorge*), ni mradi ambaeo umeleta sura mpya kwa Taifa letu na uhakika na wepesi wa maisha kwani bei ya umeme itashuka, viwanda vingi vitajengwa, wananchi watapata ajira, kutakuwa na utunzaji na uboreshaji wa mazingira na kilimo cha umwagiliaji kitaongezeka. Haya yote ni matarajio makubwa sana kwa Taifa na pia kwa mikoa inayozunguka eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa reli ya *SGR* lazima kuwe na umeme wa bei nafuu ili treni ziweze kufanya safari zake, hivyo mradi wa *Stiegler's Gorge* ni sahihi kabisa. Ni vyema, Serikali ikaanza utaratibu wa ujenzi wa skimu za umwagiliaji kwa ajili ya kilimo kwani maeneo mengi yapo kwenye bonde. Hii itasaidia uzalishaji wa chakula na ajira pia kuwa na viwanda vya kukoboa na kusaga nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara toka Ubena Zomozi hadi eneo la mradi na kutoka eneo la mradi hadi Utete – Nyamwage kwa kiwango cha lami itafungua uchumi wa nchi na matumizi ya Bandari ya Mtwara na nchi jirani. Pia utalii uliopo Kusini mwa Tanzania ikiwemo na Mafia. Pia barabara ya Kibiti – Mkoka itakapokuwa kwa kiwango cha lami itainua uchumi wetu. Ujenzi wa bwawa hilo sio kitu kigeni duniani kwani hata Ethiopia, Egypt na kwingineko wanajenga. Nimalizie hoja hii kwa kusema kelele za mlango hazizui mtu kulala.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kodi kwenye viwanda vya taulo za kike ni zuri, hii itasaidia wanawake na watoto wa kike (wasichana) kuweza kumudu kupata kununua hizo taulo. Ni vyema Serikali ikaweka utaratibu wa bei maalum pia utaratibu wa kuhakikisha maeneo mengi vijijiini, zahanati, vituo vya afya na hospitali zilizo pembezoni zinapata taulo hizo kwa urahisi ili kuhakikisha usalama wa watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kodi kwenye mawigi, hii haina faida yoyote kwa jamii uzuri au kupendeza kwa mtu ni vile unavyojiremba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kupongeza bajeti hii kutokana na kuangalia angalau baadhi ya mambo ambayo yamekuwa kero kwa wananchi walio wengi wajasiriamali. Wajasirimali wengi walikata tamaa uanzishaji wa biashara ulioendana na kodi kabla ya biashara kuanza. Wajasiriamali wengi walimalizia mitaji yao kwenye kodi hivyo kuja na punguzo la kodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kupongeza kauli ya Serikali ya kutowafungia wafanyabiashara kwani imekuwa Serikali ikipata hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuchangia juu ya hali mbaya ya halmashauri zetu hivyo zimeshindwa kutekeleza

utoaji wa asilimia nne za wanawake na mbili za mikopo kwa walemavu pia nne za vijana kutokana na vyanzo vyote vikuu vya halmashauri kuchukuliwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, urejeshaji wa fedha kutoka Serikali Kuu ni mdogo hivyo kusababisha halmashauri nydingi kushindwa kujiendesha. Naishauri Wizara ya Fedha kupunguza gharama za uhamasishaji wa uhakiki wa ardhi ambao sasa hivi ni asilimia kumi imekuwa mzigo sana kwa wale ambao wanunua ardhi kutoka kwa mmiliki mmoja kwenda kwa mwengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri *TRA* kukaa na wadau au wafanyabisahara kujua shida zao badala ya kuonekana kwa walipakodi wakati wa kufuatilia kodi tu.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuendelea kutoa chanzo cha mapato ambacho kitasaidia kukuza mapato ya Serikali na kuondokana na utegemezi wa kodi ambazo hazina uhalisia mfano wa kodi za nywele bandia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kuwa Sekta ya Utalii ni moja ya Sekta zinazochangia kwenye Pato la Taifa lakini ukweli ni kwamba hatujatumia rasilimali za utalii tulizonazo na kuwekeza ili tupate mapato ambayo kwa kweli yangesaidia kupunguza kodi kwenye maeneo mengine kama taulo za kie, nywele bandia, punguzo la *PAYE* kwa wafanyakazi, vitambulisho vya wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mchango wangu wa kuongea nilileza kidogo kwenye uwekezaji wa utalii wa fukwe (*beach tourism*), utalii wa meli (*cruising tourism*) na utalii wa mikutano, matukio (*Mice tourism*). Haya mambo hatujayaona na kuwekeza ili kuweza kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna fukwe nydingi sana za bahari kuanzia Mtwara, Dar es Salaam, Tanga, fukwe za ziwa, fukwe za visiwa. Tunahitaji kufanya *classification* za fukwe zetu ili tujue fukwe zenye mchanga, miamba na kdahalika,

lakini pia tunaweza kutengeneza *artificial beaches* kwenye maeneo ambayo bado hayajatumika (*beach resort*). Mfano kule Bagamoyo (SES). Pale tukijenga *beach resort* yenye *facility* zote. Kule Kigamboni tunaweza kujenga *connection center* zenye hadhi za Kimataifa kwa Tanzania hatuna kwakweli zaidi ya ile AICC iliyojengwa na Mwalimu Nyerere. Tunahitaji Mataifa mbalimbali waweze kuvutika kuja Tanzania maana tuna uwanja wa ndege wa kisasa, tuna ndege, tujenge *connection center* kama za Barcelona, Rwanda na kwingineko. Tuwe na *modern pitch* ambazo zina *accommodate* michezo yote na ambazo wakati mwingine inageuka kuwa *concert hall*. Hapo kwa kweli tutaongeza idadi ya watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ni wakati wa kuhakikisha *convention center* zetu ziwe *hotel* zenye sifa za kuweza kukalika/kupokea Marais wa nchi mbalimbali. Leo tuna Mkutano wa SADC lakin Jiji la Dar es Salaam sio tu halina uwezo wa kupokea ugeni huo lakini ukweli hoteli zenye sifa ya kufikia Marais ni hotel ya Hyatt tu ambayo hoteli hii ilikuwa ni ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni wakati sasa wa kuwekeza kwenye *theme parks*, najua wengi wetu tumesafiri nchi mbalimbali hata watendaji na tumeona ni jinsi gani hizi *theme parks* zilivyo. Tunaweza wekeza *theme park* katika Majiji kama Dar es Salaam pale pande *game reserve* ijengwe *theme park*, kule Mbeya pia pawe na *theme park*, Mwanza napo tuwe na *theme park* na Arusha. Hapa tunaweza kuongea na Disney ili waweze kuja kuwekeza kupitia PPP. Hakika hili likijengwa litasaidia kukuza uchumi na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ili kuweza kurahisisha usafiri kipindi watalii wamekuja na kuweza kutembelea vivutio mbalimbali, hivyo ni vyema tufanye *cruising terminal* (*cruise terminal*). Mfano SGR na uwanja wa ndege *terminal III* vinahitaji kiunganishi cha Dar es Salaam, *cruise terminal* kama ile ya Kai Fan ya Hong Kong. Ijengwe pia Mtwara *Cruise terminal*, Tanga *cruise terminal*, hakika itasaidia mtalii

anaenda Mtwara, Lindi kuona malikale *under water experience*, kule Mafia wakija Dar es Salaam wanashuka kirahisi na kuungana na SGRkuelekea Mikumi na kwingineko. Leo fukwe za Saadan ukilinganisha na Costa Rica, Mtwara na Seychelles, Dar es Salaam, Durban/Cape town. Walikuja hapa watalii walishindwa kutumia kamba, wengine ni wazee na ni aibu.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushuKuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Hotuba ya Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2019/2020. Pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandika na hatimaye kuwasilisha kwa ufasaha mkubwa katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja hii kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii ni bajeti ya matumaini sana kwa wananchi wote wa Tanzania. Bajeti hii inatoa ufanuzi mzuri juu ya kupunguza umaskini katika nchi yetu. Hii inatokana na kuangalia mahitaji ya raia maskini yamezingatiwa kwa rasilimali za Serikali. Kodi zote zinazoidhinishwa kwenye mpango huu zinawajenga zaidi maskini badala ya kuwalemaza. Wananchi wana matumaini makubwa na bajeti hii kwa kuwa Serikali imeangalia katika maeneo ya biasara na uwekezaji katika kuimarisha nafasi zote zitakazojitokeza. Bajeti hii imeakisi maisha ya kila Mtanzania mwenye ndoto ya kufikia kilele cha mafanikio. Hizo ndio mionganoni mwa sababu zinazonisukuma niunge mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa wadau katika kuandaa bajeti hii; katika hitimisho lake Mheshimiwa Waziri ametaja wadau ambao amewashirikisha katika kuandaa bajeti hii. Hili ni jambo jema sana. Ushauri wangu katika suala hili ni kuiomba Serikali kwa bajeti zinazofuatana kuwashirikisha Mabalozi wetu wanaotuwakilisha katika nchi

za nje. Hili ni kundi muhimu sana katika nchi yetu ambalo lina uelewa mzuri (*exposure*) katika nchi inazotuwakilisha. Wanaweza kutumia uzoefu wa bajeti za nchi wanazotuwakilisha na kuuleta kwa matumizi ya bajeti ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya mapato; Mheshimiwa Waziri ameelleza vyanzo vingi vya mapato ambavyo miongoni mwao ni tegemezi, lakini tuna vyanzo ndani ya nchi yetu ambavyo kama tukiviboresha itawenza kutoa mchango mkubwa sana, mfano ni Bandari bubu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari hizi zinaitwa buba kwa kukosa huduma muhimu za wafanyakazi. Ikiwa Serikali itawenza kupeleka Maafisa wa Mamlaka ya Bandari na maofisa wa *TRA*, bandari hizi zitabadilika kuwa buba na kuwa bandari *official*/na zitawenza kutoa mchango mkubwa katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa uhai wake na afya njema kwangu na kuniwezesha kutoa huu mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na wafuasi wote ndani ya Wizara hii. Mwenyezi Mungu awape afya na kuendelea vema ndani ya uwajibikaji uliotukuka ndani ya majukumu yao. Hakika umahiri wao ni makini kwa wananchi wetu na matokeo chanya yenye tija yanaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la zima la kilimo ambalo linawashirikisha karibu asilimia 75 ya wananchi wetu nchini. Tulikuwa na mikoa iliyokuwa ya uzalishaji wa mazao (*mahindi*) ya ziada na kuwa na *big four* lakini sasa nje na mwelekeo, kutohana na gharama ya pembejeo na mbolea kuwa kubwa na kuwapa changamoto wakulima. Pembejeo na mbolea kutofika kwa wakati kwenye

maeneo, pembejeo na mbolea kuwa na bei kubwa. Changamoto hizi zinapelekea wakulima kurudi nyuma kwenye uzalishaji wa ubora wa mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa uzalishaji wao tunashauri Serikali yetu kujenga Kiwanda cha Mbolea na kuchanganya pembejeo ndani ya Mkoa wa Rukwa, tuweze kupunguza gharama kwa wakulima wetu ili waweze kurejea kwenye *big four* na hatimaye tuondokane na upungufu wa chakula hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika bajeti ya mwaka huu, nitofautiane na bajeti zilizopita kwa vyanzo vilivyo bainishwa kwa makusanyo ya mapato kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri Serikali yangu katika kuongeza mapato ukurasa 43 - 44. Bado nchi yetu tuna upungufu sana na mkubwa katika usambazaji wa maji kwa wananchi wetu hasa vijijini, hata vilivyo karibu na mito, maziwa na bahari. Mapendekezo ya asilimia 10 kwa vifaa vya plastiki vinavyohusika na miundombinu ya maji. Ushauri wangu ni bidhaa zinazozalishwa nchini zenyе ubora kuwa 0% na bidhaa zitokazo nje ya nchi iwe 10%.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kuhusu ushauri wa vifaa bandia vya urembo kwa wanawake na wanaume kutohana na kupelekea kututoa kwenye uhalisia wa Utanzania wetu, ni bora ushuru kuwa ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vitengenezavyo ndani ya nchi kuwa 25% na kutoa nje 35%. Tukiona huruma tujue wazi kuwa uhalisia wa wananchi wetu wa Utanzania utatoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongeza jitihada ya Serikali ya kuunganisha nchi za jirani, mkoa na mikoa, wilaya na wilaya ambayo ni hali halisi inayoendelea katika ukamilifu wake na kurahisisha wafanyabiashara kuchukua mazao kwa wakulima na kupeleka sokoni ambako wanapata kipato cha juu na kizuri ambacho kingekuwa

vema kupatikana na wakulima. Hivyo nashauri Serikali kuona umuhimu sasa wa kuangalia vinginevyo na kuwapangia bajeti kuweka miundombinu ya kuitika mwaka mzima (masika hadi kiangazi) na kuunganisha vitongoji na vijiji na kata ambako ndiko kwenye mashamba ya uzalishaji ili wakulima wapate wepesi wa kufikisha mazao yao sokoni kwa urahisi na kuongeza vipato vyao kuliko kuwapa nguvu zaidi wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri kwa msisitizo kuhusu na kuifanya usanifu barabara ya Kibaoni - Kiliyamatundu - Miangalua na kukutana na barabara kuu ya Tunduma - Sumbawanga kuwa ya lami kwani daraja kubwa la Momba ni lenye thamani kubwa lakini linaunganishwa na barabara za vumbi sio sahihi na hatutokuwa tunalitendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 38; nashukuru kwa kazi nzuri na pongezi ya jitihada kwa Serikali katika kuwaunga mkono wananchi kwa nguvu wazitoazo kwenye maendeleo ya kujenga miundombinu ya afya, elimu kwenye maeneo yetu na kuamua kutenga bajeti ya bilioni 271.33 za kukamilisha maboma kwa 2018/2019. Hata hivyo, bado maboma yanaendelea kwani kuna baadhi ya shule za msingi, sekondari, zahanati na vituo vya afya kwa asilimia ndogo waliokamilisha miundombinu katika ukamilifu wake. Pesa itoke kwa ukamilifu ili haya maboma 144 kwenye halmashauri zetu yakamilishwe. Bajeti hii ya 2019/2020 tuiboresha na kuisimamia kutoka kwa wakati kwani maboma bado ni endelevu kutokana na elimu bure, ambayo ni faida kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINABU A. KATIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri kwa sababu tunakoelekea kwenye uchumi wa viwanda tunahitaji kuwekeza katika rasilimali watu. Rasilimali watu ya uchumi wa viwanda ni kada ya kat ihasa mafundi mchundo. Nashauri wanafunzi wa vyuo vya ufundi wenye

uhitaji wawekwe kwenye mpango wa kukopeshwa na Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo; Tanzania haiwezi kuwa Tanzania ya viwanda kama hatujaimarisha kilimo, viwanda vinavyotegemea malighafi zinazotokana na kilimo. Kilimo chetu ni bado kilimo cha mkono, tunahitaji kuwa na bajeti ya kutosha kwa ajili ya kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipunguze kodi kwenye pembejeo ili wakulima waweze kulima kilimo cha kisasa na kisicho na kikwazo chochote. Naiomba Serikali itengete bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuwaajiri Maafisa Ugani ambaao watawasaidia wananchi kulima kilimo chenyet tija ambacho kitatusaidia kupata malighafi za kutosha kwenye viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi nchini wanafanya kazi kwa kinyongo na bila ubunifu kwa sababu wana madeni yao ya muda mrefu na hasa Walimu, ndio maana elimu inazidi kushuka. Naiomba Serikali ilipe madeni hayo ili kuwamotisha watumishi pia waongezewe mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi ya mitambo ya kuchimbia visima; kutokana na uhaba wa maji nchini, naiomba Serikali iondoe kodi kwenye mitambo ya kuchimba visima ili watu wengi wachimbe visima kwani bei ya uchimbaji itashuka na hatimaye tutapunguza tatizo la maji nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kodi kwenye nywele za bandia; ni kweli tunahitaji kuongeza pato la Taifa, lakini naomba tungaangalia vile vitu vikubwa kuliko kuangalia kwenye nywele za bandia ambazo ni kama Serikali inawakandamiza wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi kukusanywa na *TRA*; kutokana na kushuka kwa makusanyo kwenye halmashauri zetu na hasa kodi zinazotokana na majengo, naomba Serikali irudishe makusanyo hayo yakusanywe na halmashauri lakini yawekwe moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, taulo za kike, nasikitika kwa kuondoa msamaha wa kodi kwenye taulo za kike. Serikali ifikirie upya uamuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Maendeleo kutokwenda kwenye miradi kwa wakati na pia kupelekwa bajeti ndogo. Katika mikoa yote pesa ya maendeleo imekwenda chini ya asilimia 50, hivyo naishauri Serikali kupeleka kwa wakati na kiasi chote kilichoidhinishwa na Bunge kipelekwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta binafsi, tatizo kubwa ninaloliona ni kwamba Serikali inachukua fedha taslimu kwenda kufanya miradi kama vile kununua ndege. Nashauri Serikali kutumia sekta binafsi kuendesha miradi hii mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Liganga na Mchuchuma; naiomba Serikali ifikirie ni namna gani inaweza kuharakisha utekelezaji wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga. Kama kuna kikwazo kwa mwekezaji, basi Serikali ibadilishe mwekezaji mwingine atakayekuwa na vigezo vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashine za *EFD*; mashine hizi ni mbovu kila zikipelekwa kwa fundi unatakiwa kulipa shilingi laki moja na nusu (150,000/=). Naiomba Serikali iangalie upya mfumo wa mashine hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimechangia kwa kuongea na malizia *point* yangu ya mwisho ambayo muda haukutosha. Naishauri Serikali kule bandarini iweke *single receiving point* ya mafuta, faida kubwa ya hii

kwana hupunguza *dermrage charges*, ambayo humpunguzia mzigo muagizaji wa mafuta au mfanyabiashara wa mafuta. Vilevile itampunguzia gharama mlaji ikiwemo gharama za kuendesha viwanda zitaungua. Serikali pia itapata faida endapo tukipunguza *dermrage change* ambazo zinaingia kwenye gharama ya uendeshaji kwa mfanyabiashara wa mafuta ambayo inaathiri mapato ya Serikali kwa maana ya *corporate tax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *single receiving point* ya mafuta hii itaondoa utunzaji wa mafuta kwenye matanki ya makampuni binafsi kuwepo unafuu wa upotevu wa mafuta kwa 3% mpaka 5% kitu ambacho hupunguza mapato ya Serikali sababu wafanyabiashara wa mafuta wanaingiza kwenye gharama za uendeshaji ambazo zinaenda kuathiri *corporate tax*. Kwa kuwa hii ni sheria watu wanataka *advantage* kukwepa kodi.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya na kuweza kuchangia katika bajeti hii muhimu ya Serikali. Naomba nianze na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mpango pamoja na Naibu Waziri wake Dkt. Kijaji kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeisikia bajeti lakini nimepata fursa ya kuisoma. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na jopo lake kwa kuyafanyia kazi baadhi ya mambo. Niwapongeze sana kwanza kwa kuondoa tozo ya uchenjuaji madini, kwa hilli niseme Mheshimiwa Waziri umesaidia sana sekta ya madini kwani kwa uchenjuaji kufanyika hapa hapa nchini kwetu itasaidia sana kuleta ajira hapa hapa nchini, tofauti na awali ambapo madini kama ya Tanzanite yalikuwa yakipelekwa nje kama India kwa ajili ya uchenjuaji ambapo tulikuwa tukipoteza ajira lakini fursa nydingi kwa nchi yetu. Pamoja na mazuri haya ya kuondoa tozo mbalimbali ikiwemo tozo ya kila mwezi ya visima (maji) bado kuna mambo ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la taulo za kike (*pads*). Kama kuna jambo Mheshimiwa Waziri naomba nichukulie na kukuomba leo basi ni suala la *VAT* katika taulo hizi za kike. Mimi ni mtoto wa kike naelewa changamoto zinazopatikana katika kipindi cha hedhi. Mimi nakaa na wanafunzi wa kike, naona, najua shida wanayoipata pindi tu wanapoingia katika siku zao. Mtoto huyu wa kike kila mwezi anapoteza takribani wiki nzima ya kutuingia darasani kutokana na kushindwa kwenda shule kwa kuwa tu anaohofia kuchafuka na kuonekana awapo shulenii na ni kwa sababu tu hana taulo ya uhakika ya kujihifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, taulo hizi za kike ziweze kuingizwa bila *VAT* ili kurahisisha upatikanaji wa taulo hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko vijjini hali ni mbaya, watoto wa kike kuna maeneo ambayo wanatumia mpaka majani kutokana na uwezo wao kuwa duni, maisha ya wananchi ni masikini, mzazi hawezi kununua *pads* hizi kwa bei iliyopo. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri acha kumbukumbu kwa watoto wa kike katika uongozi wako, wasaidieni taulo hizi zipatikane kwa urahisi; hivyo hakuna budi kuondoa *VAT* ili taulo hizi zipatikane kwa wingi vijjini na mijini na utakuwa umemsaidia sana mtoto wa kike aliyepo hata kule kwetu Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la uwekezaji katika nchi zetu zilizoendelea. Suala la uwekezaji ni muhimu sana sana. Sasa Mheshimiwa Waziri niombe Serikali yetu ipeleke pesa katika uwekezaji wote uliofanyika nchini. Kwa wakati miradi ya umeme wa Mto Rufiji Mradi wa *Standard Gauge* na bandari zote, kwa miradi hii kukamilika tutawenza kupiga hatua kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la uwekezaji niombe sana Mheshimiwa Waziri, ni lazima watu wa *TRA* watengeneze mazingira mazuri na wafanyabiashara ni lazima tuwakaribishe na kuwapa fursa wawekezaji binafsi.

Tumeona wananchi wakilalamikia hali ya biashara kuwa ngumu na tuhuma zikienda kwa *TRA*; hata namna ya ukusanyaji kodi na hasa wafanyabiashara wengine wamefikia kufunga biashara. Ni muombe sana Mheshimiwa Waziri kwa hali yoyote ile Serikali yetu ihakikishe tuna *encourage* wawekezaji kwani kwa kufanya hivyo tutaongeza ajira za kutosha na mapato pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie suala la malipo. Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango wafanyakazi hasa walimu wamekuwa wakicheleweshewa malipo mbalimbali. Niombe sana malipo kwa wafanyakazi yaweeze kufanyaika kwa wakati na madeni wanayodai Serikali basi waweze kupatiwa kwa wakati ahsante.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia napenda kuzungumzia miradi mitatu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni Mradi wa Barabara ya Wete hadi Chakechake, takribani kilomita 40; Bandari ya Mpiga Duro Malindi Zanzibar na Mradi wa Ujenzi wa *Airport* ya Pemba na hitimisho la Uwanja wa Ndege wa Unguja *Terminal*/3. Serikali ya Muungano ikishirikiana na Wizara ya Fedha wamekataa miradi hii isiendelee na Wazanzibar wasifaidike na miradi hii; uchumi wa Wazanzibar uendelee kudidimia. Nasema hivi kwa sababu Serikali ya Muungano imekataa kuweka saini kwenye miradi yote hii maana yake hawapendi kuona maendeleo katika upande wa pili wa Muungano yakinoteka.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni unyanyasaji na ni hasadi ya hali ya juu kabisa. Serikali ya Muungano inashindwa kujenga kilomita 40 Zanzibar lakini Tanzania Bara wanajenga zaidi ya kilomita 1,500 za barabara; hii kama si hasadi ni nini? Kila siku tunaambiwa tu wachochezi tukizungumzia suala la Muungano, kwamba halina umuhimu wowote kwa maslahi ya Zanzibar. Leo hii limedhihirika kwa kukataa kuweka saini; halafu tunaambiwa ni ndugu zetu wa damu. Damu gani hii ya kudhulumiwa? Huu si ndio udugu wa makopa wa kukutania kwenye sufuria, ambao hauna faida yoyote ile? Bora ukatike, udugu huu hauna tija yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali ya Muungano iweke saini ili tujenge barabara, bandari ambayo inaweza kufunga gati kwa meli zisizozidi 5 ingawa ya Bagamoyo mlikata wenyewe ambayo ingeweza kufunga nanga meli takribani 35. Mliikataa wenyewe ila sisi tunahitaji hiyo bandari na viwanja vijengwe ili kuinua uchumi wa nchi yetu. Serikali hii ya Awamu ya Tano haijui kipaumbele chake. Iliingia madarakani kwa kujigamba, kujinata na mbwembwe tele kuwa ni Serikali ya viwanda mpaka, sasa hatuoni viwanda hivyo na vichocheo vya viwanda havipewi pesa za kutosha. Tukiangalia sekta ya kilimo imetupwa mbali wala haithaminiwi. Ni wazi kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Kilimo inachangia ajira kwa asilimia 70, Pato la Taifa kwa asilimia 28.2, lakini ukuaji wake ni mdogo sana na wa kusuasua, sawa na asilimla 5.2. Hali hii inapelekea kutofikia ndoto ya Tanzania ya Viwanda. Napenda kuishauri Serikali kuondoa kodi zifuatazo ili kufikia kwenye ndoto ya Tanzania ya Viwanda.

(a) Kodi kwenye uwekezaji wa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

(b) Hali kadhalika kuondoa kodi kwenye viwanda vinavyotengeneza na kukarabati mashine, zana na pembejeo za kilimo, uvuvi na mifugo.

(c) Pia uwepo wa umeme wa uhakika.

(d) Kushirikisha sekta binafsi kwa kupitia mpango wa *PPP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mpango ayachukuwe haya na kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imewasusa watumishi wa umma ambao ni walipa kodi wa uhakika. Serikali hii imekuwa ikisuasua kuwapa watumishi nyongeza ya mshahara ya kila mwaka (*annual increment*)

pamoja na madai yao mengi kama fedha zao za likizo, kupandishwa madaraja na malimbikizo ya mishahara; jambo ambalo ni la kisheria na kikanuni. Hata wanaopandishwa madaraja halafu unastahiki pindi wakipandishwa madaraja hulipwa mshahara uleule wa mwanzo; jambo ambalo si halali. Hata hivyo katika mwaka huu wa fedha nimeona takribani trillioni saba. Hizi ni za mishahara tu hizo nyingine sijazona.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali ya Awamu ya Tano wataacha kuwakandamiza watumishi hawa? Huku ni kuwafanya maisha yao yaendelee kuwa magumu; na pia Serikali hii haina mia njema kwa watumishi hawa. Hali kadhalika kuna dalili ya kuwadhulamu mafao watumishi hawa ambao ni walipa kodi wa uhakika wa nchi hii. Tunaitaka Serikali iache mara moja tabia hii ya kuwadharau watumishi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kuhusu taulo za kike. Tunaitaka Serikali iache kigeugeu itoe hiyo kodi kama ilivyofanya awali ili watoto wetu wasitirike na kutowatoza kodi kutokana na maumbile yao na jinsi yao. Huu ni unyanyapaa na ubaguzi wa hali ya juu, kuwatoza kodi kila mwezi na wengine mwezi mara mbili kwa ajili ya maumbile yao. Jambo hili halikubaliki na hata dini zetu hazikubali. Naomba kuwasilisha na naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani na yale yenye manufaa ya Waheshimiwa Wabunge wengine. Ahsante.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kukushukuru wewe na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuweza kusimamia na kutoa machango wangu katika hoja hii muhimu ya Hali ya Uchumi wa Taifa, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti Iliyopita pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja kwa sababu zifuatazo;

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na viambatisho vyake imeandaliwa vizuri sana kwa sababu imejielekeza kwa uwazi kabisa wapi tulipotoka wapi tulipo katika kutekeleza ilani ya CCM 2015 na utekelezaji wa Mpango wa Taifa uliozingatia pia Mpango wa Maendeleo Endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa kuwa katika mwaka huu wa fedha tunaomaliza kesho kutwa Serikali imefanya kazi nzuri ya kukusanya mapato, kudhibiti mapato, yaliyokuwa yakipotea pamoja na kupeleka fedha katika miradi ya maendeleo. Mwaka huu kila mkoa umepata fedha nyingi ukilinganisha na miaka mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa sababu bajeti hii imegusa maeneo yote ambayo Mheshimiwa Rais ameyawekea mkazo tangu achaguliwe; Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana kupitia hotuba yake ukurasa wa 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa sababu bajeti ya 2019/2020 imepunguza utegemezi kwa kiwango kikubwa. Naunga mkono kwa sababu kodi zote zaidi 54 zilizokuwa vikwazo katika kukuza uchumi zimeondolewa. Naunga mkono kwa sababu vipumbele vilivyowekwa vinalenga kukuza uchumi wa taifa na kutoa huduma kwa wananchi waliotuchagua. Naunga mkono kwa kuwa bajeti hii 2019/2020 ni bajeti ya matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya naomba nijielekeze katika maeneo machache niliyoyachagua kuyatilia mkazo ambayo yanagusa wananchi ninaowawakilisha ambaao ni wanawake wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambaao walio wengi ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Kilimo. Zaidi ya Watanzania 65 wanaotajwa kujihusisha na kilimo asilimia 80 ni wanawake ambaao wanalima kilimo cha kujikimu tu, kilimo cha kutegemea mvua, kilimo cha jembe la mkono, kilimo bila utaalamu, mbegu duni, kilimo ambacho mazao yao

hayajaongezewa thamani na mazao yao kukosa soko na kukosa mitaji ya kuwekeza katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu; pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kuhakikisha kilimo chetu kinaleta tija kwa wanawake, wananchi na taifa kwa ujumla naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwaondoa wanawake katika kilimo cha jembe la mkono na kutumia nyenzo za kisasa, kama vile majembe ya kukokotwa na ng'ombe, matreksa pamoja na kupatikana tena kwa pembejeo za kilimo na kwa wakati; na hapa benki ya kilimo ihusike kikamilifu kwa sababu lengo la kuanzisha benki hii lilikuwa ni kuwakomboa wakulima wanyonge ambao wengi wao ni wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi iongeze wigo wa kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 475.052 hadi kufikia hekta 1,000.000, ikiwa ni hatua muhimu ya kutekeleza mpango ulioandaliwa na Wizara ya Maji 2018/2019. Kwa kutekeleza mpango huu kilimo chetu kitakuwa ni kilimo chenye kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuongeza wataalam wa kilimo na kuwawezesha watekeleze wajibu wao kikamilifu. Serikali ipeleke pembejeo za kilimo tena kwa wakati. Serikali kuhakikisha inawawezesha wanawake na wananchi kupata masoko ya mazao ya ndani na nje. Serikali ihakikishe kunakuwepo na viwanda vya kusindika mazao ya wakulima. Serikali iwawezeshe wanawake mitaji ya kutosha katika sekta ya kilimo ili waweze kuanzisha miradi mikubwa. Serikali itoe elimu kwa wakulima juu ya kilimo bora ili wanawake na wananchi waweze kuzalisha mazao yenye viwango vyenye ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwezesaji wa Wanawake Kiuchumi. Pamoja na kwamba wanawake ndio wazalishaji wakubwa, wanawake pia ndio walezi wa familia,

wanawake ndio hata wanapopata kipato walio wengi kipato hicho hukielekeza katika familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia fursa mbalimbali, bado wanawake walio wengi ni masikini na hata wanachokizalisha hawanufaiki nacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Manunuzi. Swali; Bunge tulipitisha Sheria ya Manunuzi iliyoweka kifungu kwamba kila manunuzi yatakayofanyika au tenda zitakazotolewa asilimia 30 zielekezwe kwa wanawake. Pia tumepitisha sheria ya kuzitaka kila halmashauri kutenga asilimia 10 kwa ajili ya kuwzesha vikundi nya kiuchumi. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri bado lipo tatizo la baadhi ya taasisi hizi kutekeleza Sheria ya Manunuzi kwa kiwango cha asilimia 70 kama ilivyoainishwa kwenye sheria baadhi ya halmashauri zinashindwa kutekeleza sheria ya kutoa asilimia 10 ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Vilevile mchango wa wanawake unaotolewa katika kulea familia haujathamanishwa katika kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali; ningependa kujua tangu sheria hii imeanzishwa wanawake wangapi wamenufaika na Sheria hii ya Manunuzi na katika maendeleo? Ni ujenzi wa barabara, ujenzi wa reli nakadhalika. Swali tumepitisha sheria ya kutenga asilimia 10 ya wanawake na vijana na watu wenye ulemavu. Tangu sheria hii imepitishwa ya kila halmashauri kutenga asimilia 10 ya mapato yake ya ndani ni wanawake wangapi wamenufaika ukilinganisha na kabla ya sheria haijarekebishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali; wanawake wengi wameanzisha vikundi nya kiuchumi; tatizo lao kubwa ni kukosa mitaji, hii ni kwa sababu baadhi ya halmashauri mapato yao yako chini hivyo vikundi havipati mikopo ya kutosha ya kuweka misingi imara ya kiuchumi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzisaidia halmashauri kuongeza vyanzo

vya mapato na kufanya uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji katika halmashauri nyingi zinazotegemea mapato yanayotokana na kilimo cha kutegemea mvua? Zikiwemo halmashauri za Musoma Vijijini, na Butiama kuititia Bonde la Bugema na Mto Mara?

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Maji kwa Wanawake na Wananchi Katika Kuchangia Uchumi wa Taifa. Kama nilivyotangulia kusema kuwa wazalishaji wetu wakubwa katika taifa ni wanawake. Wanawake walio wengi wanashindwa kufanya kazi za uzalishaji mali kutokana na tatiozo la maji. Ushauri; Serikali iendelee kutafuta fedha kwa ajili ya kuwekeza katika miradi ya maji ili kuwawezesha wanawake kuacha kutembea umbali mrefu kwenda kutafuta maji na badala yake washiriki kufanya kazi zitakazowakomboa kiuchumi. Ushauri; kwa kuwa kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri deni la Taifa linahimilika, Serikali iendelee kutafuta mikopo na fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji. Huduma hii ya maji ikiboredhwa itawakomboa wanawake ambao ndio wazalishaji wakubwa na itachochea uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upotevu wa Fedha za Miradi ya Maji. Fedha za miradi ya maji zimekuwa zikipotea na miradi kutokamiliaka kwa sababu za usanifu mbaya wa miradi hiyo na kupewa kandarasi wasio na sifa. Swali; ningependa kujua, je, Serikali imejipangaje kupata wataalamu wa kusanifu miradi na wakandarasi wenye uwezo wa kujenga na kusimamia miradi ya maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mchango wa Wanawake Unaotolewa Katika Kulea Familia. Wanawake wamekuwa mstari wa mbele katika kulea familia. Je, ningependa kujua kama mchango wa wanawake umethaminiwa na kuingizwa katika mchango wa taifa wa kukuza uchumi? Nimeomba kujua kwa sababu wanawake walio wengi wanatoa mchango katika kulea familia lakini kwa bahati mbaya mchango wao haujathaminika; hivyo, wamenituma niulize, je, Serikali inautambua?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa mapato pamoja na kuipongeza Serikali kwa kukusanya mapato na kuiwezesha Serikali kutekeleza malengo yake ikiwa ni pamoja na kuliona mishahara na kutekeleza miradi ya maendeleo ni na ushauri kidogo katika eneo hili. Serikali iendelee kufuatilia kwa karibu mianya yote ya upotevu wa mapato katika bandari, uwanja wa ndege, bandari bubu, bandari kavu, mipakani pamoja na kwenye manunuzi ya umma hasa katika miradi ya maendeleo nakadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, taulo za watoto wa kike. Nashauri Serikali iwezeshe wanawake wajenge viwanda vidogo vya kuzalisha taulo za kike na kutoa bei elekezi. Fedha inayopelekwa halmashauri kwa ajili ya maelekezo ya kununua taulo za kike ipelekwe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya ujasiriamali; changamoto zake ni kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kupora mapato ya halmashauri kwa watu ambao wanatumia miundombini ya masoko ya halmashauri. Mfano Manispaa ya Moshi kuna masoko matatu makubwa yaliyokuwa yanaipa halmashauri shilingi za Kitanzania takribani milioni mia tatu lakini wafanyabiashara/ wajasiriamali ambao wengine wana uwezo mkubwa wa mauzo ghafi ya zaidi ya shilingi milioni ishirini (20,000,000).

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali Kuu imepoteza mapato kwa vile baadhi ya wafanyabiashara/ wajasiriamali waliokuwa wanalipa kodi ambao wana maduka madogo kama dawa, migahawa na mengine kama hayo wamejifunika kwenye vitambulisho. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba ni muhimu sana kuangalia upya mpango huu wa vitambulisho vya wajasiriamali ili iweze kufanikisha

nia njema ya Serikali ya kuwatambua wajasiriamali wadogo wadogo bila kuathiri mapato ya Serikali Kuu na mapato ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *tax base* (wigo wa walipa kodi); hotuba ya mapendekezo ya bajeti inaonesha kwamba Serikali inategemea kukusanya trillioni 23.05 kwa mapato ya ndani ambapo trillioni 19.01 ni mapato yanayotokana na kodi, trillioni 3.18 mapato ya vyanzo visivyo vyakodi na bilioni 765.5 mapato ya halmashauri. Mashaka yangu kwa mapendekezo ya kiwango hicho cha makusanyo ya ndani hususani yanayotokana na kodi ni namna ambavyo Serikali itafikia malengo hayo wakati mwaka 2018/19 makusanyo kwa wastani wa kila mwezi ni trillioni 1.2 ambapo wafanyabiashara wamekamuliwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TRA* lazima ipanue *tax base* ya nchi ili utafutaji wetu wa kodi usiwaumize wafanyabiashara wachache kiasi kwamba inawafanya washindwe biashara. Kwa mfano, Watanzania walipa kodi hawazidi 2,700,000 ambapo waliosajiliwa kwenye VAT hawazidi milioni moja (1,000,000). Kwa taifa ambalo lina watu zaidi ya milioni 55, mzigo huu ni mzito sana kwa hao Watanzania 2,700,000 ambao wamekuwa wakibeba jukumu hilo kila siku la kuzalisha fedha kwa ajili ya kundi lote la Watanzania. Nashauri Serikali iyatazame kwa karibu makundi yafuatayo ili yachangie kwa usahihi katika makusanyo ya kodi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kundi la wakulima wakubwa na wa kati ambapo mpaka sasa hawajaratibiwa vizuri ili kushiriki katika wajibu wao wa kulipa kodi. Mpaka leo katika nchi yetu kundi la wakulima linawekwa katika daraja moja bila kutenganisha wakulima wakubwa na wakulima wa kati. Eneo hili linaficha watu wengi, zaidi ya asilimia tano ya wakulima ambao ni wakubwa na wa kati lakini hawalipi kodi lakini wanamiliki utajiri mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kundi la wafugaji wakubwa na wa kati. Kundi hili lazima liratibiwe vizuri ili lilipe

kodi. Mwananchi anapomiliki ng'ombe zaidi ya mia moja anapaswa kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa kulipa kodi. Kundi hili linaharibu sana miundombinu ya nchi lakini halishiriki kikamilifu katika kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kundi la watu wanaomiliki majengo makubwa na ya kat; mwananchi anamiliki ambayo ameweka wapangaji lakini hajaratibiwa vizuri katika kulipa kodi. Kundi hili ambalo ni kubwa la watu wenye kipato cha kat iimeachwa nyuma sana kwenye kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza idadi ya wafanyakazi katika Mamlaka ya TRA. Serikali katika mapendekezo yake ya bajeti inaonesha kwamba itaongeza juhudzi za kukusanya kodi. Nashauri Serikali longeze idadi ya wafanyakazi wa TRA ili waweze kufikia walipa kodi wengi zaidi kadri inavyowezekana ili kupanua tax base yetu. Serikali inatakiwa itambue kwamba kuongeza wafanyakazi katika Mamlaka ya TRA ni uwekezaji kwa vile ni kwa dhamira ya kukusanya mapato zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ukaguzi wa mahesabu unaofanywa na *TRA* kwa wafanyakabiashara. Serikali lazima ipitie upya sheria inayoipa mamlaka *TRA* kufanya ukaguzi wa mahesabu ya mlipa kodi kila baada ya miezi mitatu mpaka mitano. Sheria hii imekuwa mwiba sana kwa wafanyakabiashara kwa vile kuna ugumu wa kutunza kumbukumbu za biashara kwa miaka mitano. Pia kodi zinazopatikana baada ya ukaguzi wa *TRA* zinakuwa kubwa kiasi kwamba haziakisi uwezo wa wafanyakabiashara, hivyo kupelekea kufungwa na kufilisika kwa wafanyakabiashara. Nashauri Serikali ibadilishe muda wa ukaguzi uwe kwa kipindi kisichozidi miaka miwili kwa *TRA* kufanya ukaguzi wa mahesabu kwa wafanyakabiashara ili kuwafanya wafanyakabiashara wanapokutwa na malimbikizo, riba na faini waweze kulipa kwa kiasi kidogo kuliko malimbikizo ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa kulipa malimbikizo na faini uwe mrefu wa kutosha. Nashauri Serikali ipitie upya utaratibu wake kuhusu muda ambaao mlipa kodi anatakiwa kulipa malimbikizo, riba na faini baada ya ukaguzi wa *TRA*. Muda wa miezi mitatu kwa awamu tatu unaokubalika kikanuni za *TRA* unakuwa siyo rafiki kwa walipa kodi kwa vile kama kiasi cha malipo kitakachopatikana baada ya ukaguzi kinakuwa kikubwa inakuwa ni vigumu kwa mlipa kodi kutekeleza. Nashauri muda wa kulipa hayo malimbikizo, riba na faini uwe muda usiopungua miezi 12 na usiopungua miezi 24. Muda huo utafanya mlipa kodi kulipa kwa awamu 12 au 24 kwa kila mwezi kulipa *installment* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vyta mapato ya halmashauri; Serikali lazima itazame upya uamuzi wake wa kuchukua vyanzo vyta halmashauri kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, miradi midogo ya elimu, afya na huduma nyingine za jamii imekuwa ikitekelezwa na halmashauri hivyo kuipa nafasi Serikali Kuu kutekeleza miradi mikubwa. Ni vizuri halmashauri ziimarishe zaidi ili ziweze kuisaidia Serikali Kuu majukumu ya maeneo ya chini ambayo ndiyo yana wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, *TRA* haina wafanyakazi wa kutosha kufikia vyanzo vyote vyta kodi, hivyo, kwa kutumia halmashauri wanakuwa wamepata msaada mkubwa sana. Kwa maoni yangu, mpaka sasa bado *TRA* haijaweza kukusanya kikamilifu vyanzo vikubwa ilivyonyavyo. Nashauri Serikali iimarishe uwezo wa halmashauri ili ziwe na uwezo wa kukusanya kwa ukamilifu mapato yake.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudzi zake kubwa sana kuleta maendeleo ya Watanzania. Awamu hii ya Tano wananchi wameweza kuona utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyosimamiwa na Serikali kuitia usimamizi bora wa fedha za ndani. Watanzania kwa ujumla

wameanza kufahamu umuhimu wa ulipaji kodi na athari zitokanazo na kutolipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali iendelee kutoa elimu kwa walipa kodi kuititia vyombo mbalimbali na kuchukuliwa hatua za kinidhamu wakwepajji kodi. Pia usimamizi zaidi wa fedha uimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendelee kusimamia wafanyabiashara ambao bado wanaendelea kutumia risiti za mkono na kukwepa matumizi ya risiti za kielektroniki. Kumekuwa na baadhi ya wafanyabiashara huwalazimisha wanunuvi kulipa bei ndogo bila risiti za kielektroniki na bei kubwa kwa risiti, hivyo, malengo ya makusanyo ya fedha kutokufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti iliyopita tumeweza kuona upungufu katika fedha iliyopangwa kutolewa na wafadhili katika miradi ya maendeleo na kusababisha baadhi ya miradi kutokukamilika. Naiomba Serikali kutekeleza mpango wake madhubuti wa ushirikiano wa wadau wa maendeleo ili kuendelea kupokea misaada na mikopo kwani bado hatujaweza kusimama wenywewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele; pamoja na vipaumbele vivilivoainishwa katika bajeti hii ambapo njia na vyanzo muhimu vya mapato ya Serikali nashauri:-

(1) Kilimo na mifugo viongezewe fedha zaidi ili kuimarisha mapato zaidi ya Serikali.

(2) Utafiti uboreshwe kwa kutengewa fedha ya kutosha.

(3) Uvuvu wa Bahari Kuu uainishwe katika vipaumbele vya bajeti kwani tunapoteza rasilimali nyingi sana wakiwemo samaki kuititia meli za nje wanazovua katika mipaka yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuangalia namna itakavyowezekana kuhusu baadhi ya sheria ambazo zinatofautiana na Zanzibar na kuleta vikwazo kwa wananchi na wafanyabiashara wa Zanzibar na kwengineko nchini. Utaratibu bora ufanyike ili kuwawekea mazingira mazuri ya kibiashara na kuondoa kero zisizokuwa za lazima kila mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunaamini na kutambua kwamba biashara ndiyo mionganoni mwa vyano vikuu vya mapato ya Serikali. Juhudi za Mheshimiwa Rais kukutana na baadhi ya wafanyabiashara tunaendelea kuzipongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kusamehe jumla ya *shs. 22 billion* za Kodi ya Ongezeko la Thamani kuititia umeme unaonunuliwa na Shirika la *ZECO* Zanzibar. Kitendo hiki kimewatia moyo sana wananchi wa Zanzibar. Naiomba Serikali iendelee kutatua baadhi ya kero zinazowaletea adha wananchi kadri pale uwezo utakaporuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, niendelee kuipongeza Serikali kwa kuondoa tozo mbalimbali zilizokwuwa zinakwaza wananchi. Ni ushahidi tosha kwamba Serikali yetu ni sikivu na inajali wananchi wake. Hongera sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Mgufuli, hakika wewe ni mtetezi wa wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kutilia nguvu suala la utafiti ili kukuza na kupanua uchumi katika nyanja mbalimbali kwa uhakika.

MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji duni wa mapato unavyoathiri utekelezaji wa bajeti ya Serikali unatokana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) imeonesha udhaifu na uwezo mdogo wa ukusanyaji mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ilitakiwa kukusanya shilingi trillioni 17.315 badala yake, ilikusanya shilingi trillioni 15.386 ikiwa ni pungufu ya shilingi trillioni 1.929.

Mheshimiwa Naibu Spika, natolea mfano wa ukusanyaji wa kodi za majengo, nikuombe Waziri jaribu kuandaa mfumo wa kushirikisha Serikali za Mitaa yaani maafisa wa *TRA* wawatumie watendaji wa mitaa kwa kuwa wlae watendaji wa mitaa kazi zao za kila siku wako mitaani nyumba kwa nyumba, zoezi hili litaleta mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mfumo wa kodi umekuwa ukilalamikiwa sana kwa miaka mingi na jamii ya wafanyabiashara ambao ndio walipa kodi si shirkishi wala si rafiki, jambo ambalo limesababisha kukwepa kodi na hivyo kupunguza wigo wa walipa na mapato ya Serikali, nikuombe Waziri wa Fedha maeneo ya muhimu unda Kamati Maalum ziangalie kama tatizo hili bado linakuwa ili litafutiwe uvumbuzi.

MHE. OMAR A. KIGODA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja, pili niwapongeze Mawazili wote wawili na watendaji wao kwa bajeti zuri waliyowasilisha. Mimi nataka kujikita kwenye ushauri kuhusu suala la mwananchi kutoa mizigo bandarini mwenyewe. Niimpongeze Serikali kwa kuleta utaratibu huu, hii itasaidia sana kwa mwananchi kupunguza gharama kubwa zitokanazo na makampuni ya *clearing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba Serikali lazima itafute utaratibu au mpango ambao utamsaidia huyu mwananchi kutoa mizigo yake. Ikiwezekana kuwe na *one stop center* kwa huyu mwananchi aweze kufanya utaratibu wote eneo moja na kumaliza kila kitu na kupata mizigo wake. Niliona utaratibu kama huu Oman.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hutuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Hotuba hii imejaa majibu ya kero mbalimbali za wananchi katika sekta zote muhimu za kijamii kama vile elimu, miundombinu, umeme, reli, barabara, maji, afya, viwanja vya ndege, bandari, madini na kadhalika. Aidha, kero mbalimbali zilizokuwa zinakwaza mazingira wezeshi katika kuvutia uwekezaji nchini Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha vikwazo vilivyokuwa vinasababisha mazingira magumu kuvutia wawekezaji kuja hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi mbalimbali na tozo zilizokuwa zinakwamisha uwekezaji katika sekta mbalimbali, Serikali imechukua hatua kwa kukutana na wadau ana kwa ana. Kwa mano, Mheshimiwa Rais amekuwa akikutana na wadau muhimu katika sekta za madini na wafanyabiashara kutoka sehemu mbalimbali ambapo katika mikutano yote ambayo Mheshimiwa Rais amepata fursa ya kukutana ana kwa ana na wadau kero za nyingi zimetatuliwa na kurejesha imani ya wafanyabiashara kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa katika miundombinu wezeshi, kwa mfano Serikali imeweza kuanza ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kimataifa *standard gauge (SGR)* ujenzi wa Reli hii ukikamilika utachangia kwa kiasi kikubwa uboreshaji wa huduma katika bandari ya Dar es Salaam ambayo ni bandari muhimu kwa nchi ambazo hazipakanina bahari za Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemocrasia ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, uwepo wa *SGR* katika Tanzania itakuwa ni ukombozi wa moja kwa moja katika ukuaji wa uchumi kwa ujumla katia kusafirisha watu na mizigo ambapo huduma za usafirishaji utasaidia kupatikana kwa vitu na vifaa kwa bei nafuu na hivyo kudhibiti mfumko wa bei nchini kwani maeneo mengi reli hii inapitia katika mikoa mingi hapa nchini. Pia Serikali imeanza kuchukua hatua kuifufua reli ya Kaskazini lengo ni lilelile la

kujenga uchumi kwa usawa katika nchi yetu katika maendeleo ya watu na vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za afya zimeboreshwa kwa kiasi kikubwa ambapo vituo vya afya vingi vimejengwa na kukarabatiwa zikiwemo hospitali za wilaya na mikoa na zile za rufaa, ambapo watanzania wanapata huduma hizi muhimu na kuweza kupunguza kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vya ndege vingi vimeendelea kujengwa pamoja na Serikali kununua ndege mpya ambazo zitarahisisha usafirishaji wa watu na vitu hasa watalii. Utalii ni sekta muhimu katika kuchangia katika kukuza uchumi kwa kuwa chanzo kikubwa cha fedha za kigeni nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanza kwa ujenzi wa mradi mkubwa wa umeme wa maji katika bwawa la *Stiegler's Gorge* utakaozalisha *megawatts 2115* ni mwelekeo sahihi katika kuelekea Tanzania ya Viwanda. Kukamilika kwa mradi huu mkubwa tunayo imani kubwa kuwa tatizo ka mgao wa umeme litakuwa limepata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza sana Serikali kwa kutekeleza kwa vitendo kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kuja Dodoma na kuweza kufanikiwa kukamilisha ujenzi wa Ofisi za Wizara mbalimbali katika Mji wa Serikali Mtumba hapa Dodoma. Nasi tunaipongeza Serikali kwa kuipatia fedha Wilaya ya Mbogwe ili iendelee na ujenzi wa majnengo ya Ofisi za Mkuu wa Wilaya na jengo la Halmshauri ya Wilaya ya Mbogwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo maombi kwa Serikali kutoa fedha kwa ajili ya unejzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Butengolumasa, Iparamasa, Mbogwe, Masumbwe, Mwabomba, Nyankende, Bugomba na Ulowa, Ulowa hadi Kalina ili kuwa chachu ya maendeleo katika maeneo ambako barabara hii inamoitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ba Mipango.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kuweza kuchangia bajeti hii. Katika hatua hii nipende kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote pamoja na watendaji wote kwenye wizara hii kwa kazi kubwa wanayiofanya kwa kufanya uchumi wa nchi yetu uweze kukua vyema na huduma za jamii kuimarika. Mawaziri kwa utendaji wao uliotukuka ndiyo sababu ya Mheshimiwa Rais kuwaamini kuendelea kuhudumu kwenye Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli bajeti hii kwa kaisi kikubwa imekwenda kujibu changamoto mbalimbali kwenye jamii yetu, kwani hakuna bajeti inayoweza kujibu shida za watu wote kwa asilimia 100. Hii ni bajeti iliyozingatia maoni mengi ya Wabunge wakati wakichangia bajeto ya wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa ujenzi wa Tanzania ya viwanja hivyo ni jambo muhimu sana kuimarisha sekta ya kilimo. Tunapokwenda kuimarisha kilimo cha mazao ya kimkakati, nashauri Serikali kuendelea kuwekeza kwenye mazao ya mbegu za mafuta ya kula kama alizeti, ufuta, nazi na mchikichi, hii itatupunguzia uagizaji wa mafuta ya kula. Pamoja na mazao ya jamii ya mikunde kwani pamoja na hayo mazao hayo husaidia kukuza vipato nya jamii husika na katimaye kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto za pembejeo lipo pia tatizo la masoko kwa mazao yetu. Hivyo, naishauri Serikali kuimarisha masoko ya mazao na kuimarisha vyama vya ushirika. Hapa naiomba Serikali kuangalia sera na muundo wa Vyama vya Ushirika kwani vyama vingi vimekuwa ni vyama vya msimj wa mazao, mavuno ua mazao yakiisha na vyama husika huwa likizo na vingi havina uwezo wa kujidoresha wala watumishi wenye weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii Kanda ya Kusini bado haujapewa msukumo wa kutosha kwani viko vivutio vingi Kanda ya Kusini Mikoa ya Lindi na Mtwara havijatangazwa. Ukanda wa Kusini tunahitaji geri la utalii wa picha kwa Pori la Akiba la *Selous*, kwani utalii wa uwindaji hauna nguvu kwa sasa. Mfano Wilaya ya Liwale pamoja na kupakana na *Selous* hakuna manufaa ya moja kwa moja jwa watu wote, lakini pia Liwale kuna Boma la Mjerumani ambalo halitangazwi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sera ya kuunganisha mikoa yetu kwa barabara za lami likapewa msukumo wa kutosha, kwani bado kuna mikoa bado haijaunganishwa kwa barabara hata za changarawe. Mfano Mkao wa Lindi na Morogoro katika Wilaya za Ulanga na Liwale. Barabara ya Nangurukuru- Liwale ni barabara iliyotajwa mara nyingi hata kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Hivyo naiomba Serikali ikafikiria kujenga barabara kwa kiwango cha lami ili kuinua uchumi wa watu wa Liwale na Kusini nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze pia Serikali katika kuimarishe miundombini ya afya kwa ujenzi wa vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za mikoa na zile za rufaa sambamba na upatikanaji wa dawa na vifaatiba, lakini bado tatizo ni kubwa hasa kwa vituo vya afya. Mfano Halmashauri ya Liwale yenye kata 20 zenye jiografia ngumu zina vituo viwili tu vya afya ambapo ujenzi wake unaendelea. Vivyo basi pamoja na shukrani kwa vituo hivyo viwili naendelea kuomba Serikali katuongezea vituo vingine hasa vile ambavyo wananchi wameanza kuweka nguvu zao katika Kata za Barikiwa, Lilombe na Miruwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa LNG Lindi ni mradi wa mfano Barani Afrika nan i mradi muhimu sana kwa taifa letu hasa kwa wakazi wa Kusini, hivyo naiomba Serikali kuharakisha mazungumzo ili mradi huu uweze kuanza, kuwa na majadiliano yasiyoisha kutakatisha tamaa wawekezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji ni miradi iliyohujumiwa muda mrefu hapa nchini. Hapa naomba sasa miwapongeze Mawaziri kwenye wizara hii kuwa hatua walizoanza kuchukua. Iko miradi mingi sana ya maji imesimama, mfano katika Halmashauro ya Liwale yenye vijiji 76 ni vijiji 10 tu ndivyo vijiji vyenye miradi ya maji iliyokamiliika, vijiji 14 miradi imesimama na vijiji 51 havina maji kabisa. Hivyo naishauri Serikali kupitia miradi yote iliyosimama ba wahusika kuendelea kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria. Viko visima 28 Liwale vimechimbwa lakini havina mtandao wa mambomba, hivyo wananchi kukosa huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kusambaza mifugo nchi nzima ni lazima liangaliwe upya ni bora kuimarisha ufugaj wa kisasa kuliko hivi sasa wafugaji wanasantaa nchi nzima. Mfano, Wilaya ya Liwale yenye misitu ya asili sasa inaanza kutoweka kutoke na wafugaji kuvamia mapori bila mpangilio matokeo ya haya licha ya kusambaza mifugo tunasambaza pia mapigano ta wakulima na wafugaji.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watndaji kwa kuleta mapendekezo ya mapato na matumizi mazuri. Baada ya kuchangia kwa mazungumzo sasa napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Haja ya Kuweka Mkakati Maalum wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji. Bado nchi yetu ni ya wakulima, kilimo kitaendelea kuwa muhimili wa kuimarisha utoshelevu na usalama wa chakula, kuchangia Pato la Taifa na pia kilimo kitaendelea kuwa chanzo cha malighafi ya viwanda ambavyo tunavijenga sasa. Ili tufikie malengo hayo, ni lazima tukubali kufanya uamuzi wa maksudi wa kuwekeza katika kilimo. Tanzania ilikubaliana na nchi wanachama wa SADC kupitia Azimio la Maputo kwamba kila nchi mwanachama itenge asilimia 10 ya bajeti yake kwenye sekta ya kilimo ili kuharakisha ukuaji wa sekta hiyo. Je, utekelezaji umefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zifuatazo zinaonesha haja ya kuwekeza katika kilimo.

- (1) Eneo linalofaa kwa kilimo ni 44,000,000 Ha
- (2) Eneo linalolimwa ni 14,000,000 Ha
- (3) Eneo linalofaa kwa umwagiliaji 29,400,000 Ha
 - 3.1. *High Irrigation Dev. Potential 2,300,000 Ha*
 - 3.2. *Medium Irrig. Dev. Potential 4,800,000 Ha*
 - 3.3. *Low Irrig. Dev. Potential 22,300,000 Ha*
 - 3.4. *Eneo linalomwagiliwa (2019) 47,052 Ha. Only*
- (4) Zana za kilimo
 - 4.1. Wakulima wanaotumia zana (matreksa)-10%
 - 4.2. Wakulima waotumia (zana) wanyamakazi 20%
 - 4.3. Wakulima wanaotumia jembe la mkono 70%

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizo hapo juu zinadhihirisha maomba yafuatayo:-

- (1) Ni lazima tuwekeze kwenye ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji (*irrigation and drainage*) ili tulitumie eneo linalofaa kwa umwagiliaji ambalo kwa sasa tumeliendeleza kwa takribani 0.1%.

(2) Tunahitaji kutumia zana za kilimo ili tuweze kulima eneo lote linalofaa kwa kilimo ambalo hivi sasa tumeliendeleza kwa takribani 33% tu (angalia pia taarifa ya CAG ya March 2019 Chapter 2, p.5 sec.2.1). Hatuwezi kuendekeza hekta milioni 44 kwa jembe la mkono. Nashauri Serikali ianzishe *tractor hire and service centers* ambazo zitatoa huduma kwa wakulima wadogo kwa sababu haitawezekana kila mkulima kujinunulia zana za kilimo.

(3) *Cropping intensity and productivity*, kwa kuwekeza katika kiundombinu na mashamba ya umwagiliaji tutaweza kuongeza uzalishaji kwa kulima eneo moja zaidi ya mara moja kwa mwaka (*increased cropping intensity*) kwa kuwa maji yatakuwepo kwa kuwa maji yatakuwepo. Aidha ni rahisi kuongeza uzalishaji wa mazao katika eneo moja kwa kuwezesha upatikanaji wa maji na pembejeo na huduma za ugani (*increased productivity/ production per unit area*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Masoko ya Mazao.

(1) Tunapokuwa na ziada ya mazao, hususan nafaka, nashauri Serikali iweke utaratibu (kama inavyofanya kwenye sukari) wa kuwasimamia wafanyabiashara ili wauze ziada nje ya nchi.

(2) Serikali ianzishe mfuko wa kuhimili bei za mazao (*Price Stabilization Fund*) pindi bei za mazao zinapoanguka hasa katika soko la dunia. Mwaka 2013, Serikali, kupitia Wizara ya Kilimo ilianzisha mchakato wa *price stabilization fund* kwa mazao manne ya Korosho, Kahawa, Pamba na Tumbaku. Kwanini mchakato huo haukuendelea? Mimi nashauri wazo hilo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami nitoe mchango wangu katika hoja hii muhimu ya Bajeti Kuu ya Serikali na Hali ya Uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na uzima ili kuwa miongoni mwa viumbwe vyake kwa ajili ya kumuabudu na kupata nafasi ya kushiriki kutoa mchango wangu kweye hotuba hii ya muhimu kwa mustakabali na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, dada yangu, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Ndg. Dotto James na watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa kuchapakazi kwa bidii, uadilifu na uzalendo mkubwa na kufanikisha miradi mingi ya maendeleo mikubwa na midogo kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii inatekelezwa kwa sababu ya upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini Kuu na Serikali ya Halmashauri nchini chini ya usimamizi mzuri wa Wizara hii ya Fedha kwa kusimamia makusanyo ya mapato ya Serikali vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kumpatia fedha katika Jimbo la Morogoro kwa kituo cha afya Mkuyuni, Mikese na Gwata, kila kimoja shilingi milioni 400; na pia uboreshaji wa barabara ya Bigwa – Kisaki, Mikese – Msombizi na Ubena Zomozi – Ngerengere – Tununguo – Mvuha – Kisaki *Stiegler's* na Madamu – Kinole kwa kiwango cha changarawe na kuweza kuitikika mwaka mzima kwa majira yote ya mvua na juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uboreshaji wa barabara ya Bigwa – Kisaki kwa kiwango cha changarawe lakini bado ule umuhimu wa Serikali kuitengeneza barabara kwa kiwango cha lami uko palepale kwa sababu umuhimu wa barabara hii kwa shughuli za kiuchumi za wananchi wa Morogoro Vijiji umeongezeka, hasa shughuli za kilimo, uwekezaji wa kiwanda cha sukari cha Morogoro *Sugar* pamoja kuwepo kwa Makao Makuu ya Halmashauri ya Mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia barabara hii ya Bigwa – Kisaki ndiyo inayotumika kufika kwenye mradi mkubwa wa kielelezo wa kufufua umeme wa Mto Rufiji (*Stiegler's*). Kuwepo kwa mradi huu na Mbuga ya *Selous* kutaongeza wageni wa utalii na kuongeza mapato ya Serikali na uchumi wa taifa. Kwa umuhimu huo, barabara hii ina umuhimu na ulazima wa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kuweka barabara hii ya Bigwa – Kisaki katika bajeti ya mwaka 2019/2020 kujengwa kwa kiwango cha lami. Ombi langu kwa Serikali kuwashisha ujenzi wa barabara hiyo kwa haraka na kuongeza kiwango cha fedha za bajeti na kuzitoa kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni maombi ya vituo vya afya Kata za Kinole na Tegetero kule milimani kwenye Milima ya Uluguru ambao wako mbali na Makao Makuu ya Tarafa Mkuyani Bondeni. Pia vituo vya afya katika Kata za Ngerengere, Tununguo, Kidugalo na Mkulazi katika Tarafa ya Ngerengere ambako hakuna hata kituo kimoja chenye hadhi ya kituo cha afya ilhali ni tarafa kubwa kuliko tarafa zote kwenye Wilaya ya Morogoro. Pia tuna kambi nyangi za jeshi kituo kikuu cha garimoshi ya kisasa (*SGR*) na ujenzi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Serikali, vituo vya afya katika Kata ya Kibuko ambayo ni kata mpya, Kata ya Kiloka na Tomondo ambazo zina watu wengi sana katika Tarafa ya Mkuyuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba ujenzi wa mabweni na madarasa ya vidato vya tano na sita katika Shule za Sekondari Mkuyani, Nelson Mandela na Ngerengere ili kuwa na shule za vidato vya tano na sita kwenye makao makuu ya tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Serikali kuboresha miundombinu ya Shule za Msingi za Mkunyani, Mikese na Njia Nne Ngerengere kwa sababu zina uhitaji

mkubwa wa vyumba vyaa madarasa vya ziada kila moja zaidi ya 20 kwa kila shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchago wangu kuwasemea watu wa Morogoro Kusini Mashariki, sasa naomba kushauri Serikali katika kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982, Sura ya 290, kifungu 7(1)(g) na kufanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 kupitia kifungu cha 32(a),(b) na (c) kuhusu *produce cess* na kifungu cha 13(4) kuhusu ushuru wa huduma. Sheria hizi zinainyima Serikali mapato makubwa. Ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

(i) Makampuni yanayolima na kuchakata mazao ya miwa na mkonge kulipa kodi ya kuzalisha mazao katika halmashauri wanazolima mazao na kusamehewa kodi ya huduma kwenye halmashauri hiyo.

(ii) Makampuni makubwa yanayolima na kuuza nje ya nchi mazao yao ambao hatuna uwezo wa kukusanya kodi ya mazao kwa wanunuzi, Sheria ya Fedha ya 2019/2020 itamke kuwa muuzaji wa mkonge akusanye kodi hiyo kwa mteja wake kwa niaba ya Serikali na asipokusanya atalipa yeye mkulima mkubwa.

(iii) Mwekezaji/mnunuzi anayenunua mazao halmashauri moja na kwenda kuchakata mazao yake katika halmashauri tofauti na aliyozalisha mazao hayo anapaswa kulipa tozo na ushuru, zote mbili, yaani *produce cess* na ushuru wa mazao kwa halmashauri aliyozalisha na kulipa ushuru wa huduma (*service levy*) katika halmashauri anakokwenda kuchakata mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kuingiza mapendekezo haya katika Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019/2020 ili kuongezea mapato ya Serikali na kuimarisha mapato ya halmashauri na kusukuma maendeleo ya wananchi kwa haraka katika mikoa na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Serikali kuboresha na kupanua miradi chakavu ya maji ya zamani ya Mkuyani na Kivuma pamoja na mradi wa Pangawe – Kizinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipatia pumzi kwa siku nyingine tena. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kumshauri Mheshimiwa Rais kwa roho ya kizalendo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijatenda haki kama sikumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya nchi yetu na wananchi kwa ujumla. Ameleta mabadiliko makubwa ya kimaendeleo kiasi kwamba nikianza kuorodhesha hapa kurasa hizi hazitatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge limepokea mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2019/2020. Hakika taarifa imekaa vyema kabisa na hili nazidi kuipongeza Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara zote wananchi wamekuwa wakiguswa siku zote kuititia tozo katika mafuta na hata vinywaji lakini leo hii tunaona unafuu mkubwa uliowekwa katika hotuba hii. Tunashuhudia mapendekezo ya kufutwa kwa kodi na tozo nyingi na kuleta unafuu wa kuendeleza biashara nchini. Kwa kweli bajeti hii italeta unafuu mkubwa sana kwa wananchi, naweza sema ni bajeti ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Suala la Taulo za Kike; kama Wizara ilivyoleza katika hotuba yake, inakusudia kufuta VAT iliyo kuwa imesamehewa kwa kuwa haikuwa na

tija katika kushusha bei za taulo za kike kama Serikali ilivyotegemea. Ni kweli ndivyo ilivyokuwa na siwezi kuilaumu Serikali kwa kuja na wazo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nipendekeze kwamba kwa kuwa Serikali ilikuwa tayari kufuta kodi hiyo ili wanafunzi na wanawake wa hali ya chini kiuchumi waweze kunufalka kwa kupata nyenzo salama kipindi cha hedhi, basi itafakari upya katika suala hili na kama ikiwezekana taulo hizi zianze kutolewa bure katika shule kwa kuititia mpango wa *ku-ring-fence* ile VAT ya 18% itakayotozwa kutoka kwenye taulo za kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuisisitiza Serikali kwamba ni kweli utoaji wa taulo hizi (kwa kuanzia katika shule) utanyanya sana jinsia ya kike kielimu na kiafya. Ni imani yangu hili halitashindikana kutokana na Serikali, kuititia ruzuku za shule, yaani 10,000/= kwa kichwa imekuwa ikielekeza kiasi kwa ajili ya mahitaji muhimu ya mtoto wa kike. Hii inaleta picha nzuri ya namna gani Serikali tayari ina mpango huo wa kumsaidia mtoto wa kike katika mpango wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ni kwamba fedha hii imekuwa haitoshi kununua taulo hizo kwa ajili ya wanafunzi wa kike. Malalamiko mengi yamekuwa yakielekezwa Serikalini kwa kutotoa fedha hiyo kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali kuiangalia upya ruzuku hii ili ifikie kiwango kitakachotekeleza mchanganuo, ya 10,000/= kwa kila kichwa cha mwanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa taulo za kike, naendelea kuipongeza Serikali kwa msamaha wa *corporate tax* ambayo inasamehewa kwa viwanda vipyta. Hii inaonesha ni namna gani Serikali ina mpango wa kukuza uwekezaji katika sekta hii. Kwa kuzingatia hilo, naleta ombi maalum kwa Wizara kusamehe VAT – Ushuru wa Forodha bandarini katika malighafi za taulo za kike zinazotumika zaidi ya mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda sasa Serikali imekuwa ikisamehe ushuru wa forodha bandarini kwa bidhaa za aina ya taulo za kike pamoja na malighafi za taulo hizo zinazotumika mara moja na kutupwa ilhali malighafi za taulo zinazotumika zaidi ya mara moja zimekuwa zikitozwa kodi hiyo. Ni ombi langu Serikali iliangular hili kwa ukaribu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuanzisha programu ya *Universal Health Insurance* kwa miaka ijayo, basi naishauri kutumia fursa hiyo kuona uwezekano wa kutoa taulo za kike walau za kutumika zaidi ya mara moja (*reusable sanitary pads*) ili kupunguza maradhi na magonjwa yatokanayo na hedhi zisizo salama kwa kukosa nyenzo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hili ya kuchangia. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mpango, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Ashatu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango wangu nilioutoa kwa kuzungumza, naomba niongezee kidogo katika Sekta mbili za Mifugo na Uvuvi pamoja na Utalii. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja kuhitimisha hotuba yake anipatie majibu ya maswali kadhaa ambayo naona yana ukakasi kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunaagiza maziwa ya unga kutoka nje ya Tanzania ilhali Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na idadi kubwa ya kuwa na ng'ombe wengi Barani Afrika baada ya nchi ya Ethiopia? Mheshimiwa Waziri atueleze tunapoteza kiasi gani cha mapato kwa kuruhusu uagizaji wa maziwa haya ya unga; kwa kilo moja ya unga ina uwezo wa kuzalisha boksi nne za lita nne nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanini Serikali imeruhusu matumizi ya *imported milk* kwenye ofisi za Serikali badala ya kuelekeza matumizi ya maziwa ya ndani kama tulivyofanya katika eneo la *furniture*? Moja ya malengo ya kutoza kodi (*import tax*) ni ku-*protect home industries*, lakini tumepunguza sana kodi kwenye eneo hili; tunalindaje viwanda vyta ndani ambavyo vinatoa ajira kubwa kuanzia kwenye ufugaji, soko mpaka viwandani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali isishushe *export levy* ngozi ghafi kuliko kuendelea kuacha ngozi ghafi nyingi kuendelea kuoga ilhali viwanda vyta ndani havina uwezo wa kutumia ngozi ghafi yote tuliyonayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni eneo la maliasili na utalii. Ni vyema Serikali ikawekeza sana kwenye eneo hili. Kwa mfano kwenye Hifadhi zetu za Taifa (*TANAPA*) tulikuwa na hifadhi 16 na ni tano tu ndizo zilizokwua zina-*break even point*. Tumeongeza hifadhi nyingine tano, jumla sasa tunazo 21, na bado zinazo-*break even* ni tano (5) tu. Kwa hiyo tumeiongezea mzigo mkubwa *TANAPA*. Ombi; gawio linalopelekwa Hazina lisitishwe au lipunguzwe. Tuongeze mkakati kuhakikisha tunaongeza hifadhi zingine zinazo-*break even* kwa kukuza utalii wa ndani kwa kurekebisha na kuboresha miundombinu ya barabara na maeneo ya kuishi (makambi).

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni Msitu wa *Sao Hill*. Eneo hili linaingiza pesa nyingi kwenye Pato la Taifa lakini kuna tatizo kubwa sana kwenye eneo la miundombinu; barabara hazipitiki kabisa na ndiko kwenye eneo kubwa la uvunaji wa misitu. Ni vyema sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha akapeleka pesa kwa ajili ya kuboresha barabara za Mtili, Ifwagi, Mdafuro, Ihemu, Isipii – Mpangatuzwa mpaka Mrimba – ambako kuna pareto, chai pamoja na msitu mkubwa bila kusahau eneo la umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

MHE. OMARY M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba nimechangia hotuba kwa kuzungumza naomba tena kusisitiza juu ya hoja yangu ya kuongoza *Tax base* ambayo inaweza kuongezeka kwa kuzingatia vifungu vipya kwenye jedwali Na.2 ukurasa 42 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2014 idadi ya Watanzania ni 55,890,744 kwa tofauti ya umri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2014 Idadi ya Watanzania ni 55, 890,747 kwa tofauti ya umri:-

- (1) Umri kati ya mika 0 – 5 watu 9,628,845;
- (2) Umri kati ya 6 – 19 watu 20,836,171;
- (3) Umri kati ya 20 – 64 watu 23, 691, 680;
- (4) Umri kati ya 65 na kuendelea watu 1,734,051

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye kundi namba (3), umri wa mika 20-64 ambapo ndipo kwenye idadi kubwa. Hapa ukichukua Idadi ya watu 3,000,000 tu, tukizingatia kuwa hawa si mionganii mwa wale wadogo kwenye kundi la sekta isiyo rasmi, na ni kundi jipyaa. Wakifanikiwa kutoa shilingi laki moja (100,000) Serikali itaweza kukusanya bilioni mia tatu. Makundi mengine yaliyobaki yanaweza kusaidia Serikali kupata takribani billion mia saba; hii itakuwa imesaidia Serikali kupata takribani trillion moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania ambao hawajalipa wako wengi. Serikali inakusanya kodi kwa watu wale wale na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hawajafanya jitihada za kutosha kuongeza wigo wa idadi ya watu kulipa kodi. Nashauri; umefika wakati wa kupunguza mzigo wa Watanzania wanaolipa kodi kuwa ni wale wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku kila Mtanzania anatumia barabara, zahanati viwanja vyatungege, shule na vyuo vikuu bila kulipa kodi; ni lazima sasa kila Mtanzania aliye kodi kwa hiyari, na hili linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kutoa ushauri ni eneo la wataalamu wa *TRA* wanaofanya makadirio (*tax Assessors*). Eneo hili ndilo ambalo limelalamikiwa sana na Watanzania hususani wafanyabiashara. Hapa lazima wawepo watumishi wenye weledi mkubwa wa tasnia au elimu ya kodi; watu ambao watakuwa na uadilifu wa hali ya juu pamoja na uzoefu katika sekta ya kodi kiwe ni kigezo kikubwa. Si busara kijana awe amemaliza Chuo Kikuu na ana muda mfupi kazini halafu anapewa jukumu la ukadiriaji wa kodi

Mheshimiwa Naibu Spika, Naunga mkolo hoja.

MHE. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba niendelee pale nilipokatishwa katika mchango wangu Bungeni. Kwa maoni yangu binafsi TMX iongoze soko na WRS iishie kumsimamia mtunza ghala/mwendesha ghala, na Sheria ya Ushirika ihusike na ukusanyaji wa mazao na kuyawasilisha kwa mwendesha ghala na kusimamia malipo kwa wakulima kuititia *AMCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya mifuko inayotengenezwa na viwanda vitatu nchini kwa sasa ya kuhifadhi mazao, hasa ya nafaka, ili yasiharibike. Mifuko hiyo inapunguza *Post harvest loss* ambayo kwa sasa ni zaidi ya asilimia 40 hadi chini ya asilimia 10. Mifuko hiyo inakosa soko kwa sababu mbili kubwa. Kwanza VAT ya asilimia 18 inayosababisha bei yake kufikia sh. 5,000/= kwa mifuko mmoja na hivyo wakulima kushindwa kuinunua. Pili wakulima bado hawajaelimishwa faida na umuhimu wa kutumia mifuko hiyo na hivyo kuona bei ya 5,000/= kwa kila mifuko mmoja unaoweza kuhifadhi kilogramu 100 kuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifanye mambo mawili. Kwanza iondoe VAT kwenye vihifadhi nafaka ama vifungashio hivyo ili bei ishuke hadi 4,000/= na pili Serikali itoe elimu kwa wakulima juu ya umuhimu wa kutumia mifuko hii maalum ya kuhifadhi mazao ili yatumike kwa mwaka mzima bila ya kuharibika na wapate fursa ya kuyauza wakati bei ikiwa nzuri bdala ya kulazimika kuyauza wakati wa mavuno kipindi ambacho bei inakuwa ya chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali chini ya Uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miradi mikubwa ya kielelezo inayotekelizwa; ya *SGR*, Umeme, upanuzi wa magati ya Bandari za Dar es Salaam Mtwara na Tanga; vile vile ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi, bwawa la kuzalisha umeme katika Mto Rufiji pamoja na bwawa la kuzalisha umeme kwenye Mto Rusumo. Hakika miradi hii ni ya kihistoria na itatuaondoa kwenye umaskini wa kipato na usio wa kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia nyingine ni pamoja na kuhamishia Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kutoka Dareslaam na kuja hapa Dodoma. Dodoma ni katikati ya nchi yetu na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni historia ya kitaifa inayoandikwa na Serikali ya CCM ya Awamu ya Tano (5). Kuna historia nyingi zimeandikwa na Serikali hii ya CCM ya awamu ya Tano katika Wilaya zetu zote nchini. Kwa mfano Namtumbo kwa mara ya kwanza Serikali hii iliyoundwa na Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais na Waziri Mkuu Wilaya yetu tumejengewa kituo cha afya kimoja cha Kisasa kabisa, hospitali ya Wilaya, *VETA*; miradi mikubwa ya maji minne; umeme vijiji 43 kwa mpigo; minara ya mawasiliano katika kata 18 kati ya 21 tulizonazo; zahanati 11 kwa mpigo na kadhalika. Aidha, imetuleletea soko la mazao ya ufuta, tumbaku, soya na korosho pamoja na historia nyingine nyingi. Serikali hii idumu milele na milele, na tusiruhusu awamu nyingine ya utawala iingie

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba vituo vy alya, barabara, minara ya mawasiliano, miradi ya maji, zahanati na masoko ya mazao zaidi ili wata wa Namtumbo tuneemeke.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa michango yenu mliyotoa. Naamini Mheshimiwa Dkt. Mpango na Mheshimiwa Dkt. Kijaji wameisikia na wataalam wao pia hapa watakuwa wameisikia.

Kabla ya kuahirisha shughuli za Bunge liko tangazo la wageni:-

Tunao wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 100 kutoka Chuo cha *Tanzania Research and Career Development Institute* cha hapa Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kama wote mnavyofahamu kesho ni siku ya kupiga kura kwa ajili ya hii bajeti kwa hiyo, mnasisitizwa wote kuwepo kwa sababu kila mmoja ataitika kwa jina lake. Yule ambaye anaikubali bajeti, lakini pia yule ambaye haitaki bajeti wote wataitika kwa majina yao, ndio utaratibu uliopo kwa hiyo, mnahimizwa wote kuwepo.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 03.00 asubuhi.

(Saa 1.48 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 25 Juni, 2019, Saa Tatu Asubuhi)